16 APRILI, 2024

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

## Kikao cha Saba – Tarehe 16 Aprili, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA - KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):**

Randama ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha

2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA- KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaanza na Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Chege.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba yake nipo Mheshimiwa Nyongo.

**NAIBU SPIKA:** Kwa niaba.

Na. 79

**Hitaji la Jokofu Kituo cha Afya Kinesi - Rorya**

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO K.n.y. MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka jokofu katika Kituo cha Afya cha Kinesi - Rorya ili *mortuary* ianze kutoa huduma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Kinesi kimepokea jokofu la kuhifadhia maiti tarehe 24 Februari, 2024 kutoka Bohari ya Dawa *(MSD)* kanda ya Mwanza. Aidha, huduma inatarajiwa kuanza kutolewa mwishoni mwa mwezi Mei, 2024, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nyongo.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana; kwa niaba ya Mheshimiwa Chege, kwanza anatoa shukrani kubwa sana kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia Wanakinesi jokofu na sasa wataanza kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo maswali mawili ya nyongeza; wananchi wa Wilaya ya Maswa sasa takribani wiki tatu hawana jokofu kwa ajili ya kuhifadhi miili ya wapendwa wetu katika *mortuary* ya Maswa, inawabidi wapeleke miili kilometa 50 kwa maana ya Bariadi kwa ajili ya kuhifadhi. Leo wiki ya tatu na Maswa ni Mji mkubwa, Mheshimiwa Naibu Waziri tunaomba kujua lini wananchi wa Maswa watarejeshewa huduma hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; jokofu lililokuwepo ambalo limekwisha kuharibika lilikuwa na *capacity* ya kuhifadhi miili mitatu; je, kama mtatuletea jokofu jipya mko tayari kutuletea jokofu lenye kuhifadhi miili zaidi kwa maana ya kutoka mitatu walau kuwa miili sita? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Nyongo kwa namna ambavyo ameendelea kuwasemea wananchi wa Jimbo la Maswa Mashariki, lakini nimhakikishie kwamba Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan anajali sana huduma za afya na ndiyo maana ameendelea kujenga majengo mbalimbali ya kutolea huduma ikiwemo majengo ya kuhifadhia miili ya marehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie kwamba kuhusiana na jokofu la Hospitali ya Halmashauri ya Maswa natoa maelekezo kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Waziri wa Afya kwamba ni jambo la msingi sana hospitali ya halmashauri kuwa na jokofu linalofanya kazi. Haikubaliki hospitali ya halmashauri kukaa zaidi ya wiki tatu haina jokofu la kuhifadhia maiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niwaombe Bohari ya Dawa makao makuu wafanye tathmini ya aina ya jokofu kwa maana ya ukubwa wake linalohitajika kwa ajili ya kutunza miili ya marehemu katika Hospitali ya Halmashauri ya Maswa na wajitahidi ikiwezekana ndani ya wiki moja waweze kupeleka jokofu lile pale ili huduma kwa wananchi ziweze kwenda vizuri, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Daniel Awack.

Na. 80

**Ukarabati wa Kituo cha Afya Oldeani - Karatu**

**MHE. DANIEL A. TLEMAI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatoa fedha za ukarabati wa Kituo cha Afya Oldeani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Oldeani ni moja kati ya vituo vya afya ambavyo havina miundombinu ya kutosha ikiwa ni pamoja na jengo la kutolea huduma ya upasuaji wa dharura kwa akinamama wajawazito. Aidha, kituo cha Afya Oldeani kipo kwenye orodha ya vituo vya afya 202 kongwe vinavyohitaji ukarabati na upanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutafuta na kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya kuboresha miundombinu katika vituo vya afya kote nchini kikiwemo Kituo cha Afya Oldeani, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Awack.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kituo hiki cha Oldeani kimejengwa toka enzi za ukoloni, nini mkakati wa Serikali kuweza kukarabati Kituo hiki cha Afya cha Oldeani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali, kwanza tumekwishaainisha vituo vya afya kongwe na chakavu, lakini pia vituo vya afya ambavyo vina miundombinu pungufu ya vile ambavyo inatakiwa kulingana na *standard* ya vituo vya afya. Kituo cha Afya cha Oldeani ni miongoni mwa vituo vya afya ambavyo tayari tumeshaviainisha, tumeshafanya tathmini ya aina ya majengo yanayopungua na tathmini ya ukarabati unaohitajika.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mkakati wa Serikali upo timamu na tutahakikisha baada ya fedha kupatikana tunakwenda kuongeza majengo na kukarabati majengo katika kituo hichi cha afya, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Halmashauri ya Mji wa Mafinga kwa kutumia mapato ya ndani na kwa kushirikiana na wananchi wa Kata Bumilayinga tumejenga kituo cha afya ambacho kina *facilities* karibu zote isipokuwa hakina wodi ya kina baba na wodi ya watoto; je, Serikali ipo tayari kutu-*support* kwa kuleta fedha ili tujenge wodi ya kina baba na wodi ya watoto?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, niwapongeze wananchi wa Jimbo la Mafinga Mjini na Mheshimiwa Mbunge kwa kuhamasisha na kuchangia ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya Bumilayinga.

Nimhakikishie tu kwamba tunatambua kazi kubwa ambayo wananchi wameifanya kupitia michango yao, kupitia mapato ya ndani ya halmashauri na Serikali tunatafuta fedha kwa ajili ya kujenga wodi ya wanaume na wodi ya watoto ili kituo kile kiweze kutoa huduma vizuri.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya fedha kupatikana tutahakikisha tunapeleka pale ili kituo cha afya kikamilike kuwa na miundombinu yote, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Kituo cha Afya cha Mkwedu kilichopo katika Jimbo la Newala Vijijini hakina wodi za kulaza wagonjwa, ni lini Serikali italeta fedha ili wodi zile ziweze kujengwa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mtanda kwamba Serikali inatambua kwamba fedha zilikuja zikajenga kituo cha afya ambacho kina miundombinu pungufu ya ile inayohitajika kwa ajili ya kutoa huduma zote zinazotakiwa katika ngazi ya kituo cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote, kwamba vile vituo vya afya ambavyo tumevijenga kwa shilingi milioni 500 bado vina upungufu wa miundombinu ambayo tutahakikisha kwa awamu tunakwenda kujenga miundombinu ile kikiwemo kituo hiki cha afya katika Jimbo la Newala Vijijini, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Mwasai Kata ya Masela Wilaya ya Maswa kimechakaa, ni lini Serikali itapeleka fedha ili kuweza kukarabati kituo hicho?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Mwasai ambacho Mheshimiwa Mbunge amekitaja ni miongoni mwa vituo ambavyo vimeainishwa kwenye orodha ya vituo vya afya 202 chakavu ambavyo Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kwenda kufanya ukarabati na upanuzi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kituo hicho pia kipo kwenye orodha ambayo vitafanyiwa kazi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munde.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Manispaa ya Tabora katika Kata ya Misha kuna Kituo cha Afya cha Misha ambacho kinajengwa lakini mpaka sasa hatujajenga wodi ya mama na mtoto; je, ni lini Serikali itatuletea fedha ili tumalizie kujenga wodi hiyo ya mama na mtoto?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Kituo cha Afya cha Misha katika Manispaa ya Tabora, ni moja ya vituo ambavyo vimejengewa baadhi ya majengo, lakini havina majengo mengine ambayo ni muhimu kutoa huduma za afya kwa wananchi. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Munde kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI tayari tumeshakiingiza kwenye orodha ya vituo ambavyo vinahitaji miundombinu ya ziada ikiwemo wodi na majengo mengine ili vitoe huduma na mara fedha ikipatikana tutahakikisha tunaipa kipaumbele Misha ili kituo hicho kiweze kutoa huduma zote zinazotakiwa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Rwamlaza kwa niaba ya Mheshimiwa Anatropia.

Na. 81

**Kodi ya Mauzo ya Mazao - Kagera**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA K.n.y. MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza:-

Je, fedha kiasi gani imepatikana kama kodi ya mauzo ya kahawa, ndizi, maharage na mahindi katika Mkoa wa Kagera kwa mwaka 2010 – 2023?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 hadi 2023/2024 jumla ya shilingi bilioni 49.69 sawa na asilimia 108.28 ya makisio ya shilingi bilioni 45.89 zilipatikana kutokana na kodi ya mauzo ya kahawa, ndizi, maharage na mahindi katika Mkoa wa Kagera. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya shilingi bilioni 7.16 zinatarajiwa kukusanywa kutokana na mazao hayo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rwamlaza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana majibu ya Serikali. Mapato haya mimi nayaona kama ni kidogo na yanaashiria kwamba tija ya kilimo cha mazao hayo si nzuri; je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuhakikisha mazao haya yanalimwa na yanaweza kuleta tija zaidi katika nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zinazotuzunguka na hasa Uganda wameweza kuuza ndizi katika soko la Ulaya; je, ni mkakati

gani Serikali inao ambao unaweza kusaidia wakulima wa Kagera waweze kufaidi soko la kuuza ndizi katika soko la nje?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Rwamlaza kwamba Serikali imeendelea kuboresha sana sekta ya kilimo na masoko kwa ajili ya mazao yanayolimwa na wananchi yakiwemo mazao haya ambayo tumeyataja. Hata ukiona wastani wa miaka hiyo 10 tuliingiza shilingi bilioni 49 lakini kwa mwaka huu peke tunaingiza shilingi bilioni saba, kwa hiyo unaona kabisa kuna ongezeko katika mwaka. Jambo la msingi ni kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kuwekeza sana kwenye sekta ya kilimo kwa maana ya kilimo chenyewe pamoja na masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimhakikishie kwamba tunaamini masoko yataendelea kuongezeka na wananchi wetu wataendelea kupata masoko ya ndani na masoko ya nje yakiwemo masoko hayo ya Ulaya kulingana na fursa ambazo zitakuwa zinajitokeza, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante tunaendelea Wizara ya Viwanda na Biashara Mheshimiwa Malleko.

Na. 82

**Masoko ya Uhakika kwa Wajasiriamali**

**MHE. ESTHER E. MALLEKO** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuwasaidia wajasiriamali kuzalisha bidhaa bora na kupata masoko ya uhakika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, mipango ya Serikali katika kuwasaidia wajasiriamali kuzalisha bidhaa bora ili kupata masoko ya uhakika ni pamoja na:-

(a) Kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo *(SIDO)* na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* tunawasaidia wajasiriamali wadogo kupata maeneo na majengo ya kuzalishia bidhaa zao, pia kuwapatia mitaji kupita Mfuko wa *NEDF* na kuwapa nembo ya ubora wa bidhaa zao kwa miaka mitatu bila gharama;

(b) Kupitia *SIDO, TBS* na Wakala wa Vipimo *(WMA)* tunaendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali kuhusu kanuni za uzalishaji wenye tija, elimu ya utambuzi wa vifungashio na ufungashaji bora; na

(c) *SIDO* kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania *(TANTRADE)* tunaendelea kuandaa na kuratibu maonesho mbalimbali ndani na nje ya nchi ikiwa ni sehemu ya kuchagiza ukuaji wa soko la bidhaa zinazozalishwa na Wajasiriamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; sera ya biashara na sera ya *SMEs* zimepitwa na wakati, nini mkakati wa Serikali kuhuisha sera hizi ili ziweze kuleta tija kwa wajasiriamali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; nini mkakati wa Serikali kuweza kuwasaidia wajasiriamali kuzalisha bidhaa zenye ubora ili ziweze kuuzwa nje ya nchi na kuipatia Taifa fedha za kigeni? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Malleko kwa kufuatilia sana. Ni kweli moja ya changamoto tuliyonayo ni kuwa na sera za biashara na ile ya wajasiriamali wadogo *SMEs* kuwa za muda mrefu (Sera ya mwaka 2003). Mikakati ya Serikali sasa tumeshaanza kuzihuisha sera hizo ili ziendane na hali halisi ya soko na mahitaji ya sasa kwa wajasiriamali.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba tayari Serikali imeshaanza mchakato wa kuzihuisha sera hizo ili ziendane na hali halisi ya sasa ili kukidhi mahitaji ya wazalishaji na mahitaji ya bidhaa katika soko la ndani na la kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na mkakati wa pili tayari tumeshasema kwamba tunawasaidia wajasiriamali hawa kwanza kwa kuwakopesha na kuwapa mafunzo, lakini zaidi sasa tunaenda kuanza kujenga majengo au mitaa ya viwanda *(industrial parks)* katika halmashauri zote. Tuwaombe Waheshimiwa Wabunge, halmashauri na Serikali za Mikoa kwamba waendelee kutenga maeneo ambapo sisi kama Wizara kupitia *SIDO* tutaanza kujenga maeneo au mabanda ya viwanda ambapo humo wajasiriamali hawa wataweza kuzalisha bidhaa katika mazingira sahihi ili kukidhi ubora pamoja na kukidhi mahitaji ya bidhaa hizo katika soko la kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye uanzishwaji wa viwanda kuwasaidia wajasiriamali, *SIDO* uliowataja katika jibu la msingi imekuwa ni kikwazo kikubwa sana sana kwa walio na mitaji

midogo. Mheshimiwa Waziri unaweza kufuatilia kwa chini kuhakikisha wajasiriamali hawa wanapata huo mkopo kwa sababu masharti ni magumu na vigezo ni vigumu sana kuweza kuwasaidia watu hawa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, hoja ya Mheshimiwa Mbunge ni kweli lakini tayari mikakati ya Serikali ni kuona namna gani inawawezesha zaidi *SIDO* ili wapate mtaji zaidi wa kuweza kuwakopesha wajasiriamali wengi zaidi, kwa sababu sasa hivi wajasiriamali ni wengi kwa hiyo mahitaji ya mitaji na mikopo hii ni mikubwa sana na uwezo wa *SIDO* bado ni mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili tunataka sasa tulete sheria ya kuibadilisha *SIDO*, badala ya kuhudumia ianze kujiendesha kibiashara, hii itatusaidia kuhakikisha kuwa wanafanya kazi zao kibiashara na kukidhi mahitaji ya wajasiriamali ili waweze kupata mikopo kwa nafuu lakini kwa haraka zaidi kuliko ilivyo hivi sasa. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuiuliza Serikali ya kwamba wamekuwa wakifanya Maonesho ya Sabasaba kila mwaka na kusafirisha wajasiriamali wadogo wadogo kutoka mikoani.

Je, ni lini sasa Serikali itaimarisha maonesho katika mikoa au kanda ili kufanya ushiriki wa wajasiriamali wengi washiriki katika maeneo yao na kukuza biashara zao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kwanza nishukuru sana kwa hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwamba namna gani tunaanza kuweka mipango sasa ya kuhakikisha Maonesho haya ya Kimataifa ya

Kibiashara hapa Dar es Salaam maarufu kama Sabasaba yaweze kuenea katika mikoa mingine yote. Ni kweli tumeshaanza kufikiria hilo, lakini sambamba na hilo tunafanya na maonesho mengine si ya Sabasaba tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge hii ni sehemu ya mipango yetu na tutaona namna gani ya kuhakikisha kila mkoa uandae *either* katika bidhaa maalum au zao fulani, lakini pia kama inavyofanyika Dar es Salaam kwa bidhaa zote. Kwa hiyo, tutaendelea kufanya mikakati mbalimbali kuona namna gani maonesho haya yatafanyika katika mikoa yote na kwa nyakati tofauti.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Ngonyani.

Na. 83

**Ujenzi wa Daraja la Mitomoni – Ruvuma**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Daraja la Mitomoni linalounganisha Wilaya ya Songea na Nyasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya nyaraka kwa ajili ya kutangaza zabuni kwa mara ya pili kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Mitomoni yako katika hatua za mwisho. Zabuni zinatarajiwa kutangazwa kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2024. Zabuni za mara ya kwanza ambazo zilikamilika mwezi Machi, 2023 zilikosa

ushindani kwani ni mkandarasi mmoja tu ndiye aliyerudisha zabuni na bei yake ilikuwa juu sana na hivyo kulazimika irudiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 26 Januari, 2024 nikiwa na Mheshimiwa Stella Manyanya, Mbunge wa Nyasa nilitembelea eneo litakapojengwa daraja hili na kuzungumza na wananchi wa Kata ya Mipotopoto. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Ngonyani.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo hilo ni kwamba kuanzia mwaka 2017 wananchi zaidi ya 25 wamepoteza maisha kwa kuliwa na mamba lakini pia kwa kuzama kwenye eneo hilo.

Je, ni kwa nini Serikali haioni huruma kwa wananchi wake ambao wanapoteza maisha kwenye eneo hilo la Mitomoni na Mipotopoto?

(b) Je, Serikali haioni kama kuchelewa kujenga daraja hilo inaathiri kwa kiasi kikubwa uchumi wa Wilaya ya Nyasa na Wilaya ya Songea? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Msongozi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa kwenye ziara kwenye hii Kata ya Mipotopoto pia nilitembelea maeneo ambayo wananchi wamekuwa wakipata adha na nililazimika kusafiri kwa mtumbwi na kwa pikipiki ili kuweza kufika kwenye eneo hili ambapo tunatarajia kujenga daraja.

Kwa hiyo, Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ipo pamoja na wananchi

wa Wilaya ya Nyasa pamoja na Songea Vijijini na ndiyo maana tunafanya kila aina ya jitihada kukamilisha manunuzi, tumpate mkandasi ili tukajenge daraja la kudumu eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili linalohusu kuchelewa kujenga daraja hili, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, kama nilivyosema kufikia mwezi wa sita tutakuwa tumekamilisha hatua za manunuzi ili hatua ya ujenzi wa daraja hili iweze kuanza. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mawasiliano kati ya Mkoa wa Geita na Shinyanga katika eneo la Mwabomba na Masugwe leo ni zaidi ya siku ya tano daraja lile limejaa maji, na nimesema sana hapa Bungeni; sasa ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha daraja hili linajengwa kwa uhakika ili kuondoa adha kwa wananchi hawa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cherehani kuhusiana na eneo ambalo amelitaja, kwanza nimuagize meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Shinyanga afike kwenye eneo hili na kuhakikisha tunarudisha mawasiliano ili wananchi waondokane na adha hii ya kukosekana kwa mawasiliano. Pia nimepokea hoja ya Mheshimiwa Mbunge, ngoja niichukue tukaifanyie kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo, ajiandae Mheshimiwa Jesca.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Daraja la Mzinga linalounganisha Kongowe na Rangi Tatu litaanza kujengwa ili kuondoa msongamano wa magari yanayotoka Kusini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chaurembo kuhusu daraja; ni kweli hata yeye pamoja na Mheshimiwa Abdallah Ulega, Waziri wa Mifugo na Uvuvi eneo hili wamekuwa wakilisemea sana. Nipende kumwambia Mheshimiwa Chaurembo pamoja na wananchi wake kwamba tupo kwenye hatua za manunuzi ya kumpata mkandarasi ili kuweza kujenga daraja hili. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca, ajiandae Mheshimiwa Iddi Kassim.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alipotembelea Mkoa wa Iringa alituahidi ataanza ujenzi wa barababra ya lami mapema sana kuanzia Iringa Mjini mpaka Pawaga; je, ni lini ujenzi huo utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jesca, Mbunge wa Iringa Mjini kuhusu barabara ya Iringa – Pawaga kuwa habari njema ni kwamba tupo kwenye hatua ya kupata wakandarasi na barabara hii ni sehemu ya barabara ambazo kuna barabara ya Mtwara - Mingoyo – Masasi, lakini kuna barabara ya Songea kuelekea Njombe; na hii barabara ya Iringa – Pawaga. Kwa hiyo, kabla ya Bunge hili kuisha Juni, 30 tutakuwa tumepata mkandarasi ili kazi ya ujenzi wa barabara hii iweze kuanza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alipohudhuria utiaji wa saini wa mkataba wa ujenzi wa barabara ya Bulyanhulu – Kahama tulileta maombi kwako ya kuunganisha barabara kipande cha lami kinachotoka Kata ya Bulige kwenda Kata ya Ngaya.

Je, ni lini utekelezaji huu kuunganisha barabara ili kipande hicho kidogo cha lami kilichopo katikati ya Bulige na Ngaya kitaanza kufanya kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Iddi Kassim amekuwa akifuatilia sana ombi hili na nimpongeze sana kwa namna ambavyo amefuatilia barabara ya kutoka Kahama - Kakola ambayo tumekamilisha, tumesaini na mkandarasi ataanza *mobilization* kwa ajili ya kuanza kujenga hii barabara. Kuhusu maombi ya hiki kipande kama nilivyokuahidi tukiwa Jimboni kwako, Wizara tumeichukua na tunaifanya kazi. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maliasili, Mheshimiwa Amina Daud Hassan.

Na. 84

**Tathmini ya *Royal Tour***

**MHE. AMINA DAUD HASSAN** aliuliza: -

Je, watalii wangapi wameingia nchini tangu kufanyika kwa *Royal Tour* iliyoasisiwa na Mheshimiwa Rais ili kutangaza nchi yetu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa sekta ya utalii katika maendeleo ya nchi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano iliamua kufanya kampeni kubwa ya kuhamasisha watu kutoka sehemu mbalimbali duniani kuja kutembelea vivutio vyetu vya utalii. Kutokana na hali hiyo, Serikali kupitia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iliandaa filamu ijulikanayo kwa jina la *Tanzania The Royal Tour* ambayo ilizinduliwa Aprili, 2022. Katika filamu hiyo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa ndiye muhusika mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu filamu hiyo izinduliwe imeleta majibu chanya, ambapo kuanzia mwezi Mei hadi Disemba, 2022 kumekuwa na ongezeko la asilimia 40.38 la idadi ya watalii ambayo ilifikia 1,086,143 ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka 2021 ambapo idadi ya watalii ilikuwa 647,595. Aidha, idadi ya watalii iliendelea kuongezeka kwa asilimia 16.6 hadi kufikia watalii 1,302,271 kutoka watalii 1,086,143 kwa kipindi cha Mei hadi Disemba, 2023.

Vilevile kwa kipindi cha Januari hadi Disemba, 2023 idadi ya watalii imeendelea kuongezeka hadi kufikia watalii 1,808,205 ukilinganisha na watalii 1,454,920 waliotembelea nchi yetu kwa kipindi kama hicho mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 24.3. Hivyo ni dhahiri kuwa filamu ya *Tanzania The Royal Tour* imekuwa na matokeo mazuri sana katika sekta ya utalii na ni vema Watanzania wote kwa pamoja tukaunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina.

**MHE. AMINA DAUD HASSAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Waziri kwa majibu yake mazuri ya Serikali. Kwa kuwa filamu ya *Royal Tour* imefanya mambo makubwa katika Serikali yetu.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuiongezea maeneo yaliyobakia katika Tanzania ili Serikali yetu iweze kupata mapato mazuri? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya matokeo mazuri ya filamu hii ambayo Mheshimiwa Rais ndiye alikuwa kiongozi mkuu,

sasa Serikali imejipanga kuja na filamu nyingine ambayo itamshirikisha Mheshimiwa Rais pamoja na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, na hivi karibuni filamu hiyo itazinduliwa. Ni imani yetu kwamba filamu hii nayo itakuwa na mchango mkubwa katika kuyatangaza maeneo yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, kwa niaba yake Mheshimiwa Justin.

Na. 85

**Kuweka Vivutio vya Utalii katika Mji wa Ujiji Kigoma**

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA K.n.y MHE. KILUMBE S. NG'ENDA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka vivutio vya utalii katika Mji wa Ujiji ili watu mbalimbali duniani watembelee?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Ujiji, Kigoma ni miongoni mwa miji yenye historia kubwa ya kumbukumbu ya biashara ya watumwa na meno ya tembo. Kutokana na umuhimu huo Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na wadau katika sekta tumeanza kufanya tathmini ya kina ya njia ya biashara ya watumwa na meno ya tembo kuanzia katika Mji wa Bagamoyo, Pwani mpaka Mji wa Ujiji, Kigoma. Lengo la zoezi hilo ni kuibua fursa za utalii na kuboresha vivutio vyote vilivyopo katika njia hiyo ili kuvutia wageni na watalii kutoka ndani na nje ya nchi kutembelea maeneo hayo kwa ajili ya kuona kumbukumbu hiyo muhimu duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua nyingine ya kuboresha vivutio vya utalii wa kihistoria na malikale nchini Wizara imelenga kufanya tathmini ya maeneo yote ya malikale katika Mji wa Ujiji na maeneo mengine nchini ili kutambua umuhimu wake kwa lengo la kuyatunza kulingana na kanuni na sheria husika ili kuhakikisha kuwa uendeshaji wa shughuli za utalii katika maeneo yenye historia na malikale unafanyika kwa ufanisi mkubwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justin.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa majibu hayo kwa niaba ya Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda.

(a) Je, ni lini Serikali itaimarisha makumbusho ya biashara ya watumwa katika Mji wa Kigoma, Ujiji ili kuvutia watalii kwenye eneo hilo?

(b) Katika Wilaya ya Kilolo asilimia 80 ya Hifadhi ya Udzungwa ipo katika Wilaya hiyo, lakini hakuna lango hata moja kwa ajili ya kuimarisha vivutio vya watalii katika Wilaya ya Kilolo.

Je, ni lini Serikali itaweka mageti katika Wilaya ya Kilolo ili wataliii waweze kuingia kupitia mageti hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na hili la kuimarisha Makumbusho ya Ujiji, Serikali imekuwa ikilifanyia kazi na lipo kwenye mpango wetu. Naomba awe na subira wakati tutakapowasilisha bajeti yetu ataona jinsi ambavyo tumejipanga kuendeleza eneo hili, tunachoomba ni mtuunge mkono ili bajeti ile ipite tuweze kupata fedha za kutekeleza yale tuliyoyapanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hili la Kilolo na Udzungwa ni kweli eneo hili ni muhimu na ni miongoni mwa maeneo ambayo tumeyaweka kwenye vipaumbele vyetu vya kuweka mageti. Tunakwenda hatua kwa hatua, ninaomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira tutalifikia eneo hili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itatangaza vivutio vya utalii wa Kanda ya Mashariki ikiwemo Mikoa ya Morogoro, Pwani, Dar es Salaam na Tanga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ishengoma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari kwa sasa Serikali inafanya kazi kubwa ya kutangaza vivutio vya utalii kwenye Kanda ya Mashariki na ni kutokana na jitihada hiyo ndiyo maana tunaona idadi kubwa ya watalii wanakuja kwenye mbuga mbalimbali zilizopo kwenye ukanda huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tuendelee kushirikiana katika kutangaza vivutio vyetu vya utalii ili tuweze kupata mapato kwa nchi yetu, lakini vilevile kuongeza fursa za kiuchumi kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wilaya ya Ukerewe tayari ina vivutio vingi sana vya utalii; je, Serikali ina mkakati gani wa kuvitangaza ili vilete maslahi na manufaa kwa wilaya, lakini na Taifa kwa ujumla? Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kumjibu Mheshimiwa Mbunge swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeandaa mpango maalum wa kutangaza maeneo ya kwenye fukwe za Bahari, lakini vile vile kwenye maeneo ya visiwa. Wenzetu wa *TTB* wamefanya kazi kubwa ya kuainisha maeneo haya. Nimuombe Mheshimiwa Mbunge atuunge mkono kwenye bajeti inayokuja ili tuweze kupata fedha ya kufanya shughuli hii ya kutangaza maeneo yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri mnafanya kazi nzuri, lakini *walk the talk.* Haya maeneo mnayoyaainisha yafanyieni kazi kweli, mnakuwa na mipango mingi, lakini utekelezaji hamna, kwa hiyo tunataka watalii wengi zaidi.

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki naomba niulize swali lake la msingi….

**NAIBU SPIKA:** Halafu Mheshimiwa Esther Matiko kaa chini kwanza. *(Kicheko)*

Hatupeani nafasi kwa majina, kwa makabila, kwa dini au kwa rangi humu ndani. Kiti ndicho kitakachoamua nani anasema ndani ya Bunge.

*(Hapa Mhe. Esther N. Matiko aliendelea kusimama na kuzungumza bila kutumia kipaza sauti)*

**NAIBU SPIKA:** Kwani hili swali la Tarime au swali la nchi? Kaa chini. Mheshimiwa Neema uliza swali. *(Kicheko)*

Na. 86

**Ujenzi wa Uwanja wa Michezo Wilaya ya Tarime**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA K.n.y. MHE. MICHAEL M. KEMBAKI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga uwanja wa michezo Wilaya ya Tarime?

**NAIBU Spika:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali imejikita katika ujenzi na ukarabati wa viwanja vitakavyotumika katika Mashindano ya *AFCON 2027.* Viwanja hivyo ni pamoja na ujenzi wa Uwanja wa Arusha, Dodoma, ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa – Dar es Salaam, pamoja na Uwanja wa Uhuru uliopo pia katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Serikali ipo tayari wakati wowote kutoa ushauri wa kitaalam kwa wamiliki na wadau mbalimbali wa michezo wanaokusudia kujenga au kuboresha miundombinu ya michezo kwa kuzingatia miongozo ya mashindano ya mchezo husika ikiwemo Uwanja wa Tarime kama inavyoelekezwa katika kifungu cha 7(i),(ii) na (iv) cha Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995.

**NAIBU SPIKA:** Endelea endelea.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake; nilitaka kufahamu ni nini kauli ya Serikali, kutoa maelekezo ya kuhakikisha halmashauri zote nchini zisizokuwa na viwanja, zinajenga viwanja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia natamani kufahamu, kwa sababu michezo ni afya na michezo ni kazi, wana mpango gani wa kuhakikisha shule zote zinakuwa na viwanja vya michezo? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Michezo imebainisha kwamba shule zote na taasisi mbalimbali ziweze kuwa na viwanja mbalimbali vya michezo. Tayari nimeshaongea na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa na tumekubaliana tutahakikisha kwamba kila halmashauri iweze kuwa na viwanja vya michezo mbalimbali. Hivi sasa tuna halmashauri kama tisa tu ambazo zimeweza kutimiza maelekezo hayo. Tunataka halmashauri zote nchini ziweze kuwa na viwanja mbalimbali vya michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni maelekezo na mwongozo wa Wizara ya Elimu kwamba, hakuna shule ambayo inapaswa kusajiliwa kama haina viwanja vya michezo. Changamoto ni kwamba hivi karibuni viwanja vingi vya michezo mashuleni vimebadilishwa na kupewa matumizi mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tumejipanga kuhakikisha kwamba maeneo yote ya michezo katika shule na maeneo mbalimbali yanalindwa na kuendelezwa kwa manufaa ya Taifa letu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimo.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, je, Serikali iko tayari kushirikiana na Manispaa ya Moshi kuweza kutengeneza Uwanja wa *King George Memorial* kwa ajili ya kutumika kama uwanja wa mazoezi kipindi cha *AFCON 2027? (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi nimetembelea Moshi nikiambatana na Mbunge, Mheshimiwa Priscus Tarimo na tulitembelea Uwanja wa *King George Five*, tumekubaliana kwamba uwanja huo utatengenezwa ili utumike kama uwanja wa mazoezi kwa timu ambazo zitakuwa Jijini Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumetembelea uwanja wa *golf* pale Moshi na tayari Baraza la Michezo kwa kushirikiana na halmashauri wameanza taratibu za kuufufua uwanja wa *golf* pale Moshi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi; Uwanja wa Nangwanda Sijaona umechakaa na unahitaji marekebisho makubwa; je, Wizara kwa kushirikiana na mmiliki wa uwanja huo, wana mpango gani wa kufanya ukarabati mkubwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sera ya Michezo ya mwaka 1995 Wizara inapaswa kushirikiana na wamiliki mbalimbali wa viwanja, kutoa ushauri na maelekezo mengine ili kukarabati na kufanya viwanja viwe bora zaidi. Tutashirikiana na Chama Cha Mapinduzi ambao ndiyo wamiliki wa Uwanja wa Nangwanda Sijaona ili kuhakikisha kwamba uwanja huo unarudi katika hadhi yake kama ilivyokuwa zamani.

**NAIB SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Makamba, Mheshimiwa Oliver.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, pamoja na Serikali kuweka vipaumbele kuboresha viwanja vya mpira, vipaumbele hivyo havigusi utengenezaji wa

viwanja kwa ajili ya michezo mingine kama *netball, volleyball* na *basketball.* Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha angalau kila halmashauri inakuwa na *complex* ambayo inaweza ku-*accommodate* michezo yote ambayo inachezwa na vijana wetu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza utekelezaji wa jambo hilo na tumeanza katika Jiji la Dodoma na Jiji la Dar es Salaam ambapo tumejenga *recreation centres*, Dodoma na Dar es Salaam ujenzi unaendelea na *recreation centres* hizi zinakuwa na viwanja vyote. Kuna viwanja vya *football, netball, basketball, volleyball* na mabwawa ya kuogelea ya *olympic size*. Mpango huu sasa tukitoka katika majiji, tutakwenda katika mikoa yote na hatimaye katika halmashauri zote. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Makamba, siyo kila kitu ifanye Serikali, wewe ni Diwani, wekeni bajeti kwenye halmashauri yenu, jengeni viwanja. Mheshimiwa Oliver. *(Makofi)*

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona, changamoto iliyopo Tarime Mjini inafanana kabisa na changamoto iliyoko Wilaya ya Ngara; ningependa kujua, lini Serikali itajenga Uwanja wa Kokoto wa Wilaya ya Ngara? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oliver Semuguruka kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejipanga kwa kushirikiana na Halmashauri ya Ngara kuhakikisha kwamba Uwanja wa Kokoto uliopo Ngara unaweza kujengwa na kufikia viwango vizuri ili wananchi wa Ngara ambao Mheshimiwa Oliver

anawawakilisha, waweze kupata sehemu ya kufanya mazoezi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Mheshimiwa Jesca.

Na. 87

**Ahadi ya Mheshimiwa Rais ya Kuwasaidia Machinga – Iringa**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuwasaidia Machinga wa Iringa Mjini shilingi milioni 700 kwa ajili ya kuboresha mazingira yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inatambua umuhimu wa kutekeleza ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais ya kutoa shilingi milioni 700 kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kazi ya wafanyabiashara wadogo (Machinga) wa Iringa Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu itaendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya Fedha kwa lengo la kutekeleza ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii tangu mwezi Agosti, 2022 wameshindwa kuwasiliana na TAMISEMI na Wizara ya Fedha, wamepoteana na mpaka leo ahadi hii imeshindwa kutekelezwa na Machinga wa Iringa wanapata shida kubwa. Sasa ninaomba

tu kwamba suala hili kwa kuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, yeye mwenyewe alisikie kwa sababu ana masikio ya kusikia kwamba ahadi aliyoitoa mwaka 2022 kwa Machinga wa Iringa haijatekelezwa mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, naiomba Wizara ya Maendeleo ya Jamii, mtusaidie kama mtapata mikopo ile ya kwenu ya Wizara ili muweze kuwasaidia Machinga wetu wa Iringa na kama hilo linawezekana, Mheshimiwa Naibu Waziri naomba uni-*promise*. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ni utekelezaji na kwetu sisi ni kuzitekeleza ahadi ambazo tumezitoa. Tunaahidi kwamba ahadi zote Mheshimiwa Rais anazozitoa Wizara itatekeleza.

Mheshimia Naibu Spika, kuhusu suala la Iringa Mjini, tutashirikiana na Wizara husika kuhakikisha ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Rais inatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, fedha za wajasiriamali wadogo wadogo zipo na tutatekeleza kupitia taasisi za Serikali. Mara baada ya taratibu kumalizika basi fedha hizo zitatolewa taarifa katika halmashauri na mikopo hiyo kutolewa kwa wakati, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri mhusika.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa fursa hii, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niongezee kwamba tayari mpango wa kuwainua Machinga kiuchumi umeiva ambapo zile fedha shilingi bilioni 18.5 ambazo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alielekeza tuzitoe, zimeiva na tumeshaingia mkataba na benki husika, mwongozo

huu wa usajili wa machinga umekamilika na usajili unaendelea. Sasa tunakwenda kuuzindua mwongozo na ndani ya wiki hizi nne tunakwenda kuzindua utoaji mikopo hiyo, hivyo, kazi hii inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, *specific* kwa ajili ya Iringa, tulishawasiliana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ataona namna ya kuongeza hiyo fedha kwa ajili ya Wana-Iringa kama walivyokuwa wameahidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, simama bado, pamoja na majibu mazuri, machinga na mama lishe wanakopeshwa lakini bado wananyanyasika na mgambo. Wanashindwa kulipa mikopo yao, wananyang'anywa vyakula vyao na mali zao, hawa watu ni watu wa mazingira magumu sana na siyo kwa Dar es Salaam na Ilala, ni nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waambieni wakurugenzi wa halmashauri waache kunyanyasa watu waliojipanga. Kuna watu wamejipanga na wanafuata sheria lakini bado wanafuatwa kunyanyaswa na mgambo hapa Tanzania.

Mheshimiwa Tweve. *(Makofi)*

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, Mheshimiwa Waziri, pamoja na maelezo yako; wanawake, vijana na wenzetu wenye ulemavu ni moja ya kundi ambalo wako kwenye hawa machinga na walikuwa ni wanufaika wakubwa kwenye mikopo ile ya asilimia kumi. Ni miaka miwili sasa ile mikopo ilikuwa imesitishwa, ninataka kusikia kauli yako leo, ni lini mikopo hii itaanza kutolewa ili makundi haya waweze kunufaika na mikopo hii? Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**: Mheshimiwa Naibu Spika, kama

nilivyoeleza, fedha hizi tayari zimeshatayarishwa. Hivi sasa tunaendelea kushirikiana na taasisi za fedha, *soon* tu hizi fedha zitatolewa kwa ajili ya mikopo na wananchi wote ambao wanahitaji mikopo hiyo watapatiwa na Mheshimiwa Rais ameshaelekeza kwamba fedha hizi zitolewe kwa utaratibu maalum na sisi tunalifanyika kazi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

Na. 88

**Kuimarisha Huduma za Afya Zahanati za Jeshi la Polisi**

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA K.n.y. MHE. STANSLAUS S. MABULA** aliuliza: -

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuimarisha utoaji wa huduma kwenye zahanati zinazomilikiwa na Jeshi la Polisi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa kuimarisha utoaji huduma za tiba ndani ya Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi lina jumla ya zahanati 37 ambazo huhudumia askari, familia za askari pamoja na wananchi wanaoishi maeneo ya jirani. Katika kuimarisha huduma za tiba Serikali hutoa fedha za ujenzi wa majengo na ukarabati wa miundombinu ya hospitali, kugharamia masomo kwa madaktari na watoa huduma za tiba, kutoa fedha kwa ajili ya kununua dawa na vifaa tiba kutoka *MSD* na kuwezesha kutolewa huduma ya baba, mama na mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuboresha huduma na miundombinu ya hospitali, vituo vya afya na zahanati sambamba na upandishaji hadhi ili kukidhi ubora wa huduma za tiba ndani ya Jeshi la Polisi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kwa niaba.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali; kwa kuwa Mwanza pale Mabatini ni *hub* ya Kanda ya Ziwa, askari wote wanaotoka kwenye mikoa mbalimbali wakilazwa Bugando huwa wanakwenda pale kwa ajili ya kusubiri kliniki.

Je, Serikali kwa kuwa inaendelea, inahitaji kuboresha kuwa kituo cha afya, kabla ya kuboresha kituo cha afya, kwa nini isijenge *theatre* pamoja na wodi ili kuhakikisha kwamba hawa askari ambao wametumikia Taifa kwa muda mrefu wanapata huduma? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa kutambua umuhimu wa zahanati hii ambayo iko Mwanza kwa maana inayohudumia Kanda nzima ya Ziwa, Serikali kupitia Jeshi la Polisi itaunga mkono juhudi za umaliziaji na kuboresha zahanati hii ili kuweza kutoa huduma kwa askari wetu pamoja na wananchi walio jirani na maeneo hayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kiswaga. Mheshimiwa Ndege. *(Kicheko)*

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona, Zahanati ya Polisi katika Mji wa Babati ina upungufu mkubwa wa vifaa tiba jambo ambalo linasababisha wagonjwa kukosa baadhi ya huduma; je, ni lini sasa Serikali itapeleka vifaa tiba katika kituo hiki? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba kuna uhaba wa vifaa tiba katika zahanati aliyoisema Mheshimiwa Mbunge, lakini namhakikishia kwamba jinsi Serikali tutakavyopata fedha basi

tutapeleka vifaa tiba katika zahanati hii ya Babati ili kutoa huduma kwa ajili ya askari wetu pamoja na wananchi walio jirani. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

Na. 89

**Kudhibiti Usimamishaji wa Vyombo vya Usafiri Mara kwa Mara**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza: -

Je, Serikali inadhibiti vipi suala la vyombo vya usafiri wa umbali mrefu kusimamishwa barabarani mara kwa mara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilishaweka utaratibu wa magari kwa magari yote ya mizigo na abiria yanayokwenda umbali mrefu kufanyiwa ukaguzi na upekuzi kwenye maeneo ya mizani kwa mujibu wa Kanuni ya Udhibiti wa Uzito wa Mizigo Barabarani ya mwaka 2017 pamoja na Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Udhibiti wa Uzito wa Magari ya Mizigo na Abiria ya Umbali Mrefu Namba 1 ya mwaka 2016, lengo ni kurahisisha na kuwahisha safari za magari hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vilivyotengwa kwa ajili ya ukaguzi huo ni Vigwaza, Mikumi, Makambako Mpemba, Kasumuru, Njiku Nyakahura, Msata, Kimokouwa, Mkuranga, na Mnazi Mmoja. Pia mabasi ya abiria ya safari za ndani yatakaguliwa kwenye vituo vya mabasi na sehemu maalum zilizotengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo vyombo hivyo vya moto vitakuwa vimetenda makosa kwa kukiuka Sheria ya Usalama

Barabarani, vitachukuliwa hatua za kisheria sehemu ambapo makosa hayo yametendeka. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa kuwa, inaaminiwa ukaguzi unafanywa kwa vyombo vya safari kabla ya safari; je, Serikali ina mpango gani wa kuandaa *app* (mtandao wa kidigiti) ambao utahakikisha wakati wowote mtu unaweza kuona kama ukaguzi umefanyika kweli, hasa kwa vile kuna baadhi ya vituo vikubwa vya mabasi, utamuona kondakta anakimbia mbio anapeleka karatasi ndani, inapigwa muhuri na safari kuendelea bila kujali kama ile gari imekaguliwa, ni nzima au vipi, kwa hiyo, kusababisha madhara au ajali, kupoteza maisha na mali za watu huko mbele ya safari, Serikali ina mpango gani? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbungeu kwamba Wizara yetu ya Mambo ya Ndani iko kwenye maboresho makubwa sana, tunafanya *transformation* ili kuhakikisha kwamba magari yote ya mizigo na abiria toka yanapotoka yanapimwa uzito wake, lakini pia tunaboresha na kuhakikisha kwamba huko mbele tunakoenda pia tutaweka *app* ya kuhakikisha kwamba tuna-*track* magari yote jinsi yanavyosafiri na kuhakikisha hayaongezi mizigo na yanasafiri kule ambako yanatarajiwa kufika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kumekuwa na utaratibu wa Askari wa Usalama Barabarani kusimamisha magari tena kwa ghafla kwenye *highways* kitu ambacho kinaweza kikasababisha hata kutokea kwa ajali; sasa ninataka kujua ni lini Serikali itaanza kutumia mfumo wa kielektroniki ambao utakuwa una-*record* kama kuna

makosa yoyote yametokea kuliko ilivyo hivi sasa ili kuweza kupunguza ajali barabarani? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asha, ni kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani iko kwenye *transformation* ya kuhakikisha tunaweka kamera za usalama barabarani ili kuhakikisha magari yote yanayosafirisha mizigo na abiria pia yanakwenda salama na hakuna tena ukaguzi wa ghafla kwa jinsi ambavyo tunaendelea mbele. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Shangazi kwa niaba ya Mheshimiwa Kandege.

Na. 90

**Kujenga na Kukarabati Mahakama za Mwanzo Kalambo**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza: -

Je, nini mpango wa Serikali wa kujenga na kukarabati Mahakama za Mwanzo Wilayani Kalambo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali, naomba kwanza nianze kutoa shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu na kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini na kunibadilishia majukumu kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuja katika Wizara ya Katiba na Sheria. Ni ahadi yangu kwake Mheshimiwa Rais na Watanzania kwa ujumla kwamba nitatimiza wajibu wangu huo kwa uaminifu, weledi na bidii ya kazi sana. Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Serikali...

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa natoa shukrani kwa Mheshimiwa Rais, naomba nijibu swali sasa. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Haya jibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tumekuwa tukisema mara nyingi hapa Bungeni, Mahakama kwa muda mrefu imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya uhaba na uchakavu wa majengo hususan kwa Mahakama za Wilaya na za Mwanzo. Maeneo mengi nchini Mahakama za Mwanzo ni chakavu na majengo ni finyu hivyo kuhitaji kujengwa upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili limepewa msukumo wa kipekee kwa kuweka Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama kwa awamu. Kupitia mpango huo katika mwaka 2019/2020 imeshajengwa Mahakama ya Mwanzo Msanzi katika Jimbo la Kalambo, na katika mwaka wa fedha 2023/2024 Mahakama ya Wilaya pamoja na Mahakama ya Mwanzo ya Kasanga zinajengwa. Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ya Mwanzo Mlalo, inasadikika kuwa ni miongoni mwa Mahakama za mwanzo kabisa

hapa nchini, ambayo imejengwa mwaka 1926. Mahakama hii ni chakavu sana na iko katika hali mbaya; je, Serikali ina mpango gani mahususi wa kukarabati au kujenga Mahakama mpya katika Tarafa hii ya Mlalo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mahakama hii ni ya mwaka 1926, ni kongwe vya kutosha na inahitaji kufanyiwa ukarabati mkubwa au kujengwa upya kabisa. Ili kukabili hilo, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, tunao mpango mkakati wa kuanza kuzikarabati na kujenga upya Mahakama nchini ambazo zina hali mbaya na mwaka ujao tutakuwa na ukarabati wa Mahakama za Mwanzo 72.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutawasiliana na Mheshimiwa Mbunge na uongozi wa Mahakama, *especially* Mtendaji Mkuu wa Mahakama, ili kuona Mahakama yake itaingia kwenye ukarabati huo kwenye awamu ipi, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Uchukuzi. Mheshimiwa Mohemed Said Issa.

Na. 91

**Kuondoa Mbwa Bandari ya Dar es Salaam**

**MHE. MOHAMED SAID ISSA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaondoa mbwa wanaokagua mizigo katika meli za abiria Bandari ya Dar es Salaam kwenda Zanzibar kwa kuwa siyo rafiki kwa abiria?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Said Issa, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)* inalo jukumu la msingi la kufanya ukaguzi wa kina kwa abiria, mizigo na vifurushi vinavyopita katika maeneo ya gati za abiria *(passenger terminals)* ikiwemo gati zinazohudumia *Azam Sea Link* na majahazi *(lighter quay)* kwa ajili ya kudhibiti usalama wa abiria na usafirishaji wa bidhaa haramu kupitia maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi unaofanywa ni wa kawaida kwa kutumia midaki na pale inapotokea mizigo au vifurushi vinavyotiliwa mashaka, ndipo mbwa maalum wa ukaguzi hutumika, na ukaguzi unaofanywa kwa kutumia mbwa hauhusishi abiria na mizigo au vifurushi vyenye vyakula.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; je, Serikali itakuwa tayari kuwachukulia hatua watendaji ambao wanafanya ukaguzi wa mbwa kwa mizigo ya abiria wanaokwenda Zanzibar kuwa ni suala la kila siku?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Serikali inatoa kauli gani ili jambo hili lisijirudie rudie tena? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari na watendaji wanapofanya ukaguzi wazingatie utaratibu ambao tumeusema hapo awali, na kw asababu hiyo ikibainika yuko mtendaji ambaye anafanya kinyume na tunavyotarajia

katika tamaduni zetu, utu wetu, na kadhalika basi aweze kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu.

Na. 92

**Mpango wa Ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo**

**MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza: -

Je, mpango wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo na eneo la viwanda Bagamoyo umefikia hatua gani ya utelekezaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TPA* imekamilisha zoezi la kulipa fidia kwa wananchi wanaopisha eneo la mradi lenye ukubwa hekta 887. Kwa sasa mradi huo upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji wa uhuishaji wa taarifa ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina uliofanya mwaka 2010. Kazi hii inatarajia kukamilika ndani ya mwaka huu wa fedha 2023/2024 ili kuanza hatua za ununuzi wa mkandarasi atakayejenga bandari hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali, kupitia *TPA,* imetenga jumla ya shilingi bilioni 22 kwa ajili ya kutekeleza mradi huo. Vilevile ujenzi wa mradi huu utafanyika kwa awamu kulingana na matarajio ya ukuaji wa shehena na ongezeko la meli ambapo awamu ya kwanza itahusisha ujenzi wa magati matatu yenye jumla ya urefu wa mita 1,000 na kina cha zaidi ya mita 15.5. Pia ujenzi wa bandari hiyo ni wa kimkakati kwa kuwa, utachochea shughuli za viwanda na biashara katika eneo la Ukanda Maalum wa Kiuchumi wa Bagamoyo *(Special Economic Zone)*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza napenda kuishukuru sana Serikali yetu ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutupa matumaini ya ujenzi wa Bandari hii ya Bagamoyo baada ya kuweka jiwe la msingi mwaka 2015, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali yangu ya nyongeza ni kama ifuatavyo; kwa kuwa baadhi ya wakazi wa eneo la Pande waliahidiwa kupewa viwanja kwenye eneo la Kidagoni wakati wa sherehe za uwekaji wa jiwe la msingi mwaka 2015 na Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Kikwete na pia kuna baadhi ya wananchi bado wanadai fidia.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, upo tayari kutembelea maeneo ya Pande, Mlingotini, Kidagoni na Kondo ili kuongea na wananchi uweze kupata uhakika na wananchi hawa wapate haki zao stahiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa huu ni mradi mkubwa na kwa mara ya kwanza unatengewa shilingi bilioni 22, ili kuanza hatua za awali. Je, Serikali inatuahidi nini wananchi wa Bagamoyo, hususani vijana wetu na wanawake, juu ya kupata ajira za kitaalam na zisizokuwa za kitaalam? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, namba moja, niko tayari kutembelea eneo la Pande ili kuweza kupata picha kubwa zaidi juu ya malalamiko ambayo Mheshimiwa Subira Mgalu ameyazungumza kwamba waliahidiwa kupewa viwanja na wengine hawakupewa fidia kama walivyotarajia, lengo likiwa ni kuendelea kuleta furaha kwa wananchi wetu. Kwa hiyo,

tutapanga mimi na yeye atakapopata nafasi mimi niko tayari kwa ajili ya kwenda na bahati nzuri Bagamoyo siyo mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, namuahidi yeye, lakini siyo yeye tu, pamoja na maeneo yote ambako zinajengwa bandari, tulisema maneno haya tulipokuwa *Mbamba Bay* na pia tunasema kwa pale Bagamoyo kwamba tunapofanya mradi katika Wizara ya Uchukuzi ni lazima wananchi wa eneo husika wenye sifa wafikiriwe kwa ajili ya kupata ajira.

Kwa hiyo, nawapa uhakika akinamama wa Mkoa wa Pwani, hususani eneo hilo la Bagamoyo, mradi utakapoanza watapewa kipaumbele pamoja na vijana na watu wengine wenye uhitaji wa ajira hizo, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, njoo uweke tena Hati Mezani. Mara ya kwanza kuna maneno mliyaacha, yarekebishe kwa kumbukumbu sahihi za *Hansard*.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa, maswali yamekwisha sasa ni kipindi cha kutambulisha wageni.

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika; wageni wa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ndugu Adolf Ndunguru - Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Ndugu Sospeter Mtwale - Naibu Katibu Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Dkt. Charles Msonde - Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais,

Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Elimu); na Dkt. Mahera Charles - Naibu Katibu Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Afya). *(Makofi)*

Vilevile tunao Mhandisi Rogatus Mativila - Naibu Katibu Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Miundombinu); Ndugu John Cheyo - Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na Mhandisi Victor Seff - Mtendaji Mkuu *TARURA*. *(Makofi)*

Yupo pia Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mwenyekiti wa Bodi, Shirika la Masoko Kariakoo; Mheshimiwa Hawa jamani alikuwa Mbunge mwenzetu, hongera sana Mwenyekiti. *(Makofi)*

Tunaye pia Ndugu Richard Atufigwegwe Kasesela, *MNEC* Taifa, Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa ni Wakuu wa Mikoa kutoka Tanzania Bara, Mheshimiwa Rosemary Staki Senyamule (Dodoma), Mheshimiwa Paul Christian Makonda (Arusha); na Mheshimiwa Albert John Chalamila (Dar es Salaam), karibu Mkuu wa Mkoa wangu, karibu sana. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Martin Reuben Shigella (Geita), Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba (Iringa), jamani ana-*trot* huyo. *(Makofi)*

Tunao Mheshimiwa Fatuma Abubakar Mwassa (Kagera), Mheshimiwa Thobias Andengenya, Kamishna Mstaafu (Kigoma), Mheshimiwa Nurdin Hassan Babu (Kilimanjaro); na Mheshimiwa Kanali Evans Alfred Mtambi (Mara). Mheshimiwa Matiko mbona haupigi makofi? *(Makofi/Kicheko)*

Wapo pia Wakuu wengine wa Mikoa ambao ni Mheshimiwa Kanali, Patrick Kenani Sawala (Mtwara), Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda (Mwanza), Mheshimiwa Anthony John Mtaka (Njombe), Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere (Rukwa), Mheshimiwa Kanali Ahmed Abass Ahmed (Ruvuma), Mheshimiwa Anamringi Isaay Macha (Shinyanga), Mheshimiwa Halima Omari

Dendego (Singida), Mheshimiwa Matiko Paul Chacha (Tabora), Mheshimiwa Balozi Dkt. Batilda Salha Burian (Tanga) na Mheshimiwa Anna Gidarya, Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa Simiyu ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Itilima. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa ambao ni Wakurugenzi na Maafisa kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambao ni viongozi wa Mikoa wa Chama Cha Mapinduzi, Wajumbe wa *NEC* wa Mikoa na Wawakilishi Watendaji Kata. *(Makofi)*

Pia wapo wawakilishi wa *NGO'S* kutoka *JICA*, *KOICA*, *CRDB*, *NMB*, *Barrick Twiga Minerals*, *Carbon Center – Tanzania, Up Energy*, *The Nature Conservation* na *USAID Tuhifadhi Maliasili*. Simameni kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mchengerwa anao wageni wengine na hawa ni Wenyeviti wa Mikoa wa CCM Tanzania Bara ambao wako 26, wa-*NEC* kutoka Tanzania Bara wako 26 na Makatibu wa Mikoa 26 Tanzania Bara. Mheshimiwa Waziri naona umemaliza kila kitu sasa. *(Makofi)*

Tunao wageni kumi ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kutoka Bunge la Uganda; Mheshimiwa Olanya Gilbert - Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Rwemulikya Ibanda - Mjumbe, Mheshimiwa Isingoma Patrick Mwesigwa – Mjumbe, Mheshimiwa Ochan Patrick - Mjumbe, Mheshimiwa Naluyima Betty Ethel - Mjumbe, Mheshimiwa Paparu Lilian Obiale - Mjumbe, Ndugu Mujurizi Clare - Katibu wa Msafara, Ndugu Nsiima Emmanuel - Katibu Kamati, Ndugu Nanteza Ntalazi Olivia - Afisa Ukaguzi na Ndugu Ssalongo Willie Kunya - Afisa Ukaguzi, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni 22 wa Mheshimiwa Dorothy Gwajima, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na hawa ni viongozi wa SMAUJATA Taifa kutoka Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Jenejelly Ntate ambao ni Wanachama wa Chama cha Wafanyakazi wa Majumbani kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni 35 wa Mheshimiwa Rose Tweve ambao ni Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa UWT kutoka Wilaya ya Iringa Vijijini. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo hawa ni waumini wa Kanisa Katoliki *USA-River* kutoka Arumeru Mashariki, Mkoa wa Arusha, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 39 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 33 na walimu saba wa Shule ya Awali ya Msingi ya *Glorious Day Care, Pre and Primary School* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Wapo watumishi nane kutoka Kampuni ya *Alliance Life Assurance Limited* wakiongozwa na Mtendaji Mkuu, Ndugu Byford Mutumusakwa, wapo viwanja vya Bunge kwa ajili ya kuonesha huduma zao za Bima za Maisha, karibuni. *(Makofi)*

Yupo mgeni mwingine ni Ndugu Irene Kivo kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba Kampuni ya *Alliance Life Assurance Limited*, ipo Viwanja vya Bunge nyuma ya Ukumbi wa Msekwa, kwa ajili ya kutoa elimu ya bima ya maisha kwa Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Ofisi ya Bunge, kwanzia tarehe 15 hadi 19 Aprili.

Waheshimiwa Wabunge, mnaombwa kutembelea maonesho hayo.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Mtoa Hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba hotuba yangu yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge lako hili Tukufu *(Hansards)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mafungu 28 ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka 2023/2024 na kupitisha Mpango wa Utekelezaji wa Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutumia nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya afya njema na kutujalia ari na hamasa ya kutekeleza majukumu yetu ya Kibunge kwa manufaa mapana ya wananchi wote wa Tanzania. Aidha, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama leo mbele ya Bunge lako hili Tukufu kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango, Makadirio na Matumizi ya fedha za Serikali Mafungu 28 ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa imani kubwa aliyokuwa nayo kwangu na kuniteua kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutumia nafasi hii pia kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mbunge) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais na kuendelea kuimarisha ustawi wa watu wa Taifa la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo (Mbunge), Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga (Mbunge), Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati kwa uchambuzi, ushauri na maelekezo katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu, Naibu Mawaziri Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange na Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba; Katibu Mkuu, Ndugu Adolf Ndunguru; Naibu Makatibu Wakuu, Dkt. Charles Msonde, Dkt. Wilson Charles, Ndugu Sospeter Mtwale, Mhandisi Rogatus Mativila; Bibi Paulina Nkwama, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu; Watendaji Wakuu wa Taasisi; Wakurugenzi na watumishi wote kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha Ofisi ya Rais, TAMISEMI kufikia malengo ikiwa ni pamoja na kukamilisha hotuba hii kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatambua kazi kubwa na kazi nzuri inayofanywa na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa nchini ambao tupo nao hapa siku hii ya leo. Ninawashukuru pia Wenyeviti wa CCM 26 wa Tanzania Bara waliokuja siku hii ya leo ambao nao wapo hapa kushuhudia uwasilishaji wa hotuba hii ya Wizara ya wananchi yaani TAMISEMI. Ninawashukuru pia Wajumbe wa Halmashauri Kuu Taifa wa mikoa yote 26 ya

Tanzania Bara na Makatibu wa Mikoa Tanzania Bara 26 wa CCM ambao pia tupo nao hapa siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, salamu za pole; natoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wabunge pamoja na Watanzania wote, kwa kuondokewa na wapendwa wetu, Hayati Alhaji Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili na Hayati Edward Ngoyai Lowassa, Waziri Mkuu Mstaafu. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Francis Leonard Mtega aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali - Mbeya na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani - Zanzibar. Aidha, napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu, pamoja na Watanzania wote walioondokewa na wapendwa wao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninatoa pole kwa wananchi wote waliokumbwa na maafa mbalimbali na majanga ya asili ya mafuriko na maporomoko ya udongo yaliyotokea Wilaya ya Hanang, Mkoa wa Manyara, wananchi wa Wilaya ya Rufiji, Mkoani Pwani pamoja na maeneo mengine yaliyopatwa na maafa ya mafuriko. Ninawapa pole sana na ninamwomba Mwenyezi Mungu awajalie wepesi katika kipindi hiki kigumu wanachopitia na niwahikikishie Serikali yao ipo pamoja nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninawashukuru sana wananchi na wadau mbalimbali kwa michango yao ya hali na mali waliyoitoa na wanayoendelea kuitoa kwa ajili ya wananchi waliokumbwa na maafa hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ni utekelezaji wa Bajeti Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka 2023/2024, ukusanyaji wa maduhuli ya mikoa na mapato ya ndani; katika mwaka 2023/2024 Mafungu 28 ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI yaliidhinishiwa

kukusanya maduhuli na mapato ya ndani ya shilingi trilioni 1.19 ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.07 ya mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 127.55 sawa na 11.90%. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 55.14 ni za taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI; shilingi bilioni 261.89 ni maduhuli ya mikoa na shilingi trilioni 1.14 ni za mapato ya ndani ya halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Machi, 2024 shilingi bilioni 863.78 zimekusanywa sawa na 72.02% ya lengo na kati ya fedha hizo shilingi bilioni 848.14 ni mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa; shilingi bilioni 15.44 ni mapato ya ndani ya taasisi na shilingi milioni 193.79 ni maduhuli ya mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa; katika kipindi cha Awamu ya Sita imeendelea kuimarika ambapo makadirio yameendelea kuongezeka kutoka shilingi trilioni 1.01 mwaka 2022/2023 hadi shilingi trilioni 1.14 mwaka 2023/2024. Aidha, makusanyo halisi yameongezeka kutoka shilingi bilioni 625.32 mwezi Machi, 2023 hadi shilingi bilioni 848.14 mwezi Machi, 2024 ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 222.82.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka kumi mwenendo wa makusanyo ya mapato ya ndani ya halmashauri umeendelea kuimarika. Makisio ya mapato ya mwaka 2013/2014 yalikuwa shilingi bilioni 395.81 na mwaka 2022/2023 yamefikia shilingi trilioni 1.01 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 617.20. Aidha, makusanyo halisi katika miaka hiyo yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 323.27 hadi shilingi trilioni 1.02 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 697.76. Vilevile makisio ya mwaka 2024/2025 yamefikia shilingi trilioni 1.35 hii inaonesha dhahiri kuimarika kwa makusanyo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290, kupitia Sheria ya Fedha Na. 2 ya mwaka 2023 yamezipa Mamlaka za Serikali za Mitaa jukumu la uwakala wa kusimamia na kukusanya vyanzo vya kodi ya majengo na kodi ya pango la ardhi. Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeanza ujenzi wa moduli ya vyanzo hivi katika mfumo wa *TAUSI*

kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Ukusanyaji wa mapato kutokana na vyanzo hivi utaanza tarehe 01Julai, 2024 kwa kutumia mfumo huu wa *TAUSI*.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa fedha za taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa; hadi Machi, 2024 halmashauri zimekusanya shilingi bilioni 848.14 sawa na 74.155% ya bajeti iliyoidhinishwa. Halmashauri zimeonesha kufanya vizuri ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/2023 ambapo kiasi cha shilingi bilioni 625.32 kilikusanywa sawa na 62%. Kuongezeka kwa mapato ya ndani kunasadifu dhana ya Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliyekuwa na maono makubwa kuhusu ukusanyaji wa mapato akiamini kuwa mapato yanapaswa kukusanywa kwa ufanisi ili kuwezesha maendeleo endelevu na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maneno yake Baba wa Taifa alisema; "mapato ni damu ya maendeleo, bila ya mapato hakuna maendeleo. Nchi maskini si maskini kwa sababu hazina maliasili, zana au watu hodari. Zipo nchi tajiri duniani ambazo hazina haya. Pia maskini ni maskini kwa sababu mapato yake ni madogo." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato kumewezesha kuongezeka kwa matumizi ya fedha za mapato ya ndani kwenye miradi ya maendeleo kutoka shilingi bilioni 194.80 zilizotumika hadi Machi, 2023 ikilinganishwa na shilingi bilioni 226.05 zilizotumika hadi Machi, 2024. Aidha, shughuli zinazotekelezwa zimeainishwa katika aya ya 30 hadi 33 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Masoko Kariakoo; shirika kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam limeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa soko jipya la Kariakoo lenye ghorofa sita za juu na ghorofa mbili za chini na ukarabati wa jengo kuu la Soko la Kariakoo. Mradi ulianza kutekelezwa mwezi Januari, 2022 kwa gharama ya shilingi bilioni 28.03. Utekelezaji wa mradi umefikia 93% na maandalizi ya ufunguzi wa

soko yanaendelea ili biashara zianze mwanzoni mwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo; katika mwaka 2023/2024 Mafungu 28 ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI yaliidhinishiwa bajeti ya shilingi trilioni 9.18. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 3.52 ni fedha za maendeleo na shilingi trilioni 5.65 ni za matumizi ya kawaida, yakijumuisha mishahara shilingi trilioni 4.59 na matumizi mengineyo ni shilingi trilioni 1.06.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Machi, 2024 Mafungu 28 yamepokea na kukusanya shilingi trilioni 6.99 sawa na 76.18% ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 4.47 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida yakijumuisha mishahara shilingi trilioni 3.66; na matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 810.77 na shilingi trilioni 2.52 ni fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya utekelezaji ya bajeti kwa mwaka 2023/2024; katika mwaka 2023/2024 Mafungu 28 ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI yametekeleza shughuli zifuatazo:-

Kwanza maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa mwaka 2024; katika mwaka 2023/2024 Ofisi ya Rais, TAMISEMI iliidhinishiwa shilingi bilioni 12 kwa ajili ya maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwaka 2024. Hadi mwezi Machi, 2024 Ofisi ya Rais, TAMISEMI imepokea shilingi bilioni 5.6 sawa na 46.67% ya fedha iliyoidhinishwa. Sehemu kubwa ya fedha ambazo hazijapokelewa zinahusika na shughuli za ununuzi ambazo taratibu zake zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na uhakiki wa maeneo ya utawala yatakayoshiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2024, kuandaa rasimu ya Tangazo la Serikali la maeneo ya utawala, kuandaa rasimu ya Kanuni za Uchaguzi na kufanya vikao vya wadau wa ndani ya Serikali ili kupata maoni na kuyajumuisha katika rasimu ya kanuni zilizoandaliwa. Aidha, rasimu ya kanuni hizo zitapitiwa na wadau

wa nje ili kupata maoni yao kabla ya kuidhinishwa na kuanza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, uratibu na usimamizi wa huduma za afya ya msingi, ustawi wa jamii na lishe; Ofisi ya Rais, TAMISEMI inasimamia vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi 6,933 ambapo zahanati ni 5,887, vituo vya afya 874 na hospitali za halmashauri 172. Takwimu hizi zinaonesha kuna ongezeko la vituo vya afya ya msingi 1,663 ikilinganishwa na idadi ya vituo 5,270 vilivyokuwepo mwaka 2015 wakati wa mkakati wa kuboresha na kuanza ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mabadiliko ya utoaji wa huduma za afya ya msingi na mahudhurio ya wagonjwa. Mwaka 2023 wagonjwa milioni 26...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri dakika moja.

Waheshimiwa Wabunge, ninampisha Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri endelea. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mabadiliko ya utoaji wa huduma za afya ya msingi na mahudhurio ya wagonjwa. Mwaka 2023 wagonjwa milioni 26.9 walipatiwa huduma katika vituo vya afya ya msingi kama wagonjwa wa nje *(OPD)* na wagonjwa 854,318 walipatiwa huduma ya kulazwa. Katika eneo la mama na mtoto jumla ya akina mama milioni 1.6 walijifungua katika vituo vya kutolea huduma ya afya ya msingi na akina mama 125,318 waliokuwa na uzazi pingamizi walifanyiwa upasuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024 ziliidhinishwa shilingi bilioni 258.48 kupitia ruzuku ya Serikali Kuu, mapato ya ndani na washirika wa maendeleo kwa ajili ya

utekelezaji wa shughuli za afya ya msingi, ustawi wa jamii na lishe. Hadi Machi, 2024 shilingi bilioni 253.67 zimepokelewa sawa na 98.14% ya fedha iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zilizotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa majengo ya hospitali 45. Ukarabati wa hospitali kongwe 30, ujenzi wa vituo vya afya vituo vya afya 14, ukamilishaji wa vituo vya afya 23, ukamilishaji wa maboma ya zahanati 374 na ununuzi wa vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya vilivyokamilika ambavyo ni zahanati 364, vituo vya afya 278 na hospitali za halmashauri 31 ili huduma zianze kutolewa. Shughuli nyingine zilizotekelezwa katika afya ya msingi zimeoneshwa katika aya ya 54 hadi 63 ya hotuba yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi na uendeshaji wa elimu ya msingi na sekondari. Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaratibu usimamizi na uendeshaji wa elimu ya awali, msingi na sekondari nchini kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa. Takwimu za idadi za shule na hali ya uandikishaji zimeelezwa kwa kina katika aya ya 66 hadi ya 68 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika sekta ya elimu; Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendelea kusimamia utoaji wa huduma ya elimu msingi na sekondari ambapo katika mwaka 2023/2024 iliidhinishwa shilingi trilioni 1.72 kupitia ruzuku ya Serikali Kuu na washirika wa maendeleo. Hadi Machi, 2024 shilingi trilioni 1.26 zimepokelewa sawa na 73.45% ya fedha iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya mpango wa elimu msingi bila ada kwa shule za msingi na sekondari nchini imeleta mafanikio makubwa, ikiwa ni pamoja na ongezeko la wanafunzi wapya wanaoandikishwa kujiunga katika ngazi mbalimbali za elimu. Idadi ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza imeongezeka kutoka wanafunzi 425,743 mwaka 2016 mpango wa elimu msingi bila ada ulipoanza hadi wanafunzi 1,076,037 mwaka 2024 sawa na ongezeko la 152.74%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejidhatiti kutekeleza maelekezo ya Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 kwa kuendeleza utoaji wa elimu bila ada ili kuhakikisha wanafunzi wote wenye umri wa kwenda shule wanakwenda shule. Napenda kunukuu maneno ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliyoyasema mwaka 1966 kuhusu umuhimu wa Serikali kugharamia elimu. Baba wa Taifa alisema; "Taifa husomesha watu wake kwa faida ya Taifa lake." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwa kutambua hilo, hadi kufikia Machi, 2024 imetoa shilingi trilioni 2.31 ili kutekeleza mpango wa elimu msingi bila ada ikiwa ni ruzuku tangu kuanza utekelezaji wa mpango huo Disemba, 2015. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 758.81 zimetolewa katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Sera ya Elimu; Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeweka mpango wa kuanza kutekeleza maboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 Toleo la mwaka 2023 na kukubaliana kujenga shule za sekondari za amali 100. Aidha, katika mwaka 2023/2024 Serikali itajenga shule za amali 26 ili zianze kupokea wanafunzi ifikapo Januari, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari za mafuriko katika miundombinu ya shule; kwa kuzingatia kuwa baadhi ya mikoa imekumbwa na janga la mafuriko ambayo imeathiri miundombinu ya shule pamoja na mambo mengine na kuzuia wanafunzi kuendelea na masomo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia tumeelekeza ifanywe tathmini ya haraka ya athari zilizopatikana ili kuja na mkakati wa muda mfupi na mkakati wa muda mrefu ili kuwezesha wanafunzi warejee, kuendelea na masomo hususan wale ambao wapo kwenye madarasa ya mitihani ili waendelee na masomo yao na wafanye mitihani yao bila kuathirika. Taarifa ya tathmini itawasilishwa Serikalini kwa ajili ya maamuzi ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu ya shule; Serikali inaendelea na ujenzi wa shule mpya za msingi 302, vyumba vya madarasa 3,880, mabweni 63 ya wanafunzi wenye mahitaji maalum, matundu ya vyoo 22,418 na uzio wa mabweni katika shule 88, ukarabati wa madarasa 627 katika shule kongwe za msingi na ukamilishaji wa mabweni saba na bwalo moja. Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi wa shule mpya 25 za sekondari, madarasa 6,648, mabweni 444 na matundu ya vyoo 16,795 katika shule za sekondari. Pia Serikali imefanya ukarabati wa shule 32, umaliziaji wa maboma ya madarasa 2,441, shule za bweni tisa, maabara 132 na matundu ya vyoo 1,650. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Serikali za Mitaa; Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia Chuo cha Serikali za Mitaa kimeanzisha Kampasi ya Shinyanga ambapo jumla ya wanafunzi 167 wamedahiliwa na kuanza mafunzo kwa kozi nne za Astashahada ya Maendeleo ya Jamii na Utawala katika Serikali za Mitaa, Uhasibu na Fedha na Menejimenti ya Rasilimali Watu. Hivyo, naomba kutoa wito kwa wanafunzi waliohitimu kidato cha nne na kidato cha sita kujiunga kwenye mkupuo wa Machi na Oktoba kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Elimu Kibaha; Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia Shirika la Elimu Kibaha limeandaa mfumo wa mafunzo kwa njia ya mtandao *(e-learning management system)* kwa ajili ya kutoa elimu ya sekondari mubashara *(live teaching)* kwa shule za sekondari ili kukabiliana na upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi na hisabati. Hadi Machi, 2024 ujenzi wa mfumo unaendelea na majaribio ya kutoa elimu ya sekondari mubashara yamefanyika katika Shule za Sekondari za Kibaha na Dodoma, matarajio ni kuzifikia shule zote za sekondari hususan katika masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora, usimamizi wa rasilimali, ujenzi wa majengo ya utawala na makazi ya viongozi, utatuzi wa kero za wananchi katika Mikoa na Wilaya; Hayati Baba wa Taifa aliwahi kusema hakuna shida yoyote ya watu ambayo

tunaweza sema kuwa haituhusu. Maneno haya aliyasema Baba wa Taifa mwaka 1962 pale Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea kuyaenzi maneno hayo ambapo mwaka 2023/2024 viongozi wa Mikoa, Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri wamesikliza na kutatua kero za wananchi. Hadi Machi, 2024 jumla ya kero 16,938 zimepokelewa na kusikilizwa ambapo kero 7,322 zimetatuliwa na kero 9,616 zipo katika hatua mbalimbali za utatuzi. Aidha, kero hizo zipo katika sekta mbalimbali zikiwemo utawala, afya, elimu, ardhi, maji, barabara na nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa rasilimali watu; katika mwaka 2023/2024 Maafisa Tarafa 63 kati ya nafasi wazi 88 wameajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi. Aidha, katika kuboresha utendaji kazi, umefanyika msawazo wa watumishi wa Halmashauri zilizokuwa na watumishi wengi na kuwahamishia halmashauri zenye upungufu wa watumishi ambapo watumishi 646 walihamishwa. Vilevile Ofisi ya Rais, TAMISEMI inakamilisha taratibu za kuajiri Watendaji wa Kata 525, Watendaji wa Vijiji 1,986, Watendaji wa Mitaa 1,333 na Maafisa Tarafa 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, "Ubadhirifu Serikalini unarudisha maendeleo ya wananchi" maneno haya siyo ya kwangu, aliyasema Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mwaka 1977 miaka kumi baada ya Azimio la Arusha. Hivyo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, imeendelea kuchukua hatua kwa watumishi wanaotekeleza majukumu yao kinyume na sheria, taratibu na kanuni. Katika mwaka 2023/2024 watumishi 225 wamechukuliwa hatua za kinidhamu, kati yao Wakurugenzi ni 13, Wakuu wa Idara 30, watumishi wa sekta ya ujenzi 15, sekta ya afya nane na 159 wa kada nyingine. Aidha, Ofisi ya Rais, TAMISEMI itaendelea kuchukua hatua kwa wakati pale inapobaini ubadhirifu na uvunjifu wa maadaili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezeshaji wa ngazi za msingi za Mamlaka za Serikali za Mitaa; katika kutekeleza Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kwa Wananchi, Serikali imeendelea kuboresha utendaji kazi katika ngazi za msingi ili kuimarisha utawala bora,

maendeleo endelevu na ushiriki wa wananchi katika maamuzi yanayogusa maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu huo, Serikali katika mwaka 2023/2024 ilitenga shilingi bilioni 1.73 za matumizi mengineyo kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya posho ya mawasiliano kwa wenyeviti wa vijiji na mitaa. Hadi Machi, 2024 shilingi bilioni 1.15 zimetolewa sawa na asilimia 67 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya posho ya mawasiliano katika Halmashauri 165 ambazo mapato yake ni chini ya shilingi bilioni tano.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Chuo cha Utumishi wa Umma na Chuo cha Serikali za Mitaa imetoa mafunzo kwa maafisa tarafa 184 na watendaji wa kata 1,403 katika mikoa tisa ya Pwani, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga na Kigoma. Aidha, katika mwaka 2022/2023 Mikoa minne ya Rukwa, Katavi, Songwe na Njombe ilipata mafunzo kwa Maafisa Tarafa 56 na Watendaji wa Kata 356. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI itaendelea na utoaji wa mafunzo katika Mikoa mitano ya Simiyu, Mara, Mwanza, Geita na Kagera kufikia mwishoni mwa Aprili, 2024 ambapo Maafisa Tarafa 108 na Watendaji wa Kata 816 wanatarajiwa kushiriki na hivyo kufikisha mikoa 18 itakayokuwa imepatiwa mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa majengo ya utawala na makazi ya viongozi; katika mwaka 2023/2024 shilingi bilioni 171.34 ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa 16, ukarabati wa Ofisi za Wakuu wa Wilaya 22, Ikulu Ndogo nane, Ofisi za Maafisa Tarafa 19, nyumba 11 za Wakuu wa Mikoa, nyumba sita za Makatibu Tawala wa Mikoa, nyumba za Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mikoa tano, nyumba za Wakuu wa Wilaya 13, nyumba za Makatibu Tawala wa Wilaya nne, nyumba za Maafisa Tarafa 21, ujenzi wa majengo ya utawala katika Halmashauri 72, nyumba 39 za Wakurugenzi, nyumba 25 za Wakuu wa Idara wa Halmashauri, pamoja na

ununuzi wa samani za majengo ya utawala katika halmashauri 50. Utekelezaji wa shughuli za ujenzi, ukarabati wa majengo ya utawala na makazi ya viongozi katika Mikoa, Wilaya na Halmashauri umeainishwa katika aya ya 98 mpaka 99 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ununuzi wa mitambo, magari na pikipiki; katika kuhakikisha utekelezaji wa miradi na shughuli za maendeleo zinafanyika na kufuatiliwa kwa karibu, Serikali imeendelea kuwezesha upatikanaji wa magari ambapo hadi Machi, 2024 jumla ya magari 796 yamenunuliwa na kusambazwa katika taasisi, mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya magari hayo, 316 ni kwa ajili ya kubebea wagonjwa *(ambulance)* ambayo tulikabidhi kwa Waheshimiwa Wabunge, magari 212 kwa ajili ya usimamizi wa huduma za afya ya msingi, lishe na ustawi wa jamii katika Halmashauri 184, Mikoa 26 na Makao Makuu magari mawili, magari 134 kwa ajili ya usimamizi na uratibu wa shughuli za elimu, magari 18 kwa ajili ya usimamizi wa miundombinu ya barabara inayosimamiwa na *TARURA*, magari 83 ni kwa ajili ya viongozi wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na magari 26 kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo katika ngazi ya Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, magari saba na mitambo miwili ya barabara yamenunuliwa kutokana na fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli za maendeleo na kufungua barabara mtawalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuimarisha usimamizi, utoaji wa huduma na utatuzi wa kero za wananchi katika ngazi za msingi kwa kununua pikipiki 449 ambapo pikipiki 105 zimesambazwa kwa Watendaji wa Kata na pikipiki 344 zinakamilishwa usajili na zitasambazwa kwa Maafisa Afya wa Kata 110 na Watendaji wa Kata 234. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya barabara na usafirishaji; Ibara 57(c) mpaka (d)

ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 inaelekeza kuongeza kiwango cha barabara za changarawe kutoka kilometa 24,493 hadi kilometa 35,000 na kuongeza urefu wa barabara za vijijini na mijini zilizojengwa kwa kiwango cha lami kutoka kilometa 2,025 hadi kilometa 3,100 ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Machi, 2024 urefu wa barabara za changarawe umeongezeka kutoka kilometa 24,493 hadi kilometa 41,107.52 sawa na asilimia 17.45 ya lengo. Aidha, urefu wa barabara za vijijini na mijini zilizojengwa kwa kiwango cha lami umeongezeka kutoka kilometa 2,025 hadi kilometa 3,224.12 sawa na ongezeko la asilimia nne ya lengo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024 sekta ya miundombinu ya barabara na usafirishaji iliidhinishiwa shilingi bilioni 825.09 kwa ajili ya ujenzi, ukarabati, matengenezo ya barabara na usafirishaji kupitia Mfuko wa Barabara, tozo ya mafuta, Mfuko Mkuu wa Serikali na mashirika ya maendeleo. Hadi mwezi Machi, 2024 shilingi bilioni 682.60 zimetolewa kwa ajili ya miundombinu ya barabara na usafirishaji, sawa na asilimia 82.73 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kunukuu maneno ya Hayati Benjamin William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu kuhusu umuhimu wa barabara za vijijini ambapo alisema; "Njia moja ya kuharakisha maendeleo ya vijijini ni kuhakikisha tunajenga na kuboresha barabara za vijijini. Barabara ni kiungo muhimu katika kuunganisha vijiji na huduma za kijamii kama shule, vituo vya afya na masoko. Pia barabara zinawezesha upatikanaji wa bidhaa za wakulima kwenye masoko na kuchochea biashara na ukuaji wa uchumi wa vijiji. Hivyo, tusipuuze umuhimu wa barabara za vijijini katika juhudi za kuendeleza maeneo ya vijijini." Haya ni maneno ya Hayati Benjamin William Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita kwa kulitambua hilo, imeendelea kuyaenzi maneno haya ya Rais wa Awamu ya Tatu kwa kuendelea kutoa fedha kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini za ujenzi, matengenezo na ukarabati

wa barabara kutoka shilingi bilioni 275 mwaka 2021/2022 hadi kufikia shilingi bilioni 722.19 sawa na ongezeko la asilimia 163.44 mwaka 2023/2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili la fedha limewezesha kujenga barabara za lami kilometa 1,216.65; barabara za changarawe kilometa 17,125.2; na madaraja 2,355. Kutokana na ongezeko la fedha, kazi zimeongezeka ambapo makandarasi wa ndani wamenufaika na ongezeko hilo la fedha, hivyo wastani wa mikataba 844 ya kazi za barabara imeongezeka na kufikia wastani wa mikataba 1,826.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kupitia *TARURA* iliidhinishiwa shilingi bilioni 21 kwa ajili ya kazi za dharura ambapo hadi mwezi Machi, 2024 shilingi bilioni 50.43 zimepokelewa sawa na asilimia 240.14 kutokana na ongezeko la dharura lililosababishwa na mvua nyingi. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kurekebisha barabara zenye urefu wa kilometa 129.13, ujenzi wa madaraja 20, ujenzi wa kalavati 95, ujenzi wa mifereji ya kuondoa maji barabarani mita 6,260 na uwekaji wa changarawe kwenye maeneo ambayo barabara zilikatika na kurudisha mawasiliano kwa wananchi. Aidha, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutoa fedha ili kurejesha hali ya barabara za vijijini na mijini ambazo zimeathiriwa na mvua za msimu huu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia *DART* inaendelea kukamilisha utengenezaji na usimikaji wa mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji nauli ambao utafungamanishwa na mfumo wa kuongoza magari ikiwa ni sehemu ya maboresho endelevu ya huduma hii kwa wananchi waishio mijini, pia kuondoa mianya ya upotevu wa mapato yatokanayo na nauli. Aidha, kazi zinazoendelea kwa sasa ni usimikaji wa mageti janja. Vilevile Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia *DART* inaendelea na kazi ya kumtafuta mbia wa uendeshaji wa mradi wa mabasi yaendayo haraka Awamu ya Kwanza. Aidha, shughuli nyingine zinazotekelezwa zimeoneshwa katika aya ya 111 hadi 121 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa mifumo ya TEHAMA; katika kutekeleza agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na maelekezo ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la upunguzaji na uunganishwaji wa mifumo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeunganisha mifumo yake na mifumo mingine ya Serikali na ya sekta binafsi ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati, kudhibiti upotevu wa mapato na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imesanifu na kujenga Mfumo wa *Wezesha Portal* utakaotumika kukopesha mikopo ya asilimia kumi. Matumizi ya mfumo huu yatasaidia kuondoa changamoto zilizokuwepo awali ikiwa ni pamoja na kuondoa vikundi hewa, watu kujisajili zaidi ya kikundi kimoja, wakopaji hewa, kuimarisha usimamizi, usajili wa vikundi, utoaji na urejeshaji wa mikopo na upatikanaji wa taarifa sahihi za mikopo kwa wakati ili kuongeza tija, kuondoa upendeleo na kuongeza uwazi na uwajibikaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, mikopo itokanayo na asilimia 10 ya mapato yasiyolindwa ya Mamlaka za Serikali za Mitaa; katika mwaka 2023/2024 Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendelea kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga fedha kwa ajili ya mikopo itokanayo na asilimia kumi ya mapato ya ndani ya halmashauri yasiyolindwa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Tangu mikopo hiyo ilipositishwa mwezi Aprili, 2023 hadi Machi, 2024 fedha iliyopo kwenye akaunti za halmashauri ni shilingi bilioni 63.24. Aidha, fedha za marejesho ya mikopo zilizopo kwenye akaunti husika kwa kipindi hicho ni shilingi bilioni 63.67.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya tabianchi na biashara ya *carbon;* ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi duniani, Umoja wa Mataifa ulianzisha Itifaki ya Kyoto mwaka 1997 inayozitaka nchi zinazoendelea kupunguza gesijoto kwa asilimia tano. Njia mojawapo ya kupunguza gesijoto ni kuanzisha biashara ya *carbon* katika nchi zinazoendelea ambapo nchini Tanzania biashara hiyo kwa ngazi ya Mamlaka za Serikali za

Mitaa ilianza kuchipua rasmi mwaka 2018. Hadi Machi, 2024 halmashauri 15 zimeingia katika uendeshaji wa biashara ya *carbon*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Machi, 2024 mapato yatokanayo na uuzaji wa *carbon* yamefikia dola za Marekani 12,630,350 sawa na shilingi bilioni 30. Aidha, utekelezaji wa biashara ya *carbon* umeainishwa katika aya ya 137 hadi 142 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji vijiji na miji; Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeandaa na kusambaza Mwongozo wa Utekelezaji wa Mipango Kabambe *(master plan)* na Mwongozo wa Kukusanya, Kuchakata na Kuwasilisha Taarifa za Kijiografia za sekta mbalimbali zilizopo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutumia mfumo wa taarifa za kijiografia. Aidha, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilizijengea uwezo wa utekelezaji wa miongozo hiyo timu za menejimenti za halmashauri 56 kwenye mikoa 12 ikiwemo uandaaji wa mpango kabambe jumuishi *(master plan)* wa uendelezaji wa jiji la biashara la uwekezaji la Kwala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Utumishi wa Walimu; hadi mwezi Machi, 2024 Tume ya Utumishi wa Walimu imeendelea kuhudumia walimu 273,021 wa shule za msingi na sekondari waliopo katika utumishi wa umma. Kati yao walimu wa shule za msingi ni 181,149 na sekondari ni 91,872. Usajili wa walimu 13,130 walioajiriwa mwezi Juni, 2023 ulifanyika, ambapo walimu 13,130 wamepatiwa namba za usajili wakiwemo walimu 7,801 wa shule za msingi na walimu 5,329 wa shule za sekondari. Aidha, madai 65 ya walimu kuhusu mafao ya pensheni, mirathi na mikataba yalipokelewa na kushughulikiwa ambapo 25 yalihusu mirathi, 29 yalihusu mikataba na 11 yalihusu mafao ya pensheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Machi, 2024 Tume imeshughulikia masuala ya maadili na nidhamu kwa walimu ambapo rufaa 79 za walimu zimepokelewa na kuchambuliwa, mashauri ya nidhamu 316 ya walimu yamepokelewa ngazi ya wilaya. Aidha, nyaraka kwa ajili ya rufaa 43 zilizokatwa na walimu ziliandaliwa na kuwasilishwa kwenye mamlaka husika kwa mujibu wa sheria. Vilevile Tume inaendelea na ujenzi wa Ofisi ya Tume

Makao Makuu ambapo hadi mwezi Machi, 2024 ujenzi umefikia asilimia 37. Shughuli nyingine zimeoneshwa katika aya ya 151 – 153 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhtasari wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2024/2025; vipaumbele vya Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2024/2025; vipaumbele vya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Halmashauri vimeainishwa katika aya ya 151 hadi aya ya 154 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya maduhuli na mapato ya ndani ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI mwaka 2024/2025; katika mwaka 2024/2025 mafungu 28 ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI yanakadiriwa kukusanya maduhuli na mapato ya ndani ya shilingi trilioni 1.60 ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.14 iliyoidhinishwa mwaka 2023/2024 ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 456.89 sawa na asilimia 39.93. Mapato haya yanajumuisha shilingi bilioni 188.96 ya makisio ya kodi ya majengo ambayo yatakusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizopewa uwakala wa kukusanya kodi hiyo na kuwasilisha makusanyo hayo katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zilizotekelezwa kupitia fedha za mapato ya ndani ya halmashauri; katika mwaka 2024/2025 Ofisi ya Rais, TAMISEMI, imepanga kutumia shilingi bilioni 541.27 ya mapato ya ndani ya halmashauri. Maelezo ya kina ya shugjhuli zitakazotekelezwa yameainishwa katika aya ya 161 hadi 162 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya mapato na matumizi ya kawaida na maendeleo ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka 2024/2025; katika mwaka 2024/2025 Mafungu 28 ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI yamepanga kutumia shilingi trilioni 10.12 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Mchanganuo wa kina umeoneshwa kwenye Jedwali Namba 02.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI mwaka 2024/2025; Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2024; katika mwaka 2024/2025 Ofisi ya Rais, TAMISEMI imetenga shilingi bilioni 17.79 kwa ajili ya kuratibu na

kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024, kati ya fedha hizo shilingi bilioni nane ni fedha kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya uratibu katika ngazi ya Makao Makuu (Fungu 56) na shilingi bilioni 9.79 ni mchango wa halmashauri kupitia mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uratibu na usimamizi wa Huduma za afya ya msingi, ustawi wa jamii na lishe; katika mwaka 2024/2025, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imepanga kutumia shilingi bilioni 357.85 za ruzuku ya fedha za maendeleo za Serikali Kuu na washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zitakazotekelezwa kupitia fedha za ndani za maendeleo katika ngazi za halmashauri, ni pamoja na:-

(i) Ukamilishaji wa hospitali za halmashauri 118;

(ii) Ukamilishaji wa vituo vya afya kumi;

(iii) Ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali za halmashauri 136, vituo vya afya 44 na zahanati 386; na

(iv) Ujenzi wa miundombinu ya maji na vyoo katika vituo vya kutolea huduma za afya katika halmashauri 117.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha shughuli nyingine zitakazotekelezwa zimeainishwa katika aya ya 164 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi na uendelezaji wa elimu msingi na sekondari; katika mwaka 2024/2025 Ofisi ya Rais, TAMISEMI imepanga kutumia shilingi trilioni 1.02 kupitia ruzuku ya Serikali Kuu na washirika wa maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli katika sekta ya elimu msingi na sekondari. Aidha, shughuli zitakazotekelezwa zimeainishwa katika aya ya 166 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora, usimamizi wa rasilimali, ujenzi wa majengo ya utawala na makazi ya viongozi;

katika mwaka 2024/2025 Ofisi ya Rais, TAMISEMI imepanga kutumia shilingi bilioni 190.57 kwa ajili ya ununuzi wa magari ya viongozi wa mikoa na wilaya, kuendelea na ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa miundombinu ya mikoa ikiwemo; majengo ya utawala, Ikulu Ndogo, makazi ya viongozi na watumishi wa mikoa, wilaya na tarafa katika mikoa 26. Aidha, katika shughuli zitakazotekelezwa katika utawala bora, usimamizi wa rasilimali, ujenzi wa majengo ya utawala na makazi ya viongozi, zimeainishwa katika aya ya 168 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezeshaji wananchi kiuchumi (usimamizi wa mikopo ya asilimia kumi; naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kurejesha utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuanzia mwezi Julai, 2024 kwa kutumia utaratibu wa benki katika halmashauri kumi za majaribio ambazo ni majiji mawili, manispaa mbili, miji miwili na halmashauri za wilaya nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri 174 zilizobaki zitatumia mfumo wa Serikali baada ya maboresho yafuatayo: -

(i) Kuanzisha kitengo cha usimamizi wa mikopo katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI;

(ii) Kuundwa kwa kamati ya usimamizi wa mikopo katika ngazi za Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Halmashauri na Kata;

(iii) Kurekebisha sheria inayosimamia mikopo na kanuni zake; na

(iv) Kujenga uwezo kwa wasimamizi wa mikopo na kuongeza idadi ya wasimamizi wa mikopo kwenye ngazi ya kata ambapo hadi sasa Maafisa Maendeleo ya Jamii 787 wameajiriwa na kupangiwa kwenye kata zilizokuwa na upungufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI itaendelea kuzisimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kukusanya marejesho kutoka katika vikundi vilivyokopeshwa fedha za asilimia kumi ambapo shilingi bilioni 43.77 zitakusanywa katika vikundi vinavyoendelea kufanya marejesho. Mikopo hiyo itasimamiwa kwa umakini kuhakikisha hakuna kikundi hewa na yeyote atakayepatikana na ubadhirifu wa aina yoyote atachukuliwa hatua. Kama waungwana wasemavyo; "Akopaye akilipa huondokana na lawama." Hivyo, napenda kuwaelekeza Wakuu wa Mikoa kusimamia mikopo hiyo kwa umakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya ukusanyaji mapato; katika kuhakikisha kuwa mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yanakusanywa kwa ufanisi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI itaendelea kutekeleza mikakati iliyoainishwa katika aya ya 173 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi, ukarabati na utengenezaji wa miundombinu ya barabara, usafiri na usafirishaji; katika mwaka wa fedha 2024/2025 Ofisi ya Rais, TAMISEMI imepanga kutumia shilingi bilioni 841.19 kwa ajili ya ujenzi, matengenezo na ukarabati wa miundombinu ya barabara, usafiri na usafirishaji wa vijijini na mijini. Shughuli zitakazotekelezwa ni matengenezo wa barabara za vijijini na mijini zenye urefu wa kilometa 20,745.31; ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilometa 434.50; ujenzi wa barabara za changarawe zenye urefu wa kilometa 13,802.34; ujenzi wa madaraja 160 na ukarabati wa madaraja 21; ujenzi na matengenezo ya boksi kalvati 586 na vivuko 15; na ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa mita 141,070.54. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli nyingine zitakazotekelezwa kupitia miradi ya kuboresha miundombinu shindanishi katika miiji ya Tanzania *(TACTIC)*; programu ya kuongeza fursa za kiuchumi na kijamii nchini *(RISE);* miradi ya uendelezaji wa Bonde la Mto Msimbazi na miradi ya uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam awamu ya pili. Aidha, ukamilishaji wa utaratibu wa ununuzi wa mbia wa uendeshaji wa miradi wa mabasi yaendayo haraka awamu ya kwanza na ya pili; na kukamilisha Sheria ya Usafiri wa Umma na kuhuisha *DART* kuwa mamlaka ambapo shughuli

zitakazotekelezwa zimeainishwa katika aya ya 182 hadi aya ya 184 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa vijiji na miji; katika mwaka 2024/2025 Ofisi ya Rais, TAMISEMI itaendelea na uratibu wa utekelezaji wa Miradi ya *Green and Smart Cities* katika Halmashauri za majaribio ya Jiji la Tanga natambua Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Tanga yuko hapa na ananisikia, Mwanza na Manispaa ya Ilemela. Aidha, shughuli zitakazotekelezwa ni ujenzi wa masoko ya milango ya chuma, Mgandini na Samaki Kasera katika Jiji la Tanga; ujenzi wa Soko la Buhongwa, Ujenzi wa machinjio Nyakato katika Jiji la Mwanza na ujenzi wa masoko ya Buswelu, Mwaloni na Igombe katika halmashauri ya Manispaa ya Ilemela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Masoko Kariakoo; katika mwaka 2024/2025 Shirika la Masoko ya Kariakoo litaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Masoko ya Kariakoo Sura ya 36. Aidha, shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kurejesha huduma za biashara katika kuweka mpangilio mzuri wa biashara ili kuwarahisishia wateja kupata huduma wanazohitaji na kuboresha mazingira ya kufanyia biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Serikali za Mitaa, Shirika la Elimu Kibaha na Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa; shughuli za taaisi hizi zinapatikana katika aya ya 190 hadi aya ya 192 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2); katika mwaka 2024/2025 Tume ya Utumishi wa Walimu imepanga kutumia shilingi bilioni 20.74 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo katika maeneo yafuatayo: -

(i) Kusimamia ajira, maadili na maendeleo ya walimu kwa kuhakikisha kwamba walimu wanasajiliwa, wanathibitishwa kazini na kwa wale wenye sifa wanapandishwa vyeo na kubadilishiwa kada kwa wakati;

(ii) Kusimamia maadili na nidhamu kwa walimu wa shule za msingi na sekondari katika utumishi wa umma;

(iii) Kufanya utafiti na kutathmini hali ya walimu nchini;

(iv) Kukamilisha utengenezaji wa Mfumo wa *TSCMIS*, usimikaji wa miundombinu ya mtandao wa *internet* katika ofisi 115 za wilaya; na

(v) Kuendelea na ujenzi wa jengo la Ofisi ya Tume Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwajibikaji wa Makampuni ya Jamii *(Cooperate Social Responsibilities - CSR);* Ofisi ya Rais, TAMISEMI itasimamia utekelezaji wa miradi inayotekelezwa kwa kutumia fedha za uwajibikaji wa makampuni ya jamii ili kuhakikisha miradi inayotekelezwa inazingatia thamani ya fedha na miongozo ya matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeteua kamati ya kuandaa mwongozo wa namna ya kupokea fedha kutoka kwenye makampuni yanayotakiwa kutoa *CSR*, uwekaji wa vipaumbele na matumizi ya fedha zinazotokana na makampuni ya uwajibikaji kwa jamii katika maeneo ambayo hayaguswi na sheria na kanuni za utekelezaji wa *CSR* kama ilivyo katika sekta ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa upande wa Jiji la Dodoma, ninamshukuru Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa ambaye amechukua hatua za ufuatiliaji wa namna ya miradi inayotekelezwa kwa fedha za Uwajibikaji wa Makampuni kwa Jamii kupitia miradi ya ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje *(ring road)* ili kuhakikisha miradi hiyo inakuwa na thamani ya fedha na inafuata miongozo ya utekelezaji wa ujenzi iliyowekwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeeleza utekelezaji wa mpango wa bajeti ya mwaka 2023/2024 na kuainisha mpango wa bajeti kwa mwaka 2024/2025 kwa Mafungu 28 ambao umechangiwa na fedha kutoka Serikali Kuu, Mamlaka

za Serikali za Mitaa na Washirika wa Maendeleo wakiwemo Benki ya Dunia, Benki ya *NMB, CRDB, AZANIA,* na *DCB; UNICEF, Global Fund,* Twiga, *Barick Tanzania, European Union, JICA, KOICA, GiZ, UNCDF, CDC, USAID, SIDA, UNDP, UNFPA, UN Women, Carbon Tanzania, UNEP, WHO, AfDB, WWF, FCDO, DANIDA, CANADA, SDC SWISS,* Serikali ya Shirikisho la Ujerumani, *The Nature Conservance, Global Facility Financing* na *GAVI*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu naomba nitumie fursa hii kutoa maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kusimamia kwa umakini utekelezaji wa mpango wa bajeti kama ifuatavyo:-

(i) Kuhakikisha mnashiriki pamoja na timu ya kufanya tathimini ya athari ya mafuriko zilizoharibu miundombinu ya shule ili kuandaa mikakati ya muda mfupi na mikakati ya muda mrefu na kuwezesha wananfunzi warejee kuendelea na masomo, hususan wale ambao wapo kwenye madarasa ya mitihani ili waendelee na masomo na kufanya mitihani bila kuathirika;

(ii) Kusimamia fedha zote za Uwajibikaji wa Makampuni kwa Jamii *(CSR)* ili kuhakikisha zinatumika kulingana na miongozo ya matumizi ya fedha za umma na miradi husika kuwa na thamani ya fedha. Aidha, ninaelekeza kupata taarifa ifikapo tarehe 16 Mei, 2024 ya miradi yote inayoendelea kutekelezwa kwa fedha za Uwajibikaji wa Makampuni kwa Jamii;

(iii) Kuhakikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa zinasogeza huduma karibu kwa wananchi kwa kuanzisha kanda ya kulipia kodi;

(iv) Kuhakikisha ukusanyaji wa mapato uliolengwa unafikiwa kwa asilimia 100, ukiwemo ukusanyaji wa kodi ya majengo;

(v) Mikopo ya asilimia kumi iliyorejeshwa kwa ajili ya kukopeshwa vikundi vya wananwake, vijana na wenye

ulemavu, iliyoelekezwa kutolewa kuanzia mwezi Julai, 2024 inasimamiwa ipasavyo na kuhakikisha wanaokopeshwa si vikundi hewa na kusimamiwa marejesho yake;

(vi) Kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024 ili ufanyike kwa amani na utulivu;

(vii) Kukamilisha ujenzi wa miundombinu iliyopangwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwemo ukamilishaji wa vituo vya polisi ngazi ya kata, kutenga maeneo kwa ajili ya kujenga shule za maadilisho zitakazojengwa katika kila mkoa shule moja;

(viii) Kuhakikisha halmashauri zinazodaiwa mikopo ya michango kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa zinarejesha kwa wakati;

(ix) Kuhakikisha maagizo yote yanayotolewa na Kamati za Kudumu za Bunge yanatekelezwa kwa wakati;

(x) Halmashauri kuongeza kasi ya urejeshaji mikopo iliyokopeshwa kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi badala ya fedha hizo kutumika katika shughuli nyingine;

(xi) Nawaelekeza watendaji wa *TARURA*, Mameneja wa Mikoa na Wilaya kufanya tathimini ya kina ya athari ya mafuriko ili Serikali iweze kuchukua hatua madhubuti ya kurejesha miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko nchi nzima; *(Makofi)*

(xii) Kuhakikisha biashara ya *carbon* inaanzishwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kujifunza kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika pamoja na Halmashauri 14 ambazo zimeanzisha biashara hiyo; na

(xiii) Kusimamia kikamilifu matumizi sahihi ya fedha za umma na yeyote atakayebainika kufanya ubadhirifu atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongezee hapo kuhusu mikopo ya asilimia kumi, tumekwishatoa maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Kiongozi yeyote wa mkoa na wilaya ambaye atafanya uzembe kuwepo kwa vikundi hewa atalazimika kuwajibika. Kiongozi yeyote wa mkoa ambaye atasababisha uwepo wa vikundi hewa katika eneo lake la utawala atalazimika kuwajibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitaishukuru familia yangu pamoja na wapiga kura wangu wa Jimbo la Rufiji, nitakuwa sina fadhila. Hivyo, kipekee naishukuru kwa dhati familia yangu kwa upendo wao, uvumilivu na maombi yao katika wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yangu ya kitaifa. Nawashukuru kwa kusimama nami katika safari hii ya kuleta maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Rufiji kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya Kitaifa na Jimbo na kuniombea kila siku. Ninaahidi kuendelea kuwatumikia kwa ushirikiano nao katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla. Pamoja na majanga yaliyowapata, niko pamoja nao bila kujali usiku wala mchana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Ofisi ya Rais, TAMISEMI, maduhuli na makusanyo ya mapato ya ndani; katika mwaka 2024/2025, Mafungu 28 ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI yanaomba idhini ya kukusanya maduhuli ya mapato ya ndani jumla ya shilingi 1,601,044,595,990. Mchanganuo wa makusanyo ya mapato hayo ni kama inavyooneshwa katika jedwali namba moja kwenye hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naliomba Bunge lako likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2024/2025 yenye jumla ya shilingi 10,125,220,403,167 kwa ajili ya Mafungu 28 ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Naomba nirejee, sasa ninaomba Bunge lako likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2024/2025 yenye jumla ya shilingi 10,125,220,403,167 kwa ajili ya Mafungu 28 ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha zinazoombwa, shilingi 6,709,975,188,500 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida yanayojumuisha mishahara shilingi 5,524,636,066,000 shilingi 1,185,339,122,500 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi 3,415,245,214,667 zinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo kati ya fedha hizo shilingi 2,269,830,464,000 ni fedha za ndani na shilingi 1,145,414,750,667 ni fedha za nje. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 umeoneshwa katika jedwali namba mbili kwenye hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii, yapo majedwali ambayo yamefafanua kwa kina makadirio na makusanyo ya mapato ya ndani ya halmashauri na mgawanyo wa mapato ya ndani yasiyolindwa kwenye miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida ambayo ni sehemu ya hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii inapatikana pia kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambayo ni *www.tamisemi.go.tz.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**16 APRILI, 2024**

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, MHE. MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2024/25 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Ofisi ya Rais - TAMISEMI) (Fungu Namba 56); Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Namba 02) na mafungu 26 ya mikoa, ikijumuisha halmashauri 184 kwa mwaka 2023/24. Aidha, ninaomba Bunge lako tukufu lijadili na kupitisha mpango wa utekelezaji, makadirio na matumizi ya fedha kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu na mafungu 26 ya mikoa ikijumuisha halmashuari 184 kwa mwaka 2024/25.

## 1.1 Shukrani na Pongezi

**2.** ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya afya njema na kutujalia ari na hamasa ya kutekeleza majukumu yetu ya kibunge kwa manufaa mapana ya wananchi wote wa Tanzania. Aidha, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama leo mbele ya Bunge lako Tukufu kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango, Makadirio na Matumizi ya Fedha za Serikali kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa heshima na unyenyekevu mkubwa nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa imani kubwa aliyokuwa nayo kwangu na kuniteua kuwa Waziri wa Nchi,

Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Pia ninampongeza kwa dhati kwa kutimiza miaka mitatu na siku 28 za uongozi wake uliotukuka na unaolenga kuleta maridhiano, mageuzi, ustahimilivu na kuendelea kujenga taifa letu la Tanzania.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutumia nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza viongozi wakuu wa nchi; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais na kuendelea kuimarisha ustawi wa watu wa taifa la Tanzania.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii pia, kukupongeza kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani, mwanamke wa tatu (3) kushika nafasi hiyo na wa kwanza kutoka Afrika. Pia, ninampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukusaidia kuendesha shughuli za Bunge. Vilevile, ninawapongeza Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama (Mb.), Jimbo la Madaba, Mheshimiwa Deo Mwanyika (Mb.), Jimbo la Njombe Mjini na Mheshimiwa Najma Giga (Mb.), wa Viti Maalum kwa umakini wao wa kuliongoza Bunge lako Tukufu.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Denis Lazaro Londo, Mwenyekiti wa Kamati na Mbunge wa Jimbo la Mikumi; Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Makamu Mwenyekiti na Mbunge wa Jimbo la Kilolo na wajumbe wa kamati kwa uchambuzi, ushauri na maelekezo katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa mchango unaotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Kamati ya Kudumu ya

Bunge ya Sheria Ndogo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji Mitaji ya Serikali (PIC) na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa kuhakikisha shughuli zinazotekelezwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI zinafanyika kwa ufanisi na weledi.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** namshukuru Mheshimiwa George Simbachawene (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji na Mheshimiwa George Mkuchika (Mb.) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – IKULU (Kazi Maalumu) pamoja na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete (Mb.) Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Vilevile ninamshukuru Bw. Juma Mkomi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Dkt. Tausi Kida Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji; Bw. Lawrence Mafuru, Katibu Mtendaji Tume ya Mipango; na Bw. Xavier Daudi Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano wao mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi yetu.

**9.** **Mheshimiwa Spika,** natambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu, wakiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, Naibu Waziri anayeshughulikia afya na Mbunge wa Jimbo la Wanging'ombe na Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, Naibu Waziri anayeshughulikia elimu na Mbunge wa Viti Maalum. Aidha, natumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, aliyekuwa Naibu Waziri anayeshughulikia elimu Ofisi ya Rais – TAMISEMI ambaye ameteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) kwa ushirikiano mkubwa aliokuwa ananipa wakati wote alipokuwa akitekeleza majukumu yake. Ninamtakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yake mapya.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutumia nafasi hii kuwashukuru wataalamu wote wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI wakiongozwa na Ndg. Adolf Ndunguru, Katibu Mkuu; Naibu Makatibu Wakuu Dkt. Charles Msonde (Elimu), Dkt. Wilson Charles (Afya), Ndg. Sospeter Mtwale

(TAMISEMI), Mhandisi Rogatus Mativila (Miundombinu); Bi. Paulina Nkwama Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu; watendaji wakuu wa taasisi, wakurugenzi na watumishi wote kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha Ofisi ya Rais – TAMISEMI kufikia malengo ikiwa ni pamoja na kukamilisha hotuba hii kwa wakati.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee na kwa heshima kubwa nitumie nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Rufiji kwa imani wanayoendelea kuionesha kwangu, kwa kuendelea kuniunga mkono pamoja na majukumu ya kitaifa ambayo ninaendelea kuyatekeleza kwa manufaa ya wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninawaahidi kuwa, nitaendelea kuwatumikia usiku na mchana na sitachoka kwa kuwa lengo langu ni kuiona Rufiji iliyobora kuliko jana.

**1.2 Salamu za Pole**

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** natoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wabunge pamoja na Watanzania wote, kwa kuondokewa na wapendwa wetu, Hayati Alhaj Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili na Hayati Edward Ngoyai Lowasa, Waziri Mkuu Mstaafu. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi, Amina.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** natoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Francis Leonard Mtega aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali, Mbeya na Ahmed Yahya Abdulwakili aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani - Zanzibar. Aidha, napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu, pamoja na watanzania wote walioondokewa na wapendwa wao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, ninatoa pole kwa wananchi wote waliokumbwa na maafa mbalimbali na majanga ya asili ya mafuriko na maporomoko ya udongo yaliyotokea Wilaya ya Hanang' Mkoani Manyara, wananchi wa Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani pamoja na maeneo mengine yaliyopatwa na maafa. Ninawapa pole sana na ninamuomba Mwenyezi Mungu awajalie

wepesi katika kipindi kigumu wanachokipitia na niwahikikishie Serikali yao ipo pamoja nao. Aidha, ninawashukuru sana wananchi, taasisi, asasi za kiraia na wadau mbalimbali kwa michango yao ya hali na mali waliyoitoa na wanayoendelea kuitoa kwa ajili ya wananchi waliokumbwa na maafa hayo.

### 1.3 Majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI ina jukumu la kuratibu na kusimamia mafungu 28 yanayojumuisha: Ofisi ya Rais - TAMISEMI Fungu Namba 56 pamoja na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Wakala ya Barabara ya Vijijini na Mijini (TARURA), Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka (DART), Chuo cha Serikali za Mitaa (LGTI), Shirika la Elimu Kibaha (KEC), Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB), Shirika la Masoko ya Kariakoo (KMC), Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Namba 02, na Mafungu 26 ya Mikoa ikijumuisha Halmashauri 184.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** maelekezo ya mgawanyo wa majukumu yaliyotolewa na Hati Idhini ya Rais (Presidential Instrument) ya tarehe 30 Agosti, 2023 yanaainisha majukumu ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kama ifuatavyo: -

(i) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka (D by D), tawala za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa, maendeleo vijijini na mijini;

(ii) Kuziwezesha tawala za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kutekeleza majukumu yake ya kisheria;

(iii) Kuratibu shughuli za utoaji wa huduma mijini kama vile usafiri, usafirishaji na usafi wa mazingira;

(iv) Kusimamia shughuli za Tume ya Utumishi wa Walimu;

(v) Kusimamia shughuli za elimumsingi na sekondari;

(vi) Kusimamia na kuratibu shughuli za utoaji wa huduma za afya ya msingi, ustawi wa jamii na lishe;

(vii) Kuratibu na kusimamia mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika ofisi za wakuu wa mikoa, mamlaka za serikali za mitaa na taasisi;

(viii) Kuratibu shughuli za wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo;

(ix) Kujenga uwezo wa watumishi wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, ofisi za wakuu wa mikoa na mamlaka za serikali za mitaa; na

(x) Kusimamia utendaji wa mashirika, taasisi, programu na miradi iliyo chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS – TAMISEMI KWA MWAKA 2023/24

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilipanga kutekeleza mpango na bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo: -

(i) Kusimamia masuala ya utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma (D by D);

(ii) Kuratibu maandalizi ya uchaguzi wa serikali za mitaa kwenye vijiji 12,318, mitaa 4,263 na vitongoji 64,361 katika halmashauri 184 utakaofanyika mwaka 2024;

(iii) Kuratibu suala la usalama katika mikoa na wilaya;

(iv) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya jamii katika mikoa na mamlaka za serikali za mitaa;

(v) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa huduma za afya ya msingi, ustawi wa jamii na lishe

katika ofisi za wakuu wa mikoa na mamlaka za serikali za mitaa;

(vi) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa elimumsingi na sekondari katika mamlaka za serikali za mitaa ikijumuisha utekelezaji wa Elimumsingi na Sekondari bila Ada;

(vii) Kuratibu na kusimamia Mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato na kudhibiti matumizi katika mamlaka za serikali za mitaa;

(viii) Kuratibu ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya barabara, usafirishaji, afya ya msingi, elimumsingi na sekondari na majengo ya utawala katika ofisi za wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya na mamlaka za serikali za mitaa;

(ix) Kuratibu na kusimamia shughuli za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, ofisi za wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya na mamlaka za serikali za mitaa kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi;

(x) Kuchochea na kuhimiza ukuaji wa uchumi shindani kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla kwa kuiwezesha mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kuweka mazingira mazuri ya uanzishaji wa viwanda, biashara na uwekezaji hasa katika kilimo, mifugo, uvuvi, misitu, nyuki, wanyamapori na utalii;

(xi) Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI;

(xii) Kuratibu upelekaji wa fedha za mikopo ya asilimia kumi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika mamlaka za serikali za mitaa kwenda kwenye mfuko wa mikopo ya vikundi na kusimamia urejeshwaji wa mikopo iliyotolewa miaka ya nyuma;

(xiii) Kuratibu masuala ya michezo na utamaduni katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI, ofisi za wakuu wa mikoa, wilaya na mamlaka za serikali za mitaa;

(xiv) Kuratibu usimamizi wa masuala ya uhifadhi na utunzaji wa misitu, wanyamapori, nyuki, vyanzo vya maji, athari za mabadiliko ya tabianchi pamoja na fursa za mabadiliko hayo kupitia biashara ya kaboni (Hewa Ukaa) na udhibiti wa uzalishaji taka katika mikoa na mamlaka za serikali za mitaa;

(xv) Kusimamia mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika Ofisi ya Rais – TAMISEMI, ofisi za wakuu wa mikoa, mamlaka za serikali za mitaa na taasisi zilizo chini yake;

(xvi) Kuratibu uendelezaji wa vijiji na miji kwenye mamlaka za serikali za mitaa;

(xvii) Kuzisimamia mamlaka za upangaji katika kupanga na kuendeleza mipango miji na matumizi endelevu ya ardhi vijijini, ujenzi wa nyumba bora na kudhibiti ujenzi holela, kutunza mipaka ya maeneo ya utawala, kuzuia na kutatua migogoro inayohusu ardhi; na

(xviii) Kuratibu uendelezaji wa vijiji na miji kwa utangamano na shughuli za kilimo, uvuvi, mifugo, huduma za maji, umeme, barabara na sekta zingine za uzalishaji na masuala mengine mtambuka.

## 2.1 Ukusanyaji wa Maduhuli ya Mikoa na Mapato ya Ndani

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa ziliidhinishiwa kukusanya maduhuli na mapato ya ndani ya shilingi trilioni 1.19, ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.07 iliyoidhinishwa mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la shilingi bilioni 127.55 sawa na asilimia 11.90. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 55.14 ni za taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, shilingi milioni 261.89 ni

maduhuli ya mikoa na shilingi trilioni 1.14 ni za mapato ya ndani ya halmashauri.

***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2024 shilingi bilioni 863.78 zimekusanywa sawa na asilimia 72.02 ya lengo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 848.14 ni mapato ya ndani ya mamlaka za serikali za mitaa, shilingi bilioni 15.44 ni mapato ya ndani ya taasisi na shilingi milioni 193.79 ni maduhuli ya mikoa. Makusanyo hayo yalitokana na ada za wanachuo, tozo, ukusanyaji wa madeni, mauzo ya bidhaa mbalimbali na ushuru unaotozwa na mamlaka za serikali za mitaa kulingana na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290.

**19. Mheshimiwa Spika,** Hali ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwenye mamlaka za serikali za mitaa katika kipindi cha Awamu ya Sita imeendelea kuimarika, ambapo makadirio yameendelea kuongezeka kutoka shilingi trilioni 1.01 mwaka 2022/23 hadi shilingi trilioni 1.14 mwaka 2023/24. Aidha, makusanyo halisi yameongezeka kutoka shilingi bilioni 625.32 Machi, 2023 hadi shilingi bilioni 848.14 Machi, 2024 ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 222.82 (***Kiambatisho Na.1).***

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** ongezeko la ukusanyaji wa mapato ya ndani katika mamlaka za serikali za mitaa, limechangiwa na mikakati mbalimbali inayofanywa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, ikiwemo tathmini ya vyanzo vya mapato iliyofanyika kwa miaka miwili (2) mfululizo ya mwaka 2022/23 na mwaka 2023/24 katika halmashauri 184 na matumizi ya mfumo wa TAUSI katika ukusanyaji wa mapato.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** utumiaji wa mfumo wa TAUSI umetatua changamoto mbalimbali zilizoukabili mfumo wa awali wa *Local Government Revenue Collection Information System* (LGRCIS) ikiwa ni pamoja na kukabiliwa na ukuaji wa teknolojia, kuzuia uvujaji wa mapato na mabadiliko ya kisera na mahitaji ya watumiaji na wadau mbalimbali. Aidha, umesaidia kuimarisha makusanyo katika mamlaka za serikali za mitaa kwa kupunguza matumizi ya fedha mbichi, ucheleweshaji wa kuwasilisha fedha benki, kumwezesha mteja kufanya malipo na utoaji wa leseni za biashara na vibali vya ujenzi kielektroniki. Aidha, mfumo wa TAUSI unamwezesha mteja


kujihudumia mwenyewe mahali popote ndani na nje ya nchi na kupata huduma pasipo kufika ofisi za halmashauri.

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** mpaka sasa mfumo huu wa TAUSI umeonesha mafanikio makubwa ya ukusanyaji wa mapato, kupunguza muda wa kupata huduma za leseni na vibali, kudhibiti upotevu wa mapato yanayokusanywa kupitia mashine za kukusanyia mapato (Point of Sale - PoS) kwa kuweka udhibiti wa muda na kiasi cha kukusanya nje ya mtandao ili kuhakikisha taarifa zote za makusanyo zinafika kwenye mfumo mkuu, kuwa na taarifa sahihi za walipakodi na watumiaji kwa kutumia Namba ya Utambulisho ya Taifa (NIN).

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** mfumo wa TAUSI unawezesha kukusanya mapato shirikishi kwa kutumia namba ya kumbukumbu ya malipo (control number) moja inayojumuisha mapato ya halmashauri na taasisi nyingine. Mfano, chanzo cha ushuru wa minada na afya ya wanyama kinakusanywa kwa namba ya kumbukumbu ya malipo moja ambapo sehemu ya makusanyo inaenda mamlaka za serikali za mitaa na nyingine inaenda Wizara ya Mifugo na Uvuvi kulingana na sheria.

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka 10, mwenendo wa makusanyo ya mapato ya ndani ya halmashauri umeendelea kuimarika. Makisio ya mapato ya mwaka 2013/14 yalikuwa shilingi bilioni 395.81 na mwaka 2022/23 yamefikia shilingi trilioni 1.01 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 617.20. Aidha, makusanyo halisi katika miaka hiyo yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 323.27 hadi shilingi trilioni 1.02 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 697.76. Vilevile makisio ya mwaka 2024/25 yamefikia shilingi trilioni 1.35 hii inaonesha dhahiri kuimarika kwa makusanyo katika mamlaka za serikali za mitaa kama inavyoonekana katika kielelezo hapa chini.

Kielelezo: Mwenendo wa Makusanyo ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri 2013/14 – 2022/23




**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290, kupitia Sheria ya Fedha Namba 2 ya Mwaka, 2023 yamezipa mamlaka za serikali za mitaa jukumu la uwakala wa kusimamia na kukusanya vyanzo vya kodi ya majengo, kodi ya pango la ardhi na ushuru wa mabango. Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeanza ujenzi wa moduli ya vyanzo hivi katika mfumo wa TAUSI kwa kushirikiana na: Wizara ya Fedha; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Mamlaka ya Mapato Tanzania; Mamlaka ya Serikali Mtandao na Shirika la Umeme Tanzania. Zoezi la majaribio kwa baadhi ya halmashauri limeanza na halmashauri zote zitaanza kutumia ifikapo Julai Mosi, 2024. Natumia fursa hii kuwaelekeza viongozi wote wa mikoa, wilaya na halmashauri kuhakikisha kuwa:-

(i) Wananchi wote wanapewa elimu juu ya huduma za Serikali zinazotolewa kwa njia ya mtandao;

(ii) Wanaandaa maeneo maalumu (kanda au kata) ambayo yatakuwa karibu na wananchi ili waweze kupata msaada wa kiufundi wanapopata shida ya huduma mtandaoni;

(iii) Wanatumia eMrejesho na kuweka namba ya huduma kwa wateja kwa ajili ya kupokea mrejesho/kero kutoka kwa wananchi na kuzifanyia kazi ipasavyo;

(iv) Wananchi wanaelimishwa na kuhimizwa kulipa kodi na tozo kwa wakati kwa ajili ya kuboresha huduma; na

(v) Wanafanya maandalizi yote stahiki ya kuwezesha vyanzo vyote vipya kuanza kufanya kazi pasipo kubughudhi wananchi.

**Usimamizi wa Fedha za Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2024 halmashauri zimekusanya shilingi bilioni 848.14 sawa na asilimia 74 ya bajeti iliyoidhinishwa. Halmashauri zimeonesha kufanya vizuri ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/23 ambapo kiasi cha shilingi bilioni 625.32 kilikusanywa sawa na asilimia 62 (***Kiambatisho Na. 1).***

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuongezeka kwa mapato ya ndani kunasadifu dhana ya Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliyekuwa na maono makubwa kuhusu ukusanyaji wa mapato akiamini kuwa mapato yanapaswa kukusanywa kwa ufanisi ili kuwezesha maendeleo endelevu na kutoa huduma bora kwa wananchi. Kwa maneno yake, alielezea kuwa:

"***Mapato ni damu ya maendeleo. Bila ya mapato hakuna maendeleo. Nchi maskini siyo maskini kwa sababu hazina maliasili, zana, au watu hodari. Zipo nchi tajiri duniani ambazo hazina haya pia. Maskini ni maskini kwa sababu mapato yake ni madogo".***

**28.** ***Mheshimiwa Spika***, kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato kumewezesha kuongezeka kwa matumizi ya fedha za mapato ya ndani kwenye miradi ya maendeleo kutoka shilingi bilioni 194.80 zilizotumika hadi Machi, 2023 ikilinganishwa na shilingi bilioni 226.05 zilizotumika hadi Machi, 2024 (***Kiambatisho Na. 2***).

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 shilingi bilioni 226.05 za mapato ya ndani zimetolewa kwa ajili ya kuchangia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi kinachoishia mwezi Machi 2024. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 50.62 zimetumika kwenye Sekta ya Elimu, shilingi bilioni 39.77 zimetumika

kwenye Sekta ya Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii, shilingi bilioni 61.06 zimetumika kwenye Sekta ya Utawala. Aidha, shilingi bilioni 18.92 zimetumika kwenye Sekta ya Barabara na Usafirishaji, shilingi bilioni 15.84 zimetumika kwenye Sekta ya Biashara na Uwekezaji, shilingi bilioni 13.73 zimetumika kwenye Sekta ya Ardhi na Mipango miji, shilingi bilioni 9.69 zimetumika kwenye Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, shilingi milioni 321.47 zimetumika kwenye Sekta ya Maji, na shilingi bilioni 16.06 zimetumika kwenye Sekta nyingine.

**Ununuzi wa Boti na Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati**

**30.** ***Mheshimiwa Spika***, taratibu za ununuzi wa boti 10 zinaendelea katika Halmashauri za Wilaya za Ludewa, Ukerewe, Buchosa, Nyasa na Sumbawanga ili kuimarisha doria, ulinzi na ukusanyaji wa mapato ya ndani katika halmashauri hizo.

***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa miradi ya kimkakati unaendelea katika mamlaka za serikali za mitaa, ambapo miradi 14 imepokea fedha. Kati ya miradi hiyo miradi mitano (5) imekamilika ambayo ni ujenzi wa Soko la Kisasa la Kibada katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni, Soko la Kisasa katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Ujenzi wa Kiwanda cha Chaki katika Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, ujenzi wa Kituo cha Kuegesha Magari Makubwa – Nyakanazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo na upanuzi wa Kituo cha Mabasi cha Nyegezi katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza. Aidha, miradi tisa (9) inaendelea na utekelezaji katika hatua mbalimbali na baadhi ya miradi hiyo imeanza kutoa huduma wakati shughuli za ukamilishaji zikiendelea.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** halmashauri zimeendelea kukusanya mapato kutoka katika miradi ya kimkakati iliyoanza kutoa huduma. Katika mwaka 2023/24 halmashauri zilikisia kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 15.25 kutoka katika miradi ya kimkakati iliyoanza kutoa huduma. Hadi Machi, 2024 shilingi bilioni 7.20 zimekusanywa sawa na asilimia 47.21. Fedha hizi zimeongeza ufanisi wa halmashauri katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2023/24 wataalamu 62 wa kada za uhandisi, wakadiriaji majenzi na uchumi kutoka halmashauri 35

wamejengewa uwezo katika uandishi wa maandiko ya miradi ya kimkakati. Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha itaendelea kujenga uwezo kwa halmashauri nyingine kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**Miradi ya Kimkakati Iliyotekelezwa kwa Mapato ya Ndani ya Halmashauri**

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** halmashauri 23 zilitenga shilingi bilioni 22.60 kutoka mapato ya ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kimkakati. Hadi Machi, 2024 shilingi bilioni 13.83 zimetolewa sawa na asilimia 61.12. Miradi hiyo iliyotengewa fedha ni maghala mawili ya mazao (2), majengo manne (4) ya vitega uchumi, viwanda vitatu (3) vya matofali, machinjio tatu (3), masoko nane (8), stendi sita (6) za mabasi, vibanda vya biashara 185 na uwanja wa mpira. Kati ya miradi hiyo, saba (7) imekamilika na inatoa huduma, 21 ipo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

**Makusanyo yatokanayo na Mikopo inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa**

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI kupitia Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa ilipanga kukopesha shilingi bilioni 3.51, kukusanya marejesho ya mkopo ya shilingi bilioni 1.68 na michango ya akiba na nyongeza ya mtaji ya shilingi bilioni 2.21. Hadi Machi, 2024 mikopo ya shilingi milioni 420 imetolewa. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 270 zimetolewa Halmashauri ya Mji wa Kasulu na shilingi milioni 150 zimetolewa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele.

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** bodi imekusanya marejesho ya mikopo ya shilingi milioni 276.57 sawa na asilimia 16.5 kutoka katika halmashauri tisa (9) ambazo ni Halmashauri za Manispaa ya Singida na Morogoro; Halmashauri ya Mji wa Mbinga na Halmashauri za Wilaya ya Mbinga, Bukombe, Kishapu, Ruangwa, Pangani na Tunduru zilizokopeshwa na Bodi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi.

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** shilingi milioni 329.89 sawa na asilimia 14.93 zimekusanywa kutokana na mchango wa akiba na nyongeza ya mtaji katika halmashauri 11 ambazo ni Halmashauri

za Manispaa ya Temeke na Ubungo, Halmashauri za Mji wa Bunda na Handeni pamoja na Halmashauri za Wilaya ya Madaba, Misungwi, Itigi, Nyang'hwale, Same, Songea na Itilima. Aidha, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imezielekeza halmashauri zinazodaiwa kuweka mpango wa kurejesha mikopo katika mipango na bajeti ya mwaka 2024/25.

**Shirika la Masoko ya Kariakoo**

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam limeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa soko jipya la Kariakoo lenye ghorofa sita za juu na ghorofa mbili za chini na ukarabati wa jengo kuu la soko la Kariakoo. Mradi ulianza kutekelezwa Januari, 2022 na Mkandarasi *ESTIM Construction Ltd* ya Dar es Salaam kwa gharama ya shilingi bilioni 28.03, mtaalamu mshauri ni Shirika la Nyumba la Taifa (NHC). Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 93. Hadi Machi, 2024 mkandarasi amelipwa shilingi bilioni 17.24. Aidha, maandalizi ya ufunguzi wa soko yanaendelea ili biashara zianze mwanzoni mwa mwaka 2024/25.

**2.2 Taarifa ya Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo**

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Ofisi ya Rais - TAMISEMI Fungu Namba 56, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Namba 02 na Mafungu 26 ya mikoa yakijumuisha halmashauri 184 yaliidhinishiwa bajeti ya shilingi trilioni 9.18. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 3.52 ni Fedha za Maendeleo na shilingi trilioni 5.65 ni za Matumizi ya Kawaida, yakijumuisha Mishahara shilingi trilioni 4.59 na Matumizi Mengineyo ni shilingi trilioni 1.06.

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2024 Mafungu 28 yamepokea na kukusanya shilingi trilioni 6.99 sawa na asilimia 76.18 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 4.47 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yakijumuisha Mishahara shilingi trilioni 3.66 na Matumizi Mengineyo shilingi bilioni 810.77. Aidha, shilingi trilioni 2.52 ni fedha za Miradi ya Maendeleo ikijumuisha shilingi trilioni 2.06 Fedha za Ndani na shilingi bilioni 456.39 Fedha za Nje.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya fedha zilizopokelewa shilingi bilioni 848.14 ni za mapato ya ndani ya halmashauri ambapo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 501.98 zimetumika kwenye Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni 226.05 zimetumika kwenye Miradi ya Maendeleo (***Kiambatisho Na. 2).***

## 2.3 Mafanikio ya Utekelezaji ya Bajeti kwa Mwaka 2023/24

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, ofisi za wakuu wa mikoa na halmashauri zimefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

### 2.3.1 Maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Mwaka 2024

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Ofisi ya Rais – TAMISEMI iliidhinishiwa shilingi bilioni 12.00 kwa ajili ya maandalizi ya uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika mwaka 2024. Hadi Machi, 2024 Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepokea shilingi bilioni 5.6 sawa na asilimia 46.67 ya fedha iliyoidhinishwa. Sehemu kubwa ya fedha ambazo hazijapokelewa zinahusika na shughuli za ununuzi ambazo taratibu zake zinaendelea.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na uhakiki wa maeneo ya utawala yatakayoshiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024, kuandaa Rasimu ya Tangazo la Serikali la Maeneo ya Utawala, kuandaa rasimu ya kanuni za uchaguzi na kufanya vikao vya wadau wa ndani ya Serikali ili kupata maoni na kuyajumuisha katika rasimu ya kanuni zilizoandaliwa. Aidha, rasimu ya kanuni hizo zitapitiwa na wadau wa nje ili kupata maoni yao kabla ya kuidhinishwa na kuanza kutumika.

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na uchambuzi wa mahitaji ya vifaa vya uchaguzi (maboksi ya kupigia kura, lakiri, daftari la kuandikisha wapiga kura, nakala za kanuni, orodha ya maeneo ya utawala yatakayoshiriki uchaguzi, mihuri, wino na vidau). Aidha, imeandaliwa rasimu ya Mwongozo wa Elimu ya Mpiga Kura na Mwongozo wa Uchaguzi.

## 2.3.2 Uratibu na Usimamizi wa Huduma za Afya ya Msingi, Ustawi wa Jamii na Lishe

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI inasimamia vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi 6,933 ambapo zahanati ni 5,887, vituo vya afya 874 na hospitali za halmashauri 172. Takwimu hizi zinaonesha kuna ongezeko la vituo vya afya ya msingi 1,663 ikilinganishwa na idadi ya vituo 5,270 vilivyokuwepo mwaka 2015 wakati wa mkakati wa kuboresha na kuanza ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya.

**46.** ***Mheshimiwa Spika***, kumekuwa na mabadiliko ya utoaji wa huduma za afya ya Msingi na mahudhurio ya wagonjwa. Mwaka 2023 wagonjwa milioni 26.9 walipatiwa huduma katika vituo vya afya ya msingi kama wagonjwa wa nje (OPD) na wagonjwa 854,318 walipatiwa huduma ya kulazwa (IPD). Katika eneo la mama na mtoto jumla ya akina mama milioni 1.6 walijifungua katika vituo vya kutolea huduma ya afya ya msingi na akina mama 125,318 waliokuwa na uzazi pingamizi walifanyiwa upasuaji.

**47.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24 ziliidhinishwa shilingi bilioni 258.48 kupitia ruzuku ya serikali kuu, mapato ya ndani na washirika wa maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za afya ya msingi, ustawi wa jamii na lishe. Hadi Machi, 2024 shilingi bilioni 253.67 zimepokelewa sawa na asilimia 98.14 ya fedha iliyoidhinishwa.

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zilizotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa majengo ya hospitali 45 za halmashauri zilizoanza ujenzi mwaka 2020/21 ambapo kila halmashauri iliidhinishiwa fedha kulingana na hatua ya ujenzi iliyofikiwa. Kati ya miradi hiyo, hospitali nne (4) zipo hatua ya umaliziaji, hospitali nne (4) zipo hatua ya kupandisha kuta, hospitali moja (1) ipo hatua ya jamvi na hospitali 36 zipo katika hatua za awali za ujenzi.

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, hospitali kongwe 30 zinazofanyiwa ukarabati zimepokea fedha ambapo hospitali 10 zimeanza ukarabati na hospitali 20 zipo hatua za awali za ujenzi.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** vituo vya afya 14 vimepokea fedha kwa ajili ya ujenzi ambapo vituo vitatu (3) vimeanza ujenzi na vituo 11 vipo katika hatua za awali za ujenzi. Aidha, vituo vya Afya 23 vimepokea fedha kwa ajili ya ukamilishaji ambapo vituo vitatu (3) vipo hatua ya lipu, vitatu (3) vipo hatua ya kuweka sakafu, vitatu (3) vipo hatua ya boma, vinne (4) vipo hatua ya kuweka vigae na vituo 10 vipo katika hatua za awali za ujenzi.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** zahanati 374 zimepokea fedha kwa ajili ya ukamilishaji ambapo zahanati moja (1) imekamilika, maboma 26 yapo katika hatua mbalimbali za umaliziaji na maboma 347 yamepokea fedha na yapo katika hatua za awali za ujenzi.

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imetoa fedha za ununuzi wa vifaa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya vilivyokamilika ambavyo ni zahanati 364, vituo vya afya 278 na hospitali za halmashauri 31 ili huduma zianze kutolewa. Aidha, ununuzi wa vifaa hivyo unaendelea katika hatua mbalimbali.

**Huduma za Lishe**

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI inaendelea kusimamia utekelezaji wa afua za lishe zilizoainishwa katika Mpango Jumuishi wa Lishe wa Taifa. Wakuu wa mikoa wakisaidiwa kwa karibu na wakuu wa wilaya na watendaji wa kata wanasimamia kikamilifu utoaji wa huduma za lishe kama ilivyoelekezwa kwenye Mkataba wa Lishe uliosainiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wakuu wote wa mikoa Tanzania Bara.

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** Halmashauri zimeendelea kutenga kiasi cha shilingi elfu moja au zaidi kwa kila mtoto mwenye umri chini ya miaka mitano (5) kwa ajili ya utekelezaji wa afua za lishe. Aidha kwa mwaka 2023/24 shilingi bilioni 15.7 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa afua za lishe.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2024 shilingi bilioni 8.1 sawa na asilimia 51.2 ya fedha zilizotengwa, zilitolewa na kutumika kutoa huduma katika afua za lishe. Miongoni mwa huduma zilizotolewa ni ufuatiliaji wa maendeleo ya ukuaji wa watoto,

upimaji wa hali ya lishe ya watoto, kutoa elimu na unasihi wa lishe kwa jamii, na kuimarisha mpango wa utoaji wa chakula kwa wanafunzi shuleni.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2024 watoto 9,813,010 wenye umri chini ya miaka mitano walipatiwa nyongeza ya matone ya Vitamini A; watoto 7,421,941 walipimwa hali ya lishe ambapo 139,473 walibainika kuwa na ukondefu, 12,649 walikuwa na utapiamlo mkali na 9,266 walikuwa na uzito uliozidi.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** wanawake wajawazito 4,648,307 sawa na asilimia 96.6 ya wajawazito wote waliohudhuria katika vituo vya kutolea huduma ya afya walipatiwa vidonge vya nyongeza ya madini chuma na vitamini ya Asidi ya Foliki kwa ajili ya kuongeza wingi wa damu. Aidha, wazazi au walezi 7,694,445 wenye watoto wenye umri chini ya miaka miwili walipatiwa elimu na unasihi wa ulishaji wa watoto katika vituo vya kutolea huduma za afya.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha hali ya lishe kwa vijana balehe hasa waliopo shuleni, shule 11,952 zimeanzisha bustani za mbogamboga na matunda na wanafunzi 10,712,640 wanapata huduma ya chakula wanapokuwa shuleni. Aidha, katika kuongeza wigo wa utoaji wa elimu ya lishe katika jamii, vijiji na mitaa 15,917 iliadhimisha siku ya Afya na Lishe ya Kijiji na Mtaa. Vilevile, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeandaa makala ya kuhamasisha jamii kuhusu masuala ya lishe kwa njia ya runinga ambayo itaanza kurushwa mapema Mei, 2024.

**Huduma za Ustawi wa Jamii**

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha huduma za ustawi wa jamii kwa makundi maalumu, hadi Machi, 2024 Ofisi ya Rais – TAMISEMI imefanikiwa kuwatambua jumla ya watu wenye ulemavu 11,434 ambapo wanawake ni 6,131 na wanaume 5,303 na kuwaunganisha na huduma mbalimbali ikiwemo kuwapatia mafuta maalumu kwa watu wenye ualbino 2,960 kulingana na uhitaji wao. Jumla ya wazee 574,321 wametambuliwa katika mikoa 26 wakiwemo wanawake 359,582 na wanaume 214,739. Kati ya hao wazee 365,284 (wanawake 219,455 na wanaume 145,829)

wamepatiwa vitambulisho vya wazee kwa ajili ya msamaha wa matibabu.

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya madirisha 1,066 ya kutolea huduma za afya kwa wazee yameanzishwa kwenye hospitali 187 na vituo vya afya 879 katika halmashauri 184. Watoto walio katika mazingira hatarishi 284,308 (wakiume 183,124 na wakike 101,184) walitambuliwa na kupatiwa huduma zikiwemo mafunzo ya ufundi stadi, kadi za bima ya afya ya Jamii, vifaa vya shule na kuwaunganisha na familia zao.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kusimamia utoaji wa huduma kwa makundi maalumu, kamati za watu wenye ulemavu 7,518, kamati za ulinzi na usalama wa mwanamke na mtoto 18,126 na mabaraza ya ushauri ya wazee 20,748 yameundwa katika ngazi za mikoa, halmashauri, kata, vijiji na mitaa.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** mashauri 2,682 ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, migogoro ya ndoa na familia 5,306 yalishughulikiwa. Aidha, huduma mbalimbali zilitolewa ikiwemo, huduma ya msaada wa kisaikolojia na kijamii, huduma za afya, matunzo kwa watoto, malazi, huduma kwenye vituo jumuishi (one stop centre), mavazi, chakula, kuwaunganisha manusura wa vitendo vya ukatili na familia zao na kutoa rufaa kwenda kwenye huduma mbalimbali ikiwemo mahakamani.

### 2.3.3 Usimamizi na Uendeshaji wa Elimumsingi na Sekondari

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI inaratibu usimamizi na uendeshaji wa elimu ya awali, msingi na sekondari nchini kupitia mamlaka za serikali za mitaa. Hadi Machi, 2024 idadi ya shule zenye madarasa ya awali ni 20,316 (17,942 za Serikali na 2,374 zisizo za Serikali); idadi ya shule za msingi 20,384 (17,986 za Serikali na 2,398 zisizo za Serikali) zikiwemo shule maalumu za msingi 37 za bweni na vitengo maalumu 710. Aidha, idadi ya shule za sekondari ni 6,263 (4,894 za Serikali na 1,369 zisizo za Serikali).

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2024 wanafunzi wa elimu ya awali walioandikishwa katika madarasa ya awali ni 1,538,753 sawa na asilimia 82.1 ya lengo la kuandikisha wanafunzi 1,873,927.

Kati ya wanafunzi hao, wavulana ni 774,478 na wasichana ni 764,275 wakiwemo wenye mahitaji maalumu 3,359 ambapo wasichana ni 1,529 na wavulana 1,830.

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa masomo wa 2024, wanafunzi 1,729,180 walitarajiwa kuandikishwa darasa la kwanza, ambapo hadi Machi, 2024 wanafunzi walioandikishwa ni 1,820,139 sawa na asilimia 105.3 ya lengo. Kati yao, wasichana ni 908,179 na wavulana ni 911,960 wakiwemo wenye mahitaji maalumu 4,391 ambapo wasichana ni 1,917 na wavulana ni 2,474.

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2024 jumla ya wanafunzi 19,863 wakiwemo wasichana 9,088, wavulana 10,775 na wanafunzi wenye mahitaji maalum 254 (wasichana ni 125 na wavulana ni 129) waliandikishwa katika Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA). Idadi imepungua kwa asilimia 44.21 ikilinganishwa na wanafunzi 28,645 wakiwemo wasichana 13,691 na wavulana 14,989 walioandikishwa mwaka 2023.

**Utekelezaji wa Shughuli za Maendeleo katika Sekta ya Elimu**

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kusimamia utoaji wa huduma ya elimumsingi na sekondari ambapo katika mwaka 2023/24 iliidhinishwa shilingi trilioni 1.72 kupitia ruzuku ya serikali kuu na Washirika wa Maendeleo wakiwemo Benki ya Dunia, Twiga Barrick Tanzania na Benki ya Azania kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika sekta ya elimu. Hadi Machi, 2024 shilingi trilioni 1.26 zimepokelewa sawa na asilimia 73.45 ya fedha iliyoidhinishwa. Shughuli zilizotekelezwa mwaka 2023/24 ni pamoja na:

**Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne**

**68. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023, jumla ya wanafunzi 1,287,934 kati ya 1,545,330 waliofanya mtihani sawa na asilimia 83.34 walifaulu. Ufaulu huu ni sawa na ongezeko la asilimia 0.39 ikilinganishwa na ufaulu wa mwaka 2022 ambapo wanafunzi 1,320,700 sawa na asilimia 82.95 walifaulu.

**Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi**

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka wa masomo 2023, watahiniwa 1,092,960 kati ya 1,356,392 sawa na asilimia 80.58 waliofanya mtihani walipata sifa ya kuendelea na elimu ya sekondari, wasichana wakiwa 585,040 na wavulana 507,920 wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalumu 3,666 (wasichana 1,721 na wavulana 1,945).

**Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili**

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023 watahiniwa 471,427 wakiwemo wasichana 250,147 na wavulana 221,280 kati ya watahiniwa 527,576 sawa na asilimia 89.36 waliofanya mtihani walifaulu. Idadi ya wanafunzi waliofaulu iliongezeka kwa 14,452 kutoka wanafunzi 456,975 mwaka 2022 hadi 471,427 mwaka 2023.

**Mtihani Kidato cha Nne na Wanafunzi waliochaguliwa Kujiunga na Kidato cha Tano Mwaka 2023**

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022 watahiniwa 522,217 wa shule walifanya mtihani wa kuhitimu kidato cha nne ambapo wanafunzi 456,975 sawa na asilimia 87.51 wakiwemo wasichana 243,285 na wavulana 213,690 walifaulu. Kati yao wanafunzi 188,128 walikuwa na sifa za kujiunga kidato cha tano au vyuo vya kati. Kati ya hao wanafunzi 130,446 wakijumuisha wasichana 65,965 na wavulana 64,481 walichaguliwa kujiunga na kidato cha tano mwaka 2023 katika shule 540 za Serikali ambapo miongoni mwao, wanafunzi wenye mahitaji maalumu walikuwa ni 490 wakiwemo wasichana 218 na wavulana 272.

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha tano, wanafunzi 46,455 sawa na asilimia 35.61 wakiwemo wasichana 21,991 na wavulana 24,464 walichaguliwa kusoma tahasusi za sayansi na hisabati, wanafunzi 83,991 sawa na asilimia 64.39 wakiwemo wasichana 43,974 na wavulana 40,017 walichaguliwa kusoma tahasusi za masomo ya sanaa na biashara.

**Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita**

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa masomo wa 2023, ufaulu wa kidato cha sita kwa watahiniwa wa shule ulikuwa

asilimia 99.90 ambapo watahiniwa 96,010 kati ya watahiniwa 96,319 waliofanya mtihani walifaulu. Idadi ya wanafunzi waliofaulu imeongezeka kutoka 84,404 mwaka 2022 hadi 96,010 mwaka 2023 ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 11,606 sawa na asilimia 13.75.

**74. *Mheshimiwa Spika,*** ufaulu wa mitihani ya kitaifa umeendelea kuimarika zaidi kutokana na jitihada kubwa zinazofanywa na walimu wetu nchini pamoja na kuboreshwa kwa mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

**Michezo kwa Shule za Msingi na Sekondari**

**75. *Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais -TAMISEMI imeendelea kuhimiza na kusimamia maendeleo ya michezo katika shule za msingi na sekondari. Kwa upande wa mashindano ya michezo ya Umoja wa Michezo na Taaluma Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) yenye lengo la kutambua na kuendeleza vipaji, jumla ya wanafunzi 3,360 walishiriki michezo mbalimbali iliyofanyika Julai, 2023 katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora. Aidha, mashindano ya Umoja wa Michezo Shule za Sekondari Tanzania (UMISSETA) yalifanyika ambapo wanafunzi 3,242 walishiriki michezo hiyo iliyofanyika katika Halmashuri ya Manispaa ya Tabora Agosti, 2023. Michezo hii ilihusisha wanafunzi kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

**Mafanikio ya Mpango wa Elimumsingi Bila Ada**

**76. *Mheshimiwa* Spika**, Mpango wa Elimumsingi Bila Ada kwa shule za msingi na sekondari nchini imeleta mafanikio makubwa, ikiwa ni pamoja na ongezeko la wanafunzi wapya wanaoandikishwa kujiunga katika ngazi mbalimbali za elimu. Idadi ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza imeongezeka kutoka wanafunzi 425,743 mwaka 2016 Mpango wa Elimumsingi bila Ada ulipoanza hadi wanafunzi 1,076,037 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 152.74.

**77. *Mheshimiwa Spika,*** jumla ya maafisa elimu kata 3,932, walimu wakuu 17,618 na wakuu wa shule 4,615 wamepokea posho ya madaraka. Jumla ya wanafunzi 23,778 wa bweni, wanafunzi 49,212 wa kutwa wamepata ruzuku ya chakula na wanafunzi 12,709,290 wamepata ruzuku ya uendeshaji kwa shule za msingi

17,618. Aidha, chakula cha wanafunzi 218,473, fidia ya ada ya bweni kwa wanafunzi 218,473, fidia ya ada ya kutwa kwa wanafunzi 2,831,006 na ruzuku ya uendeshaji wanafunzi 3,049,479 kwa shule za sekondari 4,652 imetolewa.

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** ruzuku ya Elimu Bila Ada inayotolewa kila mwezi tangu kuanza kwa mpango huu mwaka 2015/16 imeongezeka kutoka shilingi bilioni 13.46 hadi shilingi bilioni 33.30 kwa mwezi mwaka 2023/24 sawa na asilimia 147.26.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** serikali imejidhatiti kutekeleza maelekezo ya Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 kwa kuendeleza utoaji wa Elimu Bila Ada ili kuhakikisha wanafunzi wote wenye umri wa kwenda shule wanaenda.

**80.** ***Mheshimiwa Spika****,* napenda kunukuu maneno ya Baba wa Taifa Mwalimu *Julius Kambarage Nyerere* aliyoyasema *mwaka 1966* kuhusu umuhimu wa Serikali kugharamia elimu alisema ***"Taifa husomesha watu wake kwa faida ya Taifa".***

**81.** ***Mheshimiwa Spika****,* Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kutambua hilo, hadi kufikia machi, 2024 imetoa shilingi trioni 2.31 ili kutekeleza mpango wa Elimumsingi Bila Ada ikiwa ni ruzuku tangu kuanza utekelezaji wa mpango huo Disemba, 2015. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 758.81 zimetolewa katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita.

**Ujenzi na Ukamilishaji wa Miundombinu ya Shule**

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea na ujenzi wa shule mpya za msingi 302, vyumba vya madarasa 3,880, mabweni 63 ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu, matundu ya vyoo 22,418 na uzio wa mabweni katika shule 88. Ukarabati wa madarasa 627 katika shule kongwe za msingi na ukamilishaji wa mabweni saba (7) na bwalo moja (1). Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi wa shule mpya 25 za sekondari, madarasa 6,648, mabweni 444 na matundu ya vyoo 16,795 katika shule za sekondari. Pia, Serikali imefanya ukarabati wa shule 32, umaliziaji wa maboma ya madarasa 2,441, shule za bweni tisa (9), maabara 132 na matundu ya vyoo 1,650.

**Ununuzi wa Vifaa vya TEHAMA**

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imenunua na kusambaza vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya vituo vya walimu 501 vifaa hivyo ni kompyuta za mezani 1,573, kompyuta mpakato 400, televisheni janja (inch 65) 200, UPS 760, projekta 560, printa 360, mashine za kurudufu 360, *zoom camera* 200, na *digital camera* 200. Pia, kompyuta mpakato 159 zimenunuliwa na kusambazwa katika Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu za wilaya 139 na Makao Makuu ya Tume. Aidha, walimu 400 na maafisa TEHAMA wa halmashauri 184 wamejengewa uwezo kuhusu usimikaji, matengenezo, na utoaji wa usaidizi wa kitaalamu kwa walimu kuhusu matumizi ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi wa matumizi ya teknolojia hii katika kufundishia na kujifunzia.

**Ununuzi na usambazaji wa Vitabu Shule za Msingi na Sekondari**

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imenunua vitabu 8,016,243 vya shule za msingi na sekondari vya masomo mbalimbali ambapo vitabu 6,430,714 vimesambazwa katika mikoa yote 26 na vitabu 1,585,529 vinaendelea kusambazwa.

**Chuo cha Serikali za Mitaa**

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI kupitia Chuo cha Serikali za Mitaa kimeanzisha Kampasi ya Shinyanga ambapo jumla ya wanafunzi 167 wamedahiliwa na kuanza mafunzo kwa Kozi Nne (4) za Astashahada ya Maendeleo ya Jamii, Utawala katika Serikali za Mitaa, Uhasibu na Fedha na Menejimenti ya Rasilimali Watu. Hivyo, ninaomba kutoa wito kwa wanafunzi waliohitimu Kidato cha Nne na Sita kujiunga kwenye Mkupuo wa Machi na Oktoba kila mwaka.

**Shirika la Elimu Kibaha**

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI kupitia Shirika la Elimu Kibaha limeandaa Mfumo wa Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (e-learning management system) kwa ajili ya kutoa elimu ya sekondari mubashara (Live teaching) kwa shule za sekondari ili kukabiliana na upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi na hisabati. Hadi Machi, 2024 ujenzi wa mfumo unaendelea na majaribio ya kutoa elimu ya sekondari mubashara yamefanyika katika Shule za Sekondari za Kibaha na Dodoma na

matarajio ni kuzifikia shule zote za sekondari hususan katika masomo ya sayansi.

### 2.3.4 Utawala Bora, Usimamizi wa Rasilimali, Ujenzi wa Majengo ya Utawala na Makazi ya Viongozi

**Utatuzi wa Kero za Wananchi Katika Mikoa na Wilaya**

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hayati Baba wa Taifa aliwahi kusema ***"Hakuna shida yoyote ya watu ambayo tunaweza sema kuwa haituhusu – J. K. Nyerere 1962 Dar Es Salaam"***

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI inaendelea kuyaenzi maneno hayo ambapo mwaka 2023/24 wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, makatibu tawala wa mikoa na wilaya wameendelea kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwemo kusikiliza na kutatua kero za wananchi. Hadi Machi, 2024 jumla ya kero 16,938 zimepokelewa na zilisikilizwa katika ngazi ya mikoa na wilaya ambapo jumla ya kero 7,322 zimetatuliwa na kero 9,616 zipo katika hatua mbalimbali za utatuzi. Aidha, kero hizo zilizopokelewa na kusikilizwa zipo katika sekta mbalimbali zikiwemo utawala, afya, elimu, ardhi, maji, barabara na nishati.

**Usimamizi wa Kituo cha Huduma kwa Wateja**

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI ina Kituo cha Huduma kwa Wateja (Contact Centre) kwa lengo la kushughulikia malalamiko na kero za wananchi. Hadi Machi, 2024 kituo kimehudumia wananchi 23,896. Aidha, masuala mengi yaliyopokelewa na kusikilizwa kutoka kwa wananchi yalikuwa katika sekta za afya, elimu na ardhi. Kituo kimekuwa msaada kwa wananchi katika kupunguza na kutatua changamoto zinazowakabili kupata taarifa sahihi zinazohitajika, mathalani miongozo mbalimbali, ufafanuzi hususan wakati wa kuomba ajira pindi zinapotangazwa, ubadilishaji wa machaguo ya tahasusi, uhamisho wa watumishi katika mamlaka za serikali za mitaa hivyo kuwapunguzia gharama za safari ya kuja Dodoma kushughulikia kero husika.

**Usimamizi wa Rasilimali Watu**

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 maafisa tarafa 63 kati ya nafasi wazi 84 wameajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi. Aidha, katika kuboresha utendaji kazi, umefanyika msawazo wa watumishi wa halmashauri zilizokuwa na watumishi wengi na kuwahamishia halmashauri zenye upungufu wa watumishi ambapo watumishi 646 walihamishwa. Vilevile, Ofisi ya Rais – TAMISEMI inakamilisha taratibu za kuajiri watendaji wa kata 525, watendaji wa vijiji 1,986, watendaji wa mitaa 1,333 na maafisa tarafa 21.

**91.** ***Mheshimiwa Spika, "Ubadhirifu serikalini unarudisha nyuma maendeleo ya wananchi" maneno haya aliyasema Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Nyerere (1977) miaka 10 baada ya Azimio la Arusha.*** Hivyo, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kuchukua hatua kwa watumishi wanaotekeleza majukumu yao kinyume na sheria, taratibu na kanuni. Katika mwaka 2023/24 watumishi 225 wamechukuliwa hatua za kinidhamu, kati yao wakurugenzi ni 13, wakuu wa idara 30, watumishi wa sekta ya ujenzi 15, sekta ya afya nane (8) na 159 wa kada nyingine.

**Uwezeshaji wa Ngazi za Msingi za Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Sera ya Ugatuaji Madaraka kwa Wananchi, Serikali imeendelea kuboresha utendaji kazi katika ngazi za msingi ili kuimarisha utawala bora, maendeleo endelevu, na ushiriki wa wananchi katika maamuzi yanayogusa maisha yao.

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu huo, Serikali katika mwaka 2023/24 ilitenga shilingi bilioni 1.73 za Matumizi Mengineyo kutoka serikali kuu kwa ajili ya posho ya mawasiliano kwa wenyeviti wa vijiji na mitaa. Hadi Machi, 2024 shilingi bilioni 1.15 zimetolewa sawa na asilimia 67 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya posho ya mawasiliano katika halmashauri 165 ambazo mapato yake ni chini ya shilingi bilioni 5. Aidha, mamlaka za serikali za mitaa kupitia mapato ya ndani ya halmashauri zimefanikiwa kupeleka shilingi bilioni 7.13 sawa na asilimia 64 ya shilingi bilioni 11.05 zilizotengwa kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi kwenye ngazi za msingi.

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Chuo cha Utumishi wa Umma na Chuo cha Serikali za Mitaa imetoa mafunzo kwa maafisa tarafa 184 na watendaji wa kata 1,403 katika mikoa tisa (9) ya Pwani, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga na Kigoma. Aidha, katika mwaka 2022/23 mafunzo kuhusu misingi ya uongozi na utawala bora, utunzaji wa siri za Serikali, sera na sheria za uendeshaji wa serikali za mitaa, maadili ya utumishi wa umma, upangaji mipango na bajeti, usimamizi wa fedha, usimamizi wa miradi, ushughulikiaji wa malalamiko na itifaki yalifanyika katika Mikoa minne (4) ya Rukwa, Katavi, Songwe na Njombe ambapo maafisa tarafa 56 na watendaji wa kata 356 walishiriki.

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea na utoaji wa mafunzo katika mikoa mitano (5) ya Simiyu, Mara, Mwanza, Geita na Kagera kufikia mwishoni mwa Aprili, 2024 ambapo maafisa tarafa 108 na watendaji wa kata 816 wanatarajiwa kushiriki na hivyo kufikisha mikoa 18 itakayokuwa imepatiwa mafunzo. Aidha, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imezielekeza halmashauri kutenga fedha kwa ajili ya kuendelea kutoa mafunzo kwa watendaji wa vijiji na mitaa.

**Ujenzi wa Majengo ya Utawala, na Makazi ya Viongozi**

**96.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24, shilingi bilioni 171.34 ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa ofisi za wakuu wa mikoa 16, ukarabati wa ofisi za wakuu wa wilaya 22, ikulu ndogo nane (8), ofisi za maafisa tarafa 19, nyumba 11 za wakuu wa mikoa, nyumba sita (6) za makatibu tawala wa mikoa, nyumba za makatibu tawala wasaidizi wa mikoa tano (5), nyumba za wakuu wa wilaya 13, nyumba za makatibu tawala wa wilaya nne (4), nyumba za maafisa tarafa 21, ujenzi wa majengo ya utawala katika halmashauri 72, nyumba 39 za wakurugenzi, nyumba 25 za wakuu wa idara wa halmashauri, pamoja na ununuzi wa samani za majengo ya utawala katika halmashauri 50.

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2024 majengo ya utawala katika halmashauri 12 yamekamilika na yanatumika na majengo 60 yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Aidha, ujenzi wa

nyumba za wakurugenzi tatu (3) zimekamilika, nyumba 37 za wakurugenzi na nyumba 25 za wakuu wa idara ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi. Vilevile, ununuzi wa samani katika majengo kwenye halmashauri tano (5) umekamilika na halmashauri 45 zinaendelea na taratibu za ununuzi.

**98.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi Machi, 2024 Ofisi ya Rais - TAMISEMI inaendelea kusimamia ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa nyumba 57 za viongozi ngazi ya tawala za mikoa ambazo ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi kama ifuatavyo; nyumba za wakuu wa wilaya mbili (2) zimekamilika, nne (4) ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, Ikulu ndogo nane (8), nyumba za makatibu tawala wa mikoa sita (6), nyumba za makatibu tawala wa mikoa wasaidizi tano (5), na nyumba za maafisa tarafa 21 zipo hatua mbalimbali za ukamilishaji. Vilevile, ujenzi wa ofisi 10 za maafisa tarafa uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo ofisi nne (4) zimekamilika na zinatumika na ofisi sita (6) zipo hatua ya umaliziaji.

**Ununuzi wa Mitambo, Magari na Pikipiki**

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha utekelezaji wa miradi na shughuli za maendeleo zinafanyika na kufuatiliwa kwa karibu, Serikali imeendelea kuwezesha upatikanaji wa magari ambapo hadi Machi, 2024 jumla ya magari 796 yamenunuliwa na kusambazwa katika taasisi, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa.

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya magari hayo, 316 ni kwa ajili ya kubebea wagonjwa (Ambulance); magari 212 kwa ajili ya usimamizi wa huduma za afya ya msingi, lishe na ustawi wa jamii katika halmashauri 184, mikoa 26 na makao makuu magari mawili (2); magari 134 kwa ajili ya usimamizi na uratibu wa shughuli za elimu; magari 18 kwa ajili ya usimamizi wa miundombinu ya barabara inayosimamiwa na TARURA; magari 83 kwa ajili ya viongozi wa mikoa na mamlaka za serikali za mitaa; na magari 26 kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo katika ngazi ya mkoa. Aidha, magari saba (7) na mitambo miwili (2) ya barabara yamenunuliwa kutokana na fedha za mapato ya ndani ya

halmashauri kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli za maendeleo na kufungua barabara mtawalia.

**101. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kuimarisha usimamizi, utoaji wa huduma na utatuzi wa kero kwa wananchi katika ngazi za msingi kwa kununua pikipiki 449 ambapo pikipiki 105 zimesambazwa kwa watendaji wa kata na pikipiki 344 zinakamilishwa usajili na zitasambazwa kwa maafisa afya wa kata 110 na watendaji wa kata 234.

**Ushirikishwaji wa Wananchi kupitia Mfumo wa O&OD iliyoboreshwa**

**102. *Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuhamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo katika ngazi za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kwa kutumia Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo ulioboreshwa (improved O&OD) ambapo hadi Machi, 2024 jumla ya mikoa 13 na halmashauri 75 zenye wataalamu 39 katika ngazi ya mikoa na 535 katika ngazi ya halmashauri walipewa mafunzo ya namna ya kuainisha vipaumbele vya jamii. Aidha, wataalamu 26 kutoka ofisi za mikoa na 394 kutoka halmashauri walipewa mafunzo kuhusu utoaji wa taarifa za ushiriki wa jamii katika shughuli za maendeleo kupitia mfumo jumuishi wa ufuatiliaji na tathmini (iMES). Mafunzo haya yameleta matokeo chanya ikiwemo kuongezeka kwa vipaumbele vya jamii katika bajeti ya mwaka 2024/25 ambapo halmashauri 130 kati ya 184 zimeweza kuweka vipaumbele vya jamii kwenye mipango yao.

### 2.3.4 Ujenzi, Ukarabati na Matengenezo ya Miundombinu ya Barabara na Usafirishaji

**103. *Mheshimiwa Spika,*** Ibara 57 (c-d) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 inaelekeza kuongeza kiwango cha barabara za changarawe kutoka kilomita 24,493 hadi kilomita 35,000 na kuongeza urefu wa barabara za vijijini na mijini zilizojengwa kwa kiwango cha lami kutoka kilomita 2,025 hadi kilomita 3,100 ifikapo mwaka 2025.

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2024 urefu wa barabara za changarawe umeongezeka kutoka kilomita 24,493 hadi kilomita 41,107.52 sawa na ongezeko la asilimia 17.45 ya lengo. Aidha, urefu wa barabara za vijijini na mijini zilizojengwa kwa kiwango cha lami umeongezeka kutoka kilomita 2,025 hadi kilomita 3,224.12 sawa na ongezeko la asilimia nne (4) ya lengo.

**105.** ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini itaendelea kufanya tafiti kwa kutekeleza kazi za ujenzi wa miundombinu ya barabara kwa kutumia teknolojia mbadala ambapo barabara nne (4) zimeendelea kufanyiwa tafiti ili kupunguza gharama za ujenzi, matengenezo na ukarabati. Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia TARURA itaendelea na uboreshaji wa miundombinu ya barabara za vijijini na mijini ili kuwawezesha wananchi kutekeleza shughuli zao za kijamii na kiuchumi.

**106.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24 sekta ya miundombinu ya barabara na usafirishaji iliidhinishiwa shilingi bilioni 825.09 kwa ajili ya ujenzi, ukarabati, matengenezo ya barabara na usafirishaji kupitia Mfuko wa Barabara, tozo ya mafuta, Mfuko Mkuu wa Serikali na washirika wa maendeleo. Hadi Machi, 2024 shilingi bilioni 682.60 zimetolewa kwa ajili ya miundombinu ya barabara na usafirishaji, sawa na asilimia 82.73 ya fedha zilizoidhinishwa.

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kunukuu maneno ya Hayati Benjamin William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu kuhusu umuhimu wa barabara za vijijini ambapo alisema:

***"Njia moja ya kuharakisha maendeleo ya vijiji ni kuhakikisha tunajenga na kuboresha barabara za vijijini. Barabara ni kiungo muhimu katika kuunganisha vijiji na huduma za kijamii kama shule, vituo vya afya, na masoko. Pia, barabara zinawezesha upatikanaji wa bidhaa za wakulima kwenye masoko na kuchochea biashara na ukuaji wa uchumi wa vijiji. Hivyo, tusipuuze umuhimu wa barabara za vijijini katika juhudi zetu za kuendeleza maeneo ya vijijini." - Benjamin Mkapa***

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita kwa kulitambua hilo, imeendelea kuyaenzi maneno ya Rais wa Awamu ya Tatu kwa kuendelea kutoa fedha kupitia Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini za ujenzi, matengenezo na ukarabati wa barabara kutoka shilingi bilioni 275 mwaka 2021/22 hadi kufikia shilingi bilioni 722.19 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 163.44.

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** ongezeko hili la fedha limewezesha kujenga barabara za lami kilomita 1,216.65, barabara za changarawe kilomita 17,125.2 na madaraja 2,355. Kutokana na ongezeko la fedha, kazi zimeongezeka ambapo makandarasi wa ndani wamenufaika na ongezeko hilo la fedha, hivyo wastani wa mikataba 844 ya kazi za barabara imeongezeka na kufikia wastani wa mikataba 1,826. Kazi zilizofanyika katika mwaka 2023/24 ni kama ifuatavyo: -

**110.** ***Mheshimiwa Spika***, fedha za Mfuko wa Barabara zimetumika kufanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 12,417.48, ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 15.64, barabara za changarawe zenye urefu wa kilomita 74.13 na ukarabati wa madaraja 20, makalavati 100 na mifereji ya kuondoa maji barabarani yenye urefu wa mita 50,563.12.

**111.** ***Mheshimiwa Spika***, fedha za tozo ya mafuta zimetumika kujenga barabara za lami zenye urefu wa kilomita 90.45, ujenzi wa barabara za changarawe zenye urefu wa kilomita 2,658.19 na ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua yenye urefu wa mita 8,298.00.

**112.** ***Mheshimiwa Spika***, fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali zimetumika kujenga barabara za lami zenye urefu wa kilomita 50.82, ujenzi wa barabara za changarawe kilomita 1,225.43, ujenzi wa madaraja 28, makalavati 60 na mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa mita 4,460.16.

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** Programu ya Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii Nchini (RISE) inaendelea na ujenzi wa barabara za Wenda – Mgama kilomita 19 na Mtili – Ifwagi kilomita 14 zilizopo Halmashauri za Wilaya ya Iringa na Mufindi mtawalia ambapo mikataba ya kazi na usimamizi ilisainiwa tarehe 20 Juni, 2023 na kazi zinaendelea. Aidha, usanifu wa barabara kilomita 50 za

mwanzo umeanza kufanyika kwa Halmashauri za Wilaya za Ruangwa, Mbogwe na Handeni.

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Kuboresha Miundombinu Shindanishi katika Miji Tanzania - *Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness* (TACTIC) unatekelezwa katika Halmashauri 12 za kundi la kwanza. Hadi Machi, 2024 kazi zilizotekelezwa ni kuandaa nyaraka muhimu za tathmini ya uzingatiaji na miongozo ya Usimamizi wa Mazingira na Kijamii, kukamilisha na kutiwa saini kwa mikataba ya ujenzi yenye jumla ya shilingi bilioni 259.13 kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kilomita 147.54 na ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua mita 24,660.

**115.** ***Mheshimiwa Spika***, katika utekelezaji wa kundi la pili la mradi kwenye miji 15, hadi Machi, 2024 kazi zifuatazo zimetekelezwa: kusaini mikataba ya usanifu; kuendelea na maandalizi ya kupata wataalamu washauri wa kusanifu miradi ya kundi la tatu kwenye miji 18 na ukusanyaji wa takwimu za msingi kwa mfumo wa GIS katika halmashauri 12 za kundi la kwanza.

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Uendelezaji wa Bonde la Mto Msimbazi upo katika hatua ya maandalizi ya ujenzi wa daraja na kupanda miti ya aina mbalimbali. Aidha, ulipaji wa fidia kwa waathirika wa bonde 2,102 kati ya 2,592 umekamilika na uandaaji wa nyaraka kwa ajili ya kuhamisha na kujenga karakana ya mabasi ya mwendokasi kutoka eneo la Jangwani kwenda Ubungo Maziwa umekamilika.

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia TARURA inaendelea na utekelezaji wa miradi kwa teknolojia za *ECOROADS, Ecozyme na GeoPolymer*. Hadi sasa kwa kutumia teknolojia ya *ECOROADS* katika Jiji la Dodoma imejengwa kilomita 1.0 ambayo imekamilika; Wilaya ya Mufindi zinajengwa kilomita 10 ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 55 na Wilaya ya Chamwino zinajengwa kilomita 6.95 ambapo utekelezaji wake umekamilika kwa asilimia 100. Aidha, ujenzi wa barabara ya Itilima Oil – Ikindilo kilomita 5.2 kwa kutumia teknolojia ya *Ecozyme* umefikia asilimia 15. TARURA kwa kushirikiana na TANROADS kupitia maabara yao

ya *Central Materials Laboratory* (CML) imeanza programu ya kufuatilia ubora na ufanisi wa teknolojia hizi mbadala ili kuona kama zinafaa na hivyo kuzieneza katika maeneo mengine nchini.

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** mojawapo ya kipaumbele cha Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia TARURA ni kutumia malighafi zinazopatikana maeneo ya ujenzi ili kupunguza gharama. Hadi Machi, 2024 TARURA imejenga madaraja 62 kwa kutumia mawe yanayopatikana karibu na eneo la ujenzi kwa gharama ya shilingi bilioni 10 ambapo ingekuwa shilingi bilioni 31.6 kama yangejengwa kwa zege.

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia TARURA iliidhinishiwa shilingi bilioni 21 kwa ajili ya kazi za dharura ambapo hadi Machi, 2024 shilingi bilioni 50.43 zimepokelewa sawa na asilimia 240.14 kutokana na ongezeko la dharura lililosababishwa na mvua nyingi. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kurekebisha barabara zenye urefu wa kilomita 129.13, ujenzi wa madaraja 20, ujenzi wa kalavati 95 na ujenzi wa mifereji ya kuondoa maji barabarani mita 6,260 na uwekaji wa changarawe kwenye maeneo ambayo barabara zilikatika na kurudisha mawasiliano kwa wananchi. Aidha, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutoa fedha ili kurejesha hali ya barabara za vijijini na mijini ambazo zimeathiriwa na mvua za msimu huu.

**120.** ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kupitia TARURA imeendelea na utekelezaji wa mradi wa Agriconnect ambapo barabara za Itulahumba - Igwachanya (kilomita 19.25)- Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Ndulilo - Itete (kilomita 8.9) - Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Lwangwa - Kejo Gas (kilomita 6.41) - Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo, Kidabaga – Bomalang'ombe (kilomita 1.10 ) - Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo na Ilolo - Ndolezi (kilomita 11.01 ) - Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Aidha, Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo katika utekelezaji wa programu hii.

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia DART inaendelea kukamilisha utengenezaji na usimikaji wa mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji nauli (Automated Fare Collection System-

AFCS) ambao utafungamanishwa na mfumo wa kuongozea magari (Intelligent Transport System - ITS) ikiwa ni sehemu ya maboresho endelevu ya huduma hii kwa wananchi waishio mijini, na pia kuondoa mianya ya upotevu wa mapato yatokanayo na nauli. Aidha, kazi zinazoendelea kwa sasa ni usimikaji wa mageti janja (Smart turnstile gates). Vilevile, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia DART inaendelea na kazi ya kumtafuta mbia wa uendeshaji wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Kwanza.

### 2.3.5 Usimamizi wa Mifumo ya TEHAMA

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI inaendelea kuimarisha mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwenye taasisi zilizo chini yake, ofisi za wakuu wa mikoa, mamlaka za serikali za mitaa, na vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi, elimumsingi na sekondari ili kuongeza ufanisi, uwajibikaji na utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Mifumo mbalimbali imefanyiwa usanifu na kutengenezwa na wataalamu wa Serikali ili kukidhi mahitaji stahiki katika maeneo ya kiutendaji yanayosimamiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na maelekezo ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, la upunguzaji na uunganishwaji wa mifumo, Ofisi ya Rais -TAMISEMI imeunganisha mifumo yake na mifumo mingine ya Serikali na ya sekta binafsi ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati, kudhibiti upotevu wa mapato na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** mifumo ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Mfumo wa Mipango na Bajeti – PlanRep, Mfumo wa Usimamizi wa Fedha za Umma ngazi za vituo, kata, mitaa na vijiji – FFARS, Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato – TAUSI na Mfumo wa Usimamizi wa Vituo vya kutoa huduma za afya – GoTHOMIS) tayari imeunganishwa na mifumo mingine kama Mfumo wa Ununuzi (NeST), Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato (GePG), Mifumo ya Leseni, Namba za Magari, Makusanyo ghafi ya mapato TRA, Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE), Mfumo wa Vitambulisho vya

Taifa (NIN), Mfumo wa Benki Kuu kupata taarifa za mabadiliko ya fedha, Mfumo wa uunganishaji wa mifumo (GoVESB, Financial Bus na HIM), Mfumo wa taarifa za vifaa tiba na madawa (eLMIS), Mfumo wa Bima ya Afya (NHIF) na Mifumo ya Benki za Biashara. Kazi ya kuunganisha mifumo mingine kama BRELA, LATRA, OSHA, BASATA, NAPA na Credit Info inaendelea.

**125. *Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI imesanifu na kujenga Mfumo wa Wezesha Portal utakaotumika kukopesha mikopo ya asilimia 10. Matumizi ya mfumo huu yatasaidia kuondoa changamoto zilizokuwepo awali ikiwa ni pamoja na kuondoa vikundi hewa, watu kujisajili zaidi ya kikundi kimoja, wakopaji hewa, kuimarisha usimamizi, usajili wa vikundi, utoaji na urejeshaji wa mikopo hiyo na upatikanaji wa taarifa sahihi za mikopo kwa wakati ili kuongeza tija, kuondoa upendeleo na kuongeza uwazi na uwajibikaji.

**126. *Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha pamoja na Benki Kuu ya Tanzania kwa kutambua dhima na walengwa imesanifu na kujenga moduli mbili katika mfumo wa Wezesha Portal kwa ajili ya usajili na usimamizi wa vikundi vya huduma ndogo za fedha (*Community Microfinance Groups*) pamoja na wahamasishaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha (*Business Microfinance Promoters*).

**127. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 kata 1,137; mitaa na vijiji 5,728 vimeanza kutumia Mfumo wa Kihasibu na Utoaji wa Taarifa za Fedha katika Ngazi za Msingi (FFARS) na kufanya jumla ya vituo 49,883 vinavyotumia FFARS ikiwemo vituo vya kutoa huduma za afya na elimu. Matumizi ya mfumo yameleta uwazi, uwajibikaji na udhibiti wa matumizi ya fedha katika ngazi za msingi za mamlaka za serikali za mitaa.

**128. *Mheshimiwa Spika***, kupitia mfumo huo, wananchi na wadau wote wanao uwezo wa kupata taarifa za mapato na matumizi ya fedha zote zinazoingia katika maeneo yao. Nisisitize usomwaji na upitiaji wa taarifa hizi, ziwe agenda ya kudumu katika vikao vyote vya kisheria katika ngazi hizo ikiwemo baraza la madiwani, kamati za maendeleo za kata na mkutano mkuu wa kijiji/mtaa.

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kuweka mfumo wa uendeshaji na usimamizi wa utoaji wa huduma za afya (GOTHOMIS) katika vituo vya kutolea huduma za afya na hadi Machi 2024, vituo 1,578 vinatumia mfumo huo. Kati ya vituo hivi, vituo 300 vinatumia Centralized GoTHOMIS ambayo ni GoTHOMIS iliyoboreshwa inayowezesha muendelezo wa huduma kwa kuwezesha taarifa kutembea na mteja kutoka kituo kimoja mpaka kituo kingine, upatikanaji wa taarifa jumuishi na *telemedicine*.

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** matarajio ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ni kufikisha mfumo ulioboreshwa na unaowekwa kwa gharama ndogo (chini ya asilimia 50 za awali) kwenye vituo vyote ndani ya mwaka 2025/26. Aidha, matumizi ya mfumo yamesaidia kudhibiti upotevu wa dawa vifaa na vifaa tiba, kudhibiti na kuongeza makusanyo ya ada za kuchangia huduma na ubadilishanaji na utoaji wa taarifa kwa wakati. Hivyo, kutokana na umuhimu wa matumizi ya GOTHOMIS, ninawaelekeza wakuu wa mikoa kuongeza kasi ya kusimamia usimikaji wa mfumo huo.

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na *Vodacom Foundation* imeendelea kuboresha mfumo wa huduma ya usafiri wa dharura kwa akina mama wajawazito na watoto wachanga (M-MAMA) ambao ulizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 06 Aprili, 2022. Tangu kuanza kwa M-MAMA katika halmashauri, akina mama wajawazito na watoto wachanga 21,800 wamehudumiwa na hivyo kusaidia kupunguza vifo vya akina mama wajawazito vinavyotokana na ukosefu au kuchelewa kupata huduma ya usafiri wa dharura. Mfumo umeanza kutumika katika Mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar kuanzia Oktoba, 2023.

**2.3.6** ***Mheshimiwa Spika,*** uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA ni zoezi endelevu kutokana na mabadiliko ya teknolojia, sera, mikakati, sheria, mahitaji na vihatarishi vya usalama kutoka kwa watumiaji wasio waaminifu. Hivyo, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya

Habari, Mamlaka ya Serikali Mtandao, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania na taasisi zingine itaendelea kuboresha mifumo hii kwa kuhakikisha kuwa mianya yote ya upotevu wa mapato inadhibitiwa na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na kufikia uchumi wa kidijitali.

### 2.3.7 Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi

**Mikopo Itokanayo na Asilimia 10 ya Mapato Yasiyolindwa ya Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuzisimamia mamlaka za serikali za mitaa kutenga fedha kwa ajili ya mikopo itokanayo na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri yasiyolindwa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Tangu mikopo hiyo ilipositishwa Mwezi Aprili, 2023 hadi Machi, 2024 fedha iliyopo kwenye akaunti za halmashauri ni shilingi bilioni 63.24. Aidha, fedha za marejesho ya mikopo zilizopo kwenye akaunti husika kwa kipindi hicho ni shilingi bilioni 63.67.

**Huduma Ndogo za Fedha**

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Benki Kuu zinasimamia utoaji wa huduma ndogo za fedha ambapo katika mwaka 2023/24 halmashauri zilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 4.70 kwa ajili ya uhamasishaji, ufuatiliaji na usajili wa vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha ambapo hadi Machi, 2024 bilioni 3.40 zimepokelewa. Vilevile, vikundi vya kijamii 6,994 vimetambuliwa, kusajiliwa na kupatiwa vyeti na kufanya idadi ya vikundi vya kijamii kufikia 49,168. Usajili wa vikundi hivi umesaidia kuleta ufanisi wa utoaji wa huduma kwenye sekta ndogo ya fedha ikiwemo upatikanaji wa huduma za mikopo ya vikundi yenye masharti nafuu.

### 2.3.8 Mabadiliko ya Tabianchi na Biashara ya Kaboni

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi duniani, Umoja wa Mataifa ulianzisha Itifaki ya Kyoto mwaka 1997 inayozitaka nchi zilizoendelea kupunguza gesijoto kwa asilimia tano. Njia mojawapo ya kupunguza gesijoto ni

kuanzisha biashara ya Kaboni katika nchi zinazoendelea ambapo nchini Tanzania biashara hiyo kwa ngazi za mamlaka za serikali za mitaa ilianza kuchipua rasmi mwaka 2018. Hadi Machi, 2024 halmashauri 15 zimeingia katika uendeshaji wa biashara ya kaboni. Kati ya halmashauri hizo, saba (7) zimeanza kupokea mapato yatokanayo na biashara hiyo na nane (8) ziko katika hatua ya kusaini mikataba ya biashara hiyo.

**135.** ***Mheshimiwa Spika****,* hadi Machi, 2024 mapato yatokanayo na uuzaji wa Kaboni (*Carbon Credit*) yamefikia dola za Marekani 12,630,350 sawa na shilingi bilioni 30. Fedha hizo zinatokana na uuzaji wa kaboni katika eneo la ukubwa hekta 690,500 kati ya hekta milioni 21 za misitu ya serikali za vijiji.

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2024 shilingi bilioni 1.88 zimepokelewa na kunufaisha wakulima wapatao 6,855 moja kwa moja katika vijiji 50 vya Halmashauri za Wilaya ya Karagwe, Misenyi, Kyerwa, Muleba, Bukoba na Ngara kutokana na biashara ya kaboni katika eneo la kilimo-misitu (Agroforestry).

**137.** ***Mheshimiwa Spika*****,** fedha za kaboni zitokanazo na uhifadhi wa misitu ya vijiji katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika shilingi bilioni 8.25 zimetumika kwa ajili ya shughuli za maendeleo na kiutawala kama ifuatavyo; utengenezaji wa madawati 1,496; ujenzi wa vyumba vya madarasa 52 katika shule za msingi 16 kwenye vijiji nane (8); nyumba 10 za watumishi kwa idara za afya, elimu na utawala katika shule za msingi tano (5), zahanati nne (4) na nyumba moja (1) ya mtendaji wa kijiji; ofisi za vijiji vinne (4); zahanati sita (6); matundu ya vyoo 128, na jengo la utawala na samani shule ya sekondari Mwese; utoaji wa Mikopo kwa vikundi 32 vyenye wanachama 386 (Village Community Conservation Bank VCCB), utoaji wa bima za afya kwa wananchi 26,273 (kaya 440); utoaji wa chakula kwa wanafunzi shule za msingi na sekondari na kulipa mishahara watumishi wa mikataba 222 (walimu, wapishi, walinzi, vibarua wa usafi na walinzi wa misitu wa vijiji).

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Kampuni ya Kaboni Tanzania wanatarajia kukabidhi hundi za

vijiji nane (8) vya Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika zenye jumla ya shilingi bilioni 14.2 ambazo ni matokeo ya uuzaji wa tani milioni 1.7 za kaboni kutoka katika misitu ya vijiji. Aidha, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Katavi na Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika inaendelea kukamilisha mpango wa matumizi ya fedha hizo.

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira na Kituo cha Ufuatiliaji wa Kaboni kilichopo Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo inaendelea kuratibu na kufuatilia biashara ya Kaboni na kuhakikisha inazingatia sheria, taratibu na kanuni zilizopo kwa maslahi ya wananchi na Serikali kwa ujumla.

**2.3.9 Uendelezaji Vijiji na Miji**

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeandaa na kusambaza Mwongozo wa Utekelezaji wa Mipango Kabambe (Master Plans) na Mwongozo wa Kukusanya, Kuchakata na Kuwasilisha Taarifa za Kijiografia za sekta mbalimbali zilizopo kwenye mamlaka za serikali za mitaa kwa kutumia mfumo wa taarifa za Kijiografia – GIS. Aidha, Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilizijengea uwezo wa utekelezaji wa miongozo hiyo timu za menejimenti za halmashauri 56 kwenye mikoa 12.

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi sasa Mipango Kabambe iliyoidhinishwa na inaendelea kutekelezwa ni ya halmashauri 23 zikiwemo za Majiji matano (5), Manispaa 12 na Miji sita (6). Aidha, Rasimu za Mwisho za Mipango Kabambe ya Jiji la Tanga na Manispaa ya Moshi zimekamilika na zinasubiri kuidhinishwa. Halmashauri zilizobaki zinaendelea kuandaa mipango hiyo ili ikikamilika iidhinishwe na kuweza kutumika.

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI inaendelea kuimarisha Uendelezaji wa Miji Midogo inayochipukia katika kuleta muunganiko wa maendeleo vijijini na mijini. Miji Midogo inayochipukia 203 na vijiji vya mfano 564 katika mpango huo vimeainishwa kwa kuzingatia kanda, jiografia ya maeneo husika na fursa zilizopo katika maeneo husika. Utekelezaji utahusisha

kupanga, kupima na utoaji wa hati miliki. Aidha, utekelezaji huo utaenda sambamba na udhibiti wa uendelezaji kwa kutoa vibali vya ujenzi ambavyo vitatolewa kielektroniki kupitia mfumo wa TAUSI.

**143.** ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wadau imekamilisha uandaaji wa Mpango Kabambe Jumuishi (Master Plan) wa uendelezaji wa Jiji la Kibiashara na Uwekezaji la Kwala kwa kipindi cha Mwaka 2022 – 2050 lenye ukubwa wa hekta 130,831. Eneo hilo limechukua sehemu za maeneo ya Halmashauri za Wilaya za Kisarawe, Kibaha na Chalinze.

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zinazoendelea kufanyika ni ukamilishaji wa eneo la maegesho la magari makubwa karibu na bandari kavu, utwaaji shirikishi wa maeneo na fidia mbalimbali, ujenzi wa barabara na vipande vya reli ili kuunganisha vitovu vya uzalishaji na usafirishaji ndani ya eneo la mpango.

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2021/22 Serikali ilitoa mkopo wa shilingi bilioni 49.47 kwa ajili ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi (KKK). Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 43.65 zilitolewa kwa mamlaka za serikali za mitaa 51 na kiasi kilichobaki kilitolewa Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Iringa na Dodoma pamoja na Chuo Kikuu cha Ardhi ambacho kilipewa fedha kwa ajili ya mradi wa upimaji wa Jiji la Mbeya.

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2024 shilingi bilioni 21.69 zimerejeshwa sawa na asilimia 49.69 kutoka halmashauri ambapo, 11 zimekamilisha kurejesha, 38 zimerejesha sehemu ya fedha na mbili (2) hazijaanza kurejesha.

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninazielekeza halmashauri kuongeza kasi ya urejeshaji mikopo waliyokopeshwa kwa ajili ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha (KKK) ardhi badala ya fedha hizo kuzitumia katika shughuli nyingine. Aidha halmashauri zilizokamilisha marejesho zinatakiwa kutumia faida inayopatikana kutokana na mauzo ya viwanja kupitia mradi wa KKK na miradi mingine kupima viwanja vingi zaidi ili kupunguza uendelezaji holela.

### 2.3.10 Tume ya Utumishi wa Walimu

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2024 Tume ya Utumishi wa Walimu imeendelea kuhudumia walimu 273,021 wa shule za msingi na sekondari waliopo kwenye utumishi wa umma, kati yao walimu wa shule za msingi ni 181,149 na sekondari ni 91,872. Usajili wa walimu 13,130 walioajiriwa mwezi Juni, 2023 ulifanyika ambapo walimu 13,130 wamepatiwa namba za usajili kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Tume ya Utumishi wa Walimu (Teachers Service Commission Management Information System - TSCMIS) wakiwepo 7,801 wa shule za msingi na 5,329 wa shule za sekondari. Aidha, madai 65 ya walimu kuhusu mafao ya pensheni, mirathi na mikataba yalipokelewa na kushughulikiwa, ambapo 25 yalihusu mirathi, 29 yalihusu mikataba na 11 yalihusu mafao ya pensheni.

**149. Mheshimiwa *Spika*,** hadi Machi, 2024 Tume imeshughulikia masuala ya maadili na nidhamu kwa walimu ambapo rufaa 79 za walimu zimepokelewa na kuchambuliwa, mashauri ya nidhamu 316 ya walimu yamepokelewa ngazi ya wilaya. Aidha, nyaraka kwa ajili ya rufaa 43 zilizokatwa na walimu ziliandaliwa na kuwasilishwa kwenye mamlaka husika kwa mujibu wa sheria.

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** tume inaendelea kusimamia mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Tume Makao Makuu inayojengwa kwenye eneo la Njedengwa. Hadi Machi, 2024 ujenzi umefikia asilimia 37, ambapo mkandarasi amekamilisha kumwaga zege la sakafu ya kwanza (*First Floor slab*) na kuanza kusuka nondo kwa ajili ya sakafu ya pili (*Second Floor*). Vilevile, tume imekamilisha awamu ya kwanza ya Mfumo wa TSCMIS na kusimika miundombinu ya mtandao wa intaneti kwenye Ofisi 24 za wilaya za Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Iringa na Wilaya ya Morogoro na Kishapu. Lengo la Mfumo huu ni kuboresha huduma zinazotolewa na Tume kwa walimu kuhusiana na masuala ya utumishi wao.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/25

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI mwaka 2024/25, yamezingatia Mpango

Mkakati wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI wa miaka mitano 2021/22 – 2025/26; mipango mikakati ya taasisi; Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati akilihutubia Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25; Sheria ya Bajeti Sura 439; Sera za kisekta; Maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; malengo yaliyomo katika Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na Agenda Afrika 2063.

### 3.1 Vipaumbele vya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2024/25 Fungu Namba 56

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga kutekeleza Mpango na Bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:

(i) Kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na ugatuaji wa madaraka kwa umma (D by D);

(ii) Kuratibu na kusimamia uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2024;

(iii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa huduma za jamii;

(iv) Kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato na kudhibiti matumizi yasiyo na tija katika ngazi zote ikijumuisha kuongeza kasi ya biashara ya kaboni;

(v) Kuratibu na kusimamia mifumo na miundombinu ya TEHAMA;

(vi) Kuendeleza rasilimaliwatu katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI;

(vii) Kuratibu na kusimamia shughuli za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa;

(viii) Kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma za jamii;

(ix) Kuratibu na kusimamia masuala ya michezo katika shule za msingi na sekondari;

(x) Kuratibu na kusimamia utendaji kazi wa taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI;

(xi) Kuratibu na kusimamia ujenzi wa miradi ya maendeleo katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI; na

(xii) Kuratibu na kusimamia shughuli za uendelezaji wa vijiji na miji kwenye mamlaka za serikali za mitaa.

**3.2 Vipaumbele vya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2024/25 Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Namba 2**

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Utumishi wa Walimu inatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo;

(i) Kusimamia ajira, maadili na maendeleo ya walimu kwa kuhakikisha walimu wanasajiliwa, wanathibitishwa kazini na kwa wale wenye sifa wanapandishwa vyeo/wanabadilishiwa vyeo kwa wakati, kusimamia maadili na nidhamu kwa walimu wa shule za msingi na sekondari katika utumishi wa umma;

(ii) Kufanya utafiti na kutathmini hali ya walimu nchini;

(iii) Uwezeshaji wa matumizi ya mifumo ya TEHAMA;

(iv) Kuboresha utunzaji wa nyaraka na kumbukumbu za walimu;

(v) Kuwajengea uwezo watumishi wa tume; na

(vi) Kuwezesha mazingira bora ya kufanyia kazi.

### 3.3 Vipaumbele vya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2024/25 Mafungu 26 ya Mikoa ikijumuisha Mamlaka za Serikali za Mitaa 184

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** ofisi za wakuu wa mikoa zinatarajia kutekeleza vipaumbele mbalimbali kama ifuatavyo:

(i) Usimamizi wa masuala ya usalama;

(ii) Uratibu wa maandalizi na uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2024;

(iii) Uimarishaji wa utawala bora, uwajibikaji na uwazi kwa kufanya vikao vyote vya kisheria;

(iv) Uratibu na usimamizi wa utoaji wa huduma za jamii;

(v) Uratibu wa uwezeshaji wananchi kiuchumi;

(vi) Kudhibiti matumizi yasiyo na tija;

(vii) Uboreshaji wa mazingira ya kufanyia kazi na makazi ya viongozi na watumishi wa mikoa na wilaya;

(viii) Uendelezaji wa rasilimaliwatu katika mikoa;

(ix) Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(x) Ufuatiliaji na utatuzi wa kero na malalamiko ya wananchi; na

(xi) Uratibu wa utekelezaji wa sera za kisekta.

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** mamlaka ya serikali za mitaa zinatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

(i) Kusimamia uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2024;

(ii) Kusimamia utoaji wa huduma za jamii na shughuli za kiuchumi;

(iii) Kusimamia na kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani ya halmashauri;

(iv) Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji;

(v) Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(vi) Uwezeshaji wananchi kiuchumi;

(vii) Utatuzi wa migogoro ya ardhi, wakulima na wafugaji, uendelezaji wa mipango miji na matumizi bora ya ardhi;

(viii) Uimarishaji wa huduma za ugani na ushirika;

(ix) Kutunza mazingira na kuongeza kasi ya biashara ya kaboni; na

(x) Kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji.

### 3.4 Makadirio ya Maduhuli na Mapato ya Ndani ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI Mwaka 2024/25

**156. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu Namba 56), mikoa na mamlaka za serikali za mitaa zinakadiria kukusanya maduhuli na mapato ya ndani ya shilingi trilioni 1.60 ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.14 iliyoidhinishwa mwaka 2023/24, ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 456.89 sawa na asilimia 39.93.

**157. *Mheshimiwa Spika,*** kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 188.96 ni makisio ya kodi ya majengo ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI ambayo yatakusanywa na mamlaka za serikali za mitaa zilizopewa uwakala wa kukusanya kodi hiyo na kuwasilisha makusanyo hayo Mfuko Mkuu wa Serikali, shilingi bilioni 55.42 ni mapato ya ndani ya taasisi. Aidha,

shilingi milioni 315.93 ni maduhuli ya mikoa na shilingi trilioni 1.35 ni za mapato ya ndani ya halmashauri.

### 3.4.1 Shughuli zitakazotekelezwa kupitia Fedha za Mapato ya Ndani ya Halmashauri

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Ofisi ya Rais – TAMISEMI imepanga kutumia shilingi bilioni 541.27 za mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya kuchangia utekelezaji wa shughuli za maendeleo kama ifuatavyo:

(i) Ujenzi na ukamilishaji wa vituo vya afya 132, zahanati 289, hospitali 21, vichomea taka 26, majengo ya wagonjwa wa nje 14, wodi 41, majengo ya kufulia matatu (3), majengo ya kuhifadhia maiti nane (8), njia za kupita wagonjwa kwenye vituo vinne (4) vya kutolea huduma za afya, maduka mawili (2) ya dawa na ununuzi wa vifaa tiba katika vituo nane (8) vya kutolea huduma;

(ii) Ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa vyumba vya madarasa 2,871, maabara za masomo ya sayansi 203 za sekondari, shule za msingi na sekondari 88, matundu ya vyoo 5,730 vya wanafunzi na walimu, mabweni 88, hosteli 24, mabwalo 19, majiko mawili (2), maktaba 6 na ofisi za walimu 48. Aidha, ununuzi wa madawati 47,192 katika shule za msingi, viti na meza 40,585 pamoja na vitanda 60;

(iii) Ujenzi wa uzio katika majengo 42 ya umma;

(iv) Ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilometa 8.4 kwa kiwango cha lami, kufanya matengenezo ya kawaida na kufungua barabara kuelekea maeneo ya uzalishaji, uwekezaji na utoaji wa huduma, kuchangia ujenzi wa barabara za mijini na vijijini kupitia TARURA na ujenzi wa vivuko vinne (4) vya watembea kwa miguu;

(v) Ununuzi wa mitambo 19 kwa ajili ya kuchonga barabara na mitambo ya kuzoa taka, trekta tano (5), magari 66 na pikipiki

56 kwa ajili ya kurahisisha utendaji kazi wa watumishi katika ngazi za halmashauri, kata, mitaa na vijiji;

(vi) Ujenzi na ukamilishaji wa majengo 44 ya utawala ya halmashauri, nyumba 346 za watumishi, ofisi 175 za kata, ofisi 67 za vijiji na ofisi 95 za mitaa;

(vii) Ujenzi wa vituo vipya 12 na ukamilishaji wa maboma 77 ya vituo vya polisi kata;

(viii) Kutekeleza miradi ya usambazaji wa maji na usafi wa mazingira ikiwemo miradi 12 ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa madampo, miradi 13 ya ujenzi wa miundombinu ya visima vya maji, miradi 11 ya ujenzi na ukamilishaji wa mifumo ya maji ambayo ni pamoja na ujenzi wa matenki na miundombinu ya kuvuna maji katika majengo ya umma;

(ix) Ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa malambo tisa (9) kwa ajili ya kunyweshea mifugo, machinjio 88, majosho 65, miradi 16 kwa ajili chanjo ya mifugo, maghala 15, miradi 2,155 ya kilimo kwa ajili ya huduma za ugani, mashamba darasa 366, miradi tisa (9) ya ugawaji wa mbegu, miradi 26 ya skimu za umwagiliaji, uchimbaji wa mabwawa 17 kwa ajili ya ufugaji wa samaki na umwagiliaji;

(x) Ununuzi wa boti 10 kwa ajili ya kuimarisha doria katika maeneo ya maziwa na bahari na miradi 13 ya uvuvi ikiwemo ujenzi wa mialo ya samaki na vichanja vya kuanika mazao ya uvuvi;

(xi) Utunzaji wa maliasili na mali kale ambapo miradi saba (7) imepangwa kutekelezwa, kuhifadhi misitu ya vijiji na halmashauri, miradi 16 ya upandaji wa miti katika maeneo ya misitu na maeneo ya wazi, miradi mitano (5) ya utalii ikiwemo ujenzi wa vituo vya utalii, na ukarabati wa maeneo yenye vivutio vya utalii;

(xii) Ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa vitega uchumi 64, kituo kimoja cha biashara, uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda

21, miradi tisa (9) ya uboreshaji wa maeneo ya wafanyabiashara ndogo ndogo (machinga), uboreshaji wa minada 55, masoko ya biashara 135, stendi 92 za mabasi na malori;

(xiii) Miradi 67 ya utwaaji wa ardhi kwa kuwalipa fidia wananchi, miradi 43 ya mipango miji ikiwemo kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi, kuandaa ramani, kuandaa mipango kabambe na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya upimaji na miradi 24 ya kupima na kuuza viwanja kwa wananchi;

(xiv) Ujenzi wa kituo kimoja cha utamaduni, miradi miwili (2) ya uendeshaji wa timu za mpira zinazomilikiwa na mamlaka za serikali za mitaa pamoja na ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa viwanja 21 vya michezo katika maeneo ya mamlaka za serikali za mitaa yakiwemo maeneo ya shule na maeneo mengine;

(xv) Kusimika mfumo wa GoTHOMIS katika vituo 77 vya kutolea huduma za afya, ununuzi wa vifaa vya TEHAMA, kufanya maboresho ya tovuti za mamlaka za serikali za mitaa na ununuzi wa PoS 914; na

(xvi) Kuongeza maeneo mapya ya biashara ya kaboni katika misitu 153 ya halmashauri na misitu 874 inayomilikiwa na serikali za vijiji pamoja na kuendelea kuhamasisha upandaji miti isiyopungua milioni 330.3 ya kuhifadhi na kutunza mazingira kwenye maeneo mbalimbali.

**159. *Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa miradi hiyo utaboresha upatikanaji wa huduma mbalimbali kwenye mamlaka za serikali za mitaa ikiwemo afya, elimu, barabara, kilimo, mifugo, uvuvi na kurahisisha uendeshaji wa shughuli mbalimbali za serikali na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi.

### 3.5 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI Mwaka 2024/25

**160. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na taasisi zilizo chini yake (Fungu Na. 56), Tume ya

Utumishi wa Walimu (Fungu Namba 02) na mafungu 26 ya mikoa (yakijumuisha halmashauri 184) imepanga kutumia shilingi trilioni 6.70 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo mishahara ni shilingi trilioni 5.52 na matumizi mengineyo ni shilingi trilioni 1.18 yanayojumuisha shilingi bilioni 815.06 za mapato ya ndani ya halmashauri.

### 3.6 Mpango na Bajeti ya Maendeleo ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI Mwaka 2024/25

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutumia shilingi trilioni 3.41 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 2.26 ni fedha za ndani na shilingi trilioni 1.15 ni fedha za nje. Fedha hizi zimepangwa kutekeleza miradi na programu mbalimbali katika mafungu 28.

### 3.7 Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI Mwaka 2024/25

#### 3.7.1 Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024

**162.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/25 Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetenga shilingi bilioni 17.79 kwa ajili ya kuratibu na kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 8.00 ni fedha kutoka serikali kuu kwa ajili ya uratibu Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Makao Makuu) na shilingi bilioni 9.79 ni mchango wa halmashauri kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya kugharamia uchaguzi huo. Uchaguzi huu utahusu uchaguzi wa viongozi katika ngazi ya msingi ambao ni wenyeviti wa vijiji, mitaa na vitongoji, wajumbe wa halmashauri ya vijiji na wajumbe wa kamati za mitaa.

#### 3.7.2 Uratibu na Usimamizi wa Huduma za Afya ya Msingi, Ustawi wa Jamii na Lishe

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutumia shilingi bilioni 357.85 za ruzuku ya fedha za maendeleo za serikali kuu na washirika wa maendeleo.

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zitakazitekelezwa kupitia fedha za ndani za maendeleo katika ngazi ya halmashauri ni pampja na:

(i) Ukamilishaji wa hospitali za halmashauri 118;

(ii) Ukamilishaji wa vituo vya afya 10;

(iii) Ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali za halmashauri 136, vituo vya afya 44 na zahanati 386;

(iv) Ujenzi wa miundombinu ya maji na vyoo katika vituo vya kutolea huduma za afya katika halmashauri 117;

(v) Kutoa chanjo kwa watoto chini ya miaka mitano (5), kutoa vitamin A na madini ya chuma kwa wajawazito katika halmashauri 184, upimaji wa Virusi vya UKIMWI, kutoa vyandarua kwa watoto chini ya miaka mitano (5) na wajawazito katika halmashauri 184; na

(vi) Kutoa huduma za lishe zilizoainishwa kwenye Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe 2020/21 - 2025/26 kwa makundi yote ya jamii wakiwemo wanawake walio katika umri wa uzazi, akinamama wajawazito na wanaonyonyesha, watoto, vijana, wanaume na wazee.

**165.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli nyingine zitakazotekelezwa kupitia Programu na miradi mbalimbali ni pamoja na:

(i) Usimamizi shirikishi wa utekelezaji wa huduma endelevu za maji na usafi wa mazingira vijijini katika mikoa 25 na halmashauri za wilaya 137 kupitia Programu ya Usafi wa Maji na Mazingira;

(ii) Usimamizi na uratibu wa utoaji wa huduma za chanjo katika halmashauri 184 kupitia Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Utoaji wa Huduma za Chanjo (GAVI);

(iii) Ufuatiliaji wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya kupitia Programu ya Kuimarisha Mifumo ya Afya (UNFPA);

(iv) Kuratibu na kusimamia usajili na utoaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto walio chini ya miaka 5, ufuatiliaji wa Programu ya Malezi Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto na utoaji wa mafunzo ya ulinzi na usalama kwa maafisa ustawi wa jamii kupitia mradi wa UNICEF katika halmashauri 184;

(v) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa afua za lishe kwenye tawala za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa, kuwajengea uwezo watumishi kuhusu kupanga na kusimamia bajeti za huduma za lishe, kuwajengea uwezo watendaji wa kata na vijiji/mitaa na kutathmini utekelezaji wake;

(vi) Kuwezesha upatikanaji wa watumishi 400 wa mkataba watakaofanya kazi katika vituo vya kutolea huduma za afya, kulipa mishahara kwa watumishi 400 watakaoajiriwa, kuratibu ujenzi na ukarabati kwa vituo vya kutolea huduma za afya 159 (hospitali 8, vituo vya afya 76 na zahanati 75) na ununuzi wa vifaa na vifaa tiba katika vituo 159 vya kutolea huduma ya Afya ya Msingi vitakavyokarabatiwa au kujengwa kupitia Programu ya Uwekezaji katika Afya ya Mama na Mtoto Tanzania (*Tanzania Maternal Child Health Investment Programme - TMCHIP*); na

(vii) Kutoa mafunzo kazini kwa watumishi wa vituo vya kutolea huduma za afya, kufanya usimamizi shirikishi katika afua za UKIMWI, kifua kikuu na malaria katika halmashauri 184 kupitia Programu ya Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria (Global Fund).

### 3.7.3 Usimamizi na Uendeshaji wa Elimumsingi na Sekondari

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Ofisi ya Rais – TAMISEMI imepanga kutumia shilingi trilioni 1.02 kupitia ruzuku ya serikali kuu na washirika wa maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli katika sekta ya elimu.

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shughuli zitakazotekelezwa ni kama ifuatavyo:

(i) Ujenzi wa vyumba vya madarasa 6,357, matundu ya vyoo 1,482, umaliziaji wa mabwalo 362 kati ya mabwalo hayo 15 ni msingi na 347 ni ya sekondari na umaliziaji mabweni 36 kwenye shule za awali na msingi;

(ii) Ujenzi wa shule mpya 184, nyumba za walimu 184 na mabweni 186 katika shule za sekondari;

(iii) Ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwenye shule za awali 3, msingi 400 na shule za sekondari 500;

(iv) Ununuzi wa kemikali za maabara katika shule mpya 234;

(v) Utoaji wa ruzuku ya Elimu Bila Ada kwa shule za msingi 17,986 na sekondari 4,894;

(vi) Ununuzi na usambazaji wa vitabu 2,215,877 kwa shule za msingi na 11,880,828 kwa shule za sekondari pamoja na vitabu na vifaa vilivyoboreshwa vya kufundishia na kujifunzia elimu ya awali kwenye shule 4,500;

(vii) Ununuzi wa vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shule 130 za msingi na sekondari;

(viii) Kutoa mafunzo ya maadili kwa wakuu wa shule 17,220, viongozi na watumishi wa TSC 460 katika ngazi ya wizara na wilaya;

(ix) Kutoa mafunzo endelevu ya walimu kazini (MEWAKA) kwenye shule za awali na msingi kwenye halmashauri 140;

(x) Kutekeleza mpango wa shule salama kwenye shule za awali na msingi 2,500;

(xi) Kuanzisha madarasa janja (smart classes) 10 kwa ajili ya ufundishaji mubashara katika halmashauri 10;

(xii) Kuandaa mwongozo wa mafunzo elekezi kwa walimu wapya wanaoajiriwa katika shule za umma; na

(xiii) Uandaaji wa kihunzi (framework) cha walimu wanaojitolea.

### 3.7.4 Utawala Bora, Usimamizi wa Rasilimali, Ujenzi wa Majengo ya Utawala na Makazi ya Viongozi

**168.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutumia shilingi bilioni 190.57 kwa ajili ya ununuzi wa magari ya viongozi wa mikoa na wilaya, kuendelea na ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa miundombinu ya mikoa ikiwemo majengo ya utawala, ikulu ndogo, makazi ya viongozi na watumishi wa mikoa, wilaya na tarafa katika mikoa 26.

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zitakazotekelezwa katika utawala bora ni pamoja na:

(i) Ununuzi wa magari 9 ya Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa katika Mikoa ya Katavi, Njombe, Iringa, Kigoma, Mwanza, Singida, Dar es Salaam na Manyara;

(ii) Ununuzi wa magari 56 ya wakuu wa wilaya na 47 ya wakurugenzi wa halmashauri;

(iii) Kuendelea na ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa miundombinu ya mikoa ikiwemo; majengo ya utawala 49, ikulu ndogo 8, makazi ya viongozi 25 na makatibu tawala wa mikoa na wilaya 17, makatibu tawala wasaidizi wa mikoa 10 na tarafa 5;

(iv) Kuendelea na ujenzi wa majengo ya utawala katika halmashauri 77 na ununuzi wa samani za majengo ya utawala katika halmashauri 21;

(v) Ukamilishaji wa nyumba 24 za wakurugenzi wa halmashauri na ujenzi wa nyumba 35 za wakuu wa idara;

(vi) Kutoa posho ya mawasiliano kwa wenyeviti wa vijiji na mitaa; na

(vii) Kuanza utekelezaji wa miradi mitano (5) ya kimkakati na kuendelea na ujenzi wa miradi 15 ya kimkakati katika halmashauri 20.

**Ufuatiliaji na Tathmini**

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** serikali imeendelea kuona umuhimu wa suala la ufuatiliaji na tathmini katika ngazi zote za Ofisi ya Rais-TAMISEMI, hivyo katika mwaka 2024/25 juhudi za ufuatiliaji na tathimini zitafanywa katika mamlaka za serikali za mitaa, mikoa na taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

**Ushirikishwaji wa Wanachi kupitia Mfumo wa O&OD iliyoboreshwa**

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kuhamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo katika ngazi za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kwa kutumia Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo Ulioboreshwa. Aidha, katika mwaka 2024/25 mafunzo yatatolewa kwa mikoa na halmashauri 54.

**3.7.5 Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi**

**Usimamizi wa Mikopo ya Asilimia 10**

**172.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kurejesha utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuanzia Julai, 2024 kwa utaratibu wa kutumia benki kwa halmashauri 10 za majaribio. Halmashauri hizo ni Majiji ya Dar es Salaam na Dodoma, Manispaa za Kigoma Ujiji na Songea, Miji ya Newala na Mbulu, Wilaya za Siha, Nkasi, Itilima na Bumbuli.

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** halmashauri 174 zilizobaki zitatumia utaratibu ulioboreshwa ili kuondoa mapungufu yaliyosababisha changamoto za awali kwa kufanya mambo yafuatayo; uanzishwaji wa kitengo cha usimamizi wa mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika Ofisi ya Rais – TAMISEMI, na uanzishwaji wa kamati za usimamizi wa mikopo katika ngazi za

ofisi za wakuu wa mikoa, halmashauri na kata. Majukumu ya kamati ngazi ya kata ni kutambua waombaji na kuthibitisha vikundi vya mikopo na kuvisajili kwenye mfumo kabla ya kuwasilisha kwenye kamati ya halmashauri.

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na kusanifu na kujenga mfumo mpya unaoitwa Wezesha Portal utakaotumika kwa ajili ya taratibu za ukopeshwaji wa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, mfumo huu utaondoa changamoto za mfumo zilizokuwepo awali kabla ya mikopo kusimamishwa.

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** maboresho mengine yaliyopangwa kufanyika ni kujenga uwezo kwa wasimamizi wa mikopo hiyo kwa kuongeza idadi ya wasimamizi wa mikopo kwenye ngazi ya kata ambapo maafisa maendeleo ya jamii 787 wameajiriwa na kupangiwa kata zilizokuwa na upungufu. Watumishi hao na timu nzima itakayosimamia mikopo hiyo katika ngazi zote itapatiwa mafunzo na wataalamu wabobezi wa usimamizi wa mikopo ya aina hiyo. Ofisi ya Rais – TAMISEMI imepanga kurekebisha sheria inayosimamia mikopo hiyo na kanuni zake ili kuongeza ufanisi. Baada ya kipindi cha mpito, tathmini itafanyika ili kubaini mfumo bora utakaotumika katika utoaji wa mikopo hiyo.

**176.** ***Mheshimiwa Spika,*** mikopo inayotarajiwa kutolewa ni shilingi bilioni 227.96 ambapo shilingi bilioni 63.67 ni fedha za marejesho zilizokuwa zikiendelea kukusanywa kutokana na mikopo iliyotolewa kabla ya kusimamishwa, shilingi bilioni 63.24 ni fedha zilizokuwa zinatengwa kwa ajili ya mikopo na shilingi bilioni 101.05 ni fedha ambazo zimetengwa kutokana na makisio ya makusanyo ya mapato ya ndani ya mwaka 2024/25.

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais -TAMISEMI itaendelea kuzisimamia mamlaka za serikali za mitaa kukusanya marejesho kutoka katika vikundi vilivyokopeshwa fedha za asilimia 10 ambapo shilingi bilioni 43.77 zitakusanywa kutoka katika vikundi vinavyoendelea kufanya marejesho. Mikopo hiyo itasimamiwa kwa umakini kuhakikisha hakuna vikundi hewa na yeyote atakayepatikana na ubadhirifu wa aina yoyote atachukuliwa hatua, kama

waungwana wasemavyo; '***Akopaye akilipa huondokana na lawama.'*** Hivyo, ninapenda kuwaelekeza wakuu wa mikoa kusimamia kwa makini mikopo hiyo.

**Mikakati ya Ukusanyaji wa Mapato**

**178. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa mapato ya mamlaka za serikali za mitaa yanakusanywa kwa ufanisi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kutekeleza yafuatayo:

(i) Kuendelea kufanya tathmini juu ya ukusanyaji wa mapato na kuendelea kubuni vyanzo vipya ili kuongeza ukusanyaji wa mapato;

(ii) Kuendelea na zoezi la kuratibu uthamini wa majengo ili kuweza kutoza kodi ya majengo kwa kutumia thamani halisi ya jengo husika;

(iii) Kuendelea kuimarisha Mfumo wa TAUSI ili kuboresha ukusanyaji wa mapato na kuziba mianya ya uvujaji wa mapato ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua kwa yeyote atakayebainika kuhusika na upotevu wa mapato;

(iv) Kuendelea kuimarisha upatikanaji wa vifaa vya kukusanyia mapato ikiwemo ununuzi wa PoS;

(v) Kuwajengea uwezo watumishi wa halmashauri ili kuongeza ujuzi na ubunifu wa ukusanyaji wa mapato ya ndani;

(vi) Kuongeza ushirikiano kati ya mamlaka za serikali za mitaa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kubadilishana taarifa za ukusanyaji wa mapato; na

(vii) Kuimarisha usuluhishi wa mapato kila mwezi.

**3.7.6 Ujenzi, Ukarabati, Matengenezo ya Miundombinu ya Barabara, Usafiri na Usafirishaji**

**179. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutumia shilingi bilioni 841.19 kwa ajili ya

ujenzi, matengenezo, ukarabati wa miundombinu ya barabara na usafiri na usafirishaji wa vijijini na mijini. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 257.03 ni za Mfuko wa Barabara, shilingi bilioni 127.50 Mfuko Mkuu wa Serikali, shilingi bilioni 325.77 ni za tozo ya mafuta ya petroli na dizeli ya shilingi 100 kwa lita, shilingi bilioni 4.03 za mapato ya ndani kupitia Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam na shilingi bilioni 126.85 ni fedha za nje.

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zitakazotekelezwa ni:

(i) Utunzaji (matengenezo) wa barabara za vijijini na mijini zenye urefu wa kilomita 20,745.31;

(ii) Ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 434.50;

(iii) Ujenzi wa barabara za changarawe zenye urefu wa kilomita 13,802.34;

(iv) Ujenzi wa madaraja 160 na ukarabati wa madaraja 21;

(v) Ujenzi na matengenezo ya boksi kalavati 586 na vivuko (drifti) 15;

(vi) Ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa mita 141,070.54;

(vii) Ujenzi wa kingo za Mto Msimbazi, kudhibiti maeneo ya juu ya Mto Msimbazi (upstreams);

(viii) Kuhamisha karakana ya mabasi yaendayo haraka kutoka Jangwani kwenda eneo la Ubungo Maziwa;

(ix) Kuboresha Miundombinu Shindanishi katika Miji Tanzania (TACTIC) kwa kujenga miundombinu katika Halmashauri 12 za Majiji ya Dodoma, Arusha, Mwanza na Mbeya; Halmashauri za Manispaa ya Kigoma, Songea, Ilemela, Kahama, Morogoro, Sumbawanga na Tabora na Halmashauri ya Mji Geita. Miundombinu msingi inajumuisha ujenzi wa masoko, mitaro ya maji ya mvua, stendi za mabasi,

maghala ya kuhifadhia mazao na kujenga barabara kiwango cha lami kilomita 147.5;

(x) Kuondoa vikwazo vya upitikaji barabarani kwenye wilaya 131 na ujenzi wa barabara kiwango cha lami Awamu ya Pili kilomita 164 kupitia Programu ya Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii Nchini (RISE);

(xi) Ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 250, kupitia Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam Awamu ya 2 ambapo kati ya hizo kilomita 132 zimefanyiwa usanifu;

(xii) Kukamilisha utaratibu wa ununuzi wa mbia wa uendeshaji wa mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Kwanza na ya Pili;

(xiii) Kudumisha usalama kwa kuimarisha ulinzi katika Mtandao wa Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka (DART);

(xiv) Kuendelea na taratibu za kubadilisha mfumo wa uendeshaji na ulipaji wa watoa huduma kutoka kupokea tozo kupita katika mfumo wa DART (Access Fee) na kuanza kutumia utaratibu wa malipo ya umbali wa mabasi yatakayokuwa yanatembea (per km mode);

(xv) Kukamilisha utengenezaji na usimikaji wa mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji nauli (Automated Fare Collection System-AFCS) wa Serikali unaosimamiwa na DART ambao utafungamanishwa na mfumo wa kuongozea magari (Intelligent Transport System-ITS) ikiwa ni sehemu ya maboresho endelevu ya huduma hii kwa wananchi waishio mijini, na pia kuondoa mianya ya upotevu wa mapato ya nauli kwenye mfumo; na

(xvi) Kukamilisha Sheria ya Usafiri wa Umma na kuhuisha DART kuwa Mamlaka.

**Matumizi ya Teknolojia Mbadala kwenye Ujenzi wa Miundombinu ya Barabara**

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Ofisi ya Rais – TAMISEMI imepanga kuendelea na majaribio ya matumizi ya teknolojia mbadala kwenye ujenzi wa miundombinu ya barabara katika Mikoa ya Pwani, Iringa, Dodoma na Simiyu ambapo jumla ya kilomita 54.15 zitajengwa kwa kutumia teknolojia ya *Ecoroads.*

**3.7.7 Uendelezaji Vijiji na Miji**

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Ofisi ya Rais – TAMISEMI itaendelea na uratibu wa utekelezaji wa mradi wa Green and Smart Cities - SASA katika Halmashauri za majaribio za Majiji ya Tanga, Mwanza na Manispaa ya Ilemela.

**183.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zitakazotekelezwa ni ujenzi wa masoko ya Mlango wa Chuma, Mgandini na Samaki Kasera katika Jiji la Tanga. Ujenzi wa Soko la Buhongwa na Ujenzi wa Machinjio Nyakato katika Jiji la Mwanza na ujenzi wa masoko ya Buswelu, Mwaloni na Igombe katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela.

**3.7.8 Shirika la Masoko ya Kariakoo**

**184.** ***Mheshimiwa Spika****,* katika mwaka 2024/25 Shirika la Masoko ya Kariakoo litaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Masoko ya Kariakoo Sura Na. 36. Aidha, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja kurejesha huduma za biashara kwa kuweka mpangilio mzuri wa biashara ili kuwarahisishia wateja kupata huduma wanazohitaji na kuboresha mazingira ya kufanyia biashara.

**185.** ***Mheshimiwa Spika****,* wafanyabiashara zaidi ya 2,200 watapangwa katika jengo jipya lenye ghorofa nane na jengo lililokarabatiwa ambapo wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi watafanya biashara na kununua bidhaa za aina mbalimbali zikiwemo pembejeo za kilimo na viuatilifu.

**186.** ***Mheshimiwa Spika,*** maeneo mengine yaliyoboreshwa ni kuwekwa kamera za kisasa za usalama, maeneo matatu (3) ya benki na mashine za kutolea fedha (ATM) nne (4) na maduka ya kubadilisha fedha. Huduma hizi zitarahisisha shughuli za kifedha na

hivyo kupelekea wafanyabiashara kutotembea na fedha umbali mrefu pamoja na maegesho ya magari 153.

### 3.7.9 Chuo cha Serikali za Mitaa

**187.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Serikali za Mitaa katika mwaka 2024/25 kitatekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa madiwani, watendaji wa kata na mitaa pamoja na watumishi wengine katika halmashauri zote nchini katika masuala mbalimbali yanayohusu uendeshaji wa mamlaka za serikali za mitaa;

(ii) Kufanya tafiti 30 na kutoa shauri elekezi 10 kwa serikali kuu, mamlaka za serikali za mitaa, mashirika na watu binafsi juu ya masuala mbalimbali ya maendeleo na kuimarisha mifumo ya TEHAMA;

(iii) Kuandaa Mtaala wa Shahada ya Kwanza ya Nyaraka na Kumbukumbu;

(iv) Kuendeleza watumishi 15 katika ngazi mbalimbali za elimu; na kujenga miundombinu ya chuo ikiwemo ofisi ndogo, jengo la mhadhara lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200 na nyumba ya mtumishi;

### 3.7.10 Shirika la Elimu Kibaha

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Shirika la Elimu Kibaha limepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Kutoa elimumsingi kwa wanafunzi 3,141 na elimu ya sekondari kwa wanafunzi 329;

(ii) Kukamilisha, kuandaa na kusimamia mfumo wa mafunzo kwa njia ya mtandao (*e-learning management system*);

(iii) Kutoa elimu ya sekondari mubashara *(Live teaching)* kwa shule za sekondari nchini;

(iv) Kuboresha utoaji wa elimu kwa wahudumu wa afya 512 katika fani ya utabibu na uuguzi kupitia Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Kibaha (KCOHAS), sambamba na kutoa

elimu ya afya dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza kwa wananchi;

(v) Kutoa elimu na mafunzo ya stadi za ujuzi na ubunifu katika fani za umeme wa majumbani, ufundi wa magari, uundaji na uungaji vyuma, ujenzi (useremala, uashi na bomba), kilimo, mifugo, upishi, na ushonaji kwa vijana 400 kwa kozi za muda mrefu na wananchi 1,000 kwa kozi za muda mfupi kwa mafunzo ya ana kwa ana na kwa njia ya mtandao (*e-learning*); na

(vi) Kuendelea na ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha.

**3.7.11 Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa**

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa katika mwaka 2024/25 imepanga kutekeleza yafuatayo; -

(i) Kukusanya marejesho ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.25;

(ii) Kukusanya michango yenye thamani ya shilingi bilioni 2.62;

(iii) Kutoa mikopo kwa halmashauri zitakazokidhi vigezo vya kukopeshwa na kufanya uwekezaji kwenye taasisi za fedha ambapo jumla ya shilingi bilioni 4.13 zitatumika;

(iv) Kukamilisha mapitio ya sheria ili kuboresha utendaji wa bodi;

(v) Kutoa mafunzo kwa ajili ya kuboresha usimamizi na utoaji wa mikopo katika mamlaka za serikali za mitaa; na

(vi) Kuweka mikakati ya kuboresha mtaji na maandiko katika taasisi na mashirika ya maendeleo.

**3.7.12 Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Namba 02)**

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Tume ya Utumishi wa Walimu imepanga kutumia shilingi bilioni 20.74 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo katika maeneo yafuatayo: -

(i) Kusimamia ajira, maadili na maendeleo ya walimu kwa kuhakikisha kwamba walimu wanasajiliwa, wanathibitishwa kazini na kwa wale wenye sifa wanapandishwa vyeo na kubadilishiwa kada kwa wakati;

(ii) Kusimamia maadili na nidhamu kwa walimu wa shule za msingi na sekondari katika utumishi wa umma;

(iii) Kufanya utafiti na kutathmini hali ya walimu nchini na kubainisha aina na mahitaji ya walimu, idadi na ngazi ya walimu wanaohitajika;

(iv) Kukamilisha utengenezaji wa mfumo wa TSCMIS, usimikaji wa miundombinu ya mtandao wa intaneti katika ofisi 115 za wilaya; na

(v) Kuendelea na ujenzi wa jengo la ofisi ya tume makao makuu.

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii kuwaelekeza waheshimiwa wakuu wa mikoa kuwasimamia wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:

(i) Kuhakikisha ukusanyaji wa mapato uliolengwa unafikiwa kwa asilimia 100 ikiwemo ukusanyaji wa kodi za majengo;

(ii) Kusimamia uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2024;

(iii) Kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya afya ya msingi, elimumsingi na sekondari kulingana na mipango iliyowekwa;

(iv) Kuimarisha vyanzo vikuu vya mapato kwa ajili ya kuchachua uchumi kama ilivyobainishwa katika mpango na bajeti wa halmashauri husika;

(v) Kujenga vituo vipya vya polisi kata 12 na kukamilisha ujenzi wa vituo vya polisi kata 77;

(vi) Kukamilisha ujenzi wa ofisi za vijiji/mitaa angalau tano (05) kwa kila halmashauri; na

(vii) Kutenga maeneo kwa ajili ya kujenga shule za maadilisho zitakazojengwa katika kila mkoa shule moja (1).

Aidha, kila halmashauri itapimwa utekelezaji wa vipaumbele hivi kwa kuzingatia mchanganuo wa miradi iliyoidhinishwa na kutengwa katika bajeti ya 2024/25 kwa kila robo mwaka.

**192.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetoa utekelezaji wa mpango na bajeti wa mwaka 2023/24 na kuainisha mpango na bajeti wa mwaka 2024/25 kwa mafungu 28 ambao umechangiwa na fedha kutoka serikali kuu, mamlaka za serikali za mitaa na washirika wa maendeleo wakiwemo: Benki ya Dunia (WB), UNICEF, Global Fund, Twiga Barrick Tanzania, EU, JICA, KOICA, GiZ, UNCDF, CDC, USAID, SIDA, UNDP, UNFPA, UN Women, Carbon Tanzania, UNEP, WHO, AfDB, WWF, FCDO, DANIDA, CANADA, SDC SWISS, Serikali ya Shirikisho la Ujerumani, Global Facility Financing na GAVI.

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, ninawashukuru watendaji wote ngazi za msingi bila kusahau wenyeviti wa vitongoji, vijiji na mitaa, watendaji wa mitaa na vijiji, watendaji wa kata, maafisa tarafa, waheshimiwa madiwani, wakuu wa idara na vitengo, wakurugenzi, wakuu wa wilaya, makatibu tawala wa wilaya na mikoa, wakuu wa mikoa na watumishi wote wa tawala za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kwa utendaji kazi wao mzuri.

**194.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru sana wananchi wa jimbo langu la Rufiji kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya kitaifa na jimbo na kuniombea kila siku. Ninaahidi kuendelea kuwatumikia na kushirikiana nao kila hatua katika kuleta maendeleo ya jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

**195. *Mheshimiwa Spika,*** kipekee, ninaishukuru kwa dhati familia yangu kwa upendo wao, uvumilivu na maombi yao wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yangu ya kitaifa. Ninawashukuru kwa kusimama nami katika safari hii ya kuleta maendeleo ya Taifa letu.

### 3.7 Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2024/25 ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI

### 3.8.1 Maduhuli na Makusanyo ya Mapato ya Ndani

**196. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, taasisi zilizo chini yake, mikoa 26 ikijumuisha halmashauri 184 inaomba idhini ya kukusanya maduhuli na mapato ya ndani jumla ya shilingi trilioni moja, bilioni mia sita na moja, milioni arobaini na nne, mia tano tisini na tano elfu, na mia tisa tisini (shilingi 1,601,044,595,990.00). Mchanganuo wa makusanyo ya mapato hayo ni kama inavyooneshwa kwenye ***Jedwali Na. 1***

***Jedwali Na. 1*: Maduhuli na Mapato ya Ndani kwa Mwaka 2024/25**

| OFISI/TAASISI | MAKADIRIO (Shilingi) |
|---|---:|
| Ofisi ya Rais - TAMISEMI | 188,960,306,000.00 |
| Taasisi | 55,427,686,590.00 |
| Mikoa | 315,939,400.00 |
| Halmashauri | 1,356,340,664,000.00 |
| **JUMLA KUU** | **1,601,044,595,990.00** |

### 3.8.2 Makadirio ya Mapato na Matumizi

**197. *Mheshimiwa Spika,*** sasa naomba Bunge lako likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2024/25 yenye jumla ya shilingi trilioni kumi, bilioni mia moja ishirini na tano, milioni mia mbili ishirini, mia nne na tatu elfu, mia moja sitini na saba (shilingi 10,125,220,403,167.00) kwa ajili ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI Fungu Namba 56, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Namba 02 na Mafungu 26 ya mikoa yanayojumuisha halmashauri 184.

**198. *Mheshimiwa Spika,*** kati ya fedha zinazoombwa, shilingi trilioni sita, bilioni mia saba na tisa, milioni mia tisa sabini na tano,

mia moja themanini na nane elfu mia tano (shilingi 6,709,975,188,500.00) ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida yanayojumuisha mishahara shilingi trilioni tano, bilioni mia tano ishirini na nne, milioni mia sita na thelathini na sita, sitini na sita elfu (shilingi 5,524,636,066,000.00) na matumizi mengineyo shilingi trilioni moja, bilioni mia moja themanini na tano, milioni mia tatu thelathini na tisa, mia moja ishirini na mbili elfu mia tano (shilingi 1,185,339,122,500.00).

**199.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya shilingi trilioni tatu, bilioni mia nne kumi na tano, milioni mia mbili arobaini na tano, mia mbili kumi na nne elfu, na mia sita sitini na saba (shilingi 3,415,245,214,667.00) zinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo kati ya fedha hizo shilingi trilioni mbili, bilioni mia mbili sitini na tisa, milioni mia nane na thelathini, mia nne sitini na nne elfu (shilingi 2,269,830,464,000.00) ni fedha za ndani na shilingi trilioni moja, bilioni mia moja arobaini na tano, milioni mia nne kumi na nne, mia saba  na hamsini elfu, mia sita na sitini na saba (shilingi 1,145,414,750,667.00) ni fedha za nje *(Mchanganuo wa fedha zinazoombwa katika mwaka 2024/25 umeoneshwa katika Jedwali Na. 2).*

**200.** ***Jedwali Na. 2*: Muhtasari wa Mpango wa Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI Mwaka 2024/25**

| Maelezo | Bajeti 2024/25 |
|---|---|
| **Matumizi ya Kawaida** | |
| **Mishahara** | |
| Makao Makuu | 10,924,055,000.00 |
| Taasisi | 62,571,116,000.00 |
| Tume ya Utumishi wa Walimu | 9,852,421,000.00 |
| Mikoa | 80,181,418,000.00 |
| Halmashauri | 5,361,107,056,000.00 |
| **Jumla ndogo** | **5,524,636,066,000.00** |
| | |
| **Matumizi Mengineyo** | |
| Makao Makuu | 28,558,997,500.00 |
| Taasisi | 3,025,634,500.00 |
| Tume ya Utumishi wa Walimu | 7,424,690,000.00 |

| Maelezo | Bajeti 2024/25 |
|---|---|
| Mikoa | 108,336,127,500.00 |
| Halmashauri – SK | 222,928,867,000.00 |
| Halmashauri – OS | 815,064,806,000.00 |
| **Jumla Ndogo** | **1,185,339,122,500.00** |
| **Jumla Matumizi ya Kawaida** | **6,709,975,188,500.00** |
| **Matumizi ya Maendeleo** | |
| **Ndani** | |
| Makao Makuu | 35,517,688,000.00 |
| Taasisi | 710,776,035,000.00 |
| Tume ya Utumishi wa Walimu | 440,359,000.00 |
| Mikoa | 79,578,865,000.00 |
| Halmashauri – SK | 902,241,659,000.00 |
| Halmashauri – OS | 541,275,858,000.00 |
| **Jumla Ndogo** | **2,269,830,464,000.00** |
| **Nje** | |
| Makao Makuu | 131,710,307,000.00 |
| Taasisi | 126,851,150,000.00 |
| Tume ya Utumishi wa Walimu | 3,024,631,667.00 |
| Mikoa | 29,717,952,000.00 |
| Halmashauri | 854,110,710,000.00 |
| **Jumla Ndogo** | **1,145,414,750,667.00** |
| **Jumla Maendeleo** | **3,415,245,214,667.00** |
| **Jumla Kuu** | **10,125,220,403,167.00** |

**201.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na hotuba hii, yapo majedwali ambayo yanafafanua kwa kina makadirio na makusanyo ya mapato ya ndani ya halmashauri na mgawanyo wa mapato ya ndani yasiyolindwa kwenye miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida ambayo ni sehemu ya hotuba hii.

**202.** ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba hii inapatikana pia kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI ambayo ni www.tamisemi.go.tz.

**203.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana hoja imekubaliwa kwa sasa, nimwite sasa Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Bunge Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo. *(Makofi)*

**MHE. DENNIS L. LONDO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye imempendeza yeye kwa niaba ya Kamati kuwasilisha kwako Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea na taarifa hii naomba Taarifa yangu yote iingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha kwako Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge, TAMISEMI kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na muundo wa taarifa, taarifa hii imegawanyika katika Sehemu kuu nne: -

(a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya awali, muundo wa taarifa na msingi wa Kamati kuripoti Bungeni matokeo ya uchambuzi wake;

(b) Sehemu ya pili inayobainisha uchambuzi wa Kamati kuhusu hali ya utekelezaji wa bajeti, mipango iliyopo kwa mwaka

wa fedha 2024/2025 na uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(c) Sehemu ya tatu ambayo inabainisha maoni ya Kamati na ushauri kutokana na maoni hayo; na

(d) Sehemu ya nne inayohitimisha na kubainisha msimamo wa Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuhusu msingi wa makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hii kuwa yamefanyiwa uchambuzi na Kamati ya Bunge - TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kumi na Nne ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 imeweka masharti kuhusu utaratibu wa bajeti za Wizara ikiwemo Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kufanyiwa kazi na Bunge leko Tukufu. Miongoni mwa masharti hayo ni bajeti hiyo kufanyiwa uchambuzi na Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Naomba kulijulisha Bunge hili kuwa Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kama ilivyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024; Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 iliitaka Kamati kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Katika mwaka huo, Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi 3,485,999,641,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukaguzi wa miradi Kamati ilitembelea miradi ya elimu, miradi ya afya na miradi ya barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* ambapo jumla ya miradi 13 ilitembelewa katika mikoa ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro na Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya ukaguzi na uchambuzi wa hali ya utekelezaji wa miradi hiyo umeainisha mambo yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu upangaji wa miradi kwa awamu; baadhi ya miradi imekuwa ikitekelezwa kwa vipinde na kwa awamu hali ambayo inapelekea utaratibu huu kusababisha gharama isiyoendana na thamani halisi ya fedha zinazotumika, kwa mfano mradi wa matengenezo ya barabara ya Nakwa katika Mkoa wa Manyara yenye urefu wa kilometa tisa kwa kiwango cha lami ambao umepangwa kutekelezwa katika awamu zaidi ya tano; katika awamu hii unajengwa kwa urefu wa kilometa 0.7. Hali hii inachelewesha upatikanaji wa tija mradi huo na matokeo chanya ya kiuchumi na kijamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ina jukumu la kusimamia, kupanga na kumilikisha ardhi, lakini pia suala la mipango miji. Miongoni mwa mambo ambayo tumeyaona kama Kamati ni uzingatiaji wa matumizi bora ya ardhi iliyopo hasa katika maeneo ya majiji, manispaa na halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukaguzi wa Kamati ilibaini kuwa ipo baadhi ya miradi katika sekta ya elimu na afya ambayo inatekelezwa bila kuzingatia uhaba wa ardhi uliopo. Kwa mfano, miradi ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje *(OPD)* na jengo la maabara katika Hospitali ya Wilaya ya Arusha. Majengo haya yanajengwa chini kwa msawazo ingawa eneo la ardhi katika hospitali hiyo haliwezi kuongezeka, tunaweza kuona mifano mingine kwa mfano Shule ya Bunge pale katikati ya mji ambapo kuna madarasa ambayo yanajengwa ya chini ukiangalia thamani ya ardhi haifanani na thamani ya jengo ambalo limekaa juu ya ardhi hiyo. Hali hii itasababisha ugumu wa utekelezaji wa miradi siku zijazo kutokana na uwezekano wa kukosekana kwa ardhi katika maeneo ya katikati ya miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati imegundua kuwa kuna changamoto ya ulipaji na mifumo ya ulipaji katika miradi ambayo inaendelea. Utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo inafanyika sambamba na malipo yanayostahili. Kwa upande wa

Ofisi ya Rais, TAMISEMI malipo hufanyika kwa mfumo wa *MUSE* na katika baadhi ya miradi imebainika kuwa kuna wakati malipo yaliyostahili yalikwama kutokana na changamoto za mfumo wa *MUSE,* jambo ambalo lilisababisha ucheleweshaji wa utekelezaji wa mradi mbalimbali n akwa mfano wa mradi uliokwama kutokana na changamoto hiyo ni ujenzi Hospitali ya Wilaya ya Meru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ina maoni kuwa mambo hayo ambayo yanaathiri tija ya miradi inayokusudiwa kwenye miradi inahitaji kutatuliwa hasa katika mwaka huu wa fedha ambao tunaanza kwa mazingatio ya miradi mipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati iliangalia suala zima la uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2023/2024 katika utekelezaji wa bajeti hii ambayo tunaijadili leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti kwenye Kamati ulifanyika sambamba na kujiridhisha iwapo ushauri uliotolewa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ulizingatiwa. Lengo ni kutafakari utoaji wa maoni na ushauri kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kulingana na uzingatiaji wa maoni na ushauri kwa mwaka wa fedha uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati ilitoa maoni na kushauri katika maeneo 16 ya utekelezaji wa bajeti hii. Naomba kusema kwamba maelezo yaliyowasilishwa na Serikali yalionesha kwamba Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati. Uchambuzi wa maelezo hayo umedhihirisha kuwa sehemu kubwa ya ushauri umefanyiwa kazi na sehemu nyingine inaendelea kuzingatiwa. Maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wa maoni yanapatikana kwenye Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa mezani kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa bajeti; hali ya ukusanyaji wa mapato ni sehemu ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Kamati ilizingatia hotuba ya Waziri

wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, aliyoitoa Bungeni tarehe 14 Aprili, 2023 akiwasilisha makadirio ya ofisi hiyo kwa ajili ya kupitishwa na Bunge. Katika hotuba hiyo jumla ya shilingi trilioni 1.1 zililengwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Ili kulisaidia Bunge kufuatilia utekelezaji wa jambo lliloelezwa Kamati ililinganisha makusanyo halisi na lengo lililokuwa limebainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulijulisha Bunge lako tathmini ya hali ya ukusanyaji wa mapato iliyobainika ni kama ifuatavyo: -

(i) Jumla ya kiasi cha fedha zilizokusanywa hadi kufikia mwezi Februari, 2024 ni shilingi bilioni 756.48 sawa na asilimia 63.8 ya lengo. Mwenendo huo unaashiria uwezekano wa kufikiwa kwa lengo, jambo ambalo linaonesha ufanisi na upangaji unaozingatia hali halisi; na

(ii) Uwiano wa mchango wa makusanyo ya maduhuli kutoka makao makuu ya Wizara na taasisi zake ikilinganishwa na mchango wa mikoa 26 na halmashauri 184 nchini unatofautiana na uwiano halisi wa makusanyo. Uwiano wakati wa makadirio ulikuwa ni asilimia nne kwa asilimia 96 za mchango wa Wizara na Taasisi zake na mikoa na halmashauri zote mtawalia. Uwiano wa hali halisi umekuwa asilimia mbili kwa asilimia 98 mtawalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa matokeo hayo ni dhahiri kuwa kuna uwezekano mkubwa wa lengo la maduhuli kuwa limetokana na hali halisi, kwa sababu hakuna tofauti ya uwiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uwezekano mkubwa wa makusanyo halisi kuzidi kidogo lengo lililowekwa, kwa kuwa makusanyo makubwa yalipatikana kabla ya kufikia mwisho wa robo ya tatu ambayo ni mwisho wa mwezi Machi, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya upatikanaji wa fedha; kwa mujibu wa Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge

imeweka sharti la kufanya uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa kulinganisha hali halisi ya mwaka unaotangulia. Kamati ilichambua kwa mtazamo huo na kubaini yafuatayo: -

(i) Jumla ya fedha iliyopokelewa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI hadi kufikia mwezi Februari, 2024 ni sawa na asilimia 68 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Kwa mwenendo huo kuna uwezekano wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupata kiasi chote cha bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Ikiwa hivyo, majukumu na mipango yote iliyopangwa ina mwelekeo wa kukamilishwa kwa wakati.

(ii) Uwiano wa bajeti ulioidhinishwa na Bunge lako umeonesha kuwa makao makuu ya Wizara – Ofisi ya Rais, TAMISEMI na taasisi zake zingepata asilimia 12 ya bajeti ya ofisi hii, na mikoa 26 Tanzania Bara na halmashauri 184 ingepata asilimia 86.6 ya bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Hali halisi ya upatikanaji wa fedha imebainisha uwiano tofauti na uliopitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwiano wa bajeti ya maendeleo kwa bajeti ya matumizi ya kawaida wakati Bunge lilipopitisha makadirio ni tofauti kidogo na uwiano wakati wa utekelezaji. Uwiano wa bajeti ya maendeleo kwa makao makuu ya Wizara na taasisi zake ukilinganishwa na bajeti ya maendeleo kwa mikoa na halmashauri zote nchini unatofautiana na uwiano halisi wa kiasi cha fedha kutoka Hazina kwa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na taasisi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi Kamati ilibaini kuwa upatikanaji wa fedha na majukumu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI makao makuu na taasisi zake ni mzuri zaidi ya upatikanaji wa fedha kwa Sekretarieti za Mikoa na halmashauri nchini ilhali makao makuu ni waratibu na Sekretarieti za Mikoa na halmashauri ni watekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya utekelezaji wa mipango kwa mwaka wa fedha 2023/2024; utekelezaji wa mpango wa Wizara na taasisi yoyote kwa mwaka wa fedha

unaoisha ni kigezo muhimu cha kupanga kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa kuzingatia hayo na kwa msingi huo kabla ya kuchambua makadirio ya mapato na matumizi Kamati ilichambua hali ya utekelezaji wa mpango wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Katika uchambuzi huo miongoni mwa mipango ilihusu ukamilishaji wa Sera ya Taifa ya Ugatuaji, Programu ya Kuimarisha Mikoa na usanifu wa mifumo ya TEHAMA katika ngazi zote za Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kamati imebaini kuwa mambo hayo yanaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa mpango kwa mwaka wa fedha 2024/2025; uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi unazingatia mipango ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Ili kukidhi mantiki ya Bunge kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kuna vipaumbele 12 ambavyo vipo katika mipango ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kama ilivyowasilishwa mezani kwako na kimsingi kama inaona kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI inatekeleza kwa vigezo vya vipaumbele hivyo 12, kwa mfano kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia na ushirikishwaji wa wananchi, Sera ya Ugatuaji wa Madaraka *(D by D)* pamoja na kusimamia mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato. Mipango inahusiana moja kwa moja na majukumu ambayo yameainishwa, kwa mfano mipango hiyo haikujitokeza waziwazi katika mipango ambayo inakususdiwa ama mwendelezo wake katika bajeti ya 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mipango iliyotekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 imeendelea kujitokeza kwa mwaka wa fedha 2024/2025; na baadhi ya mipango inayojitokeza kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni mipya na haikuwepo katika mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025; tija na manufaa ya mipango yoyote ya kuboresha shughuli za jamii ambazo kwa kiasi kikubwa zinategemea makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali ili kujiridhisha na uwezekano wa manufaa kwa umma yanayoweza kupatikana kwa mwaka wa fedha. Kamati imechambua makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais,

TAMISEMI. Uchambuzi huo umehusisha kutathmini mambo makuu matatu ambayo ni makadirio ya mapato, makadirio ya matumizi ya kawaida na makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo. Ufafanuzi wa matokeo ya uchambuzi ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uchambuzi wa maduhuli; Kamati imezingatia uhusiano uliopo kati ya uendeshaji wa shughuli za umma, ukusanyaji wa maduhuli na uwiano wa mapato wa matumizi. Kwa msingi huo uchambuzi ulifanyika kwa kulinganisha na makadrio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha ulioisha, hali halisi ya ukusanyaji wa maduhuli hadi kufikia mwezi Februari, 2024 na lengo la Serikali kuhusu ukusanyaji. Matokeo ya uchambuzi yameonesha kwenye taarifa ya Kamati iliyowasilishwa mezani kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa makadirio ya matumizi ya kawaida; uendeshaji wa shughuli za umma unategemea bajeti ya matumizi ya kawaida. Aidha, mahitaji ya kibajeti ya shughuli za uratibu hayalingani na mahitaji ya shughuli za utekelezaji. Kwa misingi hiyo Kamati ilichambua ili kujiridhisha na tofauti zinazotakiwa. Uchambuzi umebanisha yafuatayo: -

(a) Bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezeka kwa asilimia 19.4 ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(b) Matumizi ya kawaida ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na taasisi zake yameongezeka kwa asilimia tisa wakati bajeti ya matumizi ya kawaida *(recurrent)* kwa Sekretarieti za Mikoa 26 na Halmashauri 184 imeongezeka kwa asilima 19.6; na

(c) Ongezeko la bajeti ya matumizi ya kawaida linaendana na nyongeza ya vipaumbele vya mpango wa bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa makadirio ya bajeti ya maendeleo; utekelezaji wa miradi ya maendeleo

unatarajiwa kusaidia huduma kwa jamii kwa muda mrefu. Utekelezaji huo unategemea bajeti inayopitishwa na Bunge lako. Aidha, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na taasisi zake zinatekeleza baadhi ya miradi pamoja na kusimamia utekelezaji wa miradi katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Uchambuzi wa bajeti ya miradi ya maendeleo umebainisha mambo yafuatayo: -

(a) Kwa ujumla bajeti ya miradi ya maendeleo imepungua kwa asilimia mbili kwa mwaka 2023/2024 ikilinganishwa na bajeti ya maendeleo kwa mwaka huu wa fedha;

(b) Bajeti ya mandeleo kwa makao makuu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na taasisi zake imeongezeka kwa asilimia mbili; na

(c) Bajeti ya miradi ya maendeleo kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa imepungua kwa asilimia 3.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI yameongezeka kutokana na hali halisi ya baadhi ya miradi. Kamati imeridhishwa na makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri na Kamati; maelezo ya jumla; lengo la uchambuzi uliowekewa utaratibu na Kanuni za Kudumu za Bunge ni kuwezesha upatikanaji wa maoni na ushauri. Naomba kulishauri Bunge lako Tukufu lijadili makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kama unavyofafanuliwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na matokeo ya uchambuzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ukusanyaji wa maduhuli, upatikanaji wa fedha zilizoidhinisha na Bunge na vipaumbele vilivyobainishwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI Kamati inashauri mambo mbalimbali ya kuzingatiwa wakati wa

utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, baada ya uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Kamati inashauri kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, umaliziaji wa maboma ya shule na zahanati; katika kufanikisha ujenzi wa majengo mbalimbali nchini, wananchi wamejitolea kujenga majengo mengi kwa ajili ya shule na zahanati kwa ajili ya huduma za umma. Ujenzi huo ulifanyika kwa nguvu za wananchi umefikia hatua ya upauaji, lakini haujaendelezwa kinyume na maelekezo kwamba nguvu za wananchi ziishie kwenye *linter* na Serikali itamalizia kwa sababu hiyo, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Serikali itekeleze ushauri wa Kamati ulitolewa wakati wa uwasilishaji wa maoni ya Kamati kuhusu Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka 2023/2024;

(ii) Serikali itoe mwongozo na kuweka uratibu stahili katika uanzishwaji wa ujenzi wa majengo ya aina kwa nguvu za wananchi ili kupunguza ujenzi holela wa maboma na kudhibiti viwango vya ujenzi wa maboma ya majengo ya Serikali katika maeneo mbalimbali ya halmashauri zetu; na

(iii) Serikali kuzingatia ombi maalum la kibajeti lililowasilishwa na Kamati kwa Serikali kuhusu umaliziaji wa maboma hayo kupitia bajeti hii ambayo inawasilishwa kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni fedha kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu ya barabara iliyoharibiwa na mvua ambazo zinazoendelea nchini; katika kipindi cha mwaka 2023/2024 Serikali ilitenga zaidi ya shilingi trilioni moja kwa ajili ya *TARURA*. Fedha hizi zilikuwa ni nyingi na ni ongezeko ambalo limeleta matumaini kwa wananchi wetu pamoja na Bunge lako. Hata hivyo, upelekaji wa fedha hizo ulifikia 45.7%. Pamoja na kazi nzuri ambayo inafanywa na *TARURA* upelekaji wa fedha kwa *TARURA* hauridhishi na hautoiwezesha kutekeleza miradi yake kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia mwishoni mwa mwaka 2023 hadi sasa nchi imekumbwa na uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara katika maeneo mbalimbali. Hali hii imesababisha barabara nyingi hasa za vijijini kutokupitika kabisa, madaraja kusombwa na vivuko kuharibiwa. Kutokana na uharibifu huo imesababisha huduma mbalimbali za usafiri kwa wananchi kuwa ngumu. Kutokana na hali hiyo Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeweka mkakati wa kuzirejesha barabara hizo katika hali yake ya kawaida kwa kuitumia wakala *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, azma ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni kusimamia miradi ya ujenzi wa barabara na miundombinu inayoendana na barabara hizo. Inaweza kufanikiwa kwa kuongeza fedha kwa Wakala wa Barabara - *TARURA*. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuzingatia ushauri wa Kamati uliotolewa kwa Bunge lako wakati wa bajeti lililopita, na hata sasa tunarudia tena pamoja na hayo, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali kupeleka fedha *TARURA* kikamilifu na kwa wakati kuzingatia bajeti ambayo imepitishwa na Bunge lako; na

(ii) Serikali kutoa bajeti ya dharura kwa kuzingatia ombi maalum la Kamati lililotolewa kwa Serikali kwa ajili ya kusaidia urejeshaji wa miundombinu hiyo ili kurejesha hali ya kawaida kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna suala la ushirikishwaji na uwezeshaji wa wakandarasi wazawa katika utekelezaji wa miradi wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI; katika orodha ya vipaumbele vya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ushirikishwaji wa wananchi ni jambo lililopewa uzito. Aidha, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imepanga kuratibu na kusimamia miradi ya ujenzi katika ngazi zote za Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vikao kati ya Kamati na Ofisi ya Rais, TAMISEMI Kamati imebaini kuwa kwenye miradi mikubwa hasa ya miundombinu ya barabara, Serikali imekuwa ikitumia wakandarasi ambao siyo wazawa na hivyo kuwanyima

wakandarasi wazawa fursa ya utekelezaji na uwezeshaji kupitia miradi hiyo. Aidha, wakandarasi wengi wazawa huwa na mitaji midogo ambayo inaonekana kutotosheleza utekelezaji wa miradi inayoratibiwa na Serikali kutokana na ugumu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo Kamati inashauri kuwa kipaumbele cha kutoa wakandarasi wazawa kizingatiwe sambamba na kuzielekeza halmashauri nchini kuwatumia wakandarasi wazawa, lakini bila kuathiri viwango stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishaji wa shule za msingi zenye michepuo ya kingereza; katika mpango wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI unaohusu kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma za jamii yapo mambo ya msingi yanayopaswa kuzingatiwa. Msimamo wa Serikali kuhusu huduma hizo ni jambo muhimu. Katika uchambuzi wa Randama za Ofisi ya Rais, TAMISEMI Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa maoni ya Kamati kuhusu uanzishwaji wa shule za mchepuo wa kiingereza yaliyotolewa katika taarifa yake wakati Bunge linapitisha bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI Aprili, 2023 hayakueleweka vizuri katika utekelezaji wake. Kwa ujumla Kamati inaona kuwa kuanzishwa kwa shule hizi kutaleta matabaka kwa Watanzania na kwenda kinyume na Sera ya Elimu ya mwaka 2024 Toleo la 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo Kamati inashauri kuwa Serikali izingatie ushauri wa Kamati juu ya utoaji wa elimu kwa kuzingatia usawa na kuimarisha ufundishaji wa somo la kiingereza katika shule zake zote. *(Makofi)*

Mhesimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Wajibu wa Wadau wa Miradi ya Mendeleo Kurudisha Faida kwa Jamii *(CSR);* katika uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya 2023/2024 Kamati ilibaini kuwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekuwa zikipata fedha kutoka kwa watekelezaji wa miradi mbalimbali kama sehemu ya uwajibikaji wa taasisi na kampuni zinazotekeleza miradi hiyo kwa jamii *(Cooperate Social Responsibility)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Kamati imebaini kuwa miongozo ya matumizi ya fedha hizo bado haileti tija inayotarajiwa kwa wananchi. Aidha, Kamati imebaini kuwa hakuna mwongozo kwa halmashauri ya namna ya kuwatambua wadau wanaotekeleza miradi ya maendeleo kwa kuwa miradi mingi inayotekelezwa na wadau mbalimbali wa maendeleo bila wadau hao kupata fursa ya kurejesha faida kwa jamii. Kamati pia imebaini kuwa katika baadhi ya maeneo wadau hao wamekuwa wakiratibu na kutekeleza miradi hiyo wenyewe bila ya usimamizi na uratibu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo Kamati inashauri utekelezaji wa miradi hiyo uende sambamba na kusimamia utaratibu wa wajibu wa wadau hao katika kurejesha faida kwa jamii. Kutokana na hilo Kamati inashauri ifuatavyo: -

(i) Utekelezaji wa miradi hiyo ulizingatie sheria, miongozo, kanuni na utekelezaji wa miradi kwa mujibu wa kanuni za Serikali;

(ii) Usimamizi wa gharama za miradi ya fedha zinazotokana na *CSR* ufanywe kwa kufuata kanuni na taratibu za manunuzi za Serikali ili kuepuka gharama kubwa za miradi hiyo; na *(Makofi)*

(iii) Halmashauri zibainishe taasisi zake zote za kibiashara katika maeneo yake ambazo zinapaswa kutoa *CSR* na kuhakikisha kuwa taasisi hizo zinarejesha faida kwa jamii kama kanuni na sheria zinavyowataka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya halmashauri kutokana na biashara ya *carbon,* kwa kuzingatia mpango wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI wa kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato, halmashauri zimekuwa zikibuni vyanzo mbalimbali vipya vya mapato; katika vikao vya kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI Kamati ilibaini kuwa kuna chanzo cha biashara ya *carbon* kinachoziingizia mapato ya kutosha halmashauri chache ambacho bado

hakijagunduliwa ama hakijaangaliwa kwa ukaribu wake na halmashauri nyingine. Kutokana na hilo Kamati inashauri ifuatavyo:-

(i) Serikali ihakikishe kuwa eneo la biashara ya *carbon* lipewe kipaumbele kama chanzo muhimu cha mapato kwa halmashauri zote ambazo zina utajiri wa misitu;

(ii) Ofisi ya Rais, TAMISEMI ijenge uwezo wa kitengo kinachosimamia biashara ya *carbon* ili kuweza kutoa ushauri wa kitaalam kwa halmashauri nchini ambazo zina utajiri wa misitu; na

(iii) Serikali za vijiji na halmashauri zipime maeneo na kumilikishwa maeneo hayo kwa mujibu wa *GN* ambazo zinatangaza maeneo ya vijiji hivyo kama hatua ya kuweza kuhifadhi na kuitunza misitu ili iweze kuwanufaisha katika biashara ya *carbon.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utunzaji wa mazingira katika halmashauri; kwa kuwa kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato ni sehemu ya lengo la Ofisi ya Rais, TAMISEMI, uboreshaji wa mazingira ni sehemu muhimu katika kuziwezesha halmashauri kujiongezea kipato kutokana na mazingira kuweza kuwa kama chazo cha mapato kwa ajili ya biashara ya *carbon.* Kutokana na hiyo Kamati inashauri ifuatavyo:-

(i) Serikali ianzishe programu maalum katika shule za msingi na sekondari nchini kwa kila mwanafunzi anayeanza shule kupanda na kuutunza mti wake wakati wa maisha yake yote akiwa shuleni hapo; *(Makofi)*

(ii) Mashirika yanayotoa misaada ya kupanda miti yaelekezwe kujikita kwenye ujenzi wa miundombinu ya utunzaji wa miti hiyo; na *(Makofi)*

(iii) Halmashauri nchini zielekezwe kuweka sheria ndogo *(by laws)* kwa ajili ya kusimamia wajibu wa wananchi

kupanda miti na kuitunza kwenye maeneo yao ya makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhuishaji wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali, Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Sheria ya Manunuzi ya Umma; Kamati bado imebaini kwamba kuna uvujaji wa mapato katika halmashauri kote nchini, jambo hili linafanywa na watendaji wachache wasiowaaminifu, pamoja na hatua nzuri ambazo Ofisi ya Rais, TAMISEMI inachukua, bado tunatoa rai kwao kuendelea kusimamia uvujaji na kusimamia nidhamu ya watendaji wachache wasiowaaminifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali na Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Sheria ya Manunuzi ya Umma zimeweka masharti ambayo ni magumu kutekelezeka katika ngazi mbalimbali za mamlaka kwa mfano upatikanaji wa *EFD machine* kwa huduma kama mazishi ama vyakula zinazotokea katika maeneo ya vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa malengo ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka 2024/2025 ni kuratibu utoaji wa huduma kwa jamii; Kamati imebaini kuwa hoja nyingi za ukaguzi za *CAG* zinatokana na sheria hizo kutokuwa na uhalisia katika utekelezaji wake katika Serikali za Mitaa. Sheria hizo zimeleta changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali za Mitaa katika ngazi za vijiji na kata hivyo, kuzalisha hoja nyingi ambazo zinazua taharuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati katika uchambuzi wake ilibaini kuwa pamoja na utoaji huduma kwa kipindi chote hiki kuwa na mafanikio utekelezaji wa shughuli za Serikali umekuwa ukiathiriwa na mambo tuliyataja hapo juu. Kutokana na ugumu wa utekelezaji kwa kufuata sheria hizi imebainika kuwa halmashauri zimekuwa zikikutana na hoja nyingi za kihasibu kutoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili utekelezaji wa bajeti inayoombwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI izingatie uhalisia katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Kamati inashauri kuwa Sheria ya

Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sheria ya Matumizi ya Fedha za Umma pamoja na Sheria ya Manunuzi ya Umma zinahitaji kuhuishwa ili ziendane na mazingira halisi na changamoto ya utekelezaji wa shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa hasa katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taasisi za Serikali zinazofanya kazi na halmashauri kuzingatia bajeti za halmashauri; wakati wa uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka 2023/2024 katika utekelezaji wa bajeti za halmashauri Kamati ilibaini kuwa zipo taasisi ama Wizara za Serikali ambazo bajeti zake zitapita hapa na kalenda zao za mwaka zinajadiliwa ndani ya Bunge lako zimekuwa zikiandaa mikutano, warsha na semina na zikiwataka wataalam wa halmashauri mbalimbali nchini kuja kushiriki semina na mikutano hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barua za mialiko zimekuwa zikiwaelekeza Wakurugenzi wa Halmasahuri hizo kugharamia, hali hii imekuwa ikizifanya halmashauri hizo kutumia fedha ambazo hapo awali hazikuwa kwenye bajeti hiyo na hivyo, kufanya shughuli nyingine za kibajeti katika halmasahuri hizo kutotekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuelekeza mialiko yote ambayo inatoka katika Wizara na taasisi nyingine inayokwenda kwa wakurugenzi iambatane na taarifa ya walioandaa makongamano, semina na mikutano hiyo kuonesha wanawajibika vipi kibajeti ili isiathiri shughuli za maendeleo kupitia bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipatia fursa ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya TAMISEMI, lakini pia kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mohamed Omary Mchengewa, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Waheshimiwa Naibu Mawaziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Dkt. Festo

John Dugange pamoja na Mheshimiwa Zainab Katimba kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Ndugu Adolf Ndunguru pamoja na Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati tangu tulipoanza kufanya kazi nao na kushiriki vizuri kwenye uchambuzi wa bajeti ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya TAMISEMI kwa pamoja, kwa ushirikiano mzuri ambao wananipa. Wajumbe hawa ni wachapakazi na wameshiriki kikamilifu katika uchambuzi wa bajeti na kuhakikisha wanahoji kila kitu ili kupata ufafanuzi wa kina. Nawapongeza sana na naomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru watumishi wote wa Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati yetu kutekeleza majukumu yake vyema katika wakati wote ilipokutana ikiwemo wakati wa maandalizi ya Taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na taasisi zake kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia na kwa niaba ya Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu kuu nne kama ifuatavyo:-

(a) Sehemu ya Kwanza inayotoa maelezo ya awali, muundo wa Taarifa na Msingi wa Kamati kuripoti Bungeni Matokeo ya Uchambuzi wake.

(b) Sehemu ya Pili inayobainisha Uchambuzi wa Kamati kuhusu Hali ya Utekelezaji wa Bajeti, Mipango iliyopo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(c) Sehemu ya Tatu ambayo inabainisha maoni ya Kamati na Ushauri kutokana na maoni hayo.

(d) Sehemu ya Nne inayotimisha na kubainisha msimamo wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi

### 1.3 Msingi wa Uchambuzi wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuhusu msingi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kuwa yamefanyiwa uchambuzi na Kamati ya Bunge ya Tawala za

Mikoa na Serikali za Mitaa. Sehemu ya Kumi na Nne ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 imeweka masharti kuhusu utaratibu wa Bajeti za Wizara ikiwemo Bajeti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI, kufanyiwa kazi na Bunge leko Tukufu. Miongoni mwa masharti hayo ni Bajeti hiyo kufanyiwa uchambuzi na Kamati ya Bunge ya Tawla za Mikoa na Serikali za Mitaa. Naomba kulijilisha Bunge hili kuwa, Kamati ilifanya uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais TAMISEMI kama ilivyostahili.

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2023/2024 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2024/2025

### 2.1 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji

#### 2.1.1 Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha Kwa Mwaka Wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, iliitaka Kamati kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa Fedha 2023/2024. Katika mwaka huo, Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya **Shilingi 3,485,999,641,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea miradi ya elimu, miradi ya afya na miradi ya barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA). Miradi iliyotemblewa inatekelezwa katika sehemu mbalimbali za nchi ikiwemo mikoa ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro na Tanga. Jumla ya miradi 13 ilitembelewa katika mikoa hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya ukaguzi na uchambuzi wa hali ya utekelezaji wa miradi hiyo unenesha mambo yafuatayo:-

**(a) Upangaji wa Miradi katika Awamu**

**Mheshimiwa Spika**, Baadhi ya miradi imekuwa ikipangwa kutekelezwa katika vipindi mbalimbali vinavyoitwa awamu. Utekelezaji wa miradi mingi kwa utaratibu wa awamu nyingi za utekelezaji umesababisha gharama isiyoendana na thamani halisi ya fedha zinazotumika. Kwa mfano mradi wa Matengenezo ya Barabara ya Nakwa iliyopo Mkoa wa Manyara yenye urefu wa kilometa 9, kwa Kiwango cha lami ambao umepangwa kutekelezwa katika awamu zaidi ya tano (5); katika awamu hii unajengwa kwa urefu wa KM 0.7. Hali hiyo inachelewesha upatikanaji wa manufaa ya mradi huo kiuchumi na kijamii kwa umma.

**(b) Ujenzi wa Majengo Usioendana na Uhaba wa Ardhi**

**Mheshimiwa Spika**, miongoni mwa mambo ya msingi katika miradi ya ujenzi wa majengo ya umma ni uzingatiaji wa matumizi bora ya ardhi iliyopo. Katika ukaguzi wa miradi inayotekelezwa, Kamati ilibaini kuwa ipo baadhi ya miradi ya ujenzi inayotekelezwa bila kuzingatia uhaba wa ardhi. Kwa mfano, Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Wagonjwa wa Nje (OPD), Ujenzi wa Jengo la X-Ray, Ujenzi wa Jengo la Maabara na Ujenzi wa Jengo la Kuhifadhia Maiti katika Hospitali ya Wilaya ya Arusha umeanza na kuendelea kuwa na majengo ya chini ingawa eneo la ardhi ya Hospitali hiyo haliwezi kuongezeka sambamba na ongezeko la mahitaji kwa siku zijazo.

**Mheshimiwa Spika,** hali hii itasababisha ugumu wa utekelezaji wa miradi siku zijazo kutokana na uwezekano wa kukosekana kwa ardhi.

**(c) Changamoto ya Mfumo wa Ulipaji**

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo hufanyika sambama na malipo yanayostahili. Kwa Upande wa Ofisi ya Rais TAMISEMI, Malipo hufanyika kwa kutumia **Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE).** Katika baadhi ya miradi imebainika kuwa kuna wakati malipo yaliyostahili yalikwama kutokana na changamoto za MUSE kutoweza kutumika kufanya malipo kwa muda mrefu, jambo lililochelewesha utekelezaji wa mradi. Mfano wa mradi uliokwama kutokana na changamoto hiyo ni Ujenzi wa Jengo la

OPD, Ujenzi wa Kichomea Taka, Ujenzi wa Jengo la Maabara na Ukarabati wa majengo ya katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Meru. Hali hiyo inaathiri gharama na kuchelewesha utekelezaji wa miradi.

**Mheshimiwa Spika**, Ufafanuzi zaidi wa hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo unapatikana katika Kiambatisho cha taarifa hii. Kamati ina maoni kuwa, mambo hayo yanayoathiri tija inayokusudiwa kwenye miradi yanahitaji kutatuliwa kwa mwaka huu na kuwa mazingatio kwa miradi mipya.

### 2.1 2 Hatua za Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwenye Kamati ulifanyika sambamba na kujiridhisha iwapo ushauri uliotolewa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ulizingatiwa. Lengo ni kutafakari utoaji wa maoni na ushauri kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kulingana na uzingatiaji wa maoni na ushauri kwa mwaka uliopita.

**Mheshimwa Spika,** wakati wa Kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rasi TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2023/2024, tarehe 14 Aprili, 2023, Kamati ilitoa maoni na kushauri katika maeneo kumi na sita ya utekelezaji wa Bajeti hii.[1] Kwa madhumuni ya kujiridhisha na uzingatiaji wa maoni na ushauri huo, tarehe 18 - 26 Machi, 2024 Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu uzingatiaji wa maoni na ushauri huo.

**Mheshimiwa Spika,** Maelezo yaliyowasilishwa yalionesha kwamba, Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati. Uchambuzi wa maelezo hayo umedhihirisha kuwa, sehemu kubwa ya ushauri imefanyiwa kazi, sehemu nyingine inaendelea kuzingatiwa.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya maeneo 16 yaliyotolewa ushauri, yapo maeneo yaliyozingatiwa ipasavyo na mengine kwa kiwango kisichokamilika. Aidha, yapo maeneo ambayo hayajazingatiwa kabisa. Mfano wa ushauri uliozingatiwa kikamilifu ni kuhusu

[1] Tazama, Taarifa Rasmi za Bunge, Majadiliano ya Bunge ya Tarehe 14 Aprili, 2023.

uanzishaji wa mifumo itakayowezesha uagizaji wa vitendanishi, vifaa tiba na dawa kupitia MSD. Kamati ilishauri kuwa Serikali iweke mifumo hiyo ili kufikia malengo ya Serikali ya kufikisha huduma kwa wananchi kwa haraka na kwa ubora zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** maelezo ya Waziri yalionyesha kuwa TAMISEMI imeweka mfumo maalum ujulikanao kama *Redisigned Integrated Logistic Management Information System (RILS).* Hatua hiyo inatokana na usikivu wa Serikali kwa Kamati. Aidha, TAMISEMI imeahidi kuendelea kuimarisha matumizi ya Mfumo huo uliowezesha vituo vya kutoa huduma za afya kupokea bidhaa ndani ya siku 21 baada ya kuagiza tofauti na awali vilipokuwa vikitumia siku 60 hadi 90.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa ushauri ambao uzingatiaji wake unaendelea ni kuhusu utoaji wa mafunzo ya awali *(Induction)* kwa Watendaji wa Kata na Watendji wa Vijiji. Kamati ilishauri kuwa Ofisi ya Rais TAMISEMI iratibu mafunzo ya awali kwa Watendaji wa Kata na Vijiji ili kuongeza uwajibikaji katika ngazi za vijiji na kata. Taarifa ya Serikali ilionyesha kuwa mafunzo hayo yaliendeshwa kwa Watendaji wa Kata 1,758 kati ya 3956 walioajiriwa. Ushauri huu umeanza kutekelezwa lakini utaendelea kwa mikoa ambayo bado na kwa Watendaji wa Vijiji *(VEO).*

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na juhudi za Ofisi ya Rais TAMISEMI kuzingatia ushauri uliotolewa, bado haijafanikisha utekelezaji wa maeneo machache yaliyotolewa ushauri. Kwa mfano, Kamati ilishauri kuwa Serikali ipeleke fedha za kumalizia maboma ya shule, vituo vya afya na zahanati yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi ili kuondoa hasara inayoweza kupatikana kutokana na kuchakaa kwa majengo haya. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI alieleza kuwa Serikali imefanya zoezi la tathmini za viporo vya maboma hayo. Maelezo hayo ni ishara kuwa fedha hizo hazijapelekwa na kwamba hazijatengwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**2.1.3 Hatua zilizofikiwa katika Utekelezaji wa Bajeti**
**(a) Hali ya Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali**
**Mheshimiwa Spika**, ukusanyaji wa mapato ni sehemu ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Kamati ilizingatia hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, aliyoitoa Bungeni tarehe 14 Aprili, 2023 akiwasilisha Makadirio ya Ofisi hiyo kwa ajili ya kupitishwa na Bunge. Katika Hotuba hiyo, jumla ya **Sh. Trioni 1.19** zililengwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Ili kulisaidia Bunge kufuatilia utekelezaji wa jambo lililoelezwa, Kamati ililinganisha makusanyo halisi na lengo lililokuwa limebainishwa.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulijulisha Bunge tathmini ya hali ya ukusanyaji wa mapato iliyobainika. Kwa ujumla, matokeo ya uchambuzi yameonesha kama ifuatavyo:-

(i) Jumla ya kiasi cha fedha zilizokusanywa hadi kufikia Mwezi Februari, 2024 ni sh. Bilioni 756.48 sawa na asilimia 63.8 ya lengo. Mwenendo huo unaashiria uwezekano wa kufikiwa kwa lengo, jambo ambalo linaonesha ufanisi na upangaji unaozingatia hali halisi; na

(ii) Uwiano wa mchango wa makusanyo ya maduhuli kutoka Makao makuu ya Wizara na Taasisi zake ikilinganishwa na mchango wa mikoa 26 na halmashauri 184 nchini unatofautiana na uwiano halisi wa makusanyo. Uwiano wakati wa makadirio ulikuwa ni asilimia 4 kwa asilimia 96 za mchango wa wizara na taasisi zake na mikoa na halmashauri zote mtawalia. Uwiano wa hali halisi umekuwa asilimia 2 kwa asilimia 98 mtawalia.

**Mheshimiwa Spika**, kwa matokeo hayo ni dhahiri kuwa: -
i) Kuna uwezekano mkubwa wa lengo la maduhuli kuwa limetokana na hali halisi, kwa sababu hakuna tofauti ya uwiano; na

ii) Kuna uwezekano mkubwa wa makusanyo halisi kuzidi kidogo lengo lililowekwa, kwa kuwa makusanyo makubwa

yalipatikana kabla ya kufikia mwisho wa robo ya tatu ambayo ni mwisho wa mwezi Machi, 2024.

**(b) Hali ya Upatikanaji wa Fedha**

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge imeweka sharti la kufanya uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa kulinganisha na hali halisi ya mwaka unaotangulia. Kamati ilichambua kwa mtazamo huo na kubaini yafuatayo:-

(i) Jumla ya fedha iliyopokelewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI hadi kufikia mwezi Februari, 2024 ni sawa na asilimia 68.06 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Kwa mwenendo huo, kuna uwezekano wa Ofisi ya Rais TAMISEMI kupata kiasi chote cha bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Ikiwa hivyo, majukumu na mipango yote iliyopangwa ina mwelekeo wa kukamilishwa;

(ii) Uwiano wa Bajeti ulioidhinishwa na Bunge tarehe 18 Aprili, 2023 ulionesha kuwa Makao Mkauu ya Wizara na Taasisi zake pamoja na Tume ya Utumishi wa Walimu ingepata aslimia 12.32 ya Bajeti ya Ofisi hii, na Mikoa 26 Tanzania Bara na Halmashauri 184 ingepata asilimia 86.68 ya Bajeti ya TAMISEMI. Hali halisi ya upatikanaji wa fedha imebainisha uwiano tofauti na uliopitishwa na Bunge. Makao Makuu ya Wizara na Taasisi zake pamoja na Tume ya Utumishi wa Walimu imepokea aslimia 15.1 ya fedha yote iliyopokewa, na Sekretarieti za Mikoa 26 pamoja na Halmashauri 184 zimepokea asilimia 84.9 ya fedha zilizopokewa na TAMISEMI;

(iii) Uwiano wa Bajeti ya Maendeleo kwa bajeti ya matumizi ya kawaida wakati Bunge lilipopitisha makadirio ni tofauti kidogo na uwiano wakati wa utekelezaji. Bunge lilipopitisha Bajeti ya Wizara hii uwiano ulikuwa ni asilimia 33.3 kwa asilimia 66.7 mtawalia. Uwiano wa fedha zilizopatikana kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa kiasi cha fedha zilizopatikana kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni asilimia 38.03 kwa asilimia 61.07 mtawalia; na

(iv) Uwiano wa Bajeti ya Maendeleo kwa Makao Makuu ya Wizara na taasisi zake ukilinganishwa na bajeti ya maendeleo kwa mikoa na halmashauri zote nchini unatofautiana na uwiano halisi wa kiasi cha fedha kutoka hazina kwa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na taasisi hizo. Wakati uwiano wa bajeti ya maendeleo iliyopitishwa na Bunge kati ya TAMISEMI na taasisi zake kwa upande mmoja na Seketarieti za mikoa na halmashauri zote kwa upande mwingine ni asilimia 29 kwa asilimia 71 mtawalia. Lakini upokeaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa taasisi hizo ni asilimia 36.8 kwa 63.1 mtawalia.

**Mheshimiwa Spika** kwa mwenendo huo, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya majukumu ya OR - TAMISEMI Makao Makuu na Taasisi zake ni mzuri zaidi ya upatikanaji wa fedha kwa Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri nchini. Ilhali Makao Makuu ni Waratibu na Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri ni Watekelezaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilirejea majadiliano ya Wizara na Kamati ya tarehe 18 hadi 26 Machi, 2024 na kubaini yafuatayo:-

(i) Fedha zilizopokewa Makao Makuu ya Wizara ni kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya kusimamia na kuratibu uendeshaji wa shughuli za Sekretarieti za Mikoa 26 Tanzania Bara, Tume ya Utumishi wa Walimu na uendeshaji wa Makao Makuu ya Wizara.

(ii) Fedha zilizopokewa kwenye Sekretarieti za Mikoa 26 ya Tanzania Bara ni kwa ajili ya shughuli za umma kwenye Wilaya 139, Tarafa 570, Halmashauri 184, Kata 3,956, Vijiji 12,318, Mitaa 4,263 na Vitongoji 64,361.

(iii) Fedha zilizopokewa na Tume ya Utumishi wa Walimu ni kwa ajili ya kufanikisha dhima ya Tume hiyo ya kuhakikisha walimu wa shule za msingi na sekondari wanapata huduma bora kuhusu masuala ya ajira, kupandishwa vyeo na kukuza maadili.

**(c) Hali ya Utekelezaji wa Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa mpango wa Wizara au taasisi yoyote kwa mwaka wa fedha unaoisha, ni kigezo muhimu cha kupanga kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa kuzingatia msingi huo, kabla ya kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi, Kamati ilichambua hali ya utekelezaji wa mpango wa Ofisi ya Rais, TIMISEMI kwa mwaka wa fedha 2023/2024.
Katika uchambuzi huo miongoni mwa mipango ilihusu ukamilishaji wa Sera ya Taifa ya Ugatuaji, Program ya Kuimarisha Mikoa na Serikali za Mitaa na usanifu wa mifumo ya TEHAMA katika ngazi zote za OR – TAMISEMI.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa mambo hayo yanaendelea kutekelezwa. Kwa mfano, usanifu wa mifumo ya TEHAMA na uendeshaji wa tovuti 211 za OR – TAMISEMI ni mambo endelevu. Hata hivyo, utekelezaji ulipaswa kuzingatia uhusiano na ushirikiano kati ya OR – TAMISEMI na taasisi zake katika suala la usimamizi wa tovuti za taasisi hizo. Kwa mfano usimamizi wa tovuti ya Chuo cha Serikali za Mitaa ulistahili kuonekana wazi wazi katika ripoti ya utekelezaji. Aidha, maandalizi ya ukamilishaji wa Sera ya Taifa ya Ugatuaji ni jambo linalostahili kupewa uzito maalum.

**2.2 Uchambuzi wa Mpango kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa makadirio ya Mapato na matumizi unazingatia mipango ya Wizara na Taaasisi inayohusika. Ili kukidhi mantiki ya Bunge kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, Kamati ilichambua mipango ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI na kubaini yafuatayo: -

(i) Mipango ya OR - TAMISEMI inatekelezwa kwa kigezo cha vipaumbele 12 vilivyochaguliwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na ugatuaji wa madaraka kwa umma (D by D) ni kipaumbele cha kwanza. Hata hivyo,

kipaumbele hiki kimeamuliwa bila ya kuwa na Sera ya Taifa ya Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma iliyokamilika;

(iii) Kusimamia mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato ni kipaumbele kinachoendana na mahitaji kulingana na yaliyobainika wakati wa ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Kamati ilipotembelea miradi ya maendeleo ilibaini kuwa kitengo cha ufuatiliaji na uratibu kina ufanisi mdogo katika kuratibu miradi inayotekelezwa kwenye mikoa na halmashauri mbalimbali nchini;

(iv) Kwa ujumla mipango hiyo inahusiana moja kwa moja na majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI yaliyoainishwa katika Hati Idhini ya kuanzishwa kwake;

(v) Baadhi ya Mipango iliyotekelezwa mwaka wa fedha 2023/2024 haikujitokeza waziwazi katika mipango inayokusudiwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(vi) Baadhi ya Mipango iliyotekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 imeendelea kujitokeza kwa mwaka wa fedha 2024/2025; na

(vii) Baadhi ya mipango inayojitokeza kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni mipya na haikuwepo katika mwaka wa fedha 2023/2024.

### 2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, tija na manufaa ya mipango yoyote ya kuboresha shughuli za umma, vinategemea kwa kiasi kikubwa makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali. Ili kujiridhisha na uwezekano wa manufaa kwa umma yanayoweza kupatikana kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati imechambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Uchambuzi huo umehusisha kutathmini mambo makuu matatu ambayo ni: Makadirio ya Mapato, makadirio ya matumizi ya kawaida na makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo. Ufafanuzi wa matokeo ya Uchambuzi ni kama ifuatavyo:-

### 2.3.1 Uchambuzi wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia uhusiano uliopo kati ya uendeshaji wa shughuli za umma, ukusanyaji wa maduhuli na uwiano wa mapato kwa matumizi. Kwa msingi huo uchambuzi ulifanyika kwa kulinganisha na makadrio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha ulioisha, hali halisi ya ukusanyaji wa maduhuli hadi kufikia mwezi Februari, 2024 na lengo la Serikali kuhusu ukusanyaji. Matokeo ya uchambuzi yameonyesha kama ifuatavyo: -

i) Makadirio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yameongezeka kwa asilimia 14 ikilinganishwa na makadirio kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

ii) Mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024 unaonesha uwezekano wa kufanikisha ongezeko la lengo la makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2024/2025;

iii) Uwiano wa makadirio ya maduhuli kwa makadirio ya bajeti ya matumizi kwa OR - TAMISEMI kwa mwaka 2023/2024 ulikuwa ni asilimia 13.05 ya bajeti ya makadirio ya matumizi. Uwiano wa mkadirio ya maduhuli kwa bajeti ya matumizi umekuwa asilimia 13.46 ya bajeti ya matumizi kwa mwaka 2024/2025.

### 2.3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, uendeshaji wa shughuli za umma hutegemea bajeti ya matumizi ya kawaida. Aidha, mahitaji ya kibajeti ya shughuli za uratibu hayalingani na mahitaji ya shughuli za utekelezaji. Kwa misingi hiyo Kamati ilichambua ili kujiridhisha na tofauti zinazotakiwa. Uchambuzi umebanisha yafuatayo: -

i) Bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezeka kwa asilimia 19.4 ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

ii) Matumizi ya kawaida ya OR - TAMISEMI na taasisi zake yameongezeka kwa asilimia 9 wakati bajeti ya matumizi ya

kawaida *(recurrent)* kwa Sekretarieti za Mikoa 26 na Halmashauri 184 imeongezeka kwa asilima 19.6; na

iii) Ongezeko la bajeti ya matumizi ya kawaida linaendana na nyongeza ya vipaumbele vya mpango wa bajeti ya OR - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**2.3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa miradi ya maendeleo unatarajiwa kusaidia huduma kwa umma kwa muda mrefu. Utekelezaji huo unategemea bajeti inayopitishwa na Bunge. Aidha, OR - TAMISEMI na taasisi zake zinatekeleza baadhi ya miradi pamoja na kusimamia utekelezaji wa miradi katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Uchambuzi wa bajeti ya miradi ya maendeleo umebainisha mambo yafuatayo: -

i) Kwa ujumla bajeti ya miradi ya maendeleo imepungua kwa asilimia 2 kwa mwaka 2023/2024 ikilinganishwa na bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

ii) Bajeti ya mandeleo kwa Makao Makuu ya OR - TAMISEMI na taasisi zake imeongezeka kwa asilimia 2;

iii) Bajeti ya miradi ya maendeleo kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa imepungua kwa asilimia 3.7.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo chini ya OR - TAMISEMI yameongezeka kutokana na hali halisi ya baadhi ya miradi. Kamati imeridhishwa na makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo. Hata hivyo. Kamati ina maoni kwamba wakati wa utekelezaji wa bajeti hii Serikali itapaswa kuzingatia ushauri unaotolewa na Wabunge pamoja na ushauri wa Kamati.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** lengo la uchambuzi uliowekewa utaratibu na kanuni za kudumu za Bunge ni kuwezesha upatikanaji wa maoni na ushauri. Naomba kulishauri Bunge lako Tukufu lijadili makadirio ya mapato na matumizi ya OR - TAMISEMI kwa pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kama unavyofafanuliwa katika taarifa hii.

### 3.2 Maoni na Ushauri

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na matokeo ya uchambuzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ukusanyaji wa maduhuli, upatikanaji wa fedha zilizoidhiniswha na Bunge na vipaumbele vilivyobainishwa na OR - TAMISEMI, Kamati inashauri kuhusu mambo mbalimbali ya kuzingatiwa wakati wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, baada ya uchambuzi wa makadirio wa mapato na matumizi ya OR - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Kamati inashauri kama ifuatavyo: -

### 3.2.1 Umaliziaji wa Maboma ya Shule na Zahanati

**Mheshimiwa Spika**, katika kufanikisha ujenzi wa majengo mbalimbali nchini wananchi wamejitolea kujenga majengo mengi kwa ajili ya shule na zahanati kwa ajili ya huduma kwa umma. Ujenzi huo uliofanyika kwa nguvu za wananchi umefikia hatua ya upauaji lakini haujaendelezwa. Kwa sababu hiyo, Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo: -

i. Serikali itekeleze ushauri wa Kamati ulitolewa wakati wa uwasilishaji wa maoni ya Kamati kuhusu bajeti ya OR - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

ii. Serikali itoe mwongozo na kuweka uratibu stahili katika uanzishwaji wa ujenzi wa majengo ya aina hiyo kwa nguvu za wananchi ili kupunguza ujenzi holela wa maboma na kudhibiti viwango vya ujenzi wa maboma ya majengo ya Serikali; na

iii. Serikali kuzingatia ombi maalum la kibajeti lililowasilishwa na Kamati kuhusu umaliziaji wa maboma hayo.

### 3.2.2 Fedha kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu iliyoharibiwa na mvua nchini;

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2023/2024 Serikali ilitenga zaidi ya shilingi trilioni moja kwa ajili ya TARURA. Hata hivyo, upelekaji wa fedha hizo ulifikia asilimia 45.7 Upokeaji huu hauridhishi na hautaiwezesha TARURA kutekeleza miradi yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia mwishoni mwa mwaka 2023 hadi sasa nchi imekumbwa na uharibifu mkubwa wa miundombinu ya Barabara katika maeneo mbalimbali nchini kutokana na kunyesha kwa mvua kubwa za El Nino. Hali hii imesababisha Barabara nyingi hasa za vijijini kutokupitika kabisa kutokana na uharibifu huo na hivyo kusababisha huduma mbalimbali za usafiri kwa wananchi kuwa ngumu. Kutokana na hali hiyo OR - TAMISEMI imeweka mkakati wa kuzirejesha Barabara hizo katika hali yake ya kawaida kwa kuitumia TARURA.

**Mheshimiwa Spika,** azma ya OR - TAMISEMI kusimamia miradi ya ujenzi wa barabara na miundombinu inayoendana na barabara hizo inaweza kufanikiwa kwa kuongeza fedha kwa Wakala wa Baraba Vijijini na Mijini (TARURA). Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuzingatia ushauri wa Kamati uliotolewa katika Bunge la Bajeti lililopita, pamoja na hayo, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo: -

i. Kupeleka fedha TARURA kikamilifu na kwa wakati; na

ii. Kutoa bajeti ya dharura kwa kuzingatia ombi maalum lililotolewa na Kamati kwa ajili ya kusaidia urejeshaji wa miundombinu hiyo.

### 3.2.3 Ushiriki wa wakandarasi wazawa katika utekelezaji wa miradi

**Mheshimiwa Spika**, katika orodha ya vipaumbele vya OR - TAMISEMI ushirikishwaji wa wananchi ni jambo lililopewa uzito. Aidha, OR - TAMISEMI imepanga kuratibu na kusimamia miradi ya

ujenzi katika ngazi zote za Mamlaka za Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa.

**Mheshimiwa Spika,** Katika vikao vyake na OR - TAMISEMI Kamati ilibaini kuwa Serikali imekuwa ikitumia zaidi wakandarasi ambao si wazawa na hivyo kuwanyima wakandarasi wazawa fursa ya utekelezaji wa miradi hiyo. Aidha, wakandarasi wengi wazawa huwa na mitaji midogo ambayo inaonekana kutokutosheleza utekelezaji wa miradi inayoratibiwa na Serikali kutokana na ugumu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2023.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hiyo Kamati inashauri kuwa kipaumbele cha kutoa kandarasi kwa wakandarasi wazawa kizingatiwe sambamba na kuzielekeza halmashauri nchini kuwatumia wakandarasi wazawa lakini bila kuathiri viwango stahifu.

**3.2.4 Uanzishwaji na uendeshwaji wa shule za msingi za michepuo wa Kiingereza**

**Mheshimiwa Spika**, katika mpango wa OR - TAMISEMI unaohusu kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma za jamii yapo mambo ya msingi yanayopaswa kuzingatiwa. Msimamo wa Serikali kuhusu huduma hizo ni jambo la lazima. Katika uchambuzi wa Randama za OR - TAMISEMI Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa maoni ya Kamati kuhusu uanzishwaji wa shule za mchepuo wa Kiingereza yaliyotolewa katika taarifa yake wakati Bunge linapitisha bajeti ya OR - TAMISEMI (tarehe 14 – 18 Aprili, 2023) hayakueleweka. Kwa ujumla Kamati inaona kuwa kuanzishwa kwa shule hizi utaleta matabaka kwa Watanzania na pia kwenda kinyume na Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 Toleo la 2023.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hiyo Kamati inashauri kuwa, Serikali izingatie ushauri wa Kamati juu ya utoaji wa elmu kwa kuzingatia usawa na kuimarisha ufundishaji wa somo la kiingereza katika shule zake zote.

**3.2.5 Utekelezaji wa wajibu wa Wadau wa Miradi ya Mendeleo kurudisha faida kwa Jamii (CSR)**

**Mhesimiwa Spika**, katika uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/2024 Kamati ilibaini kuwa OR - TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekuwa zikipata fedha kutoka kwa watekelezaji wa miradi mbalimbali kama sehemu ya uwajibikaji wa taasisi na kampuni zinazotekeleza miradi hiyo kwa jamii *(Corporate Social Responsibility – CSR)*. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa miongozo ya matumizi ya fedha hizo bado haileti tija inayotarajiwa kwa wananchi. Aidha, Kamati imebaini kuwa hakuna miongozo kwa halmashauri ya namna ya kuwatambua wadau wanaotekeleza miradi ya maendeleo kwa kuwa kuna miradi mingi inayotekelezwa na wadau mbalimbali wa maendeleo bila wadau hao kupata fursa ya kurejesha faida kwa jamii. Kamati pia imebaini kuwa katika baadhi ya maeneo wadau hao wamekuwa wakiratibu na kutekeleza miradi hiyo wenyewe bila usimamizi na uratibu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali hiyo Kamati inashauri kuwa utekelezaji wa miradi uende sambamba na kusimamia utaratibu wa wajibu wa wadau wa miradi hiyo kurejesha faida kwa jamii. Kutokana na hilo Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo: -

i. Utekelezaji wa miradi hiyo ulizingatie sheria, miongozo na kanuni ya utekelezaji wa miradi ya Serikali;

ii. Usimamizi wa gharama za miradi ya fedha zinazotokana na CSR ufanywe kwa kufuata kanuni na taratibu za manunuzi za Serikali ili kuepuka gharama kubwa za miradi hiyo; na

iii. Halmashauri zibainishe taasisi zote za kibiashara katika maeneo yao ambazo zinapaswa kutoa CSR na kuhakikisha kuwa taasisi hizo zinarejesha faida kwa jamii.

**3.2.6 Mapato ya Halmashauri kutokana na biashara ya Kaboni**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia mpango wa OR - TAMISEMI wa kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato, halmashauri zimekuwa zikibuni vyanzo mbalimbali vya

mapato. Katika vikao vya kujadili taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya OR - TAMISEMI Kamati ilibaini kuwa kuna chanzo cha biashara ya kaboni kinachoziingizia mapato ya kutosha halmashauri chache nchini ambacho hakijagunduliwa na halmashauri nyingine. Kutokana na hilo Kamati inashauri kama ifuatavyo: -

i. Serikali ihakikishe kuwa eneo la biasahara ya Kaboni lipewe kipaumbele kama chanzo muhimu cha mapato ya halmashauri zote zilizo na utajiri wa misitu nchini;

ii. OR - TAMISEMI ijenge uwezo wa kitengo kinachosimamia biashara ya kaboni ili kuweza kutoa ushauri wa kitaalam kwa halmashauri nchini; na

iii. Serikali za vijiji, kata na halmashauri zipime maeneo na kumilikishwa maeneo hayo kama hatua ya kuweza kuhifadhi na kuitunza misitu wenyewe ili iweze kuwanufaisha katika biashara ya kaboni.

**3.2.7 Utunzaji wa Mazingira katika Halmashauri**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato ni sehemu ya lengo la OR - TAMISEMI, uboreshaji wa mazingira ni sehemu muhimu katika kuziwezesha halmashauri kujiongezea kipato kutokana na mazingira kuweza kuwa kama chazo cha mapato kwa ajili ya biashara ya Kaboni. Kutokana na hiyo Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo: -

i) Serikali ianzishe programu maalumu katika shule za msingi na sekondari nchini kwa kila mwanafunzi anayeanza shule kupanda na kuutunza mti wake wakati wa maisha yake yote awapo shuleni hapo;

ii) Mashirika yanayotoa misaada ya kupanda miti yaelekezwe kujikita kwenye ujenzi wa miundombinu ya kutunzia miti; na

iii) Halmashauri nchini zielekezwe kuweka sheria ndogo *(by laws)* kwa ajili ya kusimamia wajibu wa wananchi kupanda miti na kuitunza kwenye maeneo ya makazi yao;

### 3.2.8 Uhuishaji wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali, Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Sheria ya Manunuzi ya Umma

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali, Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Sheria ya Manunuzi ya Umma zimeweka masharti ambayo ni ngumu kutekelezeka katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa mfano upatikanaji wa mashine za EFD kwa huduma kama za mazishi au vyakula zinazotolewa maeneo ya vijijini.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa malengo ya OR - TAMISEMI kwa mwaka 2024/2025 ni kuratibu utoaji wa huduma kwa jamii. Kamati imebaini kuwa hoja nyingi za ukaguzi za CAG zinatokana na sheria hizo kuleta changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika ngazi ya kata, vijiji na halmashauri.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika uchambuzi wake ilibaini kuwa pamoja na utoaji huduma kwa jamii kwa kipindi cha mwaka 2023/2024 kuwa na mafanikio pia imebainika utekelezaji wa shughuli za Serikali za Mitaa umekuwa ukiathiriwa na zilizotajwa hapo juu. Kutokana na ugumu wa utekelezaji kwa kufuata sheria hizo imebainika kuwa halmashauri zimekuwa zikikutana na hoja nyingi za kihasibu kutoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

**Mheshimiwa Spika,** ili utekelezaji wa bajeti inayoombwa na OR - TAMISEMI izingatie uhalisia katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Kamati inashauri kuwa, Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Sheria ya Matumizi ya Fedha za Umma pamoja na Sheria ya Manunuzi ya Umma zinahitaji kuhuishwa ili ziendane na mazingira halisi ya utekelezaji wa shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

### 3.2.9 Taasisi za Serikali zinazofanya kazi na Halmashauri kuzingatia bajeti za Halmashauri

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya OR - TAMISEMI kwa mwaka 2023/2024 katika utekelezaji wa bajeti za halmashauri Kamati ilibaini kuwa

zipo taasisi zinazoandaa makongamano, warsha na semina mbalimbali na kuwaalika wataalam wa halmashauri huku zikiwaelekeza wakurugenzi wa halmasahuri hizo kugharamia. Hali hii imekuwa ikizifanya halmashauri hizo kutumia fedha ambazo hapo awali hazikuwa kwenye bajeti yao, na hivyo kufanya shughuli nyingine za kibajeti katika halmasahuri hizo kutokutekelezwa. Kamati inashauri OR - TAMISEMI kuelekeza kuwa mialiko yoyote itakayokwenda kwa wakurugenzi iambatane na taarifa ya walioandaa matukio hayo kuonesha kuwajibika kwao kibajeti.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukurani

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu kwako kwa kunipatia fursa ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), lakini pia kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu. Nawashukuru sana Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengewa (Mb), – Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Waheshimiwa Naibu Mawaziri wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Festo John Dugange pamoja na Mheshimiwa Zainab Katimba kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Wizara ya TAMISEMI, Ndg. Adolf H. Ndunguru pamoja na Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati tangu tulipoanza kufanya nao kazi na kushiriki vizuri kwenye uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee namshukuru sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga (Mb), pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja, kwa ushirikiano mzuri ambao wananipa. Wajumbe hawa ni wachapa kazi na wameshiriki kikamilifu katika uchambuzi wa Bajeti na kuhakikisha

wanahoji ili kupata ufafanuzi wa kina. Nawapongeza sana na naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Lazaro Justin Nyamoga, Mb. – **Makamu Mwenyekiti**
2. Mhe. William Vagimembe Lukuvi, Mb.
3. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb.
4. Mhe. Prof. Palamagamba John Kabudi, Mb.
5. Mhe. Sylvestry Fransis Koka, Mb.
6. Mhe. Zuberi Mohammed Kuchauka, Mb.
7. Mhe. Zacharial Paulo Issaay, Mb.
8. Mhe. Salome Wycliff Makamba, Mb.
9. Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara, Mb.
10. Mhe. Sebastian Simoni Kapufi, Mb.
11. Mhe. Amandus Julius Chingulile, Mb.
12. Mhe. Dorothy George Kilave, Mb.
13. Mhe. Elinikyo Mafuwe Saashisha, Mb.
14. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb.
15. Mhe. Mwantum Mzamili Zodo, Mb.
16. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis, Mb.
17. Mhe. Erick James Shigongo, Mb.
18. Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb
19. Mhe. Ameir Abdalla Ameir, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema, katika wakati wote ilipokutana ikiwemo Taarifa hii.

**4.2 Mwisho**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Taasisi zake (**Fungu 56, 02, 36 ,47, 54, 63, 70, 71, 72, 79, 74, 75, 76, 77, 78, 79, 80, 81, 82, 83, 84, 85, 86, 87, 88, 89, 90, na 95)** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja, jumla ya **Shilingi 10,163,499,893,167.00.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumaliza, kwa niaba ya Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ninaunga mkono hoja.

Dennis Lazaro Londo, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
16 APRILI, 2024

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wetu wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda kwenye hatua ya uchangiaji na mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe akifuatiwa na Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mheshimiwa Anna Kilango Malecela ajiandae. Endelea. *(Makofi)*

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia hotuba yetu ya TAMISEMI. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu na nikiwa wa kwanza kuchangia Kamati nyeti hii katika nchi yetu. *(Makofi)*

Kwanza kabisa, nianze kumpongeza Waziri wa TAMISEMI kwa kazi kubwa anayoifanya pamoja na Manaibu wake wote na menejimenti yake. Nampongeza sana tunatambua kazi kubwa anayoifanya kwenye nchi yetu na nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati kaka yangu Londo kwa kupitia, kuchambua na kuja kutusomea hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya, nimpongeze sana Amiri Jeshi wetu Mkuu Mheshimiwa Rais, mwanadiplomasia makini ndani ya nchi yetu, aliyeinua uchumi wetu kwa kiwango kikubwa, leo hii *TRA* wanakusanya mpaka shilingi trilioni mbili, lakini mambo yanaenda taratibu kama vile

hayaonekani, kwa kweli Mheshimiwa Dkt. Samia amefanya kazi kubwa sana na niwaambie tu kwamba Watanzania tuna Imani kubwa na Mheshimiwa Rais tunampenda na tunamthamini sana kwa kazi kubwa anazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Rais anaingia *TARURA* tulikuwa tuna shilingi bilioni 200 nchi nzima, leo hii tuna shilingi trilioni 1.4 lakini pia kwenye bajeti hii imeongezwa. Ndugu zangu wakati Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu anaingia madarakani tulikuwa na *MRI machine* moja tu Muhimbili, leo hii kila hospitali ya kanda ina *MRI,* lakini tulikuwa na *T-Scan* mbili tu nchi nzima, leo hii hospitali zetu zote za mikoa zina *T-Scan*. Imekuwa ni kuokoa maisha ya Watanzania kwa kiwango kikubwa. Wasiokuwa na uwezo wa kusafiri leo wakienda mkoani wanakuta *T-Scan, T-Scan* ilikuwa inapatikana Muhimbili tu, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia amefanya kazi kubwa sana na tutaendelea kumpongeza na kuthamini mchango wake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Munde unamaanisha *CT-Scan?*

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *TC-Scan. (Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *CT-Scan,* ahsante nadhani mmenielewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu amefanya mambo makubwa sana, leo hii watoto wetu wa elimu ya kati *(diploma)* wanapata mikopo ya kwenda kusoma elimu ya kati, zote hizi ni juhudi kubwa za Mheshimiwa Rais. Pamoja na kazi kubwa anayoifanya hakuacha kufanya miradi ya kimkakati. Miradi yote ya kimkakati imekamilika kwa karibia 90% mpaka 98%. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Bwawa la Mwalimu Nyerere alilikuta liko 37% leo hii lina 98% na imesababisha kumaliza mgao wa umeme kwa 85%, zote hizo ni kazi nzuri na kubwa anazozifanya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu. *SGR* leo hii amekamilisha kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma kwa 98%,

siyo kitu kidogo. Lakini Dodoma – Tabora – Mwanza na Dodoma – Tabora – Burundi wakandarasi wako *site* na kazi zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema iwe mvua iwe jua tutakufa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, tutapambana kuhakikisha anashinda kwa kura za heshima kwa kazi kubwa anayoifanya mwanamama huyu. Hakuna asiyejua kwamba Rais amefanya kazi kubwa na ndiyo maana wanahangaika na watahangaika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kwa kusema kwamba bajeti ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kweli inaridhisha, lakini bado niseme tutaomba sana kkwenye Bajeti hii sisi watu wa Mkoa wa Tabora na namwambia Mheshimiwa Waziri Mchengerwa kwamba, katika Mikoa yote Tanzania nzima Mkoa wa Tabora ndio mkubwa na katika sensa ya mwaka 2022 tumekuwa watu wa tatu, kwanza ni Dar es Salaam, Mwanza halafu Tabora kwa wingi wa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwneyekiti, kwa hiyo, nasema runaomba mtuongezee fedha za barabara. Mnajua mvua zinaendelea kunyesha, barabara zetu zimeharibika, ipo bajeti iliyopatikana, lakini tunataka mtuongezee kwa sababu tuna barabara nyingi na tuna eneo kubwa sana la kimkakati katika Mkoa wa Tabora. Tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri, huu ni mkoa mkubwa wa kwanza Tanzania nzima, naomba nirudie kusema kwa msisitizo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwenye eneo la afya katika Mkoa wangu wa Tabora, Manispaa ya Tabora. Manispaa ya Tabora ina kata 29, vijiji 41 na mitaa 134 kwa masikitiko makubwa ina kituo cha afya kinachofanya kazi kwa asilimia 100 kimoja tu kinachoitwa Ipuli Maili Tano. Pamoja na kwamba kituo hiki kinafanya kazi kwa asilimia 100, kina *theatre* na pia kina *mortuary,* lakini hakina jokofu. Namwomba Mheshimiwa Waziri atupatie jokofu katika kituo hiki kimoja cha afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vituo vingine viwili, Kituo cha Misha na kituo cha Tumbi, ambavyo vinafanya kazi lakini havijakamilika kwa asilimia 100. Naiomba Serikali itupe fedha kwa ajili ya kukamilisha vituo hivi kwa asilimia 100, ili katika kata 29 tuwe na vituo vitatu ambavyo vimekamilika. Kwa kweli tunahitaji mtuangalie kwa jicho la pekee kuhakikisha kwamba tunapata vituo vya afya vingi, *population* ya Manispaa ya Tabora ni kubwa, kata zetu ni nyingi, lakini hatuna vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna zahanati 23, mahitaji ni zahanati 35. Kwa hiyo, namuomba sana Mheshimiwa Waziri, wekeni jicho la kipekee katika Mkoa wa Tabora kuhakikisha mambo ya afya yanaenda vizuri. Tunashukuru kwa kazi nzuri mlizofanya, kuna zahanati moja inaitwa *Town Clinic* ambayo iko mjini, nimeiongelea sana hapa. Namshukuru Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Dugange ambaye amemuagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora ifikapo tarehe 30 alete michoro kwa ajili ya kutuongezea fedha, ili tupate jengo la mama na mtoto, tupate *theatre*, maabara na *mortuary* ili kuongeza walau idadi ya vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Town Clinic* hii imezungukwa na kata nane ambazo zina wakazi wengi wa Manispaa ya Tabora kwa hiyo, tunaomba sana mtusaidie, lakini tuna zahanati ya Itaga, Itulu na *Block Farm* ambazo nazo zimekamilika, lakini ziko kata za nje, za vijijini. Tunaomba nyumba za watumishi wa hospitali hizo za Itaga, Itulu na *Block Farm*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa wazo, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC*, tumetembea kwenye hizi zahanati, unaweza ukakuta kuna sehemu kuna vifaa tiba vyote, lakini hakuna mtu wa kuvitumia, lakini kwenye eneo hili sasa unakuta kuna mstaafu ambaye amewahi kutumia *x-ray*, *ultra sound* yuko pale, naomba Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa muandae sera ya ku-*volunteer* ili hawa watu waliopo ambao labda katoka chuo hajaajiriwa, amestaafu yuko eneo lile basi *own source* ya halmashauri imlipe posho na aendelee kuwahudumia Watanzania wa eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongea kuhusu elimu; Tabora tuna shule za zamani, shule kongwe ziko kumi; Kiloleni ipo Kata ya Mapambano, Mkoani, Mtendeni, Rufita, Itaga, Cheyo, Itonjanda, Inala, Mawiti na *Town School*. Hii *Town School* amesoma bibi yangu mzaa mama kwenye shule ile, mama yangu mzazi amesoma kwenye shule ile, hata Mheshimiwa Mama Sitta amesoma pale, shule ile haijawahi kukarabatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuja Naibu Katibu Mkuu wa Elimu tukampeleka pale akaiangalia na akaahidi kutuletea shilingi milioni 350, lakini hajaleta. Nimempigia simu zaidi ya mara tatu, kaka yangu Mheshimiwa Msonde, anasema tutaleta fedha, lakini hajaleta fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, shule hiz hazijawahi kukarabatiwa na ziko katikati ya Mji wa Tabora. Shule ile ina nafasi kubwa, *space* yake ni kubwa, naiomba Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ikajenge ghorofa pale tupate na shule ya sekondari pale pale ili watoto wetu wa Kata ya Gongoni waweze kwenda *primary* na *secondary* wakiwa pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shule ya Mawiti Malolo, Shule hii imejengwa kabla hatujapata uhuru, haijawahi kukarabatiwa. Shule hii ina upungufu wa madarasa na ina upungufu mkubwa wa walimu. Tuna upungufu mkubwa wa walimu katika hizi shule kongwe, takribani walimu 207. Shule hii Mapambano ukienda hauwezi kujua kama iko Manispaa, kaka yangu Mheshimiwa Mchengerwa tuna imani kubwa na wewe, tunajua uwezo wako, tunaomba msaada katika mkoa wetu wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa ya Tabora na Kigoma ni mikoa ambayo zamani ilikuwa imesahaulika sana. Tunaona Serikali awamu hizi imekuja kutubeba na sisi na kutunyanyua. Mheshimiwa Mchengerwa tunaomba muendelee kutu-*support*, muendelee kuhakikisha kwamba shule hizi zinafanya kazi. Tuliomba hela za *BOOST* katika shule hizi kumi, lakini hatukupata hata senti tano za fedha hizi za *BOOST*. Kwa hiyo, tunaomba sana,

Mheshimiwa Mchengerwa, mtuangalie kwa jicho la pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kidogo kuhusu shule za msingi na zenyewe hali ni hiyo hiyo, walimu ni wachache sana. Kwa hiyo tunaomba tuongaliwe kwenye suala zima la walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua sana mchango wa Serikali ya Awamu ya Sita katika Mkoa wetu wa Tabora, hususan katika maendeleo yote kwa ujumla nikianza na barabara, vituo vya afya, zahanati, shule, madarasa. Tumepata madarasa mengi, lakini mahitaji ni makubwa, kama nilivyoanza kuwaambia kwamba katika *population* sisi ni watatu kwa Tanzania nzima. Mheshimiwa Waziri nadhani hili utalizingatia na utaendelea kuhakikisha bajeti yetu ya Mkoa wa Tabora inabaki kama ilivyoletwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali kupitia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, itupatie fedha kama zilivyoombwa kwani mahitaji ni makubwa na watu ni wengi. Wilaya zetu zina *population* kubwa sana, tunaomba mhakikishe bajeti yetu hamtaipunguza wala msiweke *ceiling* zenu. Tunataka hela tulizoomba mtupatie kwa sababu, sababu tunazo, watu ni wengi sana…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Munde muda wako umeisha.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako. Sasa namuita Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela ajiandae, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri sana anayoendelea kuifanya katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini kipekee kwa kazi anayoifanya katika Wizara hii ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa sababu yeye ndiyo Waziri mwenye dhamana katika Ofisi hii ya TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa pamoja na wasaidizi wake, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, wakuu wote wa idara mbalimbali zinazounda Ofisi ya Rais, TAMISEMI, lakini kipekee niwapongeze sana Wakuu wote wa Mikoa ambao kwa bahati nzuri leo wamealikwa hapa kwa namna ambavyo wameweza kusimamia vyema suala zima la uboreshaji wa miundombinu, hasa katika kipindi hiki cha mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua utabiri wa hali ya hewa ulitabiri vizuri sana na tumeona kuna ufanisi mkubwa ambao umeongezeka kwenye Mamlaka ya Utabiri wa Hali ya Hewa, kile kitu ambacho kinatabiriwa ndicho ambacho kinatokea. Tumeona tofauti kati ya ubashiri na utabiri katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawapongeza Wakuu wa Mikoa kwa sababu ulitoka Mwongozo kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba tunawaandaa wananchi kwa taarifa mbalimbali ili kuweza kukabili hali ya mvua na hilo wamelisimamia vizuri, pamoja na mvua kuwa ni nyingi za kutosha, lakini athari haikuwa kubwa sana kama ambavyo tumezoea kuona kwa miaka ya nyuma. Kwa hiyo, kwa eneo hilo tunawapongeza sana, waendelee kuchapa kazi kuunga mkono jitihada hizi za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwa kuanza na eneo la *TARURA; TARURA* ni Mamlaka ya Serikali ambayo inafanya kazi yake vizuri sana na Waheshimiwa Wabunge

watakubaliana na mimi kwamba pamoja na changamoto ambazo zipo za kifedha, lakini kwa maana ya menejimenti, *TARURA* wako vizuri na kuna ufanisi mkubwa sana. Hili linachagizwa na ongezeko kubwa la kilometa ambazo wanaendelea kuzihudumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati *TARURA* inaanzishwa ilikuwa na eneo la kilometa 108,000 pekee, lakini hadi kufika Juni, 2021 wameongeza eneo la barabara wanazozihudumia kufikia kilometa 144,429 na hii ni kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Namba 463 ambalo limetoka kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, mvua za vuli na hizi za masika zimenyesha kwa kiwango kikubwa sana, lakini barabara nyingi vijijini bado zimekuwa ni madhubuti, ukiacha zile chache ambazo zimepata kadhia. Hii ni kuonyesha kwamba kuna usimamizi mzuri na kuna uratibu mzuri kwa hiyo, ni vyema tukawatia moyo na kuhakikisha tunawaombea fedha zaidi, ili waweze kuimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mtandao wa barabara za wilaya ambao uko imara *(stable network)* wameongeza kutoka kilomwta 24,400 za mwaka 2017 hadi kufika kilometa 43,800 na hizi ni pamoja na zile kilometa 1,800 za lami na kilometa 16,600 ambazo ni za changarawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo wameweza kujenga madaraja na kuondoa vikwazo mbalimbali. Madaraja zaidi ya 3,195, lakini kalvati zaidi ya 75,620 na pia wameweza kujenga zege katika vilima mbalimbali ambapo huko nyuma magari yalikuwa yanateleza katika maeneo hayo. Kwa hiyo, hili ni eneo ambalo kwa kweli tunapaswa kuwapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya yote *TARURA* wana shida kubwa kwamba hawana wahandisi. Namuomba Mheshimiwa Waziri, kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI tuwawezeshe *TARURA* waweze kupata wahandisi, wana upungufu wa wahandisi zaidi ya 150 hadi 200. Tunaamini kwamba wakipata wahandisi wa kutosha wataboresha hii kazi nzuri ambayo

wanaifanya, itaendelea kuimarika na kuwa bora zaidi kwa hiyo, tuwasaidie katika eneo hili waweze kupata wahandisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, nataka kuchangia eneo la *RUWASA* pamoja na Mamlaka ya Uchimbaji wa Visima, hapa kuna shida kidogo ambayo ninaiona kwenye eneo hili. *RUWASA* wanajenga miradi mikubwa ya mabilioni ya fedha, lakini kwa bahati mbaya sana hawapewi fedha za *periodic maintenance*. Kwa hiyo, mradi hata kama ni wa shilingi bilioni mbili pale unapokabidhiwa maana yake ni hakuna hela hata kidogo ambayo inakwenda kuwa kama itatokea dharura yoyote waweze kuhudumia mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linakwaza sana wananchi kwa sababu kwa mara ya kwanza tu wanapokabidhiwa mradi wanatakiwa waanze kuuhudumia. Yapo matatizo mengine ambayo labda ni chanzo cha maji kimeharibiwa, kimesombwa na mafuriko kwa hiyo, kunauwa hakuna bajeti ya kuweza kurudisha. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali ilione hili kwa kuweka pesa za matengenezo ya miradi hii mikubwa ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Mheshimiwa Rais amenunua magari ya kuchimba visima katika mikoa yote, lakini ninasikitika kuona kwamba magari yale bado hayajaleta ufanisi ambao tumekusudia. Magari mengi yamepaki hayafanyi kazi, nadhani kuna tatizo la kiutawala ndani ya Wizara ya Maji. Kwa ushauri wangu, ile mamlaka inayochimba visima ndiyo inayopaswa kukabidhiwa haya magari/hii mitambo, ili *RUWASA* abaki kuwa mteja ambaye anaenda kuchukua huduma kutoka kwa Mamlaka ya Uchimbaji Visima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilivyo sasa, magari yale yamekabidhiwa kwa *RUWASA*, *RUWASA* hawana utaalam nayo kwa hiyo, yamepaki, lakini yeye ndiye anatakiwa awe mteja. Kwa hiyo, nadhani hapa kuna suala la kutazama katika *angle* ya *management* ili haya magari yaweze kufanya kazi inavyostahiki. Mimi kwa maoni yangu nadhani mamlaka hizi mbili zikae na mmoja awe mteja mwingine mtoa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho ni, narudi jimboni kidogo, Mamlaka ya Barabara Kuu *(TANROADS)*. Tuna tatizo la barabara ya kutoka Lushoto – Magamba hadi Lukozi, kuna mlima mmoja unaitwa Kandele Kapaa au Kasichana Kadogo, kuna shida ya utelezi na pale kuna kifusi ambacho kinafaa kwa ajili ya shughuli ya kutengeneza barabara, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa tamko la kuzuia kifusi kile kisichukuliwe kwa ajili ya shughuli za barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kwa dharura tupate angalao *cubic meters* 6,300 ziweze kukarabati eneo hili la barabara yenye urefu wa kilometa 11 kwa sababu wananchi wanapata shida na magari hayapiti kwa sababu barabara inatengenezwa, lakini kifusi siyo rafiki. Kwa hiyo nimwombe sana Waziri mwenye dhamana ya Madini ndiye ambaye zuio hilo limetoka kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu lakini likielekezwa kwenye Sekta ya Madini waweze kuharakisha jambo hili, ili wananchi waweze kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nampongeza Mheshimiwa Waziri ametuletea wageni na ninamuona Mwenyekiti wangu wa Mkoa wa Tanga yuko hapa, Katibu wa Chama wa Mkoa yupo, Wenyeviti wote wa mikoa wapo na wa *NEC* wote wapo hapa. Naamini wametuona na kazi tunayoifanya, basi Mwenyezi Mungu awabariki katika yanayokuja huko mbele, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shangazi.

Waheshimiwa Wabunge, natoa Mwongozo kidogo kuhusiana na muda, kengele ya kwanza italia baada ya dakika saba, utabaki na dakika tatu, kengele ya pili inapolia maana yake ni muda umekwisha.

Sasa namwita Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALACELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kusema ninafurahi sana kuzungumza kwa unyenyekevu mkubwa na wewe ukiwa umeketi hapo mbele kwa mara ya kwanza. Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mungu kwa afya na uzima, lakini kwa sababu dakika ni kumi nitakwenda mwendo wa haraka. Naomba leo nizungumzie mambo makubwa mawili na nitayazungumza ndani ya Jimbo langu la Same Mashariki. Nitazungumzia kuhusu barabara za *TARURA* na vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na barabara za *TARURA*; kwanza ninapozungumza *TARURA* naomba Wabunge wote mfahamu kwamba, *TARURA* tunayoizungumza imezaliwa tarehe 2 Julai, 2017 kwa hiyo, mpaka sasa ni mtoto mwenye miaka saba na ilizinduliwa na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Majaliwa Majaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia *TARURA* Jimboni kwangu; Jimbo la Same Mashariki mkilisikia ni jimbo korofi, narudia tena ni jimbo korofi. Jimbo hili lina milima katika tarafa mbili, namshukuru Mungu leo nalizungumza hili jimbo, jamani samahani kidogo, nalizungumza hili jimbo…

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisaidie.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tuelewane, tupunguze sauti kidogo.

**MHE. ANNE K. MALACELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nalizungumza Jimbo la Same Mashariki mbele ya Mkuu wangu wa Mkoa Nurdin Babu yupo, ambaye ndiye mwenye jimbo hili, lakini pia nalizungumza Jimbo la Same Mashariki mbele ya Mwenyekiti wangu wa Chama Cha Mapinduzi na m-*NEC* wangu wa Mkoa wa Kilimanjaro. Wanalifahamu vizuri Jimbo la Same Mashariki kwamba ni jimbo korofi katika mkoa wa Kilimanjaro. Jimbo la Same Mashariki bila barabara linakuwa siyo jimbo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nazungumzia *TARURA* kwa kipindi cha miaka mitatu ndani ya Jimbo la Same Mashariki. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan aliingia madarakani tarehe 19 Machi, 2021, leo tunapozungumza hapa Mheshimiwa Rais. Dkt. Samia Suluhu Hassan ana muda wa miaka mitatu madarakani. Sasa katika miaka mitatu kwangu mimi Jimbo la Same Mashariki, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanya nini ndani ya jimbo langu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujenzi wa barabara za *TARURA* ndani ya Jimbo la Same Mashariki kwa miaka mitatu Serikali imefanya matengenezo ya barabara, imejenga madaraja yenye thamani ya shilingi 9,425,582,091.23. Aidha, kabla ya Awamu ya Sita, *TARURA* ilijenga barabara za thamani ya shilingi 1,050,000,000 kwa kipindi cha miaka mitatu. Sasa kwa wale ambao mnafanya mahesabu, ina maana kipindi cha miaka mitatu cha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amejenga ziada na amenipa mimi Jimbo la Same Mashariki ziada ya shilingi 8,088,782,091.23. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ina maana ongezeko ni la 763%. Sasa Waheshimiwa Wabunge, utamuondoaje Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ndani ya mioyo ya Wananchi wa Same Mashariki? Utatumia lugha gani uwaambie wananchi wa Same Mashariki Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hafai kuwa Rais, haiwezekani kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie Waheshimiwa, Tanzania nzima tunalima tangawizi tani 20,000 kwa mwaka lakini sisi Same Mashariki wenyewe tunalima tani 14,500 kwa mwaka sawa na asilimia 72. Mimi Jimbo langu bila ya hizi barabara za *TARURA* hakuna uchumi kwenye Jimbo la Same Mashariki. Naomba niseme ukweli naipongeza sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. Awamu ya Sita imeleta ukombozi mkubwa sana kwa jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelea upande wa afya; upande wa afya wakati Mama Samia Suluhu Hassan anaingia

madarakani nilikuwa na kituo cha afya kimoja kinaitwa Ndungu. Kituo cha afya hicho kilikuwa hakina *mortuary, mortuary* ilikuwa haina jokofu kwa hiyo mwananchi wangu mimi akifariki Same Mashariki kwa sababu niko mpakani na Mkoa wa Tanga, maiti nyingi zilikuwa zinapelekwa kuhifandhiwa Tanga. Jambo hili limekuwa linaniuma na nimekuwa napiga makelele sana, naishukuru Serikali ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alipoingia madarakani tu, kitu cha kwanza Kituo cha Afya cha Ndungu kiliwekewa *mortuary* yenye jokofu tena alikiweka tarehe 13 Juni, 2022. Kwa hiyo mimi naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita. Leo nikizungumza hapa zaidi ya miili 250 kuanzia alipoingia madarakani imekuwa inapelekwa *mortuary* ya Ndungu kitu ambacho nilikuwa sina kabla ya utawala wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naingia kitu cha pili, tarehe 23 Novemba, 2023 Kituo cha Afya cha Ndungu kililetewa gari la wagonjwa, namshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia ambaye aliikuta Same Mashariki ina kituo cha afya kimoja, sasa sikilizeni ndugu zangu mkae vizuri.

Sasa hivi nina Kituo cha Afya cha Mtii kimekwisha, sasa hivi nina Kituo cha Afya cha Miamba kimekwisha, sasa hivi najengewa kituo cha afya kuanzia mwezi wa tano Serikali imeshamaliza kazi zote pale, Kituo cha Afya Vunda. Sasa hivi nasubiri Kituo cha Afya cha Vuje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli, kweli kabisa unaweza ukaenda Same Mashariki pale ukazungumza neno baya kuhusu Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan? Unaweza ukaenda Same Mashariki ukazungumza kitu kibaya kuhusu Chama Cha Mapinduzi? Unaweza ukaenda Same Mashariki ukazungumza kitu kibaya kuhusu Serikali ya Chama Cha Mapinduzi? Hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba kusema ukweli, Watanzania wote mlioko ndani ya Tanzania na mlioko nje ya Tanzania, Serikali ya Awamu ya Sita ya Chama Cha Mapinduzi

inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, inafanya kazi kubwa sana. Mimi nisema ukweli siku za nyuma watu walikuwa wasema hivi huyu mama kwa nini anasema sana, huyu mama kwa nini analalamika sana. Sasa hivi wamerudi wanasema hivi mama kwa nini husemi? Kwa nini Mama Anne Kilango siku hizi husemi? Hivi hali kama hii mimi nitasema? Nitasimama nipige makelele humu ndani? Nitasimama kuisifu Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, Serikali inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan imetendea haki wananchi wa Jimbo la Same Mashariki na hapo nimezungumza kwa vitu viwili tu afya na barabara za *TARURA*. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni ya kwanza eeh?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mama Anne Kilango Malecela muda wako umeisha.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja na ninaomba Waheshimiwa Wabunge wote tuseme ukweli kuhusu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, mchango mzuri kabisa. Namwita sasa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu ajiandae.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuongea kwa muda huu na naomba kumshukuru Mungu ambaye ameendelea kutulinda na kutupigania uhai wetu katika Bunge letu hili ambalo tupo kwa wakati huu kwa ajili ya kutetea Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt.

Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anendelea kuifanya kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama Samia amefanya kazi kubwa na ametoa pesa nyingi katika maeneo yetu ya majimbo. Mama Samia Suluhu Hassan anatakiwa kupewa pongezi kubwa sana, ni mama jasiri, mwenye uwezo mkubwa, anatakiwa apewe pongezi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Waziri wa TAMISEMI pamoja na Naibu Mawaziri wote wa TAMISEMI, Katibu Mkuu wa TAMISEMI pamoja na Naibu Makatibu wa TAMISEMI. Mheshimiwa Waziri naomba kukupa pole sana kwa ajili ya maafa ambayo yametokea katika Jimbo lako, pole sana mwanangu. Naomba nikupongeze umefanya kazi kubwa sana kwa ile hali iliyokuwepo katika eneo lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mkuu wangu wa Mkoa Mheshimiwa Mwamvua Mrindoko kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya katika Mkoa wetu wa Katavi, anafanya kazi kubwa sana kuhakikisha maendeleo yanasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba nimpongeza Mkuu wangu wa Wilaya Mheshimiwa Jamila Yusuph na kumwombea gari. Wilaya ya Mpanda ni wilaya yenye jiografia ngumu kidogo na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan analeta pesa nyingi katika maeneo yetu. Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Mpanda hajapata gari toka mwaka 2016 mpaka leo hatuna gari la Mkuu wa Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba kumshukuru Mheshimiwa Waziri, nimemsikia hapa amesema kuna magari. Naomba Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Mpanda awe wa kwanza kupata hilo gari kwa sababu anapata shida sana, hana gari anahangaika. Ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri, angalia Wilaya ya Mpanda kwa kuwa ina majimbo mawili na pesa nyingi mnaleta, anahangaika kufuatilia maendeleo na kero za

wananchi. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri mtusaidie Mheshimiwa Mkuu wetu wa Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kwenye Serikali za Mitaa; katika Halmashauri ya Nsimbo toka tumeajiri Watendaji wa Vijiji toka mwaka 2016 na tuliajiri Watendaji sita tu. Katika vijiji 54 vya Jimbo la Nsimbo tuna Watendaji wachache sana. Sasa hivi tunaenda kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, nilikuwa naomba hawa walioajiriwa, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri tumesikia Watendaji wa Vijiji pamoja na Watendaji Kata wanaajiriwa. Nilikuwa naomba sana kwa sababu tunaenda kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa, ninaomba kipaumbele cha kwanza wakishaajiriwa watuletee haraka ili waweze kuzoea mazingira ya maeneo yetu kwa ajili ya maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa pamoja na vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeza *Chief* wa *TARURA* kwa kazi ambayo anaendelea kuifanya na kumpongeza Mheshimiwa Rais ameendelea kutuongezea bajeti ya *TARURA* kila mwaka. Mwaka huu kutokana na mazingira yalitokea tunaomba kwa dharura kwa miezi hii miwili, mwezi huu wa Mei na Juni tunaomba pesa za dharura zingeenda kutokana na maafa makubwa yaliyotokea katika maeneo yetu, ukizingatia kama mimi Jimbo langu la Nsimbo kuna barabara sasa hivi zimekatika, kuna barabara kubwa ya kutoka Magamba – Kapalala – Mtakuja – Mtapenda, barabara ile tayari vile vijiji vyote takribani vijiji sita havina mawasiliano. Naomba sana pesa za dharura ziende haraka kwa ajili ya kuokoa haya maafa ambayo yametokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuipongeza sana Serikali, Serikali ilitoa taarifa mapema kuwa mwaka huu kutakuwa na mvua nyingi. Ninaomba kuipongeza sana Serikali kwa taarifa kwa kuwa wananchi walijiandaa ina maana hata hizi mvua zinanyesha na maafa haya yanatokea, wananchi hawashtuki kwa sababu mliwapa taarifa mapema. Hongereni sana Serikali kwa kutoa taarifa mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tutaendelea kuomba bajeti ya *TARURA* iongezeke kwa sababu *TARURA* ina mtandao wa barabara mrefu sana pamoja na madaraja, kuunganisha vijiji na vitongoji. Nilikuwa naendelea kuisisitiza Serikali iongeze bajeti ya *TARURA* kuhakikisha inapata pesa nyingi ili yale maafa na mambo yote ambayo yametokea katika maeneo yetu yaweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye upande wa afya; naomba kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutujengea Hospitali ya Mkoa, lakini kwenye Halmashauri yangu ya Nsimbo nilipata shilingi bilioni 2.8 kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya. Vilevile nina takribani vituo vya afya vine, lakini Kituo cha Ugala na Kituo cha Itenka bado miundombinu haijakamilika. Nilipokea shilingi milioni tano, tano katika vituo viwili, Kituo cha Ugala pamoja na Kituo cha Itenka. Ninaomba basi miundombinu ya vituo vya afya hivi viweze kukamilika kwa ajili ya maslahi ya Watanzania wa maeneo ya Nsimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru na kumpongeza tena Mheshimiwa Rais, maana yake hatukwepi kwa sababu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa. Sasa hivi tunajiringia tumepata shule katika maeneo ya vitongoji, shule za shilingi milioni 200, shule za shilingi milioni 500, shule hizo ni za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali yangu, ninajua hapa sasa hivi ajira ya walimu inaongezeka kila mwaka. Unakuta shule hizi tumejenga nzuri, zina wanafunzi milioni mbili, walimu wapo watano. Nilikuwa naomba sana walimu waongezeke, ajira ya walimu iongezeke sana kwa sababu ndani ya maeneo yetu walimu ni wachache sana. Pia naomba kuipongeza Serikali kwa kuendelea na jitihada ya kuongeza watumishi wa kada mbalimbali za afya pamoja na elimu, lakini bado ni wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tuongezewe walimu pamoja na kada ya afya, madaktari pamoja na manesi

tunaomba hizo ajira ziongezeke kwa sababu kuna zahanati mpaka sasa hivi unakuta mganga yuko mmoja au anakuwepo nesi (mhudumu) ambaye anahudumia. Sasa hivi mazingira yetu ndani ya vijiji vyetu yamebadilika, vijiji vimekuwa ni kama vile tarafa unakuta kijiji kinakuwa kikubwa, kina wakazi wengi, tulikuwa tunaomba ajira ya manesi pamoja na walimu wa sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kupongeza, sekondari zetu zimeendelea kupata pesa lakini tunaomba walimu wa sekondari waongezeke. Hawa walimu wana mafao yao ambayo yamekaa muda mrefu tulikuwa tunaomba basi yale mafao au zile likizo ambazo wanadai, waweze kupewa pesa zao ili waweze kufanya kazi vizuri kwenye mazingira mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninajua Mheshimiwa Rais alitamka akiwa Mwanza kuwa kipindi hiki ataanza kujenga nyumba za walimu. Nilikuwa nakumbushia nyumba za walimu ni muhimu sana kwa sababu tumejenga miundombinu mizuri ya shule za msingi na sekondari, lakini walimu wetu hawana mazingira mazuri. Naomba walimu wetu waweze kuwekwa katika mazingira mazuri, nyumba hizo ziweze kujengwa ili waweze kuwa na usalama zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kurudisha asilimia kumi fedha za mikopo ya wanawake, vijana pamoja na walemavu. Basi sasa hivi tunaomba, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri tunaomba hizo fedha ziwafikie wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikushukuru na naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anna Richard Lupembe. Ninamwita sasa Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mheshimiwa Charles John Mwijage ajiandae.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya nami nimesimama katika bajeti hii ya TAMISEMI na mimi kueleza mazuri na changamoto ambazo zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nikiifuatilia vizuri sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwanza nampongeza kwa kazi kubwa anayofanya yeye pamoja na timu yake, lakini pia nampa pole pia kwa changamoto za mafuriko lakini pamoja na changamoto kubwa alizokuwa nazo za mafuriko, hakusita kuwasiliana na Kamati wakati wote pale ambapo tulikuwa tukimuhitaji. Nikushukuru, nikupongeza lakini pia nikupe pole. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba kuzungumzia kuhusiana na athari za mafuriko. Katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuhusiana na athari za mafuriko ambazo zimeendelea kwa mvua hizi ambazo zinaendelea. Mimi nianze kuzungumzia kwenye Mkoa wetu wa Tabora. Mimi ni Diwani kwenye Manispaa ya Tabora na sisi pale kila mvua zinaponyesha hatukosi mafuriko. Kwa kweli hali ni mbaya na tumelizungumza sana jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, katika bajeti ambayo tutapitisha, tumeomba fedha kwa ajili ya kujenga mitaro ambayo itasaidia kuondoa ama kupunguza kabisa mafuriko kwenye maeneo yetu. Sisi wananchi wa Jimbo la Tabora Mjini tunaomba sana na Mheshimiwa Waziri naomba hili ulisikie na ninajua *engineer* yuko hapa atatusikia na atajua nini ambacho tunakihitaji kwa sasa watu wa Tabora ili kuondoa mafuriko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji mitaro katika eneo la Mwalitani. Tukijengewa mtaro mkubwa kwenye eneo la Mwalitani, tutakwenda kupunguza mafuriko ambayo yapo yanaanzia kwenye maeneo hayo. Tukijengewa mtaro katika Kata ya Uledi, pale Uledi mtaro ule ukiwa mkubwa Mheshimiwa Waziri, mafuriko yatakuwa historia katika maeneo hayo, lakini eneo la

Kitete kwenda Malolo, nalisisitiza eneo hili kwa sababu watoto wetu wengi wanaosoma katika shule ya sekondari ya Kitete iliyoko Malolo, kipindi cha mvua wanashindwa kwenda shule kutokana na mafuriko makubwa yaliyopo kwenye maeneo yale. Nimwambie Mheshimiwa *Engineer* Seff kwamba tunahitaji mitaro kwenye maeneo hayo ili tuweze kupunguza mafuriko katika Jimbo letu la Tabora Manispaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zipo barabara ambazo hazipitiki kabisa na ninaomba nizizungumze kwa haraka haraka. Niishukuru Serikali imetuletea fedha kwenye maeneo ya barabara nyingine ambazo angalau wananchi sasa wanapita, lakini tunayo barabara ambayo inatoka Uramba – Tumbi imefungwa kabisa haipitiki. Shughuli za wananchi hazifanyiki kwa sababu barabara hii haifanyi kazi. Pia tuna barabara ya Kalunde – Itaga na kule kuna hospitali ambapo wananchi wanatoka huko kwa ajili ya kupata huduma za afya, barabara hii haifanyi kazi kabisa. Mheshimiwa Waziri tunakuomba, Mheshimiwa *Engineer* Seff tunakuomba mtupelekee fedha wananchi wetu waweze kuendelea kufanya shughuli zao za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Usangu ambayo inakwenda Umanga ni huko huko Kalunde, wananchi sasa hivi kipindi cha mavuno hususani ya zao letu la tumbaku wanashindwa kupitisha mazao yao ili kuweza kupeleka sokoni kwa sababu barabara haipitiki. Kwa hiyo, niombe sana katika fedha zilizotengwa tukumbukwe wananchi wa Tabora hususani kwenye Jimbo la Tabora Mjini tupelekewe fedha hizi ili wananchi wetu waweze kunufaika na kuweza kufanya shughuli zao za kujiendeleza kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie suala la zima la wamachinga. Ni ukweli wamachinga Halmashauri ya Tabora Mjini wamepewa eneo, lakini eneo lile haliendani na hali halisi ya kufanya biashara pale. Kipindi hiki cha mvua ni hatari kweli kweli, jambo hili nililionesha kwamba watu wanashindwa hata kupita kwenda kununua mahitaji kwa wale wamachinga kwa sababu maji yamejaa, hawawezi kupita bila kuvuka mto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi niombe na nililiomba hili na ninaendelea kuliomba, tunaomba maboresho ya soko la wamachinga ili vijana wetu waweze kufanya biashara kwenye maeneo yanayokidhi badala ya ilivyo hivi sasa, mabanda yale hayakidhi, lakini pia eneo lile lina maji mengi kiasi kwamba yale maji yanaweza hata kusababisha maafa na athari kubwa kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala zima la hizi fedha za *CSR* na nimwambie Mheshimiwa Waziri hizi fedha za *CSR,* TAMISEMI ndiyo watumiaji wa fedha hizi kwa maana miradi inapopelekwa pale inatumika na wananchi wetu na wananchi wapo chini ya Wizara ya TAMISEMI, lakini fedha hizi zimekuwa kama shamba la bibi, fedha hizi zimekuwa hazina mwenyewe, fedha hizi zinatumiwa isivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema hapa na akatolea mfano wa Mkoa wa Dodoma na mimi nimwambie Mheshimiwa Waziri pamoja na hatua mnazokwenda kuchukua, lakini miradi hii imeishaanza kufanyawi kazi kwa mujibu wa taarifa ya Mkoa wa Dodoma ambayo Wabunge tunayo kwenye Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu haiwezekani ujenzi wa shule utumie zaidi ya shilingi bilioni 1.3; haiwezekani hata kidogo. Tunafahamu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshusha fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa shule, shilingi milioni 500 mpaka 600 zinatumika kujenga madarasa mengi na wanafunzi wanakaa wanasoma. Leo shule ya Msingi Chilonwa ipo Ihumwa inajengwa kwa shilingi bilioni 1.3, inajengwa na wamesema madarasa yapo katika hatua ya kupandisha kuta. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri umeambiwa na wamesema fedha hizi zizuiwe, kazi inaendelea sasa hivi wanapandisha kuta. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa mchango mzuri, lakini nimpe tu taarifa kwamba fedha hizi za *CSR* ambazo amezisema lakini pia zile za Vituo vya Afya katika Jiji la Dodoma zinatekelezwa na Wizara ya Ujenzi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ujenzi tumeishakaa na zile fedha bado hazijatumika.

Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba tayari tumeshachukua hatua kuhakikisha kwamba zile fedha zinaleta thamani ya miradi husika bila kutumika zaidi ya miradi iliyowekwa kwa mujibu wa mwongozo, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachofanya mimi ni ku-*quote* Randama ya Mkoa wa Dodoma ukurasa wa tisa. Kwa hiyo, haya anayosema yeye labda sijui kwamba ameya-*quote* wapi? Lakini hii ni Randama ya Mkoa wa Dodoma na hapa imeeleza vizuri tu kwamba ujenzi upo katika hatua ya kuta, sasa mimi nisemeje tena? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna uchimbaji wa visima vya maji, visima viliwi vya maji vimechimbwa Ihumwa na Veyula kwa shilingi bilioni moja na milioni mia tatu hamsini na moja. Wamesema hapa uchimbaji huo umekamilika na maji yamepatikana kwenye kina cha mita 150 na kwa sasa wanasubiri kuweka matenki. Mheshimiwa Waziri, fedha hizo unazipata wapi? Nani atakupa wakati kazi zimeanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa niseme kuna ujenzi wa kituo cha afya unajengwa Mahomanyika kwa shilingi bilioni 2.379. Tumeambiwa hapa kwa mujibu wa randama

sisemi maneno yangu! Randama inasema ujenzi huu wa Kituo cha Afya cha Mahomanyika mkandarasi yupo katika hatua za awali za ujenzi. Tunajenga kituo cha afya kwa shilingi bilioni 2.3 halafu tunajinasibu tunamsaidia Mheshimiwa Rais, tunamsaidia nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha…

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Mbunge ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI, taarifa hiyo ililetwa kwenye Kamati kama wasilisho la *draft* ya bajeti na utekelezaji, tulishachukua hatua na nimhakikishie kwamba fedha hizo za kujenga vituo vya afya bado hazijatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuweka kumbukumbu sahihi isije ikachukuliwa kwamba fedha hizo zimetumika kujenga kituo cha afya bilioni moja, bado hazijatumika na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ujenzi tayari tumekubaliana zitazingatia thamani ya fedha, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anajua, sana sana anachokifanya hapa mimi nimemwambia na kama ulituletea taarifa baada ya randama hii tupe, mimi ni mwanakamati. Mbona sina taarifa yoyote ambayo mmefanya

mabadiliko ya hili jambo? Mbona hakuna taarifa yoyote ambayo tumeletewa kuoneshwa kwamba hizi fedha hazijatumika? Kwa nini tunaambiwa kwamba mkandarasi yupo katika hatua za awali za ujenzi, hatua za awali ni zipi? Si watu wameanza kuchimba misingi? Si watu wameishaanza kufanya kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hiyo tu kuna ujenzi wa Kituo cha Afya cha Nala ambao utatumia bilioni 2.313, hizi ni fedha za *CSR. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinacho onesha…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wamenichukulia muda wangu naomba nimalizie.

**MWENYEKITI:** Naomba uhitimishe hoja yako.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachooneshwa kwenye fedha hizi ni ukosefu wa sheria madhubuti ya matumizi ya fedha hizi, lakini ni ukosefu wa uaminifu kwa watendaji wetu kwenye maeneo haya kukubali kupokea bajeti hizi na kusema wafanye utekelezaji wakati wanajua kabisa kwamba fedha hizi ni nyingi na haziendani na uhalisia wa vituo ambavyo vinajengwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles John Mwijage halafu niombe Mheshimiwa Charles Steven Kimei, ajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia Wizara hii Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenye Mungu mwingi wa rehema kwa kunifikisha salama asubuhi ya leo hapa Dodoma, ambapo nimetoka kwenye

kikosikazi cha Mwenyekiti Mama Chatanda tukishughulika na kukusanya vifaa kwa ajili ya akina mama wenzetu waliopata maafa Wilaya ya Kibiti, Wilaya Rufiji na hapo hapo nitoe pole nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge Mchengerwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kazi yako iliyotukuka kwa kuwahudumia wananchi wako kwenye mafuriko na hii ni historia yako tangu mafuriko ya mwaka 2016, 2019 siku zote upo pamoja na wananchi wako. Nimpongeze pia kaka yangu mwingine Mheshimiwa Twaha Mpembwene kwa kazi nzuri na yeye anayofanya, kiujumla niishukuru Serikali yetu kwa kutukimbilia kwenye mafuriko haya na kipekee kwa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuwasilishia tani 300 za chakula na wadau wote mnaojitokeza kutuchangia mafuriko haya ambayo ni makubwa na maeneo mengine ambayo tutaelekea Morogoro, Mkoa wa Mbeya na Arusha sisi kwa upande wa UWT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili niliona nije kuchangia Wizara hii kwa sababu nimeamini Wizara hii Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa umemleta Mheshimiwa Rais ndani ya Bunge hili, kutokana na kazi nzuri aliyofanya umemleta Mwenyekiti na leo umeileta nchi hapa Bungeni, Wakuu wa Mikoa wote, Wenyeviti wa Chama, Makatibu wa Mikoa na Wajumbe wa *NEC* ambao ni wasimamizi wa utekelezaji wa Ilani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposimama leo kuchangia Wizara hii, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ninajisikia fahari kubwa kwa kushuhudia kazi nzuri iliyofanywa na Ofisi hii ya Rais, TAMISEMI na Serikali yetu ya Awamu ya Sita katika maeneo mbalimbali. Nasema hivyo kwa sababu nikiwa kama Mjumbe wa Kamati ya Utekelezaji UWT Taifa, chini ya uongozi wa Mama Mary Chatanda na Mama Zainabu Shomari Makamu wake tulifanya ziara katika Mikoa ya Tanzania Bara 13 ukiwemo Mkoa wa Njombe, tulikwenda Lindi, Mtwara, Ruvuma, Singida, Tabora, Shinyanga, Simiyu, Geita, Kagera na Dodoma, na kote huko tumeweza kufanya pamoja na mikutano ya hadhara 854 katika kata 854,

kipekee tumetembelea miradi 869 yenye thamani ya shilingi bilioni 670, hakika TAMISEMI ni ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi kama Subira na kama Mjumbe nilipangiwa miradi 94 yenye thamani ya shilingi bilioni 90, ninasimama ndani ya Bunge hili kusema kwa kweli *site* kipo kishindo cha Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kazi nzuri katika sekta mbalimbali, maono yake yametafsirika *site*. Maono ya sekta ya afya, tumeona majengo ya dharura kwa mara ya kwanza tangu tumepata uhuru; maono kwenye sekta ya elimu, tumeona shule za wasichana za sayansi kwa mara ya kwanza tangu tumepata uhuru, tumeona shule za msingi mpya, tumeona mabweni, tumeona maabara, tumeona miradi ya maji, tumeona miradi ya barabara, na tumeona mambo chungu mzima, hakika Mheshimiwa Rais apewe maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kwa wale wanaohoji kwanini kila jambo tunamtaja Mheshimiwa Rais? Yeye ni Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri lakini ni Mwenyekiti wa Chama chetu anakisimamia pamoja na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na ndiye mwenye maono ya asilimia zote ni lazima tutamtaja kama ambavyo wanamtaja kwenye changamoto mbalimbali zilizosalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimtie moyo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, *site* kumetakata, sisi tumeshuhudia Jumuiya pekee iliyotembea nchi nzima ni UWT chini ya uongozi shupavu wa Mama Mary Chatanda na Mama Shomari, tumeona kwa macho yetu, kuona ni kuamini kwa hiyo hatusimuliwi, hongera Mheshimiwa Waziri Mchengerwa, hongera Naibu Waziri Mheshimiwa Zainab Katimba kwa kuteuliwa, tunaamini unaweza na hongera Naibu Waziri Mheshimiwa Dugange na watendaji wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kwamba nimesemea kwenye ziara yetu, lakini ndani ya Mkoa Pwani mambo ni mazuri katika sekta zote. Sekta ya elimu ndani ya miaka mitatu tumepokea shilingi bilioni 75, tumeshuhudia shule hizo nilizosema mpya, tumeshuhudia mapinduzi makubwa ya elimu, madarasa

zaidi ya 863. Nataka niupongeze uongozi wa Chama Cha Mapinduzi, Mwenyekiti wetu Mzee Mlao na Mkuu wetu wa Mkoa hapa kwa kazi nzuri na Wakuu wa Wilaya wote wanaotufanyia ndani ya Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mapinduzi kwenye hospitali yetu ya Tumbi, kwa mara ya kwanza tuna kitengo cha *dialysis* pale, kwa mara ya kwa tuna wodi ya *ICU,* tuna jengo la dharura, tumeziona *EMD* tano katika Mkoa wetu, tumeona maboresho hospitali za wilaya katika mkoa wetu, tumeona vituo vya afya vipya kumi ndani ya mkoa wetu kwa kipindi cha miaka mitatu. Tunasema hakuna kama Mama Samia na ni ukweli katika sekta hizi amefanya makubwa kuliko kipindi chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niseme mambo mawili ambayo ni changamoto ninazoziomba kwenye Wizara hii. Naomba kwa kuwa mimi ni Mbunge wa Mkoa, ninaishi katika Wilaya ya Bagamoyo, ninakuomba Mheshimiwa Waziri hebu tafakari masuala ya Mamlaka ya Miji Mdogo. Wilaya yetu ya Bagamoyo ina Mamlaka ya Mji Mdogo ya zaidi ya miaka kumi tano, inabeba vitongoji zaidi ya 167, uendeshaji wa halmashauri ya wilaya na uendeshaji wa Baraza la Mji wa Bagamoyo imekuwa ni ngumu. Nikuombe Mheshimiwa Waziri tunayo *master plan* tayari, tunao mpango wa kuvipunguza vitongoji 167 kwenda mpaka mitaa 60. Wenyeviti wa Vitongoji siyo Wajumbe mahsusi kwenye *WDC,* inakosekana maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Mji Mdogo wa Mlandizi, tunao Mji Mdogo wa Kibiti, kwa hiyo naomba Wizara mfanye tafakuri tunapoelekea uchaguzi wa vijiji na vitongoji, miji midogo yote hapa nchini iweze kupandishwa hadhi kama ina vigezo vilivyostahili ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Bagamoyo ili kuwapunguzia wananchi gharama za kufuata huduma kwenye ofisi za kata, kwa kuwa kwenye vitongoji hakuna Watendaji wa Vitongoji na nimeona katika hotuba yako kuna mpango wa kuajiri Watendaji wa vijiji. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri tutazame kwenye Mamlaka za Miji Midogo irasimisheni yenye vigezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Mji Mdogo wa Chalinze pia, vilikuwa vijiji vimepoteza hadhi, vipo vitongoji na kuna mambo mengi yanafanywa kisera ya vijiji, kwa hiyo inapokuwa vitongoji tunakosa haki fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ninaishukuru sana *TARURA,* ninampongeza Mtendaji Mkuu wa *TARURA* pamoja na Serikali kwa kuongeza bajeti kwa kiwango kikubwa mpaka imefika shilingi bilioni 854 kwa bajeti hii kutoka shilingi bilioni 200 na kitu, haya ni mapinduzi makubwa. Namwomba kwenye barabara zetu kwa mfano barabara inayotoka kwenye Kata ya Mapinga imekuwa ikilalamikiwa sana, Kiembeni - Mingoi na maeneo ya Kiharaka wananchi wenyewe wanajichangisha kuziba viraka maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ipo barabara ya Mtaa wa Kisutu nayo haipitiki, lakini ipo barabara ya Chalinze – Talawanda kwenda Magulumatali kwenda Kiwangwa nayo ipo chini ya *TARURA*, tunaomba pamoja na dhamira ya kushughulikia maeneo ya mafuriko yaliwaharibia miundombinu kwa haraka, lakini bajeti hii tunaomba katika maeneo yaliyokusudiwa yaanishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono bajeti ya wananchi, naomba nikushukuru kwa kumleta Mheshimiwa Rais Bungeni, tumemuona na kazi yake ni njema na tunamtakia kila la kheri, tunamuunga mkono na haina kufeli, Rais itakuweka madarakani 2025. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, muda wako umeisha.

Waheshimiwa Wabunge, mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu atakuwa Mheshimiwa Charles John Mwijage, muda hauturuhusu kuwa na wachangiaji wawili, nilimtaja Mheshimiwa Kimei lakini ninamwomba awe mchangiaji wa kwanza tutakapoanza Bunge mchana. Nikuite sasa Mheshimiwa Charles Mwijage.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikupe hongera, nikupe hongera kwa kukalia kiti hicho na

nikushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia bajeti ya wananchi yaani bajeti hii ni wananchi wote acha wale wengine wananchi wa Mamelodi, hii ni ya wananchi wote, popote unapoishi TAMISEMI inakugusa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasahau napenda kuunga mkono bajeti hii na ninapounga mkono bajeti hii nizungumze na Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri Mchengerwa pale ulipotuacha na *shemela* sasa kwetu Kagera ni tofauti na kwingine. Wasanii wanashindana kusherehekea, kuna sherehe na jana Ndugu Saida ametoa rekodi mpya, kwa hiyo haya tunayosikia mengine sisi tumeshatoka tupo *another level,* tunajiandaa kusherehekea mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza TAMISEMI ni bajeti ya wananchi ni bajeti ya nchi kwa kuangalia *asset* zote, *asset* zote zinazozungumzwa ziko TAMISEMI, ukihesabu hata watu, watu milioni 60 *plus* wako TAMISEMI. Sasa mimi naichangia bajeti hii kwa mambo matatu; moja nitashukuru, pili, nitaomba na tatu ambayo ni ngumu nitashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani kwa Serikali na mimi nilisoma hesabu *primary*, ukichukua Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ywa mwaka 2020 mpaka 2025, ukahesabu kwa thamani *(the value),* ukachukua tarakimu zile ukalinganisha na kazi iliyofanyika mpaka sasa kwa *value, value to date* inazidi tulichoahidi kwa miaka mitano, anayebisha tunaweza kukutana kwenye kompyuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo naishukuru Serikali, lakini nikirudi kwetu Mheshimiwa Mchengerwa nikushukuru tena, nashukuru na nina salamu rasmi kutoka Rutoro, Naibu Katibu Mkuu wako alinipigia simu na watu wa TAMISEMI nimewapenda waliposikia natangazwa kuzungumza mwingine kanipigia simu kwamba kuna vifaa vyangu vinapelekwa jimboni, ahsante sana Mheshimiwa Mchengerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ulipokuja Muleba tulikuambia tuna mpango wa kuwarudisha watoto kutoka

ujombani kwenda nyumbani kwao, zile sekondari saba ulizosema ziende zijengwe mara moja, tukianza na Makongora ziko usawa wa *finishing*, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunakukaribisha wewe na wasaidizi wako mje tuna sherehe kubwa. Ile sherehe za mwaka 2025 sisi tunaanza mwezi wa saba na hatuna mtu wa kutuzuia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaposema kuifungua nchi maana yake ukimuuliza mtu ambaye yeye alikuwa hajui barabara kama watu wa Ngenge, ukiwauliza watu wa Kamgaza watakuambia kwamba nchi imefunguka na wataalam wa lugha wanakwambia ndiyo uzuri wa kuwa na dereva mkongwe, unapokuwa na dereva mkongwe kama mimi anajua njia zilizoziba anaweza kuzifungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru Serikali kwenye suala la mapato na nitakuja kutoa ushauri. Tumeona kutoka *site,* lakini pia tumeona kwa takwimu, mapato yamekuwa yakiongezeka. Kubwa zaidi na nitashauri ni kwa sababu ya mifumo. Naiomba Serikali kuna kazi ndogo ndogo ambazo zimebaki nyuma, Kituo cha Afya Izigo mlipotoa shilingi milioni 250 hamkuendelea najua kama hawakupewa wao alipewa mwingine. Sasa ningeomba ni wakati mzuri kwa sababu ndiyo njia panda unapopita Mheshimiwa Mchengerwa kila siku, Kituo cha Izigo ukimalizie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Mchengerwa pale kwenu Kamachumu kwao na Mheshimiwa Subira, Mheshimiwa Subira alipokuja aliona jengo la wananchi akaahidi. Sasa usimuangushe Mheshimiwa Subira pale Kamachumu alichoahidi amalizie. Yule kijana wako alinipigia simu anasema ile mitambo ya *mortuary* ya Kamachumu inapelekwa sasa hivi aliposikia nakwenda kuchangia. Unajua watu wa Kamachumu wana ndugu zao Ulaya na wapi, kwa hiyo, mtu akifa lazima apelekwe *mortuary* kusudi jamaa zake waweze kuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo maombi; uliniahidi barabara ya kwenda Rutoro. Unajua kwa maelekezo yako na kutoka mamlaka iliyo kuu mmeahidi kwamba shule tatu zijengwe

Rutoro lakini barabara itanikwamisha. Naomba *Chief* wa *TARURA* anifanyie wepesi, angalau anipe barabara za kufika, kusudi tuweze kukamilisha kazi ya watu wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile utajua kuwa wilaya yangu ina *square kilometer* 10,200; na *square kilometer* 7,200 ni maji zenye visiwa 38. Niliomba na naendelea kuomba unisaidie boti iendayo kasi imsaidie Mkuu wa Wilaya aweze kutawala vizuri hiyo sehemu, lakini iweze kuwahudumia watu wanaofanya kazi kule. Unajua katika eneo hilo la *square kilometer* 7,200 mapato ya ndani ni shilingi bilioni saba. Nilikuwa naomba hayo mahususi machache unitekelezee hayo kusudi wale watu wako roho zao ziridhike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye makusanyo; umeweza au tumeweza kukusanya kwa sababu tuliwekeza kwenye mifumo. Ninakuomba na ninakushauri uwaelekeze walioko chini yako wasi-*base* kwenye *personality* kwamba, huyu akiwekwa hapa ndiyo atakusanya. Tutengeneze mifumo na sisi Wabunge wa Muleba tumeshamuandikia Mkurugenzi aliyeletwa yule. Tunataka kumuelezea mifumo inavyofanya kazi. Mambo ya *personality* au huyu mtoto wangu hayawezi kuleta makusanyo. Makusanyo yamewezekana kwa sababu uliwekeza katika mifumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine una rasilimali nyingi, kwa sababu una rasilimali nyingi lazima utumie mtindo wa mameneja. Meneja yeyote ana sifa tatu; kwanza Meneja anapewa majukumu yaliyo wazi *(clear responsibilities);* pili, anapewa mamlaka; na tatu, anaambiwa wazi usipotimiza haya nini kitakupata. Mambo mengi yanayohojiwa na CAG na watu wengine ni kwa sababu watu hawana sifa za umeneja. Kama mtu ana majukumu yako wazi na kama ana mamlaka kwa nini anapokwenda ndivyo sivyo asiwajibike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala lingine yanakwenda pamoja, kama Mkurugenzi amepewa majukumu yake, Mkuu wa Wilaya asimuingilie; majukumu aliyopewa Mkuu wa Wilaya, polisi asimuingilie; lakini wote wafanye kazi kama timu, ndicho kitu

ambacho tunakuomba kwa rasilimali zote ulizonazo, tukiwemo na sisi watu lazima twende kwa mfumo wa kimeneja. *Butcherer* yule anayekata nyama kwenye *butcher* nikimkuta *mortuary* nitashangaa kwamba amekwenda kufanya nini. Kwa hiyo, kila mtu ajue anakwenda kufanya kazi wapi kusudi tuweze kutekeleza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la mwisho, sekta za kiuzalishaji; umekusanya kutoka wapi? Umekusanya kutoka kwenye sekta za kiuzalishaji. Kwa hiyo, lazima hata bila kuweka pesa, watendaji wa sekta za kiuzalishaji walioko katika sekta yako wapewe jukumu lao *(KPI)* la kuhakikisha mapato yale yanawezekana. Wao wasiwe vikwazo wa kutengeneza shughuli, wao wasiwe vikwazo vya watu kufanya biashara, lakini wao kwa mfano mimi huwa nasema watu kukutwa wanazurura ni ukosefu wa utendaji bora au utawala bora. Kwa nini, wale Makatibu Tarafa na Wakuu wa Wilaya na migambo wasiwakamate watu na kwenda kuwaonesha kazi ya kufanya? Kwa hiyo na yenyewe hiyo ni katika zile *KPI* ambazo zinapaswa kuwekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nataka kumalizia, niweke dogo kitendawili cha miundombinu na rasilimaliwatu. Mheshimiwa Waziri tunaomba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Naomba uhitimishe hoja.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitimisha kwa kuzungumzia kitendawili cha miundombinu na rasilimali watu. Kama tumejenga shule na hospitali tupigane chini/juu, tupeleke wataalamu kwenye miundombinu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa mara ya pili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwijage.

Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa shughuli kwa mchana huu, lakini kabla sijahitimisha kuna Taarifa ya *Bunge Marathon* iliyofanyika Jumamosi Aprili 13, Uwanja wa Jamhuri Dodoma, nitaomba niilete kwenu.

Mbio za hisani za *Bunge Marathon* zilifanyika kwa mara ya kwanza siku ya Jumamosi, terehe 13 Aprili, 2024 kwa lengo la kuchangisha fedha kwa ajili ya ujenzi wa Shule Maalum ya Sekondari ya Wavulana ya Bunge ya kidato cha tano na sita. Mbio hizo zilikuwa na kaulimbiu isemayo; "Shiriki michezo kwa maendeleo ya Taifa letu."

Kamati inawashukuru wananchi, wakimbiaji kutoka ndani na nje ya nchi walioshiriki katika *Bunge Marathon 2024*. Mbio hizi zilikuwa na ubora wa hali ya juu na zilizingatia taratibu na kanuni zinazosimamia mbio hizo. Aidha, tunawapongeza washindi wote wa mbio za *Bunge Marathon* ambao kwa jitihada zao waliweza kutunukiwa zawadi mbalimbali ikiwemo medali, fedha na tiketi za ndege.

Wito unatolewa kwa watu wote kutoka ndani na nje ya nchi, kuendelea kujitokeza katika mbio za *Bunge Marathon* katika siku zijazo. Bunge linatoa shukrani za dhati kwa wadau wote waliounga mkono na kufanikisha mbio hizo kwa kuchangia fedha, vifaa na kutoa wataalam. Tunavishukuru vyombo vya habari hususan *Azam TV* na *TBC* kwa kuhamasisha na kurusha matangazo mubashara. Tunapenda kutoa wito kwa wadau mbalimbali hasa tuliowaomba kuchangia mradi huu, kuendelea kutuchangia fedha au vifaa vya ujenzi kwa ajili ya mradi huu muhimu kwa maendeleo ya kielimu kwa vijana wetu wa kiume na kudumisha azma ya Serikali ya kuwaendeleza vijana wote wa kike na wa kiume kwa usawa pasipo kuwabagua.

Michango ya fedha inaweza kutolewa kupitia akaunti za benki au lipa namba za kampuni za simu zilizoainishwa katika matangazo yetu. Watakaopenda kuchangia vifaa wawasiliane na Ofisi ya Bunge.

Kamati inawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuonesha mfano kwa vitendo, ambapo kila mmoja amechangia fedha ili kufanikisha jambo hili. Aidha, tunawapongeza sana watumishi wa Bunge chini ya usimamizi wa Katibu wa Bunge, kwa utayari wao wa kuchangia fedha zitakazotumika katika ujenzi huo.

Kipekee, Kamati inamshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa wazo hili la kujenga Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Bunge ya kidato cha tano na sita. Hakika jambo hili ni jema na litaendelea kuwa alama itakayodumu kwa muda mrefu katika Bunge hili. *(Makofi)*

Kwa kuhitimisha, Kamati ya Maandalizi chini ya uongozi wa Mwenyekiti, inawashukuru sana kwa ushirikiano ambao mmeutoa. Imesainiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya *Bunge Marathon,* Mheshimiwa Festo Sanga. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tutakaporejea wachangiaji wetu watakuwa kama ifuatavyo, mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Dkt. Stephen Kimei, kama nilivyosema, wa pili atakuwa Mheshimiwa Dkt. Christine Christopher Mnzava na wa tatu atakuwa Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, tuanze na madaktari kwanza.

Baada ya kusema hayo nasitisha Kikao hiki cha Bunge mpaka saa 11.00 jioni. *(Makofi)*

*(Saa 7.05 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na wachangiaji wa mchana huu, nimwite sasa Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa hii. Mimi nianze kwa kumshukuru sana na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mambo anayotekeleza na Ilani ya CCM anayoitekeleza kwa kasi ambayo ni ya kutisha. Niseme kwamba hata mimi wananchi wangu wa Vunjo wameniambia nipeleke maua, nimletee maua. Kule tulikopita tukikimbiza Mwenge, tumekimbiza Mwenge tukikagua miradi ambayo Mheshimiwa Rais wetu ametupatia. Tulikagua miradi zaidi ya shilingi bilioni mbili kwa Mwenge na yote ikapita vizuri, ilisimamiwa vizuri na watendaji wake aliotupatia pale kwenye mkoa wetu akiwepo Mkuu wa Mkoa mpendwa wetu Mheshimiwa Nurdin Babu pamoja na usimamizi wa chama, Mwenyekiti wetu wa Chama Mkoa Ndugu Patrick Boisafi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kwamba Mheshimiwa Rais atatuachia hawa watendaji wanaotenda vizuri ili tuweze kumhakikishia ushindi wa kishindo mwaka 2025; kura zote aweze kuzipata na mimi nitazileta hapa na ninaamini kwamba pia ataona ushindi huo kwenye uchaguzi huu wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024. Kwa hili ninataka nimhakikishie hilo Mheshimiwa Rais, kwamba hayo maua siyo ya uongo siyo ya porojo, ni ya kweli, na kama siku atapata nafasi ikimpendeza nitampelekea pale Ikulu aweze kuyaona maua ya kweli na siyo ya maneno tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Mchengerwa, kusema kweli ninatoa shukrani za pekee kwa Waziri. Alitembelea jimboni kwangu kwenye Mkutano Mkuu wa Jimbo na akazungumza maneno mazito ambayo naamini yalijenga sana chama na yalijenga sana Serikali, alimzungumzia Mheshimiwa Rais na yote anayofanya pamoja na kwamba sisi tunafanya, lakini yeye aliyazungumza kwa ufasaha ambao anao. Kwa hiyo, ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninawashukuru Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Dkt. Dungage na Mheshimiwa Zainab Katimba ambao naamini wanamsaidia, na ndiyo sababu tunamwona Mheshimiwa Mchengerwa anaweza kumudu kusimamia mafuriko haya ambayo yanaleta madhara mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudi sasa kwenye suala zima la bajeti ya TAMISEMI. Kwanza naipongeza TAMISEMI, bajeti yao hii wameanza kwa kuzungumza maneno mazito kuhusiana na kuongeza mapato ya Serikali za Mitaa. Kusema kweli mapato ya Serikali za Mitaa ni madogo sana, wamesema yanaongezeka mwaka huu wa 2024/2025 yataongezeka kwa asilimia 23 kutoka shilingi trilioni 1.14 mwaka 2023/2024 kwenda shilingi trilioni 1.41. Hili ni ongezeko la asilimia 23; ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninaamini bado kuna mianya mingi na kuna vyanzo vingi ambavyo vimejificha, na ninaamini kwamba ni vizuri wakaangalia vizuri, na hasa baada ya kufungamanisha mifumo ya ukusanyaji kodi zile za ardhi pamoja na kodi ya majengo na mabango, baada ya kuyarejesha kwenye Serikali za Mitaa, basi waweze kujiwekea lengo kubwa zaidi. Naamini Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati anapoandaa ile *finance* ataona ni namna gani aongeze, kwa sababu usipojipa *a stench target* ina maana kwamba utabakia chini, utabweteka. Utafikia hiyo *target* mapema unaona hapa nimemaliza hiki kitu, kumbe ungeweza kupata zaidi endapo *target* ingekuwa iko juu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini hilo ni jambo zuri na ninaamini pia kwamba *issue* hii ya *carbon trading* ambayo

mapato yameanza kupatikana, tutajua zaidi kwamba mapato yanapatikana na yanagawanywa kwenye halmashauri zile na ni ngapi zitakwenda kwenye Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwenye ahadi; suala ni kwamba ahadi ni deni. Tulinadi Ilani ya Chama Cha Mapunduzi mwaka 2020, tukawaeleza watu kwamba tutaleta hiki na hiki na hiki. Kwa upande wangu wa Vunjo nilisema kwamba kwa mfano, barabara ile ya Kilema inaitwa barabara ya Nyerere ambayo ni Pofo – Mandaka – Kilema ingewekwa lami, ila haijakamilika na ni kitu ambacho pia kilipewa ahadi na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tulisema kwamba barabara ya Uchira kwenda Kisomachi nayo itapata lami, lakini pia tulisema kwamba barabara ile ya Mabogini, barabara inaanza Kahe – Chekereni, Kahe – Mabogini – *TPC* nayo itapata lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alipokuja pale kwetu Himo akatoa ahadi ya kwamba barabara ya Himo Sokoni kwenda Lotima nayo itapata lami, lakini nasikitika kwamba pale wamefanya kidogo, hapo Himo kuteremka kwenda Lotima imefanywa mita 800, *which is a joke,* na kule kwingine wamefanya danadana, haiendi sana. Kwa hiyo, watu bado wanasubiri na ninaamini hilo ni jambo litakalonipa matatizo kidogo. Unajua tunamaliza muhula, mimi ninaona kama tumemaliza muhula kwa sababu hii ni bajeti yetu ya mwisho tunayoweza kupitisha na inaweza kutusaidia chochote kwenye kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze moja ambalo nitamwomba Waziri anapokuja kuhitimisha atuoneshe ni namna gani atatuongezea chachandu pale Himo, mji ule ni giza. Mheshimiwa Waziri tunaomba ututengee fungu ambalo litaweka taa katika Mji wa Himo angalau chache kwa kuanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba nashukuru, Serikali imefanya mambo mengi sana kama nilivyosema. Tulikuwa na bajeti ya mwaka huu, kwa mfano bajeti kuu ya jimbo langu ni kama shilingi bilioni 12, hizo ni fedha ambazo kwa miaka mitano

ya awamu ya tano hatukuzipata kwenye jimbo lile, lakini tumezipata kwa mwaka huu mmoja. Kwa hiyo, ni jambo kubwa na watu msione wivu, mimi nilimwonea wivu Mheshimiwa Kilango, lakini na mimi nikaangalia kwangu niko vizuri. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutupatia hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata fedha na niseme kwamba tumepata vituo vya afya vitatu. Tulikuwa hatuna kituo cha *virtually* cha Serikali, kilikuwa ni mfano wa Kituo cha Afya Mwika pale Msae, lakini sasa tumepata na wameweza kutukarabatia kile Kituo cha Kirua Vunjo na wametupatia Kituo kipya cha Marangu na kingine cha kule Kahe Magharibi. Naishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimebakia sasa hiki kituo kikongwe cha Mwika Msae, pale kinahitaji ukarabati na kuongezwa majengo ya mama na mtoto, jengo la upasuaji na jengo la maabara. Kwa hiyo, ninaamini kwamba hili litafanyika katika hii bajeti inayokuja kwa sababu ni jambo ambalo tulikuwa tumeliahidi, na ninaamini ni jambo ambalo litatusaidia kutupeleka mbele kwenye mambo yetu tutakayokwenda kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *issue* ya uwekezaji, kwenye mapato kuna watu wanasema tuongeze tena au tuingize tozo kwenye simu. Mimi nawaomba jamani tusiweke tozo kwenye simu kwa sababu hizi simu kusema kweli ni fursa kwa wawekezaji, hata kwa vijana wadogo wadogo, ni fursa kwa mambo mengi tunayoyafanya ya kiuchumi. Kwa hiyo mimi naomba tusiguse simu tena. Tuendelee na nyingine kama hizi *carbon trading* na mengine mengi kama nilivyosema, tuongeze mapato ya halmashauri na ya mamlaka za Serikali za Mitaa, tulijaribu kuongeza huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye uwezeshaji, mimi ninafikiri hivi, sasa hivi hakuna kituo au mahali pamoja ambapo mtu anaweza akasema mjasiriamali ukienda utapata ushauri wa uwekezaji na utaweza kupata mkopo au fedha. Kuna ile mifuko yetu mingi ambayo tunasema sijui mifuko ya uwekezaji 64, mimi nashauri hivi, Mheshimiwa Waziri aje azungumze na Mheshimiwa

Waziri wa Fedha ili tuweze kurekebisha Sheria ya *TIB* iinyime *TIB* kutoa mikopo kwa wateja wakubwa wa biashara na badala yake ijikite kwenye kuanza ku-*manage* zile fedha za wawekezaji, wazi-*manage* na iwe ni kwamba ni benki ya wajasiriamali na benki ya *startups*/watu wanaoanza miradi watapata ushauri *(advisory services)* pale, wanaweza kufanya biashara na wakaanza biashara kwa namna ambayo wameshapata kile kinachoitwa ni *incubation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo mimi nashauri lifanyike na ninaamini hilo litaleta utofauti mkubwa. Hata hiyo *issue* ya asilimia kumi kwa uwiano wa 4:4:2 wangeweza wakafungua pia hiyo hiyo benki ikawa na uwezekano...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kimei, muda wako umekwisha. Naomba uhitimishe.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umeisha mapema, lakini naunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kimei, nimwite sana Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Ishengoma Kikoyo, Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na mimi kunipa nafasi kuweza kutoa mchango wangu kwenye hotuba iliyopo mbele yetu, hotuba ya TAMISEMI.

Kwanza niwapongeze sana Waziri pamoja na Naibu Mawaziri kwa kazi kubwa ambayo mnafanya. Kwa kweli Wizara ya TAMISEMI ni Wizara ambayo inaakisi wananchi wa Tanzania, ni Wizara ambayo zaidi ya asilimia 80 iko huko vijijini. Wizara hii ina kazi kubwa sana. Kwa hiyo, nawapongeza kwa kazi kubwa

ambazo mnazifanya, lakini nawapa pole kwa yale ambayo yanaendelea katika halmashauri mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mungu ametujalia tumeweza kupata mvua, lakini mvua hizi zimeweza kuleta madhara. Kila halmashauri kwa namna moja ama nyingine imeathirika na mvua hizi, barabara zimekatika, hakupitiki, hakuna mawasiliano, lakini pia tumepoteza watu wengi sana. Kwa hiyo nawapa pole sana, nampa pole Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya. Ukiangalia kwa mwaka wa fedha huu ambao tunakwenda kuumaliza, katika Mkoa wa Shinyanga zaidi ya asilimia 70 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge hili zilipokelewa, haijawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote nimekuwa nikiuliza, ni kwa nini mpaka tunafika bajeti nyingine fedha zinakwenda chini ya asilimia 50, lakini kwa mwaka huu wa fedha tunaoumaliza Mkoa wa Shinyanga umepokea zaidi ya asilimia 74. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliidhinishiwa takribani shilingi bilioni 243 na mpaka sasa hivi tumekwisha kupokea zaidi ya shilingi bilioni 171, sawa na asilimia 70. Ninaamini Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan ina dhamira thabiti ya kuwatumikia wananchi kwa weledi. Katika Mkoa wa Shinyanga, mimi nitazungumzia Mkoa wangu wa Shinyanga kwa sababu wanawake wa Mkoa wa Shinyanga walinichagua ili niwawakilishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Shinyanga katika sekta ya elimu tumeweza kuongeza shule 24 na mojawapo ikiwa ya wasichana ambayo iko Manispaa ya Shinyanga. Watoto wa kike walikuwa wanapata shida sana, ni vizuri kuchanganyikana *gender* zote lakini inapofika kwenye ule umuhimu wa mtoto wa kike na *risk* ambazo anakutana nazo, kwa kitendo cha Mama Samia kutoa fedha kujenga sekondari za wasichana kila mkoa

kwa kweli imesaidia sana kuweza kuongeza ufaulu wa watoto wetu, hasa watoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za msingi nazo kwa Mkoa wa Shinyanga tumeongezewa, tumejenga shule 26, kutoka shule 586 mpaka kufikia shule 612 mwaka 2021 hadi 2023. Kwa kweli kwetu sisi Mkoa wa Shinyanga tuna kila sababu ya kumshukuru Mama Samia kwa sababu Mama Samia ndiye mwenye Serikali, ndiye Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi. Tuna kila sababu ya kumpongeza, iwe asubuhi, iwe jioni, iwe usiku, ni lazima tumpongeze kwa sababu ndiye aliyebeba Ilani ya Chama Cha Mapinguzi, ndiye anayenadi Sera za Chama Cha Mapinduzi na ndiye aliyebeba dhamana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye vyumba vya madarasa vimeongezeka, ukija kwenye maabara zimeongezeka kutoka maabara 236 mpaka maabara 293; vijana wanajifunza kwa vitendo. Hapo nyuma ilikuwa mtoto anachukua masomo ya sayansi, lakini hana sehemu ambayo anaweza ku-*practice,* lakini kwa sasa hivi kwa fedha ambazo zimetolewa vijana wanapata fursa ya kuweza ku-*practice* masomo ambayo wanayasoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye sekta ya afya; sisi Wabunge ni mashahidi, Bunge lililopita tulishuhudia *ambulance* nyingi zimepaki hapi nje. Kila Mbunge katika jimbo lake alipata *ambulance*. Hata kama hajakabidhiwa mpaka leo lakini *ambulance* zipo, hii ni *achievement* moja kubwa sana. Hii inamaanisha nini? Vifo vya akina mama wajawazito vimepungua, tumeona kabisa kwamba vifo vimepungua. Kwa hiyo, tuna sababu ya kuishukuru Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi kwa jitihada kubwa ambazo zinafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya afya japo kuna mazuri yanafanyika, lakini kuna mapungufu, tumeona bado kuna upungufu mkubwa wa wafanyakazi. Kunapokuwa na upungufu wa wafanyakazi ufanisi wa utendaji kazi unapungua, lakini kumekuwa na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali kwa

wale wafanyakazi ambao wanakiuka misingi na maadili ya utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iliweza kutokea katika Wilaya yangu ya Kahama, wafanyakazi walifanya uzembe, mama akafariki akiwa hospitali na Serikali iliweza kuchukua hatua *immediately*. Japo tulimpoteza yule mama, lakini Serikali ilionesha utayari wa kushughulika na matatizo kwa haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi kile alikuwepo Mkuu wa Mkoa dada yangu Mheshimiwa Christina Mndeme, aliunde tume na ile tume ilifanya uchunguzi; lakini Serikali kwa kutumia vyombo vyake nayo ikaunda tume. Tume ile ilichunguza ndani ya wiki mbili ikaweza kugundulika kwamba ni kweli wafanyakazi wale walifanya uzembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, wafanyakazi wanapokosea sehemu moja kuwapeleka sehemu nyingine siyo kutibu tatizo kwa sababu tabia aliyokuwa nayo katika kituo "x" atakwenda kuifanya kituo "y". Kwa hiyo, ninaomba sana mabaraza ya kitaaluma yachukue hatua ambazo ni kali kuweza kutoa fundisho kwa wale ambao wanakiuka...

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Dkt. Ishengoma kuna taarifa kutoka kwa Naibu Waziri.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siyo Dkt. Ishengoma, ni Dkt. Mnzava.

**MWENYEKITI:** Samahani, Dkt. Mnzava.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, nakushukuru na ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava kwa mchango mzuri; lakini nimeomba tu nimpe taarifa kwamba Ofisi ya Rais TAMISEMI chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri tulishakubaliana, kama ambavyo tulifanya Kahama, bila kuhamisha watumishi waliofanya makosa, mtumishi yeyote akifanya makosa kwenye sekta ya afya adhabu yake siyo kuhamishwa kituo kupelekwa kituo kingine. Adhabu yake ni kuchukuliwa hatua za kinidhamu na za kisheria kadri ya taratibu.

Kwa hiyo, naomba nikuhakikishie kwamba tutaendela kufanya hivyo kadri ya miongozo. Tumeshawaondoa wale watumishi, wapo ambao wamenyang'anywa leseni na vilevile wapo ambao wamefukuzwa kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Dkt. Mnzava unaipokea hiyo Taarifa?

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naipokea japo najua kuna ambao walihama, lakini ninaomba kabisa kwamba mtu anapofanya kosa adhibiwe *accordingly*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa kuna suala zima la mafuriko, tumeona Kibiti, tumeona Arusha, tumeona mikoa mingine hata Shinyanga katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga tulipata mafuriko katika Kata ya Mwamala, kuna watu kadhaa waliweza kufariki, lakini kuna ambao nyumba zao zilibomoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana kwa jinsi ambavyo Serikali imesema imetenga fedha, imeongeza fedha kwa ajili ya kukabiliana…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa mud awa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Dkt. Mnzava, naomba uhitimishe hoja yako muda wako umeisha.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina sababu ya kukataa kuunga mkono hoja kwa sababu bajeti

hii inakwenda kukidhi mahitaji ya Watanzania walio wengi wanaishi vijijini, kwa hiyo ninaunga mkono hoja na tunamwambia Mama Dkt. Samia aendelee kuchapa kazi wanawake na wananchi wa Mkoa wa Shinyanga tupo naye bega kwa bega, iwe jua, iwe mvua, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Nimwite sasa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mheshimiwa Salome Makamba ajiandae.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa muda na mimi nichangie na nikupongeze kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wetu hapa Bungeni, lakini niwapongeze Wizara kwa ujumla, ndugu zangu wanaoongoza Wizara hii kubwa na muhimu hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niwape pole Watanzania wote hasa ambao wanapitia kwenye mafuriko na majanga mbalimbali ambayo yamesababishwa na mvua kubwa na kwetu Muleba pale tulikuwa na mafuriko yakaharibu miundombinu, lakini niishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu. Nakumbuka Dada yangu Jenista Mhagama, tuliongea akatusaidia pale Muleba, wanakushukuru sana kwa msaada ambao mlitupatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wengine walivyochangia wengi, nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kupitia Wizara hii na viongozi wote wa Wizara hii ni wasikivu hongereni sana. Mheshimiwa Mchengerwa, ulitutembelea Mleba pale, ukaja pale na tunakushukuru na tulikuandalia zawadi, tukasema utakaporudi utapewa zawadi ya senene, lakini hujarudi na ulisema utakaporudi utakuja kukagua hospitali ya wilaya na ulisema iwe imekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Wizara ya TAMISEMI, tunaendelea na ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Muleba na tumechelewa sana. Nikushukuru Mheshimiwa Waziri ulipokuja ulitoa maelekezo kwamba ziletwe shilingi bilioni moja, Mheshimiwa Waziri bado Muleba tunasubiri bajeti ya kukamilisha ujenzi wa

hospitali ya wilaya. Najua wewe ni Waziri kijana na unajua kukimbiakimbia, tunakuomba hata kabla hatujamaliza bajeti hii ukarudi Muleba ukatusalimie ukaangalie yale uliyoyaagiza kama yamekamilika, lakini ninahakika kwa bajeti hii zile pesa ambazo tumeomba kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Muleba tunaomba tukakamilishe hili zoezi. Wilaya ya Muleba ni kati ya wilaya kongwe, lakini ni wilaya ambayo haikubahatika kuwa na hospitali ya wilaya, ni kipindi chako hiki kwamba tunataka tujenge na tuandike historia upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muleba tumepata vituo vya afya vitatu, Jimbo la Muleba Kusini, lakini Mheshimiwa Waziri ulivyotutembelea na hii ulitoa *commitment* pale, ulitupa ahadi ya kituo cha afya kwa ajili ya Kata ya Kimwani, nimeangalia kwenye randama nikapitia kwenye bajeti, lakini najua kuna mambo mengine sijayaona vizuri, sijakiona hiko kituo cha afya, najua wewe ni msikivu ndugu yangu msomi mwezangu tunaomba sasa hayo uliyoahidi kipindi kile usiyasahau kwenye bajeti hii. Ulienda mbele ukatuahidi zahanati pale baada ya wananchi kumlilia Mama Samia kwamba akina mama wanasafiri umbali mrefu kufuata huduma za afya, ukatuahidi ukasema Kata ya Burungura naipa zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kwenye hii bajeti ambayo tunaipitisha, mimi nakuunga mkono, naiunga mkono bajeti nzima ili yale ambayo tuliyaahidi na yale ambayo uliyaahidi Muleba yakatekelezwe katika bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muleba tunaendelea na ujenzi wa zahanati, nawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Muleba Kusini, wamejitahidi kujenga zahanati kwa nguvu yao na mengi tunayo maboma kama Zahanati ya Kabirizi, Zahanati ya Kashanda, Burungura, Kakoma, Bihanga, hizi zahanati zote zipo *level* za maboma. Sasa naomba mtakapopitia kwenye bajeti yetu nimeona kwenye hotuba yako, umeongelea ukamilishaji wa maboma, nakuomba Muleba sisi tumeshaanza, sasa tunaomba ukatuunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwiwa Mwenyekiti, niombe kuwapongeza baadhi ya wananchi ambao wamejitoa mhanga, hapa nimtambue ndugu yangu Prosper Rweyendela, alitoa majengo akatoa ardhi kwa ajili ya kuanzisha Kituo cha Afya Ijumbi. Yeye lengo lake ilikuwa tupate Kituo cha Afya Ijumbi, lakini nashukuru wilaya yangu kupitia Idara ya Afya na Mkurugenzi wangu wameisajili kama zahanati, lakini nakuomba Mheshimiwa Waziri, hiki kituo cha afya ambacho aliyetupatia ardhi, aliyetupatia majengo bure hatukulipa chochote, lakini lengo lake lilikuwa kiwe kituo cha afya. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri na sisi tukamuunge mkono tukatimize azma yake badala ya kuibakiza kama zahanati, isajiliwe kama kituo cha afya na nitoe wito kwa watu wote ambao wana mali, ambao wapo tayari kujitolea waige mfano wa ndugu yangu Prosper Rweyendela alimaharufu kama *PR* wakatoe kidogo kati ya walichonacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongelea vituo vya afya Muleba vipo vitatu, viwili vimejengwa kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Sita, nikushukuru Mheshimiwa Waziri mmetupa fedha, lakini hatujakamilisha ipasavyo ujenzi wa vile vituo viwili vya afya. Nikuombe unapopita, sisi tunasema unapowazuru wengine na mimi usinipite Mheshimiwa Mchengerwa, katusaidie ili tuweze kukamilisha vile vituo vya afya ili vibaki vifikie *standard* iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakinni tuna kituo kingine Mheshimiwa Waziri, kilijengwa miaka ile ni cha zamani, lakini kuna majengo kama manne yapo *idle* yaani hayajakamilishwa na najua kwa nguvu na juhudi uliyonayo na kazi anayoifanya Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, nikuombe Mheshimiwa Waziri utakapofika Kagera au yeyote atakaye tembelea Kagera, akatembelee Kituo cha Afya Kimea, ni kituo pekee cha kizamani, lakini kina majengo mengi ambayo hayajakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye elimu, naishukuru Serikali yetu ya Awamu ya Sita kwa kazi kubwa ambayo tumeifanya kujenga madarasa mazuri ya sekondari na hapa nashukuru sana, imetupatia sura mpya ya elimu yetu hasa kwenye miundombinu, lakini pamoja na kazi hiyo nzuri ambayo

imefanyika nawaomba na hapa nitoe ushauri Mheshimiwa Waziri, mnapotuletea vyumba vya madarasa kama hivi ambavyo mmetupatia juzi, tunaomba mkatusikilize na sisi, tunajenga shule mpya kwa nguvu ya wananchi na sisi lengo letu ni kupunguza umbali wa wanafunzi kufuata sekondari zilizopo. Sasa mnavyotuletea vyumba vipya na sisi tunajenga shule zetu mpya, Muleba Kusini pekee mwaka huu, Awamu hii ya Sita tumejenga shule zaidi ya 18 za nguvu ya wananchi. *(makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa vile vyumba mnavyotuletea ni bora mkavipeleka kule ambako wananchi wapo na ambako tumeanza kujenga sisi wenyewe ili mkatuunge mkono tukakamilishe zile shule azma ya Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan iweze kukamilika ya kuwapunguzia watoto wetu kusafiri umbali mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunayo sasa kazi mbele yetu ya shule za msingi, kwa kweli kazi na nguvu iliyoelekezwa shule za sekondari nadhani tulipofikia Mheshimiwa Waziri tupo katika hatua nzuri, twende sasa kwenye shule za msingi kwa sababu shule nyingi za msingi hasa zile kongwe kusema kweli katika Wilaya yangu ya Muleba hasa mjini pale zina sura ambayo haipendezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TARURA*, tumesema tumepata maafa makubwa sana na nashukuru Serikali kupitia *TARURA*, mimi kwangu tulipata mafuriko makubwa sana, tukapewa fedha zaidi ya shilingi milioni 200 kurekebisha ile miundombinu, lakini haitutoshi Mheshimiwa Waziri. Tunawaomba mkatuangalie hasa sisi ambao tunatoka Mikoa ya Kagera au Kanda ya Ziwa. Kagera tuna mvua nyingi, hayo mafuriko mnayoyasikia sisi tumeyazoea, tunaomba mnapoleta pesa kwa ajili ya miundombinu Mikoa ya Kagera tukaipe kipaumbele cha kipekee kutokana na jiografia yetu. Mvua tuna misimu miwili na pesa mnayotuletea mara nyingi sana inaishia kwenye kukarabati badala ya kujenga miundombinu mipya, tunashukuru miundombinu mingi inapitika japo kwa shida na kutokana na sababu ambazo nimezisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mfuko wetu wa Jimbo wa *TARURA* tunakuomba Mheshimiwa Mchengerwa, mtuangalie hasa hii mikoa ambayo ina mvua nyingi, ambayo jiografia yetu inatufanya tutumie fedha nyingi kwenye kukarabati barabara badala ya kujenga barabara mpya, sasa muwe mnatuangalia, mtuangalie kama mnavyoangalia kwenye majiji, mtuangalie kama mnavyoangalia maeneo mengine ambayo yanapata maafa, kwetu mvua ni neema ndiyo, lakini inatusababishia mambo makubwa ambayo wakati mwingine hatuyataki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru Ofisi ya *TARURA* Kagera na Ofisi ya *TARURA* Wilaya yangu, wanafanya kazi nzuri sana. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, utakapokuja kufanya majumuisho hapa mtuangalizie hata vitendea kazi, nawaangalia vijana wako ambao wapo pale Muleba, gari moja na lenyewe tulipata ndiyo hivyo hivyo. Katika wilaya ambazo ni kubwa kama Wilaya ya Muleba, Mheshimiwa Waziri muwe mnawaangalia hata wafanyakazi wenu, wanakimbizana kwa kutumia gari hilo hilo moja na wakati mwingine kuna maafa sehemu moja hawezi kufika kwa sababu wana gari moja. Kwa hiyo, naomba na hao tuangalie waweze kuwatumikia wananchi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kwenye uongozi, mnapoteua Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi nawaomba muwape semina tuanze kujua mipaka ya madaraka yao...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kikoyo, muda wako umeisha.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga hoja mkono, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nakushukuru Mheshimiwa Dkt. Kikoyo. Nimwite sasa Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Makamba, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ajiandae.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, lakini nianze kwa kukupongeza kwa sababu tumekuamini na tumeona tangu asubuhi unavyotuongoza Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mchengerwa na timu yake kwa kuja kuwasilisha bajeti yao ya utekelezaji wa shughuli za Serikali lakini kwa namna ambavyo Wizara hii ndiyo imekuwa kama roho yetu, mmetutendea haki katika majimbo yetu yote tunawashukuru sana Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwape pole Watanzania, lakini niwape pole pia ndugu zangu wananchi wa Mkoa wa Lindi, lakini wananchi wa Lindi Mjini pamoja na jirani zetu wa Mchinga kwa maafa makubwa yaliyotokea na mvua ambazo zinaendelea. Tunajua kwamba wananchi wetu wameathirika lakini miundombinu mbalimbali imeathirika, mashamba na mazao ya wananchi yameathirika vibaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niiombe Serikali kuhakikisha kwamba wananchi hawa tunawaangalia ili kurudisha hali zao na miundombinu ambayo imeharibika kwa haraka Serikali iweze kurudisha hali ilivyo ili wananchi maisha mengine yaweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo anajitoa kuwatumikia wananchi wa Tanzania, lakini kuhakikisha kwamba analeta maendeleo makubwa, lakini kuleta mapinduzi makubwa nchini Tanzania na hakuna asiyeona, watu wote tunashuhudia mambo mbalimbali ambayo yanaendelea katika maeneo yetu, hakika ni mapinduzi makubwa sana katika sekta ya afya, sekta ya elimu, sekta ya maji, lakini sekta ya barabara, nishati pamoja na maeneo mengine. Ama hakika tumpe maua yake Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika miaka mitatu hii ametutendea haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wana-Lindi mjini tumefaidika sana, Lindi Manispaa tumepata fedha zaidi ya shilingi bilioni 120 na zimetekeleza miradi mbalimbali. Sisi Lindi Mjini peke yake tumepata zaidi ya shilingi bilioni 75 na zimekwenda kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Sekta ya afya tumepata shilingi bilioni 15 zimejenga zahanati, vituo vya afya, hospitali ya wilaya, lakini tuna hospitali ya mkoa kwa maana ya hospitali ya rufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumepata faida kubwa sana katika sekta ya afya, lakini pia katika sekta ya elimu nako pia tumepata zaidi ya shilingi bilioni 15 zimetekeleza shule za msingi, shule za awali lakini shule za sekondari pamoja na miundombinu mbalimbali, lakini bado pia sekta ya maji tumepata zaidi ya shilingi bilioni 40 zimetekeleza miradi mbalimbali ya maji. Kwa hiyo, katika miaka mitatu ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumepata faida kubwa sana na ni mwanamke shujaa, mwanamke shupavu, hakuna mfano wake, sisi kama wanawake wa Tanzania, wanawake wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hatuna sababu ya kutomuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na yule ambaye anamsema mama huyu ama kweli akili yake kidogo ina matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio makubwa ambayo tumeyapata, lakini bado tunazo changamoto katika sekta ya afya. Ukiangalia kwenye Kituo cha Afya cha Ng'apa, tunahitaji fedha shilingi milioni moja kukamilisha chumba cha upasuaji, lakini pia tunahitaji kukamilisha kituo hiki kiweze kufanya huduma za upasuaji lakini kulaza wagonjwa pamoja na chumba cha kujifungulia.

Kwa hiyo, TAMISEMI tumeleta *BOQ* yetu tunahitaji fedha kwenda kukamilisha kituo cha afya hiki, kituo hiki cha afya kinatarajia kuhudumia wakazi karibu 5,000; kwa hiyo, tunaomba kwa haraka watusaidie ili tuweze kukamilisha na tuweze kuwafanya wananchi wetu wasiweze kutembea umbali mrefu kwenda kutafuta huduma za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Kituo cha Afya cha Kata ya Makonde, kituo kile kipo katikati ya mji na kituo kile kinahudumia wakazi 22,320 na kinahudumia kata kumi zote za mjini lakini kituo kile bado ni kidogo, hakina chumba cha upasuaji na hakina chumba cha kulaza wagonjwa wa ndani. Kwa hiyo, kwa sababu ya eneo lile ni dogo tunahitaji kupandisha kwenda juu kwa maana ya kujenga jengo la ghorofa. Tunahitaji shilingi milioni 900 mtusaidie ili tukamilishe jengo hili liweze kuwahudumia wananchi wa Lindi Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna eneo la *TARURA,* tunashukuru sana kwamba Serikali inatupatia fedha kila mwaka shilingi bilioni tatu na milioni 600. Fedha hizi ni ndogo sana, ukiangalia jiografia ya manispaa ilivyo, kwanza ina majimbo mawili, lakini hali ya jiografia kuna milima na mabonde. Kwa hiyo, hata utengenezaji wake wa barabara na ukiangalia kuna udongo wa mfinyanzi, eneo lingine linalazimika kuweka zege, lakini maeneo mengine tunalazimika kuweka lami. Kwa hiyo, ningeiomba Serikali kutuongezea bajeti ya *TARURA* kutoka shilingi bilioni tatu na milioni 600 kwenda shilingi bilioni saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mvua kubwa zilizonyesha na kuharibu miundombinu mbalimbali, tumefanya tathimini na kuleta maombi maalum ya kurudisha miundombinu ili iweze kukaa sawa, kiasi cha shilingi bilioni moja ili iweze kwenda kufanya kazi katika eneo la Lindi Mjini na kurudisha hali ya barabara kuwa salama na wananchi waweze kutumia barabara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo changamoto *TANROADS*, ukiangalia eneo lililopata mafuriko, Kata ya Mwenge, Rahaleo, Ndolo pamoja na kule Ng'apa changamoto kubwa katika Kata ya Mwenge ni kukosekana kwa mfereji mkubwa unaoweza kubeba maji mengi. Nimekwenda *TANROADS* miaka mitatu mfululizo kwenda kuomba kurekebisha maeneo hayo ili kuwafanya wananchi wa Lindi Mjini wasidhurike na mvua zinazoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mchengerwa, umeona ulipokuja Lindi, nyumba zote zilizo barabarani zina ukuta mkubwa na mrefu kwenye mlango wa mbele na mlango wa nyuma. Mtu akitaka kuingia anakunja nguo mpaka juu ya magoti apandishe mguu ndipo aingie ndani, ni changamoto sana. Ninaomba Serikali itazame namna ya kurekebisha haraka, ili wananchi wawe na furaha ya kuishi katika nchi yao ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna changamoto katika eneo la Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Mchengerwa ninaomba anisikilize, TAMISEMI hamtambui kwamba manispaa mmetuongezea Jimbo la Mchinga, maana yake ni pale tuna vituo vya afya, tuna zahanati, tuna madarasa na tuna watumishi wako pale na wanahudumiwa na Manispaa ya Lindi. Changamoto iliyopo ni kuna ruzuku haziji tena pale kwa ajili ya watumishi hawa pamoja na kuja kutoa huduma katika maeneo ya shule 37 ambazo mmetuongezea. Kwa hiyo, bado ruzuku inakwenda Halmashauri ya Mtama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa watambue kwamba Manispaa ya Lindi imeongezewa Jimbo la Mchinga, lakini bado tuna mitaa 117, lakini TAMISEMI bado hamtambui kwamba tuna vijiji 47 kwa hiyo, hamtutendei haki, kuna fedha ambazo tunazikosa zinakwenda Mtama. Sasa mtambue kwamba manispaa ina mitaa 117 na tuna vijiji 47. Kuna fedha za madaraka, kuna fedha za likizo, kuna fedha mbalimbali za ruzuku ambazo haziji manispaa na hivyo kuwakatisha tamaa watumishi ambao wanafanya kazi na ni stahiki yao kupata fedha hizo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mchengerwa ninaomba muyapitie tena mafaili muweze kuangalia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamida muda wako umekwisha, kengele ya pili. Ninaomba uhitimishe. *(Makofi)*

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, lakini ninaomba sana TAMISEMI walitazame hilo na watutendee haki. Kuhakikisha kwamba tunafuata fedha hizo fedha za *OC, capitation* na fedha nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono. Ahsante sana, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah. Ninamwita sasa Mheshimiwa Salome Makamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi. Mheshimiwa Mama Salma Kikwete, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye Wizara ya hii ambayo kimsingi Waziri wake ni Mheshimiwa Rais na amekasimu mamlaka haya kwa Waheshimiwa Mawaziri walioko mbele yetu kwa ajili ya kumsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia nakupongeza wewe kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge, ni nafasi nzuri na umeitendea haki kwa kweli, unatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme Mawaziri hawa wa TAMISEMI ni Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na naanza kwa kutoa pole kwa Mjumbe mwenzetu, Mheshimiwa Mchengerwa, kwa mafuriko makubwa yaliyompata kule jimboni kwake. Ninajaribu kufikiria katika muktadha alionao, yaani Mheshimiwa Mbunge umeingia Bungeni una miaka zaidi ya mitatu unapambana kuweka vivuko, unapambana kuweka madaraja, unapambana kutengeneza barabara na mitaro, halafu leo ukifika pale unakuta miundombinu yote imefunikwa na maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lililompata mwezetu ni kubwa, lakini ninasema hili limetupata wote Tanzania nzima. Ndio maana siku nilipokuwa ninachangia humu ndani katika Bunge lililopita kuhusiana na janga kubwa linaloendelea kwenye nchi hii na kiasi

cha fedha zinazopelekwa kwenye *TARURA* kwa ajili ya kukabiliana na janga hilo wote tulikuwa tunazungumza lugha moja. *(Makofi)*

Mheshiwa Mwenyekiti, ninaomba busara ya Serikali, ipeleke fedha za *TARURA,* hali ni mbaya. Hali ni mbaya, wananchi wanakufa, watu wanapoteza makazi. Sasa hivi karibu robo tatu ya Wabunge humu ndani tupo kwenye heka heka ya kupeleka vyakula, malazi na matandiko kwa ndugu zetu ambao wamepatwa na mafuriko. Serikali ilione jambo hili kwa kipekee na hata wakipitia mchango wangu uliopita kwa karibu dakika zote nilizopewa na Bunge lako nilisisitiza tupeleke fedha za *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninajifunza utaratibu wa kupongeza, ninajifunza na nasema ninajifunza kwa sababu, umefika wakati naona mengi ya yale niliyokuwa ninayapigia kelele yamefanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa Kampeni za mwaka 2020 pale kwangu Shinyanga, moja kati ya hoja zangu kubwa ilikuwa ni kuhusu Soko Kuu la Shinyanga, Soko la Mitumba Ngokolo na shule ya wasichana. Ukija Shinyanga sasa hivi tuna soko la kisasa la ghorofa limejengwa na Mheshimiwa Rais, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, hatuwezi kubeza jitihada hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Soko la Mitumbani…

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa Taarifa msemaji, pamoja na mchango

wake mzuri, namwambia chama chake kilikuwa hakitekelezi Ilani, sisi tumetekeleza Ilani na hayo yote tumeyafanya, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome Makamba, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Katambi usinichokoze, leo ninataka niongee taratibu kwa sababu, *pressure* ya Mheshimiwa Waziri kutokana na mafuriko iko juu sana, kwa hiyo, ninataka nimsaidie asije akasema mimi ndio nimemmalizia. Kwa hiyo, usinichokoze. *(Makofi/Vicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Shinyanga tulikuwa na Soko la Mtumbani ambalo wafanyabiashara, wamachinga wengi, walikuwa wanaishi kwenye mazingira magumu sana ikinyesha mvua hawafanyi biashara. Leo tuna soko zuri, la kisasa, la staha na watu wetu wanafanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetoa shilingi 3,000,000,000 kujenga Shule ya Wasichana ya Sayansi Shinyanga Mjini. Wametekeleza yale niliyowaahidi wananchi wa Shinyanga mwaka 2020, ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba niunge pale alipoishia dada yangu Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, kuhusiana na hizi fesha za *CSR* na kwa bahati nzuri tulipata muda wa *break* nikatafakari. Mimi nimefanya kazi kwenye *private sector* tena kwa hawa wanaoitwa wawekezaji ambao ndio wanatakiwa kutoa fedha za *CSR*. *(Makofi)*

Mhesmiwa Mwenyekiti, katika maeneo mengi hawa watu wakitoa hizi fedha wanazitoa na masharti kwamba zijengwe kwa mujibu wa sheria za kimataifa. Kwa muktadha huo, kwa mujibu wa sheria za kimataifa hautambui *force account,* kwa mujibu wa sheria za kimataifa ni lazima uweke *consultant*, kwa mujibu wa sheria za kimataifa utapewa hela ya *mobilization,* lakini hautambui *local* fundi, hautambui chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndio matokeo ya kusikia Uwanja wa Mpira Geita umejengwa kwa shilingi bilioni mbili na ushee na haujaisha. Hayo ndio matokeo ya kusikia Kituo cha Afya Mwendakulima, Kahama, kimejengwa kwa zaidi ya shilingi milioni mia tano na ni kituo cha afya. Hayo ndio matokeo ya kusikia leo hapa Dodoma kuna visima viwili vimechimbwa kwa shilingi bilioni 1.3 na ndio tunasikia leo Dodoma Nala wamejenga shule ya msingi kwa shilingi bilioni 2.3, hii haikubaliki.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii haikaubaliki, hiyo mikataba ya kwenda kujenga shule tunavyo viwango vyetu vya Kitaifa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome Makamba, samahani kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina shida na mchango wa Mheshimiwa Salome Makamba, kwanza nampongeza kwa mchango wake, lakini pia naipongeza Kamati ya TAMISEMI ambayo katika ushauri kwa Serikali wameshauri tuupitie utaratibu wa utekelezaji wa miradi ya *CSR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe Taarifa, ili aweze kuendelea na mchango wake, baada ya kusoma Taarifa ya Kamati na mchango wa Mheshimiwa Salome na Mheshimiwa Hawa, nimepitia taratibu za ujenzi wa miradi hii pamoja na utaratibu na miongozo kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, nimegundua masuala kadhaa ambayo ninaomba niyaseme ili kumsaidia Mheshimiwa Salome aweze kuchangia…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza ni kwenye kujenga vituo vya afya; Ofisi ya Rais, TAMISEMI mwongozo

wao ni majengo sita, kwa maana ya *maternity, laboratory, theatre, laundry* na *OPD,* lakini kwa miradi ya *CSR* kwenye majengo kuna idadi ya 22. Kwa hiyo, kuna *discrepancy* ya idadi ya majengo kwa mwongozo wa upande wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na kile ambacho kimejengwa na mradi. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili, hata *square meters* za haya majengo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwenye mwongozo wa haya majengo sita niliyoyataja jumla ya *square meters* ni 1,165, lakini…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ninaomba umalize.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampa Taarifa, ili aweze kuendelea na mchango wake. Ninachotaka kusema…

**MWENYEKITI:** Una dakika chache, kama tatu za kutoa Taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba, miradi ya *CSR* kwa sababu huwa ni michango ya Wadau, ninakubaliana na hoja ya Kamati kwamba, Wizara ya ujenzi…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ujenzi tukae na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tupitie na kutoa

Mwongozo, ili tunachokijenga kupitia miradi ya *CSR* kwa sababu, hapa tunazungumza kuna miradi inajengwa kwa *force account*…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ninaomba umalize Taarifa yako kusudi tupate majibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia.

Kwa hiyo, kutokana na ushauri wa Kamati ninaelekeza *TANROADS* kusimamisha utekelezaji wa hii miradi ya *CSR*. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka tutakapopitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Wizara ya Ujenzi na kutoa mwongozo kama Kamati ya Bunge ilivyosema. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Makamba, muda wako umeisha, lakini, je, unaipokea hiyo Taarifa?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani muda ukaisha…

**MWENYEKITI:** Unaipokea hiyo Taarifa?

Ipokee kwanza Taarifa halafu tutaamua. Muda wako nilikuwa ninaulinda kwa hiyo, unapokea Taarifa?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Taarifa yenyewe sijaielewa, yaani ni *confusion* tu halafu unaniambia kwamba, muda wangu umeisha.

**MWENYEKITI:** Basi ninakupa dakika mbili umalizie mchango wako.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa inasemaje?

**MWENYEKITI:** Unaipokea Taarifa au haupokei? Kama haujaielewa sema hauipokei au unaipokea?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa yenyewe sijaielewa.

**MWENYEKITI:** Basi endelea na mchango wako, ninakuongezea muda wa dakika tatu umalizie mchango wako. *(Makofi)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba nishauri na namshauri Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, sisi TAMISEMI ndio tunaotekeleza hiyo Miradi ya *CSR* yeye Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ndio ana dhamana ya hiyo mikataba. Ninaomba nimshauri aisitishe hiyo mikataba.

**MBUNGE FULANI:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti)*.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Ndicho alichosema? Nimeipokea Taarifa kama amesitisha mikataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi ambayo imeanza kutekelezwa. Kwa mujibu wa taarifa iliyokuja kwenye Kamati inasema kuna miradi ya ujenzi imefika hatua ya maboma ni bora tuivunje tulipe fidia ya kuvunja mkataba, ni bora nusu shari kuliko shari kamili. Kuna miradi ambayo wameshachimba hivyo visima wanasubiri malipo. Wasilipwe, ni heri twende Mahakamani, bora nusu shari kuliko shari kamili, kwa hiyo, ninashauri hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwenye hoja ya Kamati inayohusiana na shule za kiingereza; kumetokea *trend* ya halmashauri kutumia fedha za mapato ya ndani kwenda kujenga shule za *english medium,* shule za kiingereza wakidai kwamba wanafanya biashara. Sasa kwa kufanya hivyo wanawachukua walimu wetu ambapo hata Katibu Mkuu wa TAMISEMI hajui kama ikama ya Walimu wake imepunguzwa, hao Walimu wamekwenda kufanya kazi kwenye shule ambazo ni biashara ya halmashauri, hiyo ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, usimamizi wa shule hizi unagharimu watumishi wa halmashauri; na tatu, *selection* ya wanafunzi wanao kwenda kwenye shule hizi za kiingereza haizingatii Katiba yetu inayosema lazima watoto wote wapate usawa katika kupata elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninashauri, Tanzania hii ya leo siyo ya mwaka 1960, Tanzania hii ya leo hakuna sehemu unaweza kwenda ukakosa shule ya *english medium,* mwenye uwezo wa kupeleka watoto kwenye shule ya kiingereza na apeleke, lakini halmashauri ibaki kwenye jukumu lake la msingi la kuwahudumia watoto wetu na kuhakikisha wanapata elimu sawa na kwa manufaa sawa. Kwa kufanya hivyo kwanza, watarudi kwenye msingi wa Katiba, watarudi kwenye Sera ya Elimu ya kuzingatia kwamba, watoto wote wanapata elimu sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ninataka niseme, hoja nyingi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambazo zina *query,* zina mashaka, zinaigusa *Local Government* ambayo ni TAMISEMI na hoja hizo ni kwa sababu, zinadai uthibitisho wa matumizi ya fedha ambayo kimsingi hauwezi kuthibitishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipeleka hela *TANAPA,* Bodi ya *TANAPA* inakaa inafanya maamuzi, matumizi yanafanyika, shughuli imekwisha. Ukipeleka hela halmashauri ni lazima Mkurugenzi aitishe Baraza la Madiwani, aanze na Kamati ya Fedha, aitishe Baraza la Madiwani na Baraza la Madiwani likifanyaje, aende akatoe elimu kwa wale watu ili waweze kujua tunaposema hewa ya ukaa, sijui hewa ya kaboni maana yake ni nini? Hawaelewi awapige semina, awalipe posho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akitoka hapo hela zinachukuliwa zinaingizwa kwenye akaunti, tuseme anajenga shule. Akaunti ya shule ipo *dormant,* hela zinadunda zinarudi Hazina. Hela zikirudi Hazina kuna huyu bwana anaijita *Pay Master General,* yeye anasema hivi ili niweze kuzirudisha hizo hela ni lazima tujadili huku, yaani Bunge limekaa limepitisha bajeti, mjadala unaanza, ile hela

mpaka ije irudi ikafanye jambo lililokusudiwa *it is a nightmare*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana kwa busara ya Kiti chako, sheria inayohusiana na matumizi, mapato, matumizi ya fedha kwenye *Local Government,* iwe tofauti na sheria ya jumla ya manunuzi na ya *Public Finance*. Hapo tutapunguza mashaka kwenye Halmashauri zetu na tutawasaidia hawa watendaji ambao wengi ni wasomi waweze kutumia utashi, weledi na ubunifu wao kuendesha Halmashauri. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nakushukuru sana. Muda wako wa nyongeza umeisha.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunakwenda kwa mchangiaji anayefuata Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Mama Kikwete ameomba achangie kesho na niombe Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta ajiandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mwongozo wa Mwenyekiti. Mwongozo wako.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipatia fursa hii leo kuweza kuchangia hotuba ya bajeti ya TAMISEMI…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unauchuna?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakoso, hebu subiri, nita-*entertain* Mwongozo tutakapomaliza. Endelea mchangiaji.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anayezungumza ni Iddi Kassim Iddi siyo Mheshimiwa Kakoso. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoendela kuifanya kwenye Taifa letu hili la Tanzania. Pia nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kaka yangu Mchengerwa unafanya kazi kubwa sana ninakushukuru sana. Ninampongeza dada yangu, Mheshimiwa Zainab Katimba kwa uteuzi, hongera sana, bila kumsahau Naibu Waziri, ndugu yangu, Mheshimiwa Dkt. Dugange kwa kazi kubwa ambayo unaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nacchukua fursa hii kumpongeza Mtendaji Mkuu wa *TARURA,* kaka yangu Seff, kwa kazi kubwa anayoifanya na nimpe pole kwa changamoto ambazo anaendelea kukumbana nazo baada ya mvua kuongezea na barabara nyingi sana kuharibika kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Msalala ninachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa wema aliotutendea sisi Wana-Msalala. Ni kweli kabisa ametupatia fedha nyingi sana za kukamilisha miradi mbalimbali kwenye Jimbo letu la Msalala. Ninasema alivyokuwa akizungumza mama yangu hapa Mheshimiwa Anne Kilango, amezungumzia habari ya ujenzi wa vituo vya afya kwenye Jimbo la Same Mashariki, Same Vijijini *I think.*

Mimi ninasema kwenye Jimbo la Msalala Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ndani ya miaka yake mitatu ameweza kutupatia vituo vya afya vitano ikiwa vyote vimekamilika na kingine kinajengwa, ametupatia kiasi cha shilingi milioni 500 tumekamilisha Kituo cha Afya Kata ya Isaka, ametupatia shilingi milioni 500 tumekamilisha Kituo cha Afya Maluguru, ametupatia shilingi milioni 500 tumekamilisha Kituo cha Afya Burige, Ametupatia shilingi milioni 500 nyingine tumekamilisha Kituo cha Afya Segese na ametupatia fedha nyingine shilingi bilioni 500 tunajenga Kituo cha Afya Kata ya Mwanase hakuishia hapo,

kwenye sekta ya afya ametupatia fedha nyingi za kununua vifaa tiba katika maeneo ya zahanati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwenye sekta ya afya tayari tumekamilisha zahanati zaidi ya 34. Mheshimiwa Rais hakuishia hapo akasema hapana, nataka niwape fedha muanzishe ujenzi wa Chuo cha *Nursing*, Chuo cha Kada ya Afya; hivi tunavyozungumza chuo kimekamilika, mwezi wa nane kitapokea wanafunzi ambao wataanza kupata mafunzo ya kada ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hakuishia hapo, ametupa shingi bilioni mbili, akasema hapana, vijana wa Jimbo la Msalala wanahitaji kupata elimu ya fani mbalimbali kwa sababu ya uwepo wa mgodi ambao unahitaji fani mbalimbali katika kupata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akatupatia bilioni mbili ambapo tayari Chuo cha *VETA* kinaendelea na ujenzi na hivi karibuni kitakamilika na mwaka kesho tunapokea wanafunzi wanatakaoenda kusoma Chuo cha *VETA* kwenye maeneo hayo. Kubwa, baba lao Mama, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweza kusaini mkataba na kupatia fedha kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa barabara inayotoka Kata ya Bulyanhulu kwenda mpaka Kahama. Haya ni matunda Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye Jimbo la Msalala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Msalala lilipokea fedha nyingi sana kwenye miradi mbalimbali. Tulikuwa hatuna umeme zaidi ya vijiji 64 kwa sasa hivi tunavyozungumza vijiji vyote 64 vinaenda kupatiwa umeme na vitakamilika. Sambamba na hilo kwenye miradi ya maji ametupatia fedha nyingi, tayari tuna mradi mkubwa ambao unaenda kukamilika Kata ya Mwalugulu, tuna mradi mkubwa zaidi ya bilioni 11 kwenye Kata ya Busangi na wenyewe unaenda kukamilika na kwenye miradi ya maji na penyewe ametupatia fedha nyingi ambayo inaenda kukamilisha miradi ya maji kwenye Jimbo la Msalala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya elimu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu na penyewe ametupa fedha nyingi mno, tuna zaidi ya shule sita mpya kwenye Jimbo la Msalala, tunayo shule moja imekamilika Kata ya Ikinda shilingi milioni 500, tunayo shule moja imekamilika shilingi 1,200,000,000 kwa ajili ya watoto wa kike kwenye Jimbo la Msalala. Kwenye sekta ya elimu na penyewe Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametupa fedha nyingi sana katika kukamilisha sekta ya elimu kwenye Jimbo la Msalala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye Jimbo la Msalala mwaka 2025 kura zake zipo za kutosha kabisa. Mheshimiwa Waziri Mchengerwa tupelekee salamu zetu wananchi wa Jimbo la Msalala mwambie asiwe na shaka, atulie, Jimbo la Msalala lipo salama, Jimbo la Msalala wananchi wote wanasubiri mwaka 2025 ili waweze kumpigia kura za kutosha. Mheshimiwa Waziri kama ikukupendeza zaidi wananchi wa Jimbo la Msalala wapo tayari, muelekeze Mkurugenzi alete masanduku ya kura tupige kura ukakae nazo mwenyewe zitamkuta Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichangie kwenye sekta ya *TARURA*, tunashukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na nimempongeza hapa Mkurugenzi Mkuu kaka yangu Seff kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya. Ni kweli tunafahamu kwamba changamoto ya hali ya hewa na mvua nyingi zimezidi kwenye maeneo hayo na zimeharibu miundombinu, lakini ninaamini kabisa baada ya mvua kukoma fedha nyingi ambazo zimetengwa kwa ajili ya kurekebisha barabara zitaenda kurekebishwa na zitaanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nimwombe Mheshimiwa Waziri kwenye Halmashauri ya Msalala na hasa Wilaya ya Kahama, Wilaya hii ya Kahama ina halmashauri tatu kwa maana ya Jimbo la Msalala, Jimbo la Ushetu na Jimbo la Kahama Manispaa. Nikuombe sana, hapo nyuma tulikuwa na Mameneja wa *TARURA* ambao walikuwa wanatusaidia sana kuweza kusimamia barabara na kuweza kusimamia wakandarasi

wanaojenga barabara kwenye maeneo yale, lakini utaratibu ule baadaye ulikuja ukaondolewa na matokeo yake akabaki meneja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri kwenye wilaya nzima tuna kata 58 hivi huyu meneja mmoja tu hata kama ataamua kuzunguka kijiji kimoja kimoja maana yake mwaka mzima utaisha bila yeye kukaa ofisini, hatafikia maeneo yote yale. Sasa nikuombe, utaratibu huu urudi, mameneja hawa waweze kurudishwa ili waweze kwenda kusimamia barabara vizuri kwenye maeneo yetu ili wananchi waweze kunufaika na maeneo hayo…

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa wapi?

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cherehani.

**TAARIFA**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa mzungumzaji, ni kweli Jimbo la Ushetu peke yake lina kata 20, vijiji 112 na vitongoji 560 lakini Msalala ina kata 18. Kwa hiyo, meneja mmoja wa *TARURA* kuhimili majimbo yote matatu ni kazi ngumu sana. Hali ya barabara ni mbaya kwa meneja mmoja haiwezekani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naipokea taarifa hiyo kwa mikono miwili na niongezee tu hapo Mheshimiwa Waziri tayari na hata tunapozungumza nikuombe sana utoe maelekezo kwa Mtendaji Mkuu wa *TARURA* aweze kumwelekeza meneja kwenda ku-*secure* barabara ya

mawasiliano yanayotoka Kata ya Nyang'hwale na Jimbo la Msalala…

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Ng'enda.

**TAARIFA**

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mzungumzaji ambaye kwa kweli anachangia vizuri sana. Suala la Mameneja wa *TARURA* hata katika halmashauri zetu mmekwenda kuchukua madaraka ya utawala wa Serikali Kuu kila penye *DC* mmoja kunakuwa na Meneja mmoja wa *TARURA*. Mimi kwangu kuna halmashauri mbili, Manispaa ya Kigoma Ujiji na Halmashauri ya Wilaya, Meneja wetu wa *TARURA* ni mmoja, vijiji ni vingi, mitaa ni mingi na maeneo makubwa. Kwa hiyo, namuunga mkono katika hoja yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi unapokea taarifa hiyo?

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hiyo kwa mikono miwili, lakini nikuombe uniongezee dakika tatu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, *TARURA* wanaendelea na kazi, niombe sana na hili Mheshimiwa Waziri nitashika shilingi yako ya mshahara wako kama hili hautakuja na majibu ya kuonesha ya kwamba ni lini sasa na mkakati wa Serikali ni lini mtaenda kuhakikisha ya kwamba mnawarudisha mameneja hawa ili waweze kutusaidia kwenye maeneo hayo? Hili nitashika shilingi Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimezungumza habari ya fedha nyingi sana ambazo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amezileta kwenye Jimbo la Msalala, ni takribani ya zaidi bilioni 200 zimekuja kwenye Jimbo la Msalala tu pekee yake, na ndiyo jimbo ambalo kimsingi kabisa kwenye Mkoa wa Shinyanga limepokea

fedha nyingi sana kwenye maeneo yale. Sasa Mheshimiwa Waziri hapa tusikilizane, tunamsaidiaje Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenda kusimamia fedha hizi na miradi hii ili iweze kuleta tija kwa wananchi? Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, nimekuletea malalamiko mengi sana, nakushukuru umeweza kuchukua hatua mbalimbali lakini na hili niombe uchukue hatua haraka sana. Wananchi wa Jimbo la Msalala wana matarajio makubwa sana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa fedha zinazokuja na matarajio yao ni kuhakikisha kwamba fedha anazoleta Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan zinaenda kwenye miradi iliyokusudiwa na miradi hiyo inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi limetokea tatizo Mheshimiwa Waziri, kuna fedha tumeletewa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan shilingi milioni 300 kununua vifaa tiba; shilingi milioni 100 imeenda Isaka, shilingi milioni 100 imeenda Mwalugulu na shilingi milioni 100 nyingine imeenda kwenye kata nyingine. Fedha ambayo imetengwa kwenda kununua vifaa tiba, imetengwa kwa ajili ya kwenda kununua majokofu ya kwenda kuhifadhia damu lakini badala ya kwenda kununua majokofu ya kwenda kuhifadhia damu yenye thamani ya kiasi cha shilingi milioni 115 wameenda kununua *fridge* za shilingi milioni mbili/mbili…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi muda wako umekwisha.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniongeze dakika mbili nimalizie hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hitimisha hoja yako kwa sekunde mbili.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi. Namwita sasa Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota ajiandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hoja ya Wizara ambayo ni muhimu sana kwenye maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuleta fedha nyingi za maendeleo kwenye Wilaya ya Tanganyika. Tumepata fedha zaidi ya shilingi bilioni 240 zinazokuja kutekeleza miradi ya afya, elimu na kwenye majengo ya utawala. Vilevile tumepata fedha kwa ajili ya miundombinu ya barabara za vijijini, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa fedha nyingi alizozileta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na eneo la *TARURA;* kwanza nimpongeze *Engineer* Seff kwa kazi kubwa sana ambayo ameifanya kwa kuleta fedha za maendeleo kwenye Wilaya ya Tanganyika, japo fedha hizo zimeletwa lakini zipo changamoto ambazo zina uhitaji wa kwenda kufanyiwa ufanisi zaidi. Nimwombe sana Mkurugenzi wa *TARURA* aiangalie Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika kwa sababu tuna zaidi ya kilometa 1,160 zinazohudumiwa na *TARURA*. Hali ya barabara ni mbaya sababu ya mafuriko ambayo yamekuwepo kwenye Wilaya ya Tanganyika, kwa hiyo tunahitaji fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana *engineer* aliwahi kuja pale kwenye eneo la Ifinsi na alikwenda eneo la Ziwa Tanganyika kwenye Daraja la Mto Fume, Kata ya Kapalamsenga. Ifinsi imekamilika daraja, lakini eneo lile la ziwani najua yupo na anaelewa ninachokisema kwa sasa, tunahitaji lile daraja aweze kwenda kulishughulikia, atume wataalamu na aweke fedha ili wananchi waweze kupata huduma. Kwa sasa wananchi hawana huduma ya aina yoyote kwa sababu daraja halipo na wananchi wanapata wakati mgumu sana wa kupata mahitaji yao kwa sababu daraja lile ni kiunganishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta fedha kwenye eneo la afya. Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ina hospitali ya wilaya moja, lakini mazingira yake bado tunahitaji fedha kwa ajili ya kuikamilisha iweze kukamilika na ifanye kazi kama inavyotarajiwa. Tunahitaji fedha za *fence* ya hospitali ya wilaya lakini tunahitaji vitendea kazi kwa ajili ya hospitali. Hospitali hiyo inatoa huduma kwa kiwango cha chini sana kwa sababu ya kukosa vitendea kazi. Nimwombe Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja yake aiangalie Hospitali ya Wilaya ya Tanganyika kwa kupeleka fedha za kutosha ambazo zitawasaidia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunalo tatizo kubwa sana la uhaba wa watumishi; Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika kwenye kada ya afya tuna tatizo kwenye hospitali ya wilaya upungufu wa watumishi 200, kwenye vituo vya afya tuna tatizo la watumishi zaidi ya 100 ambao wanahitajika kwenda kutoa huduma kwenye vituo vya afya na hospitali ya wilaya. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aangalie umuhimu wa kutuletea wafanyakazi kwa maana ya watumishi kwenye vituo vya afya na hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo bado tuna upungufu makubwa sana kwenye shule za sekondari na shule za msingi. Tuna upungufu wa walimu zaidi ya 1,000 ambao wanahitajika baada ya kupeleka miundombinu mingi ambayo imepelekwa kwenye halmashauri ya wilaya. Tunazo shule nyingi, shule za sekondari na shule ambazo zina uhaba mkubwa sana wa walimu. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla watuletee walimu ili waweze kutoa elimu ambayo itawasaidia wananchi kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie eneo la utawala; Halmashauri yangu ya Wilaya ya Tanganyika Mkuu wa Wilaya hana gari. Halmashauri ina kilometa za mraba 17,000 Mkuu wa Wilaya anatembea na gari la kuazima kutoka halmashauri na gari lenyewe haliwezi kuhimili kutembea halmashauri yote kwa wakati. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri miongoni mwa magari ambayo yatanunuliwa kwa ajili ya kupelekwa wilayani, naomba

kipaumbele upeleke Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, *DC* ana kazi kubwa sana, anatembea maeneo makubwa na anafanya kazi ngumu kwa sababu hana vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika hana ofisi, Ofisi ambayo anaitumia ni ofisi ya halmashauri. Sasa nikuombe Mheshimiwa Waziri, uangalie umuhimu wa kupeleka kwenye bajeti hii tupate Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ambayo itakuwa inatoa huduma kwa wananchi. Hili ni eneo ambalo ni muhimu ili Serikali iweze kufanyakazi yake na mwakilishi wetu aweze kufanya kazi ambayo atawatendea haki wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado hatuna Ofisi ya *DSO;* Wilaya ya Tanganyika karibu asilimia kubwa ya eneo la utawala hakuna ofisi zinazofanyakazi kwenye maeneo hayo. Kwa hiyo, tukuombe sana Mheshimiwa Waziri uje na mkakati wa kukamilisha tatizo la uhaba wa vitendea kazi, magari pamoja na ujenzi wa ofisi kwenye Wilaya ya Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru sana Serikali imejenga miundombinu, lakini bado tuna maeneo ambayo tunaiomba Serikali iyafanyie marekebisho, tunazo shule kongwe ambazo zimejengwa toka enzi za ukoloni, tunahitaji marekebisho ya shule hizo. Shule hiyo ni Shule ya Karema, hali ya mazingira ya Shule ya Karema ni mbaya pamoja na Shule ya Ikola. Kwa hiyo, tunaomba maeneo hayo waweze kuyasaidia na waweze kufanya ukarabati mkubwa kwenye shule ambazo ni kongwe na za muda mrefu. Maeneo hayo tukiyafanyia kazi tutawasaidia sana wananchi na huduma ile itakapokuwa imekamilika itatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumwomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie sana kwenye eneo la uboreshaji wa barabara za vijijini. Hali tuliyo nayo Wilaya ya Tanganyika ni ngumu, mafuriko yapo kila kona na tunahitaji sana huduma ya Serikali ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu. Ninavyoongea leo hii, Watanzania wengi kwenye Jimbo la Wilaya ya Tanganyika wapo kwenye mahema ambayo wanasubiri huduma kutoka

Serikalini. Wabunge wengi tunajitahidi kupeleka misaada kupitia nguvu za wananchi na sisi wenyewe kama Wabunge, lakini bado nguvu tunayoitumia ni ndogo, hivyo tunahitaji msaada ambao unaweza ukawasaidia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kakoso. Namwita sasa Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyopo mezani. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na wakati huo nashukuru sana ushirikiano ninaoupata kwa wananchi wa Urambo na familia yangu jambo ambalo linanipa moyo sana katika ufanyakazi wangu hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu kwa kazi kubwa anayofanya. Ninaweza nikachukua muda mrefu sana kuelezea mambo makubwa aliyotufanyia katika Jimbo la Urambo au Wilaya ya Urambo, lakini lazima nitaje angalau machache; kwa mfano sasa hivi tuna kituo cha kupoozea umeme kinachoendelea kujengwa naishukuru Serikali. Tuna bwawa kubwa la maji ambalo linaendelea kujengwa, lakini pia kuna mradi wa maji ya *Lake Victoria* ambayo yanaletwa Urambo, Kuna barabara nyingi tu za *TARURA* ambazo zimejengwa, shule ndiyo usiseme, shule nyingi za wasichana za sekondari na za msingi. Kwa kweli tunamshukuru sana Dkt. Samia na tunamwombea uhai mwenyezi Mungu amsaidie na ampe nguvu za kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali yake na hasa hii Wizara tunayoifanyia kazi siku ya leo ambayo imeweka hoja mezani, kwa kuanzia Waziri mwenyewe Mheshimiwa Mchengerwa hongera sana, na kazi hiyo

unaiweza, lakini pia Manaibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Dugange, Mheshimiwa Zainab Katimba, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi na *TARURA* mnafanya kazi kubwa sana ya elimu na afya. Kwa kweli hii Wizara inabeba majukumu makubwa kwa sababu waliposhusha madaraka mkoani na kweli wameshusha madaraka mkoani, hii Wizara ina kazi kubwa sana hongereni na Mwenyezi Mungu awape nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia hoja kwa kupongeza kazi kubwa sana inayofanywa na idara zote, lakini kwa leo naomba nizungumzie *TARURA*. *TARURA* inafanya kazi kubwa sana, hongereni sana na hasa kipindi hiki cha mvua barabara zinaharibika kila wakati. Kwa kweli tunaomba Mwenyezi Mungu awape nguvu wafanyakazi wote wa *TARURA,* lakini tuiombe Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia iongeze fedha ili waweze kufanya kazi kubwa hasa mwaka huu ambapo barabara nyingi za mijini na vijijini zote zimeharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, niende kwenye suala la wafanyakazi; unapozungumzia afya, unazungumzia madaktari, wauguzi na kadhalika na unapozungumzia elimu maana yake ni kwamba unataja walimu. Mimi naomba nijikite kwanza kwenye hizi mbili ambazo nimezifanyia utafiti kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapowathamini hawa walimu kubwa na hawa wafanyakazi katika Wizara ya Afya, tunawathamini wakiwa kazini lakini tuwathamini pia wakistaafu. Kwa sababu wamefanya kazi kubwa sana ya kuendelea elimu, kutupima na kutuendeleza sisi kiafya. Kwa mfano, mimi sasa hivi hapa mezani kwangu nina orodha ya walimu 53 ambao wamehenya kazini, wametumikia Wizara yetu ya Elimu, katika shule za sekondari na msingi lakini sasa hivi wanahangaikia mafao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya Wizara ya TAMISEMI kwa kushirikiana na Utumishi na Hazina ili waone jinsi gani ya kuliweka sawa hili jambo. Wastaafu wanapomaliza kazi zao,

wanapokwenda kutafuta mafao yao hasa wakienda *PSSSF*, wanaambiwa wewe hela ulizostahili ni hizi, lakini hauwezi kupata kwa sababu ulipopandishwa madaraja mshahara wako haukurekebishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua ziko juhudi zingine ambazo zimeshachukuliwa na Serikali za kuona kwamba wanaanza kurekebisha mshahara halafu wapandishe daraja, lakini bado kuna tatizo hasa wale waliostaafu siku nyingi, tunaomba hili suala mlifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina orodha hapa ya walimu wanaolia machozi, wanalia machozi tangu wamestaafu hawajapata fedha zao, wakienda *PSSSF* wanaambiwa haujarekebishiwa wewe, kwa hiyo kalete fedha na wapo wengine ambao wameona ili apate fedha zake *PSSSF* wanakwenda kukopa fedha halafu wanapeleka kule ili wapewe mafao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa watu ambao wameitumikia nchi hii kwa uaminifu, kutufundishia watoto wetu na kutibu wagonjwa wetu, kwa kweli wasipitie kipindi hiki. Naamini kabisa Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia na hasa kwa sasa hivi Wizara ya TAMISEMI ilivyo, imepata wachapakazi, kwa kweli suala hili lifanyiwe kazi vizuri kwa kushirikiana na Hazina ili mtu anapostaafu isiwe ni mateso sasa. Ushahidi ninao hapa kutoka Urambo, wananchi wangu wanavyolia, lakini mimi nilikuwa nafikiria siyo hawa, hawa ni mfano tu, lakini naamini nchi nzima wako watu wanaolalamika kwa hili. Kwa hiyo, nilikuwa naomba suala hili lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadharika, wako waliostaafu lakini mpaka leo wanaomba fedha za kuchukua malori waweke mizigo yao waende nyumbani kwao na hawapati. Sasa anabaki hapo hapo au anakwenda kule anasema *place of domicile*, kwa sababu mtu akiajiriwa anaandika kwenu wapi, sasa anabaki hapo hapo kwa sababu hajapewa fedha za kuchukua mizigo yake aende. Kwa hiyo, mimi nafikiri tuthamini kazi za walimu na hawa wafanyakazi wa afya, lakini siyo pale wanapokuwa kazini

tu, hata wakistaafu tuendelee kuwaenzi ili na wenyewe waendelee kuishukuru nchi yao ambayo wameitumikia kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kuzungumzia kwa siku ya leo ni suala la maboma ya vituo vya afya, zahanati na shule. Mpaka sasa hivi maboma yaliyoko nchini kwetu ambayo yalianza kujengwa, wananchi pengine walipewa moyo au waliomba ruhusa na wakaruhusiwa kujenga, wamejenga lakini mpaka leo majengo hayajaisha, naamini kabisa mengine mkituma wataalam watawaambia hata majengo yale hayafai sasa hata kumaliziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna maboma 4,427 nchi nzima, kwa upande wa afya ni 1,253 lakini kwa shule ndiyo 3,744, maboma ambayo yapo yamekaa tu. Wananchi walijitolea muda wao wakabeba mawe, lakini hayajaisha. Kwa hiyo, mimi naomba kwa Serikali hebu ipange fedha, itafute fedha ili maboma yaliyoanzishwa na wananchi yakamilishwe, tusiwavunje moyo wananchi wanapojitolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni uhaba wa wafanyakazi. Kwa mfano, mimi Wilayani kwangu ninao Madaktari wanne tu kwenye hospitali ya Wilaya, kwa hiyo tuna uhaba wa madaktari 18, acha wafanyakazi wengine. Madaktari tu nina uhaba wa madaktari 18 na wafanyakazi wengine, wauguzi na kadharika, wakati huo huo tunajua kabisa mtu ni afya, kwa hiyo, mimi ninaomba kabisa Serikali ije na mpango mzuri zaidi wa kupata wafanyakazi ili watu waweze kutibiwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia shule kuna upungufu mkubwa sana wa walimu lakini jana, tulikwenda hapo katika Shule ya *Bunge Girls* kwenye *graduation,* tulikuta mtu anajitolea tangu mwaka 2021, wote tukashangaa pale hee! Sasa aliposimama, alipoitwa jina lake kwenda kuchukua cheti cha *appreciation* ya kazi nzuri, wanafunzi wote eeeheee! Kwa mwalimu ambaye amekuwa anajitolea tangu mwaka 2021; wote tuliokwenda kule ni mashahidi. Ombi langu sasa ni nini? Hebu naomba tuweke

utaratibu wa uwachukua wale walimu waliojitolea, wanaofanya kazi nzuri, utaratibu ueleweke. Najua siyo kwamba walimu wote Tanzania ni waaminifu, lakini mkiweke utaratibu wa kuwagundua kweli walimu ambao wamejitolea na wanafanya kazi nzuri kama wale tuliowaona pale, tena ni Walimu wawili tuliowaona pale *Bunge Girls* ambao walishangiliwa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, narudia kusema hongereni sana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nawashukuru sasa, ahsante sana kwa kazi nzuri wanayoifanya na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mama Sitta. Nimwite sasa Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani na Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, ajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hoja iliyo mbele yetu ambayo ni ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na mimi naungana na Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mchengerwa na Watendaji wake kwa hotuba nzuri ambayo ameeleza, lakini pia nampongeza Mheshimiwa Mchengerwa na wasaidizi wake, Naibu Mawaziri hawa wawili, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange na Mheshimiwa Zainab Katimba kwa usikivu, hii ni timu ambayo inafikika, inajibu meseji na inachukua hatua haraka. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mchengerwa na timu yako, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia TAMISEMI tuna timu ya watendaji ambao vilevile wanawajibika, wakiongozwa na Katibu Mkuu. Nawapongeza Manaibu wote na Wakurugenzi kwa kazi nzuri ambazo mnazifanya. Kwa kweli TAMISEMI ipo kwa wananchi,

wanajibu *message* saa 24, wanachukua hatua saa 24 na pale tunapotoa taarifa ambazo zinatakiwa kuchukuliwa hatua za haraka basi hatua zinachukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nampongeza Mheshimiwa Rais ambaye ni Waziri mwenye dhamana kwa Wizara hii ambayo ameikasimisha kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais kwa kazi nzuri ambazo anazifanya. Kwa kweli nikianza kuhesabu mazuri na yale ambayo amewafanyia Wana-Nanyamba tutamaliza muda. Nanyamba ameanzisha kongani ya viwanda vya ubanguaji wa korosho ambapo korosho yote Tanzania itabanguliwa pale, tuna mradi mkubwa wa umwagiliaji wa Arusha Chini. Vilevile katika kipindi chake tuna ujenzi wa vituo vya afya vitatu, tuna Mradi wa *TACTIC* ambao unaenda kuibadilisha Nanyamba iwe mji wa kisasa, tuna ujenzi wa stendi mpya, ujenzi wa kituo cha mabasi, ujenzi wa barabara ya lami kilometa tano, lakini pia tuna ujenzi wa ghala. Kwa kweli sisi Wana-Nanyamba hatuyumbi, hatubabaiki na kura zake Mheshimiwa Rais zipo za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza mchango wangu kwa kuizungumzia *TARURA*. Ninasema nitaizungumzia *TARURA* kwa sababu ya *performance* yake ambayo imeonekana. Kama walivyosema wachangiaji wengi ni mtoto wa miaka saba, lakini matokeo yake ni makubwa. Hongera sana Mtendaji Mkuu *Engineer* Seff na hongera watendaji wa *TARURA* na mimi kwa Mkoa wangu nampongeza *Engineer* Zuwena, ambaye ni Meneja wa *TARURA* Mkoa na *Engineer* Nunu, Meneja wa *TARURA* Wilaya kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Hivi karibuni kuna daraja lilikatika kati ya Nanyamba na Kikaya, mpakani na Msumbiji lakini kwa usikivu na uharaka wao, ndani ya wiki tatu, sasa mawasiliano yamesharejeshwa na *TARURA* kweli ipo kazini. Hongereni sana *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa *TARURA* lazima tuwasemee, wana changamoto ya rasilimali fedha, ni lazima tuchukue hatua za makusudi, tuwaongezee fedha ili kazi nzuri ambayo *TARURA* wanaifanya iweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili *TARURA* ina changamoto ya rasilimali watu. Tuna changamoto ya ma-*engineer*, kwa mfano, mimi katika Wilaya yangu, Meneja wa *TARURA* ana Halmashauri tatu, Manispaa ya Mtwara, Halmashauri ya Mtwara na Halmashauri ya Mji wa Nanyamba, lakini ana changamoto ya watumishi wa kutosha. Kwa hiyo, naliomba Bunge na Serikali tuchukue hatua za makusudi ili TAMISEMI ipewe kibali maalum cha kuajiri ma-*engineer* na wapelekwe kwenye Wilaya zetu wakafanye kazi nzuri ambayo imeanza kufanywa na *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili utajikita kwenye upungufu wa watumishi; kwenye mikoa na halmashauri za pembezoni tuna upungufu mkubwa sana wa watumishi, naiomba TAMISEMI wakati wa kugawa mgao wa watumishi waangalie mikoa ya pembezoni. Kwa mfano, Mkoa wangu wa Mtwara kwenye sekta ya afya mahitaji ni watumishi 6,088 waliopo ni watumishi 2,153 tu, tuna upungufu wa watumishi 3,955 sawa na asilimia 65, watumishi waliopo ni asilimia 35 tu ya mahitaji yetu. Kwa hiyo, huu ni upungufu mkubwa, uwekezaji mkubwa ambao tumefanya kwenye sekta ya afya athari yake au *impact* yake haiwezi kuonekana vizuri kwa wananchi kwa sababu ya changamoto kubwa ya watumishi ambayo inaonekana. Naomba tuchukue jitihada za maksudi ili watumishi waajiriwe katika idara hii ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye sekta ya elimu bado kuna changamoto kubwa ya upungufu wa walimu, kwa hiyo, lazima kibali cha ajira kitolewe ili walimu waajiriwe, na naishauri TAMISEMI tutumie vigezo vya upungufu wa walimu uliopo katika maeneo yetu. Hii ajira ya karibuni kulikuwa na maelezo yaliyopita kwamba halmashauri zote za mji hawatapewa walimu. Mheshimiwa Waziri Halmashauri zingine zina sura zote mbili za mji na vijiji, unaposema Halmashauri za Mji hazitapata walimu, unasababisha *chaos* kubwa na upungufu mkubwa sana wa walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Nanyamba hatukupata hata mwalimu mmoja kwa sababu ni Halmashauri ya

Mji, lakini tuna upungufu wa walimu 300. Kwa hiyo, naomba tunapopata ajira ya walimu, mgao uzingatie mahitaji halisi ya walimu na siyo kusema kwamba Halmashauri ya Mji au ya Manispaa wasipate, tuangalie uwiano wa walimu na wanafunzi uliopo ili tuweze kugawa walimu hao kulingana na mahitaji ya Wilaya na Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa tatu utajikita kwenye mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa; Mamlaka ya Serikali za Mitaa kama tulivyoona kwenye bajeti hapa makusanyo yao ni madogo sana, na vyanzo vingi vya mapato kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa havina uhakika, lakini vyanzo hivi vichache vilivyopo bado havisimamiwi vizuri. Udhibiti ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa siyo wa kutosha, kuna fedha nyingi zinapotea kabla hazijapelekwa halmashauri na fedha nyingi hazisimamiwi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile halmashauri nyingi hasa za vijijini zinategemea chanzo kimoja tu cha ushuru wa mazao *(produce cess)*. Ni muda muafaka sasa wa kuangalia vyanzo vyetu vya mapato ili Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa tuwe na vyanzo vya uhakiki. Vyanzo vingi vya uhakika vipo Serikali Kuu, vyanzo vya Serikali za Mitaa havina uhakika na havikusanyiki; na kama vinakusanyika basi ni kwa gharama kubwa. Kwa hiyo, ni muda muafaka wa kuangalia vyanzo vyetu vya mapato ili Mamlaka za Mitaa ziweze kujiendesha, tukifanikiwa kufanya hivyo siyo lazima halmashauri zote zikapange foleni pale Hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kichekesho kwamba leo Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inapanga foleni sawa na Halmashauri ya Mji wa Nanyamba, haiwezekani, halmashauri nyingine kubwa lazima zi-*graduate*, hatutarajii kama Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na majiji mengine tuwawekee *limit* kwamba ninyi ruzuku yenu mtapata asilimia kadhaa. Tunapowapa ruzuku kama halmashauri hizi ndogo ndogo za vijijini na wao wanabweteka hawakusanyi, ni lazima tufike mahali sasa tuwe na uhakika kwamba halmashauri za vijiji zinakuwa na vyanzo vyake na halmashauri za mijini

zinakuwa na vyanzo vyake. Vilevile, tuwawekee *category* kwamba wewe wa Ilala, utegemezi wako kwa Serikali Kuu utakuwa asilimia kadhaa na wewe wa Nanyamba utapata asilimia kadhaa, haiwezekani wote wa mjini na kijiji wote wategemee Hazina... *(Makofi)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa maombi maalum...

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Salome Makamba.

**TAARIFA**

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpa taarifa mzungumzaji anachangia vizuri na nakubaliana kabisa na hoja yake kwamba hizi halmashauri zipewe *treatment* tofauti kutokana na uwezo wao wa ukusanyaji wa mapato. Kwa mfano, kwenye fedha za *SEQUIP* zile shilingi milioni 440, Jiji la Dar es Salaam walipewa milioni 470, wakati huo huo maeneo mengine walipewa milioni 470 kwa lengo la kujenga shule ikamilike. Jiji la Dar es Salaam wakaishia kujenga msingi kwa sababu wenyewe wanataka shule ya ghorofa wakati kwako Nanyamba ulimaliza shule yote ikakamilika na wanafunzi wanaendelea kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nakubalina na wewe kabisa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Chikota, unapokea Taarifa hiyo?

**MHE. ABDALLAH DADI CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa yake na kwa mara ya kwanza amechangia vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maombi matatu; ombi la kwanza, ninampongeza mkuu wangu wa mkoa kwa kazi nzuri anayoifanya hata kama yupo hapa Mheshimiwa Sawala, lakini pili ni Mkuu wangu wa Wilaya Mheshimiwa Mwanahamisi Munkunda anakabiliwa na changamoto ya usafiri, huyu *DC* ni mchapakazi mzuri sana, anazo halmashauri tatu, Manispaa ya Mtwara, Halmashauri ya Mtwara na Halmashauri ya Mji wa Nanyamba lakini hana usafiri, atafanyaje kazi katika halmashauri hizi tatu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, mfahamu kwamba hii Wilaya ya Mtwara inapakana na Msumbiji, huyu *DC* anatakiwa afike Kitaya na Kilambo kama Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, na changamoto za mpaka wetu mnazifahamu, Mheshimiwa Mchengerwa nategemea nikimaliza hotuba hii unitumie meseji kwamba gari ya *DC* wako ni namba fulani. Kipaumbele apewe Mkuu wa Wilaya ya Mtwara kwa *location* ya Wilaya yetu na changamoto zilizoko kule mpakani. Nafikiri Mheshimiwa Mchengerwa hautaniangusha, wewe ni mchapakazi, mimi ninakuamini na hiyo gari ya Mtwara utaipeleka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunayo Shule ya Sekondari Dinyecha, kuna uwekezaji mkubwa sana Mheshimiwa Mama Samia amepeleka zaidi ya shilingi bilioni mbili. Tuna sekondari ya kidato cha tano kwa wasichana, tunaomba fedha za kujenga uzio, tuna zaidi ya wanafunzi 700 wa kidato cha tano na cha sita, ni wasichana tunaomba uzio kwa ajili ya usalama wa watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu la mwisho ni kwamba tunajenga Kituo cha Afya Nyundo kwa nguvu za wananchi, TAMISEMI tengeni fedha mkamilishe hicho kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chikota ahsante sana. Sasa namuita Mheshimiwa Aida Khenani, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mheshimiwa Martha Festo Mariki, ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati naanza kuchangia niseme kwamba tumepokea taarifa ya Mheshimiwa Waziri kuhusu changamoto iliyojitokeza hapa ya miradi ya *CSR*, ni vizuri Bunge lako Tukufu likaweka mwongozo maalum wa mikataba ya namna hii kuipitia yote nchi nzima, kama hili lililozungumzwa wameshachukua hatua, basi wapitie kwenye miradi yote nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu jambo hilo kufanyika Makao Makuu ya Serikali na Chama Dodoma, eneo kama hilijambo hili kufanyika ni aibu kubwa sana. Sasa hili limetokea Dodoma maeneo mengine bado hatujajua, kwa hiyo, ninaliomba Bunge lako Tukufu kuwe na mwongozo maalum wa kwenda kupitia hii miradi yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na *TARURA* kwa sababu ya muda, sote tunatambua majukumu ya *TARURA* na uwajibikaji wake.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naisubiri hiyo taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi pia ninaungana na mchangiaji kuhusiana na suala la *CSR*, naunga mkono taarifa ya Serikali kwamba wanaenda kuvunja mkataba wa miradi ya *CSR* hapa Dodoma na wanaenda ku-*review* sheria ya *CSR* kuona kwamba Serikali za Mitaa zinahusika katika utekelezaji wa miradi hiyo. Kwa hiyo, kama Kamati tunakwenda kufuatilia kwa karibu, nashukuru mchangiaji, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida Khenani unaipokea taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati?

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea taarifa ya Mwenyekiti na inaonesha kabisa kwamba hata Kamati ilikuwa haina taarifa kwamba wamevunja kwa hiyo umakini unahitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee, sote tunatambua umuhimu wa *TARURA* na tunatambua majukumu waliyonayo *TARURA*; pamoja na bajeti kuongezeka jukumu walilonalo *TARURA* kuna haja ya Serikali kuendelea kuongeza bajeti kulingana na majukumu waliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuongeza bajeti, pia kuna maeneo ambayo robo tatu ya barabara zake zinategemea *TARURA* peke yake. Kwa hiyo, pamoja na ugawaji wake ni lazima tuanze kuangalia maeneo yenye changamoto zaidi iwe tofauti na ambavyo inatolewa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuongeza fedha *TARURA*, Mheshimiwa Waziri naomba unisikilize, *TARURA* ni kitu kikubwa sana ambacho tunakitegemea kwenye Taifa letu. Pamoja na ukubwa wake na changamoto ya fedha bado wana changamoto ya watumishi. Watumishi takribani 849 wanahitajika *TARURA*. Sasa kama wanategemea hiki chombo ki-*perform* vizuri ni lazima tuwape watumishi wa kutosha. Shida iko wapi kama tunatenga fedha tunaongeza bajeti bado wanachangamoto ya watumishi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nategemea Waziri ameshafanya vizuri huko alikotokea, lazima tukupime kwenye hili dude kubwa hili TAMISEMI, kwa sababu ukiangalia Wizara yenyewe kwa mujibu wa sheria, Mheshimiwa Rais mwenyewe ndiye Waziri wa hii Wizara. Sasa mnapofanya vibaya, hatumsaidii Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa na kasumba moja, kutenga ni jambo moja na kupeleka hizo fedha ni jambo lingine. Fedha ziende kwa wakati ili tuwapime hawa *TARURA* kwa *performance* ambayo wanafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza mwaka juzi, mwaka jana na mwaka huu nazungumza. Mheshimiwa Waziri naomba unisikie, wakati naelezwa na wananchi wangu, nilipozungumza mwaka jana watu sita walikuwa wamekufa kwenye Kivuko cha Mabatini Namanyele, kivuko kimoja. Wakati huo nazungumza kivuko kimoja watu wanakufa, leo ninavyozungumza watu nane wamekufa. Wananchi wangu wamenituma wakaniambia kamuulize Waziri anataka mpaka nani afe ndiyo achukue hatua? Mimi nakuletea huo ujumbe, mnasubiri nani afe ndiyo mchukue hatua kujenga hicho kivuko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wamefariki, wamefariki na watu wazima. Tunataka nini au ndiyo utekelezaji wenyewe wa Ilani wa namna hii? Watu wameshakufa nane tunasubiri nini? Mimi Mbunge nimeshazungumza mara kadhaa shida iko wapi? Ndiyo maana wanauliza tunasubiri mpaka nani afe ndiyo tuchukue hatua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu wa hilo jambo nikuombe Mheshimiwa Waziri, pamoja na kwamba ni wajibu wako, najua kwamba hii Wizara ni kubwa sana, lakini eneo kama hili la *TARURA* pamoja na mafuriko siyo Rufiji tu, yaani hapa nazungumza Kata ya Kirando kuna mafuriko, Kata ya Itete kuna mafuriko, Kata ya Kabwe kuna mafuriko, Kata ya Korongwe kuna mafuriko. Kwa hiyo, wakati mwingine ninapozungumza ndiyo maana nasema pamoja na kuongeza bajeti, bajeti iendelee kuongezeka eneo kama la kwangu robo tatu ni *TARURA*, si

*TANROADS*. Kwa hiyo, unaweza ukaona *TARURA* walivyo na mzigo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nizungumze jambo lingine kwa sababu ya muda kuhusu miradi ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa maeneo yote nchini. Natambua kwamba kuna ujenzi wa madarasa, vituo vya afya na zahanati. Jambo hili, litakuwa na maana zaidi kama tunapoongeza idadi ya madarasa iendane na idadi ya walimu. Shida kwetu si majengo, shida kwetu ni elimu kwa Watanzania. Mnapopeleka kujenga zahanati na kituo cha afya mmewekeza kwa fedha za Watanzania walipa kodi. Msipopeleka watoa huduma mmewafanya watu wafe kwa matumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi hatukuwa na shida na jengo, kama ni jengo si hata kwangu mtu anaweza akajifungulia? Tuna shida na daktari na tunahitaji huduma itolewe kwa Watanzania. Kwa hiyo, mimi nategemea kwa sasa tutajikita kulingana na idadi ya uwekezaji tujikite kupeleka watumishi pamoja na vifaa tiba kwenye hayo maeneo ambayo tumewekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye elimu msingi peke yake na nitatolea mfano wa Nkasi peke yake, tuna upungufu wa walimu 175; kwenye afya peke yake na yenyewe 175, na sekondari tuna upungufu wa walimu 202. Tunawategemea wakina Mama Samia wengine watoke Nkasi labda kama hatuna mpango tunaamini kule Nkasi hawezi kutoka Rais. Lazima tuwekeze kwenye elimu ili tuwapate Marais wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema maendeleo ya jamii, kwenye Halmashauri ya Nkasi peke yake tuna upungufu wa watumishi saba, hao ambao mnaenda kuwarundikia mambo kibao na mnarudisha hiyo asilimia kumi. Upungufu huo ambao nauzungumza hapa; watendaji wa kata Nkasi peke yake hawapo watendaji 15, hivi hao mnasubiri Malaika Gabriel mbona wapo wenye sifa ya kuajiriwa, tunasubiri nini kwenye hilo jambo?

Malaika Gabriel ashuke ndiye akawaajiri? Sasa mnataegemea tukusanye mapato vipi wakati hizo kata hazina watendaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji wa vijiji 25 na hilo mnahitaji malaika aje ashuke wakati watu wapo wenye sifa na mmeshindwa kuwaajiri. Sijui kuna shida gani kwenye Serikali hii kwenye suala la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine pamoja na mengi tunayoyafanya tusipoelekeza kwa watumishi ni changamoto, naona muda unakimbia sana. Jana wakati nauliza swali hapa kwamba Serikali imekuwa ikijibu kwamba hawana mpango wa kuanzisha maeneo mapya ya kiutawala, nimezungumza suala la Mamlaka ya Mji Mdogo Namanyele. Mheshimiwa Waziri kama Serikali iliweza kuwapa Mamlaka ya Mji Mdogo toka mwaka 2004 na Mkoa wa Rukwa toka mwaka 1974, tulipopata Mkoa wa Rukwa ndiyo mkoa ambao una halmashauri chache kuliko mikoa yote Tanzania, sisi watu wa Rukwa mnatuonaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani mmetupa Mamlaka ya Mji toka mwaka 2004 halafu wale wananchi wanahukumiwa kuanzia upande wa umeme kwa kutumia sheria ya mipango miji kwamba wale wako mjini kwa hiyo watalipia shilingi 320,000 wakati maisha yao ni ya vijijini. Kwa hiyo, huku mnakataa kupandisha kuwa Halmashauri ya Mji wakati wanahukumiwa kwa kupitia hiyo hiyo mamlaka ya mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nina mambo mawili kwenye hilo jambo. Mheshimiwa Waziri, *either* muifute hiyo mamlaka kwamba hamhitaji sasa hivi au nendeni mkaipandishe hadhi kwa kuwa tumekidhi vigezo. TAMISEMI mmewapeleka Tume wameenda kule waamekuja wakasema tumekidhi vigezo na wametumia gharama za Serikali, mna shida gani kuipandisha hadhi? Basi ifuteni sasa maana tumechoka kuzungumza. Tutatumia lugha gani sasa ili mweze kutuelewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo halifurahishi na wananyanyaswa, wanakusanya mapato hawapewi. Mkurugenzi anang'ang'ania zote kwa sababu inaonekana kale ka mamlaka

kapo kihuni kihuni tu. Sasa kama haieleweki ifuteni turudi kwamba hatuna Mamlaka ya Mji kuliko kuwatesa upande mmoja wananchi na upande mwingine mnashindwa kutimiza wajibu wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri, natambua kuna utaratibu wa kupeleka miradi yaani wewe huwezi kutenga shilingi milioni 50 ya kwenda kumalizia ujenzi wa zahanati ukafananisha Kinondoni na Nkasi. Wale watu kusafirisha saruji tu kutoka Dar es Salaam mpaka Nkasi ni shilingi ngapi? Msitoe pesa *uniform* wakati mnajua changamoto ni tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtawalaumu watumishi, leo kama mnachangamoto ya ma-*engineer,* mnawachukua walimu mnawakopa ndiyo wakasimamie miradi, leo tunakuja kuwalaumu wakati hawakusomea hiyo kazi, tutakaa hapo sana. Ninachotaka kusema kama mmeamua kujenga madarasa 40, bei ya Dar es Salaam isifafananishwe na Nkasi, fanyeni tafiti kabla ya kupeleka fedha ili tupeleke fedha ambazo zinaendana na mazingira. *(Makofi)*

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Ilete. *(Kicheko)*

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mtemvu huku.

**MWENYEKITI:** Bahati mbaya muda wa mchangiaji umeisha, kwa hiyo, Taarifa haitapokelewa.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, na namalizia kwa kusema miradi ya kimkakati mmekuwa mnatueleza hapa kwamba…

**MWENYEKITI:** Naomba uhitimishe.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti wangu nahitimisha, dakika moja tu; miradi ya kimkakati mmekuwa mnasema lazima wataalamu wetu waandike maandiko. Hao

wataalamu mnawaleta ninyi Serikali hatuwaleti sisi wananchi. Msituhukumu kwa mapungufu ya watumishi kushindwa kuandika maandiko, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida Khenani, ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi na nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyotutendea mema sisi wananchi wa Liwale, lakini vilevile shukrani za pekee zimwendee Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Mawaziri na watumishi wote waliopo kwenye hii TAMISEMI, kwa kweli wanachapa kazi na kazi zao zinaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo naomba nianze na maombi baadaye nije na ushauri; ombi langu la kwanza, sisi tulikuwa na mradi wetu wa kimkakati wa stendi ya Wilaya ya Liwale Mjini pale. Kwa mara ya kwanza fedha zilikuja mwaka 2018 zikarudi, mwaka 2023 zimekuja tena na zinakaribia kurudi. Naomba ndugu zetu wa TAMISEMI, wahasibu ninyi mnajua mambo yenu huko kwa nini mpaka leo fedha hizo hazijatumika. Naomba fedha hizi mwaka huu zisivuke mwaka tena, tunaomba zifanye kazi ili ile stendi ya pale Liwale Mjini ianze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la pili, shule chakavu; shule nyingi za kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Liwale zimejengwa miaka ya 1970. Kwa hiyo, shule nyingi sasa hivi zimechakaa, hapa nina mfano wa shule chache tu; Shule ya Msingi Kipule, Shule ya Msingi Mtawango, Shule ya Msingi Mkutano, Shule ya Msingi Lilombe, Shule ya Msingi Mangirikiti, Shule ya Msingi Kipelele, Shule ya Msingi Mbaya, Shule ya Msingi Mkutano; hizi shule zimechakaa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule ambayo kuingia mwanafunzi darasani ni maamuzi yake apitie wapi maana hamna mlango. Kwa hiyo, mimi naomba TAMISEMI mtusaidie angalau tukipata hata madarasa manne manne kwenye shule hii mtakuwa mmetusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la tatu; Halmashauri ya Wilaya ya Liwale ina kata 20 lakini kata zake nyingi hazisomani kwa maana kwamba ukitaka kwenda kwenye Kata A lazima uje Liwale Mjini. Halmashauri hii ina miaka 51, barabara zetu za kwenye kata hatujaweza kuziunganisha, maana yake ni nini sasa? Hii inatuongezea hata namna ya kuendesha halmashauri gharama inakuwa kubwa, kwa sababu kupeleka mtihani kwenye shule moja unapeleka mpaka urudi Liwale Mjini ndiyo uende kupeleka kwenye kata nyingine. Kwa hiyo, jambo hili tunaomba sana mtusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, barabara kwa kuanzia, kuna barabara ya Barikiwa – Mkutano, kuna barabara ya Mkutano – Kimambi, kuna barabara Barikiwa – Mlemwe, kuna barabara ya Mpengele – Mpigamiti; kata hizi zote hazijaunganishwa. Tunawaomba ndugu zetu wa TAMISEMI mtusaidie kutuunganishia hizi barabara ili ziweze kupitika kirahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la tatu, ni kuhusu watumishi; tunao uhaba mkubwa sana wa watumishi na leo ni mara yangu ya tatu nachangia kuhusu watumishi Wilaya ya Liwale. Sasa mmekuwa na utaratibu wa kuleta watumishi Wilaya ya Liwale ili waje kuchukua namba baadaye mnawahamisha. Hili jambo halikubaliki na mimi naomba niseme, kama utaratibu ndiyo huo, basi mtuachie wale walioko kule msituletee wengine, kwa sababu haiwezekani mmeleta watumishi 50 au 80, ndani ya mwaka mmoja wanabaki kumi au 20. Jambo hili halikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niwaambie TAMISEMI; hawa watumishi pamoja na kwamba mnawahamisha ndani ya mwaka mmoja, wakikaa zaidi ya mwaka mmoja hawahami tena, fursa zilizoko kule ni kubwa. Wakizoea mwaka mmoja tu

wanajenga majumba kule, wanaoa kule, wanaolewa kule, hawahami tena. Kwa hiyo, mimi naomba kama mnawaleta kule wachukue namba ili waondoke, msiwalete, hilo ndilo ombi langu la nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakwenda *TARURA;* kwanza niunge mkono maoni yote ya Kamati; tumepeleka maoni tisa, yale maoni tisa kama TAMISEMI mtayachukua na kuyafanyia kazi, mtakuwa mmemtendea haki Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu ndiyo mwenye Wizara, kinyume chake mtakuwa mmemchonganisha Rais na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoa maoni tisa, naomba yote yafanyiwe kazi kikamilifu. Tumesema *TARURA;* kwanza mimi niwashukuru sana *TARURA*. Katika taasisi za Serikali, kama kuna taasisi tano zinazofanya vizuri huwezi kuiacha *TARURA*. Hapa nitoe angalizo, kuna taasisi moja TAMISEMI inaitwa Tume ya Utumishi wa Walimu. Mheshimiwa Waziri hebu nena na hiyo taasisi, walimu hawako salama, walimu hawana furaha, walimu wana manung'uniko moyoni, taasisi hiyo ipo. Jambo hili halizi kuwa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Utumishi wa Walimu eeh?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu hawako salama na hii tume, hebu chungulia chungulia huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri katika Sheria ya Manunuzi na Sheria ya Matumizi ya Fedha ya Serikali; hivi miundo ya taasisi zote za Serikali inafanana? Kama muundo wa taasisi haufanani iweje Sheria ya Manunuzi ifanane? Unamwambia Mkurugenzi wa Kijijini, akienda kupeleka maiti kijijini akimpelekea anahitaji *EFD Machine*, majeneza yenyewe wanatengeneza wale vijana wa mtaani, hiko chakula chenyewe wanapika mama ntilie kule leo mnamwambia atoe *EFD machine*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa siku wanasema kwamba hiyo hoja ya ukaguzi, haina shida itafutwa. Kwa nini muweke hoja ambazo zitakuja kufutwa, kwa nini msiondoe kabisa? Yaani mnatengeneza hoja eti kwa sababu tu itafutwa basi iendelee kubaki tu. Kwa nini tusitengeneze sheria ambayo tukajua kwamba sheria hii ina kwenda *Local Government*, sheria hii inakwenda hospitali za Serikali? Kuchanganya changanya hizi sheria wakati miundo ya hizo taasisi tunazoenda kuongoza au wanazoenda kuzitumia hazifanani haileti mantiki, hebu twende mbele zaidi tuangalie kwamba hii Sheria ya Manunuzi ya leo kule kijijini inafaa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa nina wasiwasi, hawa wanaotengeneza hii mifumo ya *NeST,* sijui kama wanatoka vijijini. Hivi mtu anayetoka Mpigamiti anaweza akakubaliana kwamba gari la Mkurugenzi wa Liwale limeharibika tairi aingize kwenye *NeST* ili mtu wa Kigoma a-*supply* matairi Liwale, inawezekana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wanaotengeneza hii mifumo inawezekana si wenzetu na sijui wamesoma wapi? Kama wamesoma sidhani kama ni watu wa vijijini kama wametoka Mpigamiti hivi, labda wametoka Marekani; kwa sababu mtu wa kawaida haiwezekani gari la Mkurugenzi Liwale limeharibika tairi, *supplier* atoke Kigoma, matairi Lindi pale yapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwenye dunia ya leo tuna uhaba wa kushindwa kujua bei ya tairi? Tuna uhaba wa kujua *spare* ya gari fulani inauzwaje mpaka tuingize ingize humu kwenye ma-*NeST*, sijui *TAUSI?* Yaani ni vurugu vurugu tu hivi hivi ilimradi tuibiwe. *(Makofi)*

Mimi nataka niseme ukweli, ni dhambi kubwa sana kumwambia Mkurugenzi wa Halmashauri anakuja Dodoma asubuhi na jioni, anaacha gari kule hazina matairi, aje kule aingie kwenye *NeST* ndiyo aombe matairi. Kumpa Mkurugenzi shilingi milioni tano au sita aje anunue matairi hapa apeleke kule apeleke na risiti ni wizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii bei ya tairi na ya *spare* ya magari nani asiyejua? Acheni hizo tabia jamani twende na wakati, na ninyi mnaotengeneza tengeneza hivi vi-*NeST, NeST* hebu muangalie. Kweli tunakwenda na mazingira tuliyonayo au mnaiga tu kwa sababu mmesoma huko Ulaya, mmeingia kwenye mitandao mmeona wenzetu wanafanya nini na nyie mnabeba kama ilivyo mnatuletea hapa mahali ambapo ni tofauti kabisa na uhalisia, twende na wakati. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka, muda wako umekwisha.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Martha Festo Mariki, atafuatiwa na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, ajiandae.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika bajeti ya Wizara ambayo inagusa kabisa maisha ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na afya njema. Kipekee kabisa nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu kipenzi kwa jinsi ambavyo anafanya kazi kubwa katika Taifa letu la Tanzania na kwa namna ambavyo anafanya kazi kubwa kwa sisi wananchi wa Mkoa wa Katavi, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu. Ninaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi kwa kuleta pesa zaidi ya shilingi trilioni 1.2 ndani ya miaka mitatu ya mama yetu kipenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wananchi wa Mkoa wa Katavi, tunazidi kumwombea Mheshimiwa Rais wetu, kwanza kwa

kuboresha Sekta ya afya; ametuletea pesa nyingi sana kwa kujenga hospitali za wilaya, kujenga vituo vya afya pamoja na zahanati. Wananchi wa Mkoa wa Katavi katika miaka mitatu ya Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia, tumeweza kupata vituo vya afya zaidi ya 20 na zahanati zaidi ya 36. Hayo yote ni mapenzi ya Mheshimiwa Rais wetu kuhakikisha kwamba sekta ya afya inaboreshwa katika Mkoa wa Katavi. Hivyo, sisi kama wananchi wa Mkoa wa Katavi tunasema ahsante sana Mheshimiwa Rais wetu na tunaendelea kukuombea Mwenyezi Mungu azidi kukupa maisha marefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee sana niendelee kushukuru kwa ajili ya pesa zilizokuja katika Mkoa wa Katavi ambapo zilivyokuja katika Mkoa wetu wa Katavi, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wetu wa Katavi, sitoacha kumpongeza kwa usimamizi mzuri sana wa pesa hizi nyingi zilizoletwa ndani ya miaka mitatu ya uongozi Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mheshimiwa Waziri ninakupongeza pia pamoja na Naibu Mawaziri wako wawili na watendaji wote wa Wizara hii ya TAMISEMI kwa jinsi ambavyo mnafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wananchi wa Mkoa wa Katavi katika Wilaya ya Tanganyika kuna Kata inaitwa Kata ya Ilangu, ni kata ya kimkakati na ni kata ambayo ina *population* kubwa sana ya wananchi. Tayari wananchi wale wameanza kujichanga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya. Mama zangu wa kata ile wanatembea umbali mrefu kwenda kupata huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana, kwa kuwa wananchi wameshaonesha juhudi za kuanza kujenga kituo cha afya, niiombe Wizara husika muweze kutenga fedha kwa ajili ya kuwajengea wananchi wale kituo cha afya ili waweze kuepukana na kutembea umbali mrefu, hususani mama zangu wanaokwenda kujifungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI pamoja na mambo mazuri yanayofanyika katika Wizara hii, tuna upungufu mkubwa sana wa watumishi katika sekta ya afya. Mkoa wa Katavi pekee tuna uhaba wa zaidi ya asilimia 57;

tuna watumishi ambao ni sawa na asilimia 43, kwa hiyo, uhaba ni asilimia 57 utaona kwamba pamoja na Serikali imepeleka fedha nyingi sana na kuonesha juhudi, lakini bado wananchi hawapati huduma iliyokusudiwa kutokana na kwamba watumishi ni wachache katika sekta hii ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hospitali kama Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe pale watumishi ni wachache, unakuta daktari ni mmoja yeye pekee awahudumie wagonjwa wengi na hivyo inasababisha zile fedha ambazo Mheshimiwa Rais amepeleka hazioneshi ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe, watumishi hawa katika mikoa hii ya pembezoni ukiwemo mkoa wangu wa Katavi wana ukosefu mkubwa sana wa nyumba za watumishi. Ukiangalia Halmashauri ya Nsimbo watumishi wa sekta ya afya wanalazimika kuja katika maeneo ya mjini kwa ajili ya kupanga nyumba. Kama unavyoelewa hospitali hizi zenye *level* ya wilaya nyingi zilijengwa maeneo ambayo unakuta ni mbali na makazi ya wananchi na hivyo wanalazimika kuja kupanga nyumba maeneo ya mjini. Nimwombe Mheshimiwa Waziri wetu aweze kuangalia nyumba za watumishi ili waweze kuwahudumia wananchi kwa ukaribu na kwa ufanisi uliokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuwa katika Mkoa wetu wa Katavi katika sekta ya elimu amefanya kazi kubwa kwa kutupatia fedha nyingi ikiwemo fedha za miradi ya *BOOST*. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kuboresha sekta ya elimu katika Mkoa wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na maboresho hayo zipo changamoto; changamoto ya kwanza ni pamoja na uchakavu mkubwa wa shule kongwe zilizojengwa miaka mingi iliyopita. Kuna shule zimejengwa miaka ya 1970 lakini shule hizo mpaka sasa ukiziangalia kwa kweli mazingira hayaridhishi. Sasa niiombe sana Serikali yetu, kwa kuwa shule hizo kwa sasa ni muda tunaona ni muda wa *El-Nino,* mvua zinanyesha nyingi, kwa hiyo ni hatarishi sana kwa watoto wetu wanaotumia vyumba vile vya madarasa kwani kuta zinaweza kuwaangukia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo niiombe sana Wizara ya TAMISEMI watenge fedha kwa ajili ya kuboresha shule kongwe zote nchini zikiwemo hizi za Mkoa wa Katavi kama Shule za Katumba na Mtapenda ambazo kwa kweli ni kongwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa pia nizungumzie suala la *TARURA*; nianze kuwapongeza *TARURA* kwa kazi kubwa wanayoifanya, nimpongeze sana mtendaji mkuu wa *TARURA Engineer* Seff kwa kweli anafanya kazi nzuri, lakini pia pamoja na uchache na Wabunge hapa tumesema kwamba *TARURA* iongezewe fedha, lakini ni ukweli usiopingika kwamba hata kama fedha zikiongezwa tunamwomba *Engineer* Mkuu wa *TARURA* sana ashuke kule chini aangalie ipo changamoto katika eneo la *TARURA*. Kumekuwa kuna ujenzi wa mitaro ambayo haina kiwango, wanatumia madini ambayo hayana kiwango kwenye ujenzi. Hivyo niombe sana Mheshimiwa Waziri washuke kule chini kuweka kuangalia nini kinachosababisha mitaro inajengwa lakini ikinyesha mvua kidogo tu mitaro yote inakuwa imeharibika, hii imetokea si kwa sababu ya mvua hizi zilizonyesha kwa mwaka huu, hata miaka ya nyuma mitaro imekuwa inajengwa chini ya kiwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nini kinachosababisha wanajenga barabara ambazo pia zinakuwa hazina mitaro kiasi kwamba mvua ikinyesha inakwenda kuharibu ile barabara yote na miundombinu inakwenda kuharibika na hivyo kuisababishia Serikali hasara kubwa, lakini pia inasababisha fedha hizi za *TARURA* pamoja na kwamba ni ndogo, zinakuwa hazitumiki kwa ufanisi na hivyo kusababisha matatizo mengi katika maeneo ya miundombinu ya barabara za wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la mwisho ambalo niombe wananchi wa Usevya daraja lile ambalo lilikuwa limejengwa tayari limekuwa limeelemewa na mvua zilizonyesha kwa kiasi kikubwa katika mvua za mwaka huu. Kutokana na hali hiyo kumekuwa hakuna mawasiliano kwenda katika makao makuu ya halmashauri. Niwaombe sana muweze kututengea fedha kwa ajili ya daraja hili la Usevya ili liweze kujengwa kwa

kiwango na kunusuru wananchi wetu katika mafuriko haya yanaoyoendelea katika mikoa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitumie fursa hii pia kutoa pole kwa maeneo yote nchini ambayo yamekumbwa na mafuriko liliwemo eneo la Rufiji anapotokea Mheshimiwa Waziri wetu. Nitumie fursa hii kuwapa pole wananchi wenzangu wa Mkoa wa Katavi kutokana na mvua zilizonyesha juzi. Hivi ninavyozungumza Mkoa wa Katavi hatuna mawasiliano kutoka Katavi kwenda Kigoma wala Katavi kwenda Rukwa. Tunaiamini Serikali yetu ni sikivu, ma-*engineer* wa *TARURA* tayari wapo pale kuhakikisha kwamba changamoto hiyo inakwenda kutatuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee sasa tuseme sisi wananchi wa Mkoa wa Katavi tunazidi kumwombea Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa anayoifanya na sisi wananchi wa Mkoa wa Katavi tunasema kwa kweli ilani imetekelezwa na Mheshimiwa Rais wetu hatuna tunachomdai, mambo ni madogo yaliyobaki na tunaamini yatarekebishwa na tunaendelea kumwombea heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana, ahsante sana Maheshimiwa Martha Mariki. Nimuite sana Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mheshimiwa Michael Mwakamo ajaindae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia mada hii ya Wizara ya TAMISEMI jioni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya maisha aliyotujalia wakati huu tunapojadili taarifa hii ya TAMISEMI sisi wote Wabunge humu ndani. Kwa kweli kwa namna ya pekee hii hali ya kutujalia afya

njema ndiyo imetufanya tuwasemee Watanzania wetu wote wakati huu wakitutazama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kwanza kwa namna ya pekee niungane na wale Wabunge wote waliompongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa inayofanyika na mimi Jimbo la Mbulu Mjini niseme tu kazi kubwa imefanyika kwa namna ya pekee katika kila sekta sina sababu ya kupoteza muda. Kazi hizo nyingi zilizofanyika zimegusa sana maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Mchengerwa, Waziri wa TAMISEMI kwanza kwa kazi kubwa pamoja na timu yake yote ya Naibu Mawaziri, watendaji wote wa Wizara, lakini pia na taarifa ya Kamati kwa jinsi ambavyo imechakatwa na kuletwa kwenye Bunge hili. Niseme tu kwamba taarifa hii iliyoletwa kwenye Bunge ni sehemu ya taarifa kubwa ambayo imejadiliwa na Kamati kwa muda wote wa kipindi cha Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pia pole nyingi kwa ndugu yetu Mheshimiwa Mchengerwa na wananchi wa Rufiji kwa jinsi ambavyo walipata kadhia ya mafuriko hivi punde. Watanzania tunawaombea Wana-Rufiji Mwenyezi Mungu awabariki na awaondolee kadhia hii iliyowapata hivi punde, na maeneo mengine hapa nchini kwa jinsi ambavyo hali ya mafuriko yameisumbua Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia nafasi hii kwa namna ya pekee sana kuizungumzia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hii ni Wizara kubwa, Wizara yenye nchi nzima, kila mahali unapokwenda huikosi halmashauri kwa ndiyo Serikali ya wananchi na halmashauri ipo kila mahali. Mara nyingi fedha nyingi za halmashauri zinazotolewa hazitoshi kwa sababu mahitaji ni makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Wizara na Serikali fedha zote tunazopitisha kwenye bajeti ya Wizara ya TAMISEMI Serikali ijitahidi kuzitoa ili kukidhi haja na matarajio ya Watanzania. Yote

tunayoyaahidi humu ndani kwa namna ya pekee au tunayoyajaridi Watanzania wanasubiri Dodoma saivi namna ya kutatua matatizo mengi yaliyopo kwenye sekta mbali mbali hasa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumza elimu umeisema TAMISEMI. Kitengo chote cha elimu TAMISEMI ndicho kinachoshusha fedha chini na ndicho kinachosimamia sekta ya elimu, lakini pia miundombinu, rasilimali na shughuli zote za kila siku, na fedha hizo zinapokosekana shughuli nyingi zinakwama kule chini. Afya ni TAMISEMI pia ni eneo kubwa sana. Kwa mfano tukizungumzia elimu. Jimbo la Mbulu Mjini ndilo jimbo pekee katika Mkoa wa Manyara lenye shule kongwe. Kwa historia ya shule ya kwanza iliyojengwa kule Jimboni Mbulu ilijengwa mwaka 1907. Niishukuru sana Serikali wamejenga shule mpya inayorithi ile shule sasa hivi watoto wanasoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nina shule takribani 20 sasa hivi; tayari tumeshajenga shule mpya mbili na tayari tunasubiri shule mpya mbili, lakini pia wamekarabati shule tisa katika shule 20 zilizokuwa zimejengwa kabla ya uhuru. Niiombe Serikali itume timu kule Mbulu ione umuhimu wa shule hizi kongwe kubadilishwa kuwa shule mpya na kubadilishwa kuwa shule mpya na kubadilisha mazingira yake kwa sababu Wilaya ya Mbulu ilianzishwa na mkoloni 1905 hizo shule zote zilizo kongwe sasa hivi nyingi hazifai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo kwa namna ya pekee naipongeza Serikali kwa sababu hata hizo tisa zinazokarabatiwa ni shule nyingi zimepeleka hela na hela zimejenga miundombinu nzuri tunaishukuru sana Serikali, lakini iendelee kutoa jitihada za namna hiyo. Kutokana na ujenzi huu wa vituo vya afya na zahanati tumenufaika sana, lakini bado kuna maendeleo ya kata ambazo kwenye baadhi ya kata ambazo ni za kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ichukue jukumu la kwenda kujenga Vituo vya Afya vya Murray, Nambis, Gehan pamoja na Bunyoda, hayo ni maeneo ya pembezoni. Wizara ielewe kuwa Jimbo la Mbulu Mjini tuna kata kumi vijijini na kata saba zipo mjini.

Hayo maeneo ya vijijini ni maeneo ya mbali sana, pengine kilometa 40, kilometa 30, kilometa 50 wananchi wanahitaji huduma, na vituo vyote vitatu vilivyojengwa tayari vipo kwenye maeneo ya pembezoni hayapo mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo hata hizo kata tunazoombea pamoja na maeneo mengine nchini; kwa sababu tunapozungumza kama Bunge lazima tuone maeneo yenye uhitaji mkubwa katika kata zetu na katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo jingine ni eneo la *TARURA;* kwa kweli tusifichane *TARURA* fedha tulizonazo za mwaka huu unaoisha Juni haitasaidia hata asilimia 50 kurudisha huduma ya Barabara. Kwa hali ya mvua na uharibifu tulioupata tuna kila sababu ya kuitazama *TARURA* kwa macho mawili na waongezewe fedha za dharura ili huduma za usafiri zirudishwe katika majimbo yote nchini, kwa sababu athari zinaonekana ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa bajeti hii tunayojadili hatuwezi kufanya kitu chochote kwa kuwa tayari tumeshaathirika kwa kiasi kikubwa na tunaishukuru Serikali kwa hatua inazochukua kwa pale ambapo maeneo yamekuwa magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbulu Mjini kwa kuwa tuna maeneo ya vijijini na maeneo ya mjini, kwa mfano saivi ukitaka kwenda Kata ya Bunyoda huwezi kufika kuna eneo ambalo barabara imejifunga, lakini unapokwenda Tarafa ya Nambis kule Hailoto tuna maeneo ya barabara yamejifunga. Tunawashukuru watendaji wa *TARURA* waliopo kwenye wilaya, mikoa na hata huku makao makuu kwa jinsi wanavyojitahidi, lakini bila fedha jitihada hizi hazitasaidia kwa sababu utatuzi wa matatizo hayo unahitaji fedha na jinsi ya kurudisha miundombinu ambayo tayari imeathiriwa. Kwa hiyo, naiomba Serikali itazame upya hatua za dharura ili kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka nilizungumze ni miradi ya *TACTIC*. Mimi ni mnufaika wa *TACTIC* kwa kuwa nipo kwenye mpango wa ujenzi wa miradi ya *TACTIC*

ya maboresho nchini kwenye miradi ya ujenzi wa soko, dampo, stendi na ujenzi wa barabara za lami. Niiombe Serikali tufanye mchakato huu, kwa kuwa tuna tatizo la wataalamu ngazi za mikoa zisaidie namna ya miradi hii iweze kutelekelezwa kwa wakati katika maeneo ambayo tunakwenda kutekeleza miradi hii ili wale wenzetu wabia wa maendeleo wasikate tamaa, watusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbulu Mjini ni mji ambao hauna soko, stendi, dampo, machinjio na wala hauna barabara za lami mjini, zipo chache. Tunaishukuru Serikali wamejitahidi kujenga bararara za lami, lakini bado tuna mahitaji makubwa kama mji mkongwe. Kwa hiyo niiombe Serikali ijitahidi katika usimamizi wa hii miradi kwa ngazi ya mikoa, kwa ngazi ya Wizara, mikoa na halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie eneo la ujazaji wa nafasi wazi za watumishi wanaostaafu. Tunapata pengo kubwa sana, hivi sasa tumeanza shule mpya na madarasa tumejenga mapya. Sasa ile kuleta msawazo wa wanafunzi kwenye madarasa, lakini pia na ile hali ya kujenga shule mpya imeleta uhitaji mkubwa wa walimu katika majimbo yetu. Tunaiomba Serikali itafute namna mbadala ya kuomba kibali cha ajira kwa Mheshimiwa Rais ili tuape walimu ili waweze ku-*cover,* kuzuia na kupunguza upungufu mkubwa unaotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi, muda wa wanafunzi unaenda, walimu ni wachache sana na kwa hivyo kwa nchi nzima tunapata pungufu mkubwa sana. Kwa hiyo, tukipata ajira hizi za mbadala pia na ile ajira ya kwenye bajeti itasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili la ajira mbadala tuirudishe halmashauri. Kwa nini nashauri hivi; mwalimu anastaafu kwa mfano mwaka huu wa fedha, tunasubiri mpaka kibali cha ajira mpya wakati mshahara wa yule mwalimu upo na anaweza kuajiri pengine labda hata walimu wawili. Kwa hiyo, halmashauri ikipewa kibali cha kuajiri hao walimu itasaidia sasa kujaza ile nafasi mapema na pengo hilo linaweza na yule mwalimu

aliyeajiriwa anaweza kujaza hilo pengo na kutoa huduma kwa wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie upelekaji wa fedha za ujenzi wa maboma. Tumeleta maboma nchi nzima kila Mbunge ameleta maboma. Tunaiomba Serikali itusaidie fedha za maboma ya afya na maboma ya elimu kwa maana yale yote yaliyojengwa na wananchi kwa sababu tayari tuna maboma yana miaka sita, miaka nane, miaka saba lakini kwa kweli hatujaweza kuunga juhudi za wananchi ili yale maboma yaweze kujengwa na yaweze kutoa huduma kwa wananchi wetu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha kabisa, nikuombe tu uhitimishe hoja yako.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana naomba niunge mkono hoja tuendelee na kipindi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zacharia. Nimwite sasa Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mheshimiwa Michael Mwakamo atafuatia na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile ajiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia Wizara hii muhimu na kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mchengerwa pamoja na timu yake makini sana ya wasaidizi ninayoiona pale, kwa jinsi ambavyo wanamuwakilisha vizuri Mheshimiwa Rais katika dhamana kubwa waliyopewa ya kuendesha Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya TAMISEMI yameanza kutajwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ukienda Sura ya Nane Madaraka ya Umma, Ibara 145(1) inatamka juu ya uwepo wa vyombo vya Serikali za Mitaa, Mikoa, Wilaya na Vijiji. Halafu ukienda Ibara ya 146(1) inazungumzia

madhumuni yakuwepo kwa Serikali za Mitaa ambayo ni kupeleka madaraka kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maudhui haya yameakisiwa vizuri kabisa katika ile Hati ya Mheshimiwa Rais Namba 30 ya mwaka 2023 ambayo ndiyo inayoiongoza Ofisi ya Rais, TAMISEMI kutekeleza majukumu yake katika mikoa yote 26, wilaya 139 na halmashauri 184. Kwa hiyo, ukiangalia TAMISEMI ina majukumu mapana sana na kwa sababu hiyo ninapata hofu kidogo juu ya bajeti yake ya upande wa mafunzo kama inatosha na pia kama ina-*focus* kwenye maeneo ambayo yanagusa majukumu yake ya Kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majukumu haya yaliyotajwa ina maana kwamba TAMISEMI ndiyo inayobeba Ibara ya Nane ya Katiba ambayo kila mtu ukimsikia wanaharakati wanapozungumza wanasema Ibara ya Nane Mamlaka ya Serikali yanatoka kwa wananchi, na wanaoyabeba yale kwa kiasi kikubwa ni TAMISEMI. Sasa tunahitaji mafunzo kwa kina sana kwa watendaji wote wa TAMISEMI kuanzia vitongoji, vijiji, kata, tarafa, yaani mwananchi akimuona Mtendaji wa Kijiji asianze kuona mahabusu, asianze kuona ushuru, asianze kuona mgambo, bali aione pia ile Ibara ya 146(2) ya kuimarisha demokrasia katika eneo lake na kuitumia ili kuharakisha maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nasisitiza kwamba demokrasia inayozungumzwa ambayo inatekelezwa na TAMISEMI siyo ya maneno ya jukwaani bali ni demokrasia ambayo inaharakisha maendeleo, hilo ni jukumu lao. kwa hiyo nadhani tunahitaji mafunzo kwa kiasi kikubwa sana ili kubadilisha mfumo wa kufikiri kwa baadhi ya waendaji wetu hasa kule chini. Tukifika hapo hata mabango yatapungua viongozi wetu wanapokwenda kufanya ziara, na hata wanaohoji juu ya uhalali wa TAMISEMI kusimamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa nadhani pia wataishiwa na hoja kama wakikutana na watendaji ambao wapo *trained* anaojielekeza katika mwelekeo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye Jimbo langu la Mwanga. Wananchi wa Jimbo la Mwanga wamenituma

salamu nyingi za shukrani kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwanza kwa ajili ya miradi mingi sana ambayo ameileta katika Jimbo letu la Mwanga. Mwanga kwa kipindi hiki cha miaka mitatu inatelekeza miradi ya zaidi ya shilingi bilioni 51 na sehemu kubwa ya miradi hiyo ikiwa iko chini ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba hii siyo Wizara ya Maji, lakini wananchi wa Mwanga hawatanielewa nikimtaja Mheshimiwa Rais hapa bila kutaja mradi wa maji wa Mwanga-Same-Korogwe ambao tunausubiri kwa hamu mwezi wa sita tunywe maji kama ambavyo Mheshimiwa Rais mwenyewe ametuahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wanashukuru kwa ajili ya timu nzuri ya watendaji ambayo tumeletewa kuanzia ngazi ya Mkoa, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa Nurdin Babu na timu yake, Mkuu wangu wa Wilaya Abdallah Musa Mwaipaya pamoja na timu yake ya wataalam. Kazi inayofanyika ni nzuri sana na inatupa *support* hata sasa Wabunge kutekeleza majukumu na inatoa *support* kubwa kwa chama katika kutusimamia hata sisi Wabunge kutekeleza majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naona kengele ya kwanza imeshalia, niseme yafuatayo, mpaka sasa hivi kila kata yangu ya Wilaya ya Mwanga tayari ina shule, tunachoomba ni mabweni hasa katika shule zifuatazo; Shule ya *Usangi Day,* Shule ya Sekondari Lang'ata, Shule mpya ya Kitoloa, Shule ya Kishengweni na Shule ya Sekondari Mandaka. Shule hii ya Sekondari Mandaka ina Mkuu wa Shule wa kipekee sana ambaye amefanya juhudi pamoja na wazazi na wadau wengine wameshajenga mabweni takribani matatu, tunaomba apewe nguvu katika kumalizia kazi aliyoifanya na kuanzisha nyingine mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano ipo kwamba shule zetu zenye mabweni katika Wilaya ya Mwanga, Shule ya Dkt. Asha-Rose Migiro, Nakamwala ni moja kati shule bora kitaifa kutokana na hali kwamba wananchi wote wanakaa kwenye yale maeneo ya shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoomba sasa juu ya shule mpya na nianze kutanguliza shukrani kwa sababu ninazofununu, tunaomba sasa ziende kuwa shule za michepuo hasa mchepuo wa ufundi. Wilaya yetu ya Mwanga, muasisi wa wilaya yetu ya Mwanga Mzee wetu Cleopa David Msuya alitujengea sana mila ya kujenga nyumbani, watu wanajenga sana. Kwa hiyo, wateja wapo wa kazi za ufundi, tunaomba shule za michepuo ya ufundi ili vijana waweze kupata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye vituo vya afya, tuna vituo vya afya vipya kama vitatu, kuna kituo kiko Kisangara, kuna Kituo cha Kigonigoni na Kituo cha Kirya na hivi ni vituo vipya vya kimkakati. Kituo cha Afya cha Kirya tunaomba sana kipatiwe nyumba za watumishi kwa sababu uelekeo ambako kipo ni mwelekeo ambao ni mgumu kidogo kwa watumishi wa afya kupata nyumba za kupanga na kile kituo kinahudumia Wilaya za jirani kama Simanjiro na Same, sasa tunaomba kitiliwe mkazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya zamani, Kituo cha Kagongo ambacho kiko Kata ya Lang'ata, Kituo cha Afya Kifula pamoja na vile vituo vya zamani kwenye maeneo yaliyojengwa vituo vya afya vya kimkakati vinahitaji ukarabati mkubwa, tunaomba Serikali Wizara itupie macho hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye upande wa barabara, niungane na wenzangu kuwapongeza sana wenzetu wa *TARURA* wanafanya kazi nzuri sana katika Wilaya yangu ya Mwanga. Barabara zimejengwa vizuri pamoja na changamoto ya hali ya hewa, lakini wanajitahidi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichomekee kwa haraka hapo, ninawashukuru *TARURA* kwa kutimiza ahadi ya taa za barabarani, nimepata taarifa imeanza kutekelezwa eneo la *Mombasa Store* kwenda Hospitali ya Wilaya. Ninaomba sana mkimaliza hapo basi muelekee na maeneo mengine, nina uhakika hata wenzetu wa *TANROADS* nao watajifunza kwenu na wataendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara mpya ya *CD Msuya by-pass* tunaomba itiliwe mkazo kumaliziwa kwa sababu inaungana na *VETA* ambayo Mungu akipenda itaisha mwezi wa saba kama ile barabara itakuwa haijaisha italeta changamoto. Tunaomba *special attention* kwenye barabara mbili za Kata ya Ngujini na Kilomeni. Kata hizi zilitunza sana mazingira na kwa sababu zilitunza mazingira zinapata mvua nyingi, kwa hiyo, zinapata sana changamoto ya miundombinu yao ya barabara kuharibiwa mara kwa mara. Kwa hiyo, tunaomba sana barabara za kwenye kata hizi mbili za Kilomeni na Ngujini zitiliwe mkazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nipongeze sana *TARURA* kwa sababu wameanza mradi wa kihistoria wa barabara itakayounganisha kata hizi mbili. Barabara ile ikitiliwa mkazo ikikamilika basi ni rahisi hata mambo kama vituo vya afya vikiwa kwenye kata moja wanaweza waka-*share* kwenye kata mbili, huu ni mradi wa kihistoria tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Usangi kwa Kihindi kilometa 11, kilometa sita zilikuwa zinapitika, kilometa tano ni mpya zimejengwa kwa umakini wa hali ya juu sana niwapongeze sana *TARURA* kwa ajili hiyo. Lakini zile kilometa sita kutokana na changamoto ya hali ya hewa ya mvua zimeharibika sasa. Kwa hiyo, tusipopata fedha za dharula angalau tukatengeneza maeneo korofi, uwekezaji mkubwa ambao umefanyika kwenye zile kilometa tano unaweza ukawa ni hasara. Kwa hiyo, tunaomba sana tupate fedha kwa ajili ya kumalizia maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la watumishi ni changamoto katika halmashauri yetu, karibu idara nane ambazo ni nyeti hazina Wakuu wa Idara ni watu wanao-*act.* Kwa upande wa afya tuna tatizo la wataalam wa mionzi na ma-*physiotherapist,* kwa hiyo, tunaomba eneo hili pia litazamwe kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, tunaishukuru sana TAMISEMI kwa umakini wao na kazi nzuri ambayo imefanyika Jimboni Mwanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja, kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo**.** Sasa nimwite Mheshimiwa Michael Constantine Mwakamo, atafuatiwa na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo ajiandae.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipatia nafasi ya kuchangia na awali ya yote nichukue nafasi hii kutoa pole nyingi kwa Mheshimiwa Rais kwa majanga makubwa yanayolikuta Taifa la mafuriko ambayo yanasababisha kumfanya awe kwenye wakati mgumu wa kufikiria namna ya kuweza kuwasaidia wananchi wake kumudu kupata maisha yanayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo napenda kutoa pole nyingi kwa Mkuu wa Mkoa wangu wa Pwani, maana tangu mafuriko yatokee kule Rufiji na Kibiti, kwa kweli mara zote anashinda huko, ameshirikiana na Wabunge wa eneo husika. Kwa kweli niwape pole nyingi sana lakini niwaombee Mungu awape nguvu za kuhakikisha kwamba wanakabiliana na changamoto zilizopo kwa sababu kila jambo hupangwa na Mola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi na pole hizo, pia nitoe shukrani za kutosha kwa Mheshimiwa Rais na Serikali yake kwa namna ambavyo wanatekeleza miradi ya maendeleo katika nchi hii hususan kwenye Jimbo langu la Kibaha Vijijini, lakini pamoja na hayo nawashukuru wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini kuendelea kuniombea, kuendelea kumwombea Mheshimiwa Rais na kujitolea katika kila jambo ili kuweza kutimiza malengo ya kutekeleza miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niweze kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa namna ambavyo amewasilisha taarifa yake, nimeisikiliza na kwa kweli kwanza niungane na yeye na Serikali kwa ujumla, namna ambavyo imeweza kuona katika lile suala zima la miradi ya *CSR* kusitisha ile

mikataba kwa sababu kwa kweli ilikuwa ni chaka lingine ambalo wananchi walikuwa wakisikiliza matumizi ya kwenye miradi hii wanashindwa kuelewa kama miradi hiyo inatekelezwa ndani ya nchi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu haiwezekani miradi inayofanana na miradi inayosimamiwa na Serikali iwe inatumia pesa tofauti. Kwa hiyo, nawapongeza kwa kuchukua maamuzi haya na niwatakie kila la kheri katika utaratibu wanaotaka kwenda kupitia kanuni na kuweza kutoka na kanuni zinazoweza kusaidia kutekeleza miradi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo niendelee kulizungumzia suala zima la utekelezaji wa miradi kwenye maeneo yetu na niipongeze Serikali kwa namna ambavyo mtiririko wa fedha kwenye halmashauri mbalimbali ukienda. Sisi kwenye Jimbo letu la Kibaha Vijijini hadi sasa tunapozungumza zaidi ya asilimia 80 ya fedha zilizotakiwa kuja kwa miradi ya maendeleo ya mwaka wa bajeti inayoendelea zimeshafika na miradi imetekelezwa. Naipongeza sana Serikali na Wizara ya TAMISEMI kwa namna ambavyo wanazitoa fedha kwa ajili ya kwenda kutekeleza miradi mbalimbali. Hata hii asilimia 20 iliyobaki, tatizo unalikuta kwamba siyo suala la Serikali kushindwa kupeleka fedha ila ni miradi ambayo inatakiwa ikamilike halafu *certificate* ipelekwe. Kwa hiyo, unakuta ni tatizo la wakandarasi kushindwa kukamilisha kazi zile ambazo walipaswa kuzitekeleza ili waweze kulipwa.

Kwa hiyo, nawapongeza sana na niwaombee kuendelea kufanya hivi kwa sababu Watanzania wana matumaini makubwa na utekelezaji wa shughuli za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto kwenye mtiririko wa hii miradi, miradi inapokea fedha, inakwenda kutekelezwa, lakini unakuta miradi mingi haikamiliki. Sasa niombe Serikali na nimwombe Mheshimiwa Waziri na timu yake ambayo sina mashaka nayo, wajaribu kupita kwenye hizi halmashauri, wajaribu kuangalia sababu za msingi zinazosababisha miradi isitekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kifua anacho na anao wataalam wa kuweza kuchukua hatua kwa wale wanaofanya makusudi, lakini kwa kweli zipo sababu nyingine zinasababishwa na mazingira ya kijiografia kufanya miradi hii siende. Kwa hiyo, ifike sehemu watakapogundua sababu za kweli zilizosababisha miradi isikamilike wasisite kutoa fedha kukamilisha miradi ile kwa sababu wananchi wanasubiri kupata huduma kutoka kwenye miradi iliyokamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kuna suala zima na mimi nilizungumze la *TARURA*, sote tunafahamu kwamba barabara nyingi katika majimbo yetu ni za vijijini, barabara zinazohudumiwa na *TANROADS* ni chache. Barabara nyingi zinahudumiwa na hawa *TARURA* ambao fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara hizo ni chache sana.

Kwa hiyo, niombe Serikali ione namna ambavyo inaweza ikaongeza mafungu katika baadhi ya hizo halmashauri ili hizi barabara ziweze kupata huduma zinazostahili, kwa sababu barabara zilizoko kijijini ndio zinazotakiwa kutoa mazao, ndio zinazotumika katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo, sasa kama zitakuwa zinapata fedha chache kutakuwa na hali duni ya kuweza kuzihudumia na sababu hiyo inaweza ikasababisha wananchi warudi nyuma kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mwaka huu tumesikia kila kona mafuriko, tumeona mvua zilivyokuwa nyingi, barabara nyingi zimefumuka na bahati mbaya mvua zimeanza kunyesha wakandarasi wakiwa *site* wanaendelea na kazi hii, na barabara nyingi wakandarasi walikuwa ni wale wanaotengeneza barabara za vumbi. Kwa hiyo, mvua imeharibu kazi zote ambazo zingine zilishatangulia kufanywa, niwaombe warudi kupita tena na watoe maelekezo kwa *TARURA* huko wilayani, waweze kuzipitia, waone madhara yaliyopatikana baada ya mvua kunyesha ili waweze kufanya ukarabati unaostahili, kwa sababu maeneo mengine ni maeneo ya kimkakati kuna viwanda vinaendelea kujengwe vya wawekezaji, wawekezaji wanashindwa kutoa bidhaa zao kutokana na hali halisi ya mvua zinazoendelea. Kwa hiyo, niombe

sana Serikali iweze kufikia utaratibu wa kuweza kutuma pesa na kuweza kukamilisha miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, wengi wamezungumza na hili jambo ambalo limezungumzwa pengine na mimi kwangu lina nafasi yake. Tuna shule nyingi sana chakavu, tunashukuru kuna miradi inayoendelea kwenye utekelezaji wa shule mpya, lakini shule chakavu ambazo zilitangulia kabla hizi zinazojengwa ni shule ambazo zina sura mbaya kama ambavyo amezungumza Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa kuwa kuna baadhi ya maeneo mwanafunzi anaamua atokee wapi, anaweza akaingilia mlangoni akatokea dirishani kulingana na shule zilivyokuwa. Ninaamini kabisa pamoja na kuwepo na pesa nyingi za kuweza kutengeneza shule mpya kutakuwa na uwezo wa kutafuta mbinu za kuweza kufanya ukarabati wa shule hizi ili zifanane na hizi shule ambazo zinajengwa sasa hivi na wananchi waweze kwenda kufurahia huduma inayotolea. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nikushukuru sana, muda wako umekwisha Mheshimiwa Michael Mwakamo.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Simon Lusengekile, atafuatiwa na mchangiaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kunipa nafasi nami nichangie hotuba ya Waziri wetu wa TAMISEMI. Nimshukuru sana Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa leo. Kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anazofanya kwenye nchi yetu ikiwepo kuleta fedha nyingi kwenye majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni nikiri tumepokea magari mawili kutoka kwa Mheshimiwa Rais tuliyokabidhiwa na

Mheshimiwa Waziri wetu wa TAMISEMI kwa ajili ya Busega, tunashukuru sana kwa kweli, yanaenda kutusaidia kwa sababu moja ni *ambulance* lakini moja ni kwa ajili ya ufuatiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili la shukrani, nimwombe sasa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu apeleke salaam zangu za pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais. Hapa juzi tumeona Serengeti yule Bwana Mhasibu aliyebeba hela shilingi milioni 189 kama sikosei kusafirisha kwenye basi, sasa nilikuwa nawaza huyu jamaa alikuwa anafikiria nini. Kweli leo unasafirisha karibu shilingi milioni 180 kwenye basi, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu ameonesha uzalendo mkubwa wa kuhakikisha kwamba anaokoa fedha za Serikali, lakini pia anamsaidia Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yako, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu pamoja na Naibu Makatibu Wakuu pamoja na Wakurugenzi wa idara mbalimbali, niwapongeze sana kwa kazi kubwa mnazofanya. Pia nimpongeze Mtendaji wa *TARURA* kwa kweli wanafanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba miundombinu ya barabara inaimarika kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, sasa niseme mambo machache kwa ajili ya wananchi wa Busega, Mheshimiwa Waziri, wananchi wa Busega wamenituma mambo machache. Jambo la kwanza, Mheshimiwa Rais tarehe 4 Februari, 2022 alipita pale Lamadi akaahidi kuwapatia soko pamoja na stendi wananchi wa Lamadi. Sasa kazi ya Mheshimiwa Rais alishamaliza, kazi ya Mheshimiwa Rais alishaahidi akamaliza, sasa imebaki kazi kwako Mheshimiwa Mchengerwa kuhakikisha kwamba Busega pale Lamadi tunapata soko pamoja na stendi. Sisi kama wilaya tayari tumeshakabidhi kwako *document* ya gharama kwa ajili ya ujenzi wa soko pamoja na stendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba walau hata mojawapo kwa mwaka huu wa fedha ambao tunaingia kwenye bajeti basi

utupatie kimojawapo au vyote ili tuweze kuanza utekelezaji wa miradi hii ya kimkakati ambayo Mheshimiwa Rais aliahidi na tayari tulishafanya usanifu na kuhakiklisha kwamba walau *TBA* wanaleta kwako ili uweze kujua mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti yako nilipokuwa nasoma sijaona sehemu ambako umeweka hii miradi ya kimkakati. Sasa nikuombe na ninaomba uniweke kabisa kwenye orodha ya watu watakaoshika shilingi yako kama hutakuja na majibu ya lini sasa miradi hii au mradi mmojawapo utaanza lini pale Lamadi. Tunahitaji kuwa na soko litakalo gharimu zaidi ya shilingi bilioni tatu pamoja na stendi itakayogharimu zaidi ya shilingi bilioni mbili. Kwa hiyo, tunaomba sana, haya ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais aliahidi pale na alielekeza yafanyike haraka na mimi kama Mbunge wa Jimbo wana Lamadi wamenituma niyalete kwako ili uweze kuwapatia fedha tuanze ujenzi wa hii miradi ambayo iliahidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, nikuombe sana, nikuombe sana utupatie fedha, uingize kwenye mpango wako wa mwaka wa fedha 2024/2025 ili tupate fedha kwa ajili ya ujenzi wa miradi hii ambayo nimeisema pale Lamadi mradi wa soko pamoja na stendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo niseme jambo moja ambalo hata mwaka jana wakati nachangia hotuba ya Wizara ya TAMISEMI nilisema. Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Dugange akiwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Simiyu alipandisha hadhi Zahanati ya Kiloleli na kuwa Kituo cha Afya, alipandisha hadhi Zahanati ya Lukungu na kuwa kituo cha afya, lakini tunavyozungumza leo vina-*apply* kwa jina la kituo cha afya, lakini hakuna majengo ambayo yanakidhi kuitwa kituo cha afya, hakuna majengo ambayo yamejengwa yanayokidhi kuwa kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine nikuombe tena mtani wangu, rafiki yangu Mheshimiwa Mchengerwa angalia wananchi hawa wa Kiloleli, angalia hawa wananchi wa Lukungu, haya ni mambo ambayo yalifanyika chini ya Dkt. Dugange

alipandisha hadhi vituo hivi na sasa jukumu hili bado linarudi kwake, alilikwepa kule Simiyu akiwa Mganga Mkuu akaenda kugombea bado linarudi kwake, ni Naibu Waziri wa TAMISEMI, nenda ukamalize haya ambayo uliyaanzisha. Ulianza vizuri ukiwa Mganga Mkuu na sasa uko TAMISEMI na bahati nzuri sana uko TAMISEMI - Afya kwa hiyo, bado uko pale pale usikwepe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, mnong'oneze hapo Mheshimiwa Waziri tumalize tatizo la Kiloleli na Lukungu, vituo hivi vya afya vifanye kazi kwa hadhi kama ambavyo vilikusudiwa. Nikuombe sana tufanye hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine limechangiwa hapa na Wabunge juu ya maboma ambayo yamejengwa na wananchi. Tuna maboma mengi sana ambayo yamejengwa na wananchi, lakini pamoja na hayo hata Busega tuna maboma zaidi ya 80 ya shule ambazo zimeanzishwa na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana sasa tuje na mkakati ni kwa namna gani tunawasaidia wananchi ambao walishaanzisha maboma yao, maboma kwa ajili ya watoto, maboma kwa ajili ya vituo vya afya, maboma kwa ajili ya zahanati ili tuweze kuyakamilisha. Lazima tuje na mkakati, kuna muda mwingine tunashukuru tunapokea fedha kwa ajili ya madarasa mapya kutoka Serikalini, tunashuru sana, lakini wananchi wanahoji kwa nini tunajenga mapya wakati yale ambayo yapo wao wamejenga, yameshakamilika kwa *level* ya boma mpaka sasa hivi bado hatujayamalizia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri uje na mkakati wa namna gani maboma ya wananchi wa Busega tunakwenda kuyakamilisha, ni kwa namna gani maboma ya wananchi wa Rufiji yanaenda kukamilika, ni lazima tuje na mpango kama nchi, ni lazima tuje na mpango kama Wizara tuweze kukamilisha maboma ambayo yamejengwa na wananchi. Si hivyo tu ni lazima wananchi tuwape faraja, kwa sababu sisi tukienda kule tunawaambia anzisheni maboma, sasa ni mwanzo mzuri wananchi wamefanya, lazima sisi tufanye jukumu letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kwenye eneo la hayo maboma, kuna maboma ya fedha za Serikali yaliyokamilika, nataka ni-*cite* mfano mdogo sana, shule hizi za mikoa za wasichana. Wazo la Mheshimiwa Rais na wazo la Wizara lilikuwa safi sana na Mheshimiwa Rais alishamaliza kazi yake, Mheshimiwa Rais alishatoa fedha zaidi ya shilingi bilioni tatu zimeshaenda kujenga shule hizi za mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimeenda wapi pale kuna hii shule iko barabarani hapa Solya iko Singida, Manyoni, nikawa nawaza mbona majengo mengi, kama Kamati tumepita pale tumetembelea, majengo ni mengi na wanafunzi waliopo ni *form one,* hata nyumba yako Mheshimiwa Mchengerwa, kama hauishi inaharibika, ni lazima sasa tuoneshe *value for money, value for money* sio kuwepo na majengo peke yake ni ile *outcome* ambayo tumetarajia ili tuoneshe *value for money* ya hizi shule ni lazima tuyafikie malengo ambayo tulitarajia kwa sababu malengo hayakuwa kujenga majengo peke yake. Malengo ni pamoja na watoto kuingia huku kusoma, shule kama zile zina madarasa ya *form one, form two, form three, form four,* lakini wanafunzi waliopo ni wa *form one* yanasubiri yale mengine kuja kumaliza sijui miaka mitatu mbele ndiyo waingie watoto wafike *form four*. *Dormitories* pia sasa ni lazima, ili kuonesha *value for money* kama tulitarajia kupeleka watoto pale, basi tuchukue watoto wa *form two* na kama inawezekana hata *form three* waliopo kwenye shule nyingine, tuwabebe tuwapeleke pale, ili yale madarasa yafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna sababu ya kujenga madarasa ambayo yamekaa *idle,* hayafanyi kazi na mwisho wa siku yataharibika. Mheshimiwa Waziri mimi naomba sana muangalie hapa, ili tuoneshe *value for money* ya yale majengo tuliyoyajenga ikiwa ni pamoja na ku-*provide quality* ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Simon Lusengekile. Sasa namwita mchangiaji wetu wa mwisho, Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa fursa na mimi niweke mchango wangu kwenye hii Wizara yetu ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambayo kimsingi tunasema ndio Wizara ambayo ina-*deal* moja kwa moja na maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kukupongeza wewe kwa nafasi hiyo uliyopo hapo, kumbuka kuwa wewe ni jirani yangu kwa hiyo, mimi najivunia kuwa na rafiki ambaye ni jirani yangu na yuko hapo na unafanya vizuri na kwa mazingira hayo sasa uniache nichangie vizuri usije ukanibana kwenye muda. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mchengerwa na timu yake ya Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Dkt. Dugange pamoja na Mheshimiwa Katimba. Nawapongeza kwa kazi nzuri na kwa kweli, wanatupatia ushirikiano tunapokuwa na shida mbalimbali wanatusikiliza. Nawaomba waendelee kuwa *humble* namna hiyo, ili tuendelee kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi hii pia nampa Mheshimiwa Waziri pole kwa majanga yaliyotokea kwenye eneo lake. Ninaamini Mwenyezi Mungu atatenda kwa nafasi yake na wale wananchi watanusurika na maisha yataendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoendelea nayo ya kuwahudumia Watanzania na kwa miradi mingi sana ya maendeleo inayokuja kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Singida Kaskazini tumepata miradi mingi sana ya afya, elimu na barabara hasa barabara za vijijini. Bajeti ya *TARURA* hivi sasa iko kwenye shilingi bilioni mbili kutoka shilingi milioni 600, 700, lakini leo tuna bilioni

mbili *plus*, ni kazi nzuri ya Mheshimiwa Rais. Hivyo, tuna wajibu wa kuendelea kumwombea, kumtia moyo na kumuunga mkono. Pale anapofanya vizuri ni lazima tumpe tano zetu na pia tunasema mitano tena kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwenye eneo la afya, kwenye Jimbo langu la Singida Kaskazini tumeendelea kupata fedha kwenye maeneo mbalimbali hasa kwenye vifaatiba. Hospitali yetu ya Wilaya ya Ilongero pamoja na vituo vya afya vya Msange, Mgori na kile cha Makuro tumepata vifaatiba, madaktari kwa maana ya watumishi japo siyo wengi, tulipata 48 ni hatua nzuri na tumepata *ambulance* mbili katika wilaya, ni jambo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutupa sisi Wabunge heshima ya kukabidhi *ambulance*. Tunakushukuru sana na tulifanya lile jukumu kwa heshima kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumepata *standby generator* katika hospitali ya wilaya na ile ya Msange ingawa bado hazijaanza kufanya kazi, lakini hatua iliyobakia ni ndogo kuliko hii iliyokwishafanyika. Hivyo, ninaishukuru sana Serikali kwa hatua hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili la afya ninaomba niwasilishe changamoto kadhaa, mojawapo ni kumalizia Kituo cha Afya cha Boma na Kituo cha Afya cha Ngimu. Siku Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye Jimbo langu, pale Sagara, nilimweleza na Mheshimiwa Waziri alipokea, akanipa majibu mazuri yenye matumaini na wananchi walisikia. Mheshimiwa Waziri nakuomba tena leo hii jambo hili ulichukulie *very serious* utusaidie fedha zije kwenye Kituo cha Afya cha Ngimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku alipoteuliwa Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Katimba, nilimtumia ujumbe na nilinong’ona naye nikamkumbusha. Kwa hiyo, naomba nitumie tena hii fursa kuwakumbusha tupate fedha kwenye kile kituo cha afya ili wananchi wetu waweze kupata huduma. Eneo lile liko kwenye Bonde la Ufa jambo ambali linafanya mazingira yake

kuwa ni magumu kwa upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wetu, hususan wazee na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Kituo cha Afya Kinyagigi ambacho wananchi wamejitolea na wamekijenga. Hata hivyo, bado kuna jengo la *OPD* linahitajika pamoja na kumalizia baadhi ya maeneo na bajeti yake siyo kubwa, hivyo nimwomba Mheshimiwa Waziri atupe kipaumbele, akiweke moyoni mwake kituo kile anapokumbuka Singida basi akumbuke Kituo cha Afya cha Kinyagigi, ili tupate fedha na wananchi wetu wapate huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ninapenda kuli-*address* ni la kukamilisha miundombinu ya Hospitali ya Wilaya pale Ilongero; kuna maeneo ambayo naomba yatazamwe kwa ukaribu, moja ikiwa ni *mortuary,* pale hatuna *mortuary,* kwa hiyo, ninaomba ili tunapopata zile dharura basi tuweze kuhudumiwa. Vilevile, kuna shida ya *walk ways,* wagonjwa wanapotoka kwenye chumba cha upasuaji kwenda wodini wanapata tabu, lakini pia hospitali ile haina uzio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye wilaya yangu kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi wa sekta ya afya pamoja na elimu; kwenye afya peke yake tuna upungufu wa watumishi 454, kwa hiyo, naomba sana Serikali itutazame kwa ukaribu, ili tuweze kuondoa changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye elimu; wenzangu na hata Kamati pia wamesema, na nisingependa kurudia, pengine maeneo haya Wizara ingeyachukua na iyatazame kama kipaumbele kwa sababu wanapozungumza Wabunge wengi hapa inamaana ni tatizo kubwa. Hata kwenye Jimbo langu la Singida Kaskazini mambo ni yale yale, kuna shule kongwe za miaka ya 1950 leo ukienda yale majengo hayafanani kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru tumepata shule mpya mbili za msingi, zenye *package* nzima, shule mpya mbili za sekondari na wananchi wanapata huduma, lakini sasa zile shule kongwe nazo zitazamwe kwa jicho la karibu. Kuna shule ambazo

zimechoka kabisa yaani hazifai hata kutazamwa, kwa mfano, kwenye Jimbo la Singida Kaskazini kuna Shule ya Msingi Ghata, Shule ya Msingi Nkwae, Ughandi, Semfuru, Msimihi, Itaja, Ghalunyangu, Matumbo na Lamba, shule hizi ziko hoi kweli kweli kwenye miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri alichukue hili na alitazame kwa ukaribu angalau tuboreshe miundombinu ya shule hizi, ili wananchi wetu wapate huduma ambayo inaendana na mazingira tuliyonayo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la watumishi katika shule za msingi nalo litazamwe kwa karibu, walimu ni wachache sana. Eneo hili linahitaji kutazamwa kwa jicho la karibu sana *country wise*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna shida ya *hostel,* wanafunzi wanatembea umbali mrefu mno ili waweze kufika shuleni kwa mfano, Shule ya Msingi Pohama, Misinko, Modeda, Mughunga, Msisi, Mrama, Maghojoa, Mwasauya pamoja na Makuro, watoto wetu ni wadogo na wanatembea umbali mrefu sana. Kwa hiyo, ninashauri eneo hili tulitazame kwa karibu ili tuwapunguzie adha watoto wetu wanapokwenda shuleni. Mtoto anachoka, njiani anakutana na changamoto nyingi wakati anaenda shule, kwa hiyo, anafika darasani akiwa tayari amepoteza matumaini. Hivyo ni vizuri eneo hili nalo tulitazame kwa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho kwenye uchangiaji wangu wa leo ni eneo la barabara za vijijini kwa maana ya *TARURA*. Kwa kweli, tunashukuru kuwa mvua ni neema, hata hivyo, zimetuletea matatizo, barabara zimeharibika mno. Kwa kweli wananchi wanapata tabu sana, kwa hiyo, naomba madaraja; lile Daraja la Mpambaa tulipata fedha shilingi milioni 600, lakini naona hakuna kinachoendelea, Daraja la Mgori limekuwa likiua watu mara kwa mara. Hata juzi kuna watu wamefariki pale kwa sababu maji huwa yanajaa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona umewasha *microphone*…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha kabisa.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi, naomba sana kile Kijiji cha Mokulu kiwe kijiji kamili kwa sababu wale wananchi wanahitaji sana. *(Makofi)*

Baada ya kusema haya ninaomba kuunga mkono hoja, lakini haya tuliyozungumza pamoja na kwamba, muda ni mchache naomba yafanyiwe kazi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana jirani yangu, Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa shughuli zetu za leo, naahirisha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.47 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 17 Aprili, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*